BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini – Tarehe 16 Mei, 2016

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWEMYEKITI: Tukae. Katibu!

NDG. RAMADHANI ABDALLAH – KATIBU MEZANI: Hati za Kuwasilisha Mezani.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. COSATO D. CHUMI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MWENYEKITI: Ahsante, Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa kama kawaida yetu, swali la kwanza Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga. Hayupo? Kwa niaba yake Mheshimiwa Chegeni.

Na.165

Wafanyakazi Kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi Wanavyotaka

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. JAPHET N. HASUNGA) aliuliza:-

Sheria ya Mahusiano Kazini ya mwaka 2004 inawataka wafanyakazi kujiunga na vyama vya wafanyakazi vya kisekta; walimu na wafanyakazi wengine wamekuwa wakiingizwa kwenye vyama hivyo bila ya wao wenyewe kukubali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaruhusu wafanyakazi kujiunga na vyama vya wafanyakazi wanavyotaka kwa hiari badala ya kuwalazimisha?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004 imeeleza bayana kuwa wafanyakazi wanayo haki ya kuanzisha au kujiunga na vyama vya wafanyakazi wanavyovipenda wenyewe pasipo kumlazimisha mtu yeyote. Hivyo ni makosa kwa mtu yeyote, awe ni mwajiri au chama cha wafanyakazi, kumlazimisha mwanachama kujiunga na chama pasipo ridhaa yake. Taratibu ni kwamba mfanyakazi anatakiwa kujaza fomu namba *TFN 6* ili kutoa idhini yake kujiunga na chama anachokipenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena kutoa wito kwa waajiri wa vyama vya wafanyakazi kuzingatia matakwa ya sheria kwa kutowalazimisha wafanyakazi kujiunga na vyama vya wafanyakazi pasipo ridhaa yao. Hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya waajiri na vyama vya wafanyakazi vitakavyokiuka matakwa ya sheria hii ili kuruhusu wafanyakazi kuunda vyama vya wafanyakazi katika maeneo yao ya kazi. Hata hivyo Serikali inatoa onyo kwa waajiri wanaokiuka sheria za kazi kwa kuwalazimisha wafanyakazi kujiunga na vyama vya wafanyakazi wasivyovitaka. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa waajiri wanaokiuka sheria za kazi.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini inafahamika kabisa kwamba vyama hivyo vya wafanyakazi vinakuwa vinachukua matakwa na mahitaji ya wafanyakazi wenyewe. Na kwa kuwa Serikali imekuwa ikiwasaidia sana waweze kuingia katika vyama hivi na Serikali hapa imetoa agizo kwamba itawachukulia hatua waajiri ambao wanawazuia kujiunga na vyama hivi.

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa sababu baadhi ya wafanyakazi wanakuwa wamefanya kazi lakini wanakuwa na madai yao mbalimbali ambayo hawajalipwa na Serikali. Kwa mfano, Chama cha Walimu Tanzania kina madai mengi sana Serikalini lakini madai hayo bado hayajalipwa. Je, kupitia bajeti hii, Serikali itatoa tamko la kuwalipa walimu madai yao na malimbikizo yao?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tamko Serikali itasema nini, naomba nirudie katika majibu yangu ya msingi ya kwamba Serikali kupitia Sheria Namba 6 ya mwaka 2004 imeendelea kutoa msisitizo kuwataka waajiri wote kuruhusu wafanyakazi wajiunge katika vyama vya wafanyakazi. Na jambo hili ni la kisheria na Kikatiba, na vilevile sisi Tanzania tumekubaliana na ile *ILO Convention* Namba 87 ambayo inazungumza kuhusu uhuru wa wafanyakazi kujiunga katika vyama vyao.

Kwa hiyo, nichukue tu fursa hii pia kuwataka waajiri kwa kutoa tamko tena ya kwamba wahakikishe kwamba wanawaruhusu wafanyakazi wao wote kujiunga na vyama vya wafanyakazi kwa sababu hii ni haki yao ya kimsingi ya kushirikiana kama ambavyo imesemwa kwenye sheria na kwenye Ibara 20 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Chatanda, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongezea katika majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri,katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Ni kwamba, katika suala zima la madai ya walimu, tumezungumza kwamba sasa hivi Ofisi ya Rais - TAMISEMI inafanya uhakiki wa madai yote. Lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba walimu wote ambao wanadai, na si walimu peke yake bali katika kada mbalimbali, katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha unaokuja basi madai yote tuweze kuya-*address;* kila mtu afanye kazi kwa *morale* katika mazingira yake ya kazi.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Chatanda.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa walimu wamejiunga na *PSPF* lakini walimu hawa wanapoomba mikopo watu wa *PSPF* wanachelewa sana kuwapa majibu na kuwakamilishia haki yao ya msingi ambapo wengine wanakuwa wamekaribia kustaafu wanataka wajiandae. Je, Serikali inawaelezaje walimu hawa ambao wanakaribia kustaafu na wanahitaji wapate huo mkopo wanawacheleweshea kuwapa mkopo huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ni haki ya walimu waliojiunga katika mfuko wa *PSPF* kupata mkopo pale ambapo wamekidhi yale masharti yanayohitajika, kwa maana umri ule wa kustaafu ambao kwa mujibu wa taratibu za sasa za mfuko ule, tayari wamekwishakuanza kutoa mikopo kwa walimu ambao wamekaribia umri wa kustaaafu kuanzia miaka 55 wakishapeleka maombi yamekuwa yakifanyiwa kazi.

Nichukue tu fursa hii kuwaomba walimu wote ambao watakuwa wamekidhi masharti na vigezo vya kupata mkopo basi wafike katika ofisi zao kwa ajili ya kuweza kupata huduma hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea. Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe.

Na. 166

Matokeo Mabaya Katika Shule za Serikali Nchini

MHE. LUCIA M. MLOWE aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi kubwa la wanafunzi wa shule za Serikali za msingi na sekondari wanaofeli kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi katika darasa moja dhidi ya mwalimu mmoja kwa wanafunzi huku wakifundishwa kuanzia saa moja na nusu hadi saa kumi na nusu jioni, na kufanya walimu wakose muda wa kutosha wa kusimamia kazi za wanafunzi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na changamoto hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha elimu nchini kwa kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani, Serikali imeendelea kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali ilitenga shilingi bilioni 67.83 ambazo zimepokelewa na zimetumika ka ajili ya ukarabati, ujenzi na umaliziaji wa vyumba vya madarasa, vyoo vya walimu na wanafunzi, ujenzi wa nyumba sita *(multiple unit houses)* na uwekaji wa umeme *(grid house solar)* katika shule za sekondari 528 nchini kote. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017 zimetengwa shilingi bilioni 48.3 kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na juhudi katika ujenzi wa miundombinu, Serikali inatarajia kuajiri walimu wapya 35,411 kwa shule za msingi na sekondari ili kuongeza idadi ya walimu hivyo kupunguza mzigo mkubwa uliopo kwa walimu kwa lengo la kuongeza tija katika sekta ya elimu hapa nchini.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mlowe.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza na nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa sababu kuu za ufaulu duni ni miundombinu mibovu ya ufundishaji na kujifunza. Je, Serikali imeweka mkakati gani kwa shule za Njombe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa waathirika wakuu ni wasichana, kwa sababu wanapewa kazi nyingi na wazazi wao majumbani, je, Serikali ina mkakati gani kumsaidia mtoto huyu wa kike?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la miundombinu mibovu, hili ni kama tulivyosema katika bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha kwamba tumeelekeza katika maeneo mbalimbali ili angalau kuongeza *speed* kwenye hii changamoto tuliyo nayo hivi sasa ya wanafunzi wengi sana tuliowasajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo vilevile kuwafanya walimu wafundishe katika mazingira rafiki. Ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu mkoa wa Njombe peke yake tumetenga kiwango cha fedha cha kutosha ili kuhakikisha maeneo mbalimbali yanaweza kufikiwa. Ndiyo maana tukifanya rejea ya bajeti yetu tuliyopitisha hapa hapa, siwezi kukupa takwimu halisi, lakini tumeugusa Mkoa wa Njombe kuangalia kipaumbele hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la miundombinu Mheshimiwa Mbunge nadhani na wewe ni mpiganaji mzuri katika eneo hilo. Ukiachia miundombinu, vilevile miongoni mwa mambo ambayo yanachangia sana ni suala zima la malezi. Wakati mwingine wazazi wanakuwa *irresponsible*, hawawajibiki vya kutosha kuhakikisha watoto wao wanawasimamia kwa karibu.

Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie wakati napita pita maeneo mbalimbali, kuna maeneo mengine utakuta madarasa yapo ya kutosha, hali kadhalika walimu wa kutosha lakini shule zile tulizozipitia hakuna hata mwanafunzi aliyepata *division one* au *division two*. Kwa bahati mbaya zaidi unaweza kukuta walimu wengi wa sayansi hakuna lakini wa *arts* wapo na bado huwezi ukaona "C" moja au "B" moja ya Kiswahili wala ya *civics*; ni kwamba *concentration* ya watoto imekuwa chini. Kwa hiyo, jukumu letu kubwa sambamba na kuongeza miundombinu tuna changamoto kubwa ya kuwahamasisha wazazi kusimamia suala zima la taaluma za watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuwaokoa vijana wetu wa kike. Ni kweli suala la mimba kwa watoto wa kike limekuwa kubwa, ndiyo maana mchakato wetu sasa hivi ni tunajielekeza katika ujenzi wa shule za sekondari za bweni hasa kwa upande wa wanawake. Lengo letu ni kuhakikisha zile changamoto zinawapata watoto wanapokwenda shuleni ziweze kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Afya wiki iliyopita alisema kwamba wale mabaradhuli wanaohakikisha wanaharibu watoto wa watu, tuhakikishe wanachukuliwa hatua kali ili hawa watoto wa kike waweze kupata elimu yao kama ilivyokusudiwa.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kumekuwa na tabia ya walimu kuto-*report* kwenye mikoa ambayo inaitwa mikoa ya pembezoni kama Mkoa wetu wa Lindi. Je, kuna mkakati gani mwaka huu wa kuhakikisha kwamba walimu watakaopangwa watakwenda Lindi kutatua tatizo kubwa la walimu lililopo kwenye shule zetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana. Anataka kujua ni lini tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, wiki iliyopita nilisema kwamba kuna tatizo, si mkoa wa Lindi peke yake, ukienda Katavi, Kigoma, Mara, Sumbawanga na maeneo mengine. Tumesema mwaka huu tu tunaajiri walimu wapatao 35,000, lakini walimu wengine wakipelekwa kule hawaendi; na kwa bahati mbaya wengine wakienda wanataka kuishia pale pale mjini. Na ndiyo maana tumetoa maelekezo mwaka huu kwamba walimu wote watakaokwenda ku-*report* wahakikishe wanafika vituoni.

Naomba kutoa rai, mwaka huu tumepeta maombi mengi sana ya walimu ambao ndani ya miaka mitatu, minne walishindwa ku-*report* wakaenda *private schools,* sasa hivi *private schools* hali imekuwa mbaya, wanakuja kuomba tena ajira Serikalini.

Tuombe kutoa maelekezo; kwamba walimu watakaoshindwa kufika katika vituo vyao wasitarajie kuja kuomba mwakani baada ya kuona kwamba wamekosa nafasi katika *private schools*. Hili ni agizo letu na tutaenda kulisimamia kwa nguvu zote.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea, Mheshimiwa Stanslaus Mabula kwa niaba yake Mheshimiwa Kemi.

Na.167

Vifaa Tiba Katika Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA (K.n.y MHE. STANSLAUS S. MABULA) aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana inahudumia zaidi ya wakazi 300,000 wakiwemo wanaotoka Wilaya za jirani lakini haina vifaa tiba kama vile *x-ray, ultrasound* na kadhalika huku ikiwepo ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne mwaka 2013 lakini mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezwa.

Je, ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa na kuipatia hospitali hiyo vifaa tiba vya kutosha ili kuokoa maisha ya watu wengi wanaopoteza maisha kwa sababu ya kukosa huduma hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa mashine ya *x-ray* katika utoaji wa huduma za afya, Halmashauri ya Jiji la Mwanza katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 imetenga shilingi milioni 133.14 kwa ajili ya ununuzi na kufunga mashine ya *x-ray* katika Hospitali ya Nyamagana. Aidha, *ultrasound* ipo katika hospitali hiyo na inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri pia katika mwaka wa fedha 2016/2017 imetenga shilingi milioni 33.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye vituo mbalimbali vya afya vinavyotoa huduma za afya ndani ya Wilaya ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana. Aidha Halmashauri imetenga shilingi milioni 10.5 kwa ajili ya matengenezo ya vifaa vya hospitali.

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa majibu ya Mheshimiwa waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa la vifaa hivyo kwenye Hospitali hii ya Wilaya ya Nyamagana, na ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2013. Sasa je, ni lini vifaa hivi vitaletwa kwenye hospitali ya Wilaya ya Nyamagana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana inahudumia wananchi zaidi ya 300,000 kwa hiyo inaelemewa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza inafika mahala inashindwa kutoa huduma stahiki. Pamoja na

hayo, Halmashauri ya Jiji imejitahidi na kuongeza jengo la wodi ya wanaume na watoto ambayo hazikuwepo. Je, Wizara inampango gani wa kutusaidia ili wodi hizi ziweze kukamilika? Ahsante

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nadhani ni mara ya pili Mheshimiwa Kemi anauliza swali la sekta ya afya katika Mkoa wa Mwanza, kwa hiyo nimpongeze sana kwa kuona kwamba suala la afya ni muhimu sana. Lakini katika suala zima la ni lini *x-ray* italetwa, nimesema hapa kwamba kila kitu ni *budgeting* na bajeti ya mwaka huu tumetenga karibuni milioni 133. Lengo kubwa ni kwamba *x-ray* iweze kununuliwa na iweze kufika. Jukumu letu kubwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ni kuhakikisha kwamba pesa hizo mwaka huu wa fedha zinapatikana ili ahadi aliyoweka Mheshimiwa Rais iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujengwa kwa wodi pale, nipende kusema kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI itashirikiana na ninyi watu wa Mwanza kuhakikisha wodi ile inafanya kazi. Sambamba na hilo nipende kuwashukuru wenzetu wa Vodacom ambapo juzi kupitia vyombo vya habari nimeona wanafanya usaidizi mkubwa sana katika hospitali ya Sekou Toure pale Mwanza. Lengo letu ni kwamba wadau wanaoshiriki kama kama hivi na sisi Serikali tunasaidia kwa kiwango kikubwa kupeleka huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Kemi kwamba Serikali itaungana na watu wa Mwanza, itaungana na Bwana Mabula, Mbunge wa Nyamagana na ninyi Wabunge wa Mwanza wote kuhakikisha suala la afya katika mkoa wa Mwanza, kwa sababu ni Jiji kubwa inaimarika vizuri kutokana na *population* kubwa iliyokuwepo katika eneo hilo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Lyimo Susan! Jiandae Mheshimiwa Ulega.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia suala la uhaba wa bajeti lakini naomba kuuliza; *Benjamin Mkapa Foundation* wamejenga vituo vya afya kule mkoa wa Rukwa ambako kuna matatizo makubwa sana; kwa mfano kuna Zahanati ya Kala - Nkasi, Milepa – Sumbawanga, Ngorotwa – Kalambo pamoja na ile ya Kishapu na wamekabidhi kwa Halmashauri toka Juni 2014, lakini mpaka leo havijatumika wakati kuna

matatizo makubwa sana, ni kwa nini Serikali haijaweza kuvitumia vituo hivyo? *(Makofi)*

MWENYEITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, kwa nini? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Pamoja na majibu mazuri naomba nimsaidie Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu kwamba suala hili ni kwa nini, ni kwa sababu taratibu za makabidhiano bado zinaendelea. Pindi taratibu hizo zitakapokamilika tutakabidhi majengo hayo kwa Halmashauri.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ulega.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo hili la kifaa cha *x- ray* katika Hospitali ya Nyamagana ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI amelijibu na sisi katika Hospitali yetu ya Wilaya ya Mkuranga linatusumbua; je, Serikali inaweza kutuhakikishia kwamba katika mgao huo wa vifaa tiba hivi hospitali ya Wilaya ya Mkuranga itakuwa ni miongoni mwa hospitali zitakazopata kifaa hiki cha *x-ray* ili kuwaondoa wana Mkuranga na adha ya kusafiri umbali mrefu mpaka Dar es Salaam katika Hospitali ya Temeke? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Hospitali ya Mkuranga haina *x-ray*, hali kadhalika na Hospitali ya Mafia na maeneo mengine yote. Lakini katika harakati zilizofanyika sasa hivi wenzetu wa Mafia angalau kupitia Mbunge Mheshimiwa Dau sasa wamepata *x-ray,* nadhani wiki iliyopita walinijulisha kwamba Mafia inapata *x-ray*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Mkuranga vilevile tunajua kweli hakuna. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge tukae pamoja, kwa sababu katika bajeti ya mwaka huu nadhani haikutengwa, lakini tutakaa kwa mikakati ya pamoja tuangalie jinsi gani tutafanya kuwashirikisha wadau mbalimbali ambao katika njia moja au nyingine wanaweza kutusaidia kupata *x-ray* kwa sababu kifaa hiki ni muhimu sana ukiangalia au ukizingatia suala zima la ajali za pikipiki zinazotokea maeneo mbalimbali ambapo lazima mtu apimwe aangaliwe jinsi gani amepata majeruhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nilipenda kuongezea yale majibu, kwamba vile vifaa havijafunguliwa katika hospitali nyingine. Kweli mimi nimepita maeneo mbalimbali, nilipita mpaka Bukene kwa rafiki yangu Mheshimiwa Zedi

kuona *center* ambazo hazijafunguliwa; na tumetoa maagizo, ndiyo maana hata juzi hapa nimezungumza kwa ukali sana juu ya suala zima la Hospitali ya Singida. Lakini nimesikia, na leo nimekutana na Mbunge wa Singida amesema lile jambo limeshashughulikiwa sasa, hata vile vitanda havihami kutoka katika Hospitali ya Rufaa ya Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika ziara zangu ambazo natarajia kuzifanya, lengo langu ni kufika katika Nyanda za Juu Kusini kuhakikisha kwamba kwa sababu tunapeleka madaktari wapya maeneo mbalimbali hizi zahanati ambazo hazijafunguliwa; ambapo tunawashukuru sana wenzetu wa *Mkapa Foundation*, wamefanya kazi kubwa sana; *center* hizi zinafunguliwa ili wananchi wapate huduma katika maeneo yao ya karibu zaidi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa majibu ya nyongeza kwenye maswali yote yanayohusu vifaa tiba kama *x-ray* hapa nchini kwamba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendesha mradi mkubwa wa vifaa tiba unaoitwa *ORIO*. Mradi huu utahusisha ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kufanyia uchunguzi wa magonjwa kama *MRI, CT Scan, x-ray, ultrasound* na vifaa vingine na kuvitawanya nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Hospitali ya Mkuranga kwa mujibu wa kumbukumbu zangu ni mojawapo ya vituo ambavyo vitapatiwa mashine ya *x-ray*. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa, Mheshimwa Albert Ntabaliba Obama.

Na. 168

Barabara ya Mnanila – Kasulu

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara ya Mnanila – Kasulu yenye urefu wa kilometa 42 kwa lami.

(a) Je, lini barabara hiyo itaanza kujengwa?

(b) Zile kilometa nne ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba zingeanza kujengwa kwa kiwango cha lami katika Makao Makuu ya Wilaya ya Buhigwe utaanza lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Ntabaliba Obama, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mnanila – Kasulu yenye urefu wa kilometa 48 ni barabara ya mkoa chini ya Wakala wa Barabara Nchini *(TANROADS)* na inaunganisha Wilaya tatu za Kasulu, Buhigwe, Kigoma na nchi jirani ya Burundi. Barabara hii ni sehemu ya barabara ya Kibondo – Kasulu – Manyovu yenye urefu wa kilometa 250 ambayo kazi ya usanifu wa kina inaendelea ikiwa ni hatua muhimu katika ujenzi kwa kiwango cha lami. Utekelezaji utafanyika kupitia wahisani wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* chini ya Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya kukamilika kwa usanifu, taratibu za ujenzi kwa kiwango cha lami zitafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa kipande cha barabara kilometa mbili katika makao makuu ya Wilaya ya Buhigwe, Halmashauri imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu ambao utasaidia kujua gharama za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Kukamilika kwa hatua hiyo, kutawezesha Serikali kuweka katika mpango na kutenga bajeti ili kuanza ujenzi.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Obama.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwanza nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Buhigwe, kupongeza Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. Kwanza pongezi zimuendee Mheshimiwa Rais mwenyewe, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kuikazania barabara hii alipokuwa Waziri wa ujenzi. Lakini niendelee kupongeza Wizara ya TAMISEMI, nayo imechukua juhudi hiyo ili iweze kujengwa. Lakini naomba nimpongeze tena Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuiweka kwenye mpango barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali moja dogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye Jimbo letu na Wilaya yetu ya Buhigwe makao makuu ya Wilaya yamebadilika kutoka Kasulu kwenda Buhigwe lakini tunazo barabara nyingine ndani ya Halmashauri yetu ambazo inabidi zichongwe kwa ajili ya

kufika makao makuu na kupunguza urefu wa kuzunguka. Tunazo barabara kama nane ambazo zinahitaji kama shilingi milioni 950. Naomba ushauri wako.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, anataka ushauri tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tukiweka rekodi sawa, Mheshimwa Obama toka kipindi chote cha miaka mitano ambapo alikuwa kama *partner* wangu wa karibu zaidi alikuwa akizungumzia maeneo haya ya barabara zake na amefanikiwa kuhakikisha kwamba wamehamisha makao makuu. Lakini nikijua wazi kwamba Sera ya Barabara tunaanza kipaombele katika zile barabara za kwanza zilizokuwa bora zaidi. Maana sera ya barabara ndiyo ilivyo hivyo; zile barabara ambazo hazijafunguliwa zinapewa kipaumbele cha mwisho zaidi.

Mheshimiwa Mweyekiti, sasa kwa sababu barabara hii kwa jinsi Mheshimiwa Mbunge alivyouliza ni barabara mpya, lengo ni ku-*connect* vizuri, kurahisisha ule umbali uwe mfupi zaidi. Nimsihi Mheshimiwa Mbunge, hili ni jambo jema, wananchi lazima wapate huduma, lakini nipende kuwahamasisha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo mumuunge mkono Mbunge huyu sasa katika vile vipaumbele vya kufungua barabara hizo mpya; kwa sababu hii ni barabara ya ndani ya Halmashauri, jambo hili katika Kamati ya Uchumi hali kadhalika katika Kamati ya Fedha na Baraza la Madiwani muangalie jinsi gani sasa mtatumia *own source* japo angalau kuanza kulifungua. Ofisi ya Rais TAMISEMI katika suala zima la kufungua barabara zake za vikwazo tutaangalia jinsi gani kwa njia moja au nyingine zile Halmashauri za pembezoni zote ambazo zina changamoto kubwa za miundombinu ya barabara tutaziangalia kwa jicho la karibu ili wananchi waweze kupata huduma za kijamii katika maeneo yao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa sera zinaelekeza kwamba barabara zinazounganisha mikoa zitajengwa kwa kiwango cha lami na kuna barabara inayotoka Mbulu kuja Karatu kwa maana inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara, ni barabara ya siku nyingi; ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera zetu nimezieleza wazi, sera hizo zinatafsiriwa vizuri katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Na Ilani ya Chama cha Mapinduzi

imesema itawafikia wananchi wote hasa kuunganisha hii mikoa. Kama eneo hili linaunganisha Mkoa kwa Mkoa, Waziri wa Miundombinu akifika katika hotuba yake hapa nadhani atatuelezea mchanganuo wa mambo mengi zaidi. Kikubwa zaidi ni kwamba katika utekelezaji wa Ilani, maeneo yote yaliyoainishwa kwamba yatafikiwa, kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, jambo hilo litafanyika.

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Nsanzugwako. Waziri wa Ujenzi.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti,…

MWENYEKITI: Akijibu huyu biashara imekwisha.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kesho tuna bajeti yetu, na barabara zote ambazo zitajengwa kwa kiwango cha lami tutaeleza kwa kina kesho. Naomba Waheshimiwa Wabunge muwe wavumilivu mpaka kesho mtasikia mambo yote. Ahsanteni.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri, tunaendelea. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii na Jinsia, Mheshimiwa Mbena…

MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, umeshaniruhusu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ameshasema mambo yote kesho. Mheshimiwa Mbena. Kwa niaba? *Okay,* uko mwenyewe.

Na. 169

Hatua za Kisheria kwa Wanaowatelekeza Watoto

MHE. PROSPER J. MBENA aliuliza:-

Watoto wengi nchini wameendelea kudhalilishwa kwa kukosa malezi bora ya wazazi wao hali inayosababisha waishi maisha ya kuombaomba na kwa kuwa baadhi ya wazazi wanaosababisha hali hiyo ni wanaume wanaoharibu maisha ya wasichana kwa kuwapa mimba na kukwepa jukumu la kulea watoto wanapozaliwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwabaini wanaume hawa na kuwafikisha mahakamani kwa kosa la kuwatelekeza watoto na kuwasababishia mateso na kuwanyima haki zao za msingi?

(b) Je, ni lini Serikali italeta Bungeni muswada wa kufanya marekebisho katika sheria husika ili kuwashughulikia wazazi wanaowatelekeza watoto wao kwa kutowahudumia ipasavyo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mipango mbalimbali ya kuwababini wanaume wanaotelekeza familia na vitendo vingine vya unyanyasaji. Mipango hiyo ni pamoja na Mpango wa Muitikio wa Kitaifa wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto wa mwaka 2013 hadi 2016 na Mpango wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake wa mwaka 2005 – 2015. Mipango hiyo hivi sasa inaunganishwa kuwa mpango mmoja wa Kitaifa ili uweze kukidhi haja za upatikanaji wa taarifa zinazohusu ukatili dhidi ya watoto na wanawake ikiwemo utelekezaji wa familia. Kupitia mpango huu, Serikali itahamasisha jamii kuibua vitendo vya ukatili ikiwa ni pamoja na kuwabaini wahusika na vitendo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara yangu imeanzisha mtandao maalum wa mawasiliano kwa ajili ya kutoa taarifa mbalimbali za ukatili dhidi ya watoto *(the child helpline number 116)* ambapo mtoto mwenyewe au mtu mwingine kwa niaba ya mtoto huweza kuripoti tukio lolote la ukatili dhidi ya watoto. Vilevile, Wizara inatekeleza Mpango wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto wa mwaka 2013 – 2017 na kupitia mipango hii jamii zimekuwa zikielimishwa masuala mbalimbali yanayohusu ukatili, unyanyasaji na mazingira hatarishi kwa watoto na wanawake ili waweze kutoa taarifa ya matukio hayo yanapotokea na kuwabaini wahusika ili kuchukuliwa hatua stahiki.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 imezingatia suala zima la utoaji wa malezi, matunzo na ulinzi kwa kutoa majukumu kwa wazazi, walezi, jamii pamoja na Serikali. Aidha, kifungu cha 14 cha sheria hiyo kimeweka adhabu kwa wazazi au walezi watakaokiuka kutoa malezi bora kwa kulipa faini ya shilingi milioni tano za kitanzania au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijapokea changamoto yoyote inayohitaji marekebisho kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki cha sheria.

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tatizo hili ni kubwa sana nchini kwetu na kwa kuwa wahusika Wizarani wanaonekana kutolitambua vizuri ukubwa wake pamoja na kwamba watoto wa mitaani wanaonekana kila siku; je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuanzisha *register* pale Wizarani kwake ambako itapokea majina ya wanaume pamoja na wanawake wachache ambao wanatelekeza watoto wao ili aweze kuwa na kumbukumbu nzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri atakubali kupokea ushauri binafsi kutoka kwa wadau wanaokerwa na tatizo hili ili ushauri huo aweze kuutumia katika kuleta mapendekezo ya kurekebisha Sheria Namba 21 ya Watoto? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu, kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti naanza na la (b), Serikali iko tayari sana kupokea ushauri kutoka kwa mtu yeyote Yule.

Lakini (a) kwamba Serikali kuanzisha *registers* pale Wizarani namba nijibu kwamba Serikali kupitia Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 ambayo ilitungwa na Bunge lako Tukufu, kwenye kile kifungu cha 94 inatoa mamlaka kwa Halmashauri yaani Serikali za Mitaa kuwabaini watoto wote wa mitaani na kuwahudumia.

Kwa maana hiyo Waheshimiwa Wabunge tusikwepe jukumu hili kusimamia utekelezaji wa sheria hii kwenye Halmashauri zetu. Lakini kusema jambo hili litashughulikiwa *centrally* pale Wizarani wakati watoto wako kwenye Serikali za Mitaa ni kujaribu kuweka urasimu ambao hauhitajiki.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote na Halmashauri zetu tukiwa kama viongozi wajumbe kwenye Halmashauri hizi, tuweke mikakati mahsusi ya kuwahudumia watoto hawa kule kule kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Komu ajiandae, Mheshimiwa Shangazi.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Nimesikia majibu ya Serikali kwa upande wa jinsi Serikali zitakavyoshughulika na hawa watu ambao wanaleta matatizo, lakini kuna matatizo ambayo yanasababishwa na Serikali. Kwa mfano kule Moshi Vijijini katika Kata ya *TPC*

watoto wa kike wanatembea kilometa kumi, saba kutoka eneo linaitwa Chemchem kwenda kutafuta shule iliko, na haya ni mashamba ya miwa ambapo kuna mambo membo mengi sana yanaweza kutokea hapo katikati, kuomba *lift* na vitu kama hivyo. Sasa Serikali inaweza kutuambia nini kuhusiana na hali kama hiyo; labda kujenga mabweni kwenye shule za aina hiyo ambazo ziko mbali kiasi hicho?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya mwanza nilizungumzia suala ambalo Mheshimiwa Komu amelisema na hili linanipa faraja kubwa sana, kuona kila Mbunge hapa anasimama katika ajenda ya kumuokoa mtoto wa kike, hili naomba nishukuru sana. Na katika hili naomba niwaambie Wabunge tutaendelea kwa kadiri iwezekanavyo kuhakikisha kwamba tunasimika mabweni maeneo ya jirani, lakini sio mabweni peke yake, tutahakikisha kwamba jinsi gani tunafanya nguvu ya pamoja kwa ajili ya kuleta *solidarity* hata kwa wazazi; kwa sababu kuna maeneo mengine mabweni yamejengwa lakini watoto wanapenda kukaa uswahilini au kutembea mbali zaidi kwa sababu kuna mambo yao yale ya ku-*discuss* zaidi wanayoyapenda.

Kwa hiyo, sisi tutahakikisha kwamba tunasimamia na kuhamasisha wazazi wote; lakini kama Ofisi ya TAMISEMI inaliona hilo kwa sababu Wizara ya Afya imejielekeza vya kutosha katika kumuokoa mtoto wa kike na Wabunge wote, mimi naamini jambo hili tutafanikiwa kwa karibu zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Shangazi!

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Napenda kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri. Kumekuwa na ongezeko kubwa la akina mama wanaojifungua kwa operesheni, na suala hili lilikuwa linahusishwa pia na maadili ya madaktari wetu. Je, Serikali ina tamko gani kwamba suala hili ni suala la kitaalam au ni mmomonyoko wa maadili miongoni mwa madaktari? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kujifungua kwa *operation* ni jambo ambalo haliwezi kuwa la kukiuka maadili, bali ni jambo la kitaalamu. Kuna sababu na vigezo mahususi ambavyo hupelekea daktari akafanya uamuzi wa kumpeleka mama mjamzito kwenda kujifungua kwa njia ya *operation (caesarean section)* na kitu chema sana kufanya uamuzi huo kwa sababu huokoa maisha ya mama

na mtoto kuliko kusubiria kujifungua kwa njia ya kawaida ambapo mama mjamzito anaweza akaingia kwenye hali hatarishi.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

Na.170

Mradi wa Madini na Umeme wa Joto ardhi

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Katika Halmashauri ya Mbeya kuna mradi wa uchimbaji wa madini unaotarajiwa kuanza kwenye eneo la Mlima Songwe, lakini pia kuna mradi mwingine mkubwa wa joto ardhi kwenye Kata za Swaya, Ijombe na Bonde la Songwe.

(a) Je, kwa nini Serikali Kuu haihusishi Halmashauri ya Mbeya katika mradi hiyo ili elimu iweze kutolewa kwa wananchi?

(b) Je, wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini watanufaika vipi na miradi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu Namba 95(1)(b) cha Sheria Sheria ya Madini Namba14 ya 2010, kabla ya kuanza utafutaji na uchimbaji wa madini, mmiliki wa leseni husika hutakiwa kupata kibali cha kumruhusu kuingia na kushughulika na utafutaji na uchimbaji wa madini kutoka kwenye Halmashauri za zilaya pamoja na mkoa. Kampuni za *Cradle Resources Ltd/RECB Co. Ltd.* ilipewa leseni tatu za uchimbaji wakati wa madini ya *niobium*. Leseni hizo ni ML 237, 238 na 239 zilitolewa mwaka 2006 zenye jumla ya ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 22.06. Kwa sasa kampuni hiyo inakamilisha maandalizi kabla ya kuanza kwa ujenzi wa mgodi huo ifikapo mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa utafiti wa madini hayo ya *niobium* kampuni ya *Cradle Resources Ltd/RECB Co. Ltd.* inayomiliki leseni ilijitambulisha kwa uongozi wa mkoa wa Mbeya ikiwa ni pamoja na Gereza la Songwe ambapo mradi huo upo. Aidha, kampuni hiyo hivi sasa iko kwenye mazungumzo ya Gereza la Songwe pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani

kuona namna ya kulihamisha Gereza hilo kabla ya kuanza uchimbaji kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *niobium* utakuwa na faida kubwa kwa uchumi wa viwanda ikizingatiwa kwamba Serikali inajikita katika kufufua na kukuza viwanda nchini. Miongoni mwa matumizi ya madini haya ni kutumika kama *alloy* kwenye chuma kwa kuboresha uimara wake. Vilevile madini hayo hutumika katika kutengeneza mabomba mathalani mabomba ya kusafirisha gesi asilia. Matumizi mengine ya madini haya ni matengenezo ya sumaku pamoja na utengenezaji wa injini za ndege na *rocket*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *Tanzania Geothermal Development Company Limited (TGDC)* ni kampuni tanzu ya Shirika la Umeme nchini *(TANESCO)* ambayo imepewa dhamana ya kusimammia miradi ya kufua umeme wa joto ardhi katika Ziwa Ngozi lililopo kati ya Mbeya Vijijini. Mradi huu pia utazalisha umeme wa megawati 20 kwa kuanzia na baadaye utaweza kuzalisha megawati 100. Shughuli za utafiti wa mradi huu zilianza mwaka 2015 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2018 kwa kuzalisha umeme wa megawati 20. Mwezi Agosti 2015, kampuni ya *TGDC* iliendesha mafunzo kwa viongozi wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, watendaji wa Kata na vijiji wa Mbeya yaliyolenga kuwajengea uelewa wananchi hao. Aidha, mafunzo kama hayo yalitolewa kwa njia ya mihadara kwa wananchi wa Vijiji vya Ijombe, Mwakibete, Nanyara na Swaya vinavyozunguka maeneo yanayofanyiwa utafiti wa joto ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na joto ardhi kutumika kuzalisha umeme manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi wanaozunguka eneo la mradi ni pamoja na kutumia maji ya moto majumbani lakini pia katika vitalu vya kilimo. Kadhalika itatumika katika kufugia samaki, kukausha mazao, kujenga mabwawa ya kuogelea na kwa matumizi mengine ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla miradi ya uwekezaji hunufaisha wananchi wa eneo husika katika ukuaji wa shughuli za kiuchumi na ajira. Miradi hii miwili itakapotekelezwa wananchi wa Halmashauri ya Mbeya Vijijini, Rungwe, Mbeya pamoja na Watanzania wote watanufaika kwa kupata ajira, ushuru pamoja na tozo mbalimbali pamoja na huduma za jamii.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Mwenyekiti, na pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi wa haya madini adimu duniani pamoja na joto ardhi ni muhimu sana kwa uchumi wa viwanda, naomba *commitment* ya Serikali, moja, je, ni lini wataanza uchimbaji wa joto ardhi ili tuweze kutumia kwenye viwanda vyetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pili, naomba pia *commitment* ya Serikali pamoja na mradi wa Ziwa Ngozi, je, Serikali imetoa leseni ngapi za uchimbaji na uzalishaji wa madini na nishati ya joto ardhi katika sehemu zingine hapa kwetu Tanzania? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya ni lini tunaanza, utafiti umeshafanyika, unaonesha kwamba ili upate umeme wa joto ardhi unahitaji kuwa na *temperature* ambayo iko katikati ya nyuzi 180 mpaka 240 *celsius*. Sasa bahati nzuri hii ya Ngozi iko zaidi ya 240. Kwa hiyo, kinachofuata sasa kwa miezi michache ni kwamba inabidi tuchoronge miamba pale chini tuweze kujua kuna mvuke kiasi gani ambao utaendesha mashine ya kuzalisha umeme wa kiasi gani. Kwa hiyo, tutatoa hiyo tarehe baada ya kujua tuna mvuke wa chini kiasi gani yaani *steam*.

Mheshimiwa MWenyekiti, na leseni ngapi zimetolewa, ni kwamba tumeshatengeneza ramani ya nchi nzima ambayo inaonesha maeneo yote ambayo tunaweza kuendeleza joto ardhi. Kwa sasa hivi ukiacha ya Ngozi, Mbeya eneo lingine ni la Luhoi kilometa kama 70 Kusini Mashariki mwa Dar es Salaam, halafu na lingine liko sehemu za Kusini mwa Morogoro na Ziwa Natroni kwa hiyo maeneo ni mengi lakini tunaenda hatua kwa hatua.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Shabani Shekilindi.

MHE. SHABANI O. SHELIKINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la umeme wa *REA* ni suala la Kitaifa, je, ni lini Serikali itawapatia umeme wananchi wa Makanya, Ngwelo, Kwemashai, Gare na maeneo yote yaliyoba katika Jimbo la Lushoto?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Makanya pamoja na Ngwelo ambayo yalizungumzwa na Mheshimiwa Mbunge ambayo kwa sasa hayajapata umeme, taratibu zinazofanyika sasa ni kukamilisha upatikanaji wa umeme kwenye maeneo ya *REA* Awamu ya Pili na maeneo aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge, maeneo matatu kwa sasa yameshawekwa kwenye orodha ya maeneo ambayo yatapatiwa umeme kwenye *REA* Awamu ya Tatu inayoanza mwezi Julai mwaka huu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, *sorry*! Mheshimiwa Tizeba.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pia kwa kuniona.

Suala la umeme katika vijiji vingi hapa nchini bado halijawekwa wazi kuhusiana na maeneo ya visiwa. Jimbo langu tu kwa mfano linavyo visiwa 25. Nisizungumzie Jimbo la Mheshimiwa Mwijage huko Gozba, Bumbire na maeneo mengine.

Sasa mimi ningependa tu Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini labda atuambie ni kwa namna gani Wizara au Serikali kwa ujumla imejipanga kufikisha umeme katika maeneo haya ambayo kimsingi si rahisi sana kufikisha umeme wa Gridi ya Taifa?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba visiwa vyetu vinahitaji kupata umeme na cha kwanza vilivyopata umeme ni visiwa vya Zanzibar ambapo tumejenga *cable* chini ya bahari. Wao wana megawati 100 lakini mahitaji ya Zanzibar ni megawati 50, kwa hiyo wanayo 50 zaidi. Na Mheshimiwa Tizeba yeye mwenyewe anafahamu kisiwa cha kwanza kabisa katika Ziwa Victoria kupata umeme ni kisiwa chake ambacho kwa mara ya kwanza tumepitisha *cable* chini ya Ziwa Victoria, na tumemuomba Waziri Mkuu akazindue huo umeme kwa sababu ni wa kipekee kabisa. Na hivi sasa Kisiwa cha Ukara vilevile wamepatiwa umeme na ni mtu binafsi aliyewekeza umeme pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wote ni kwamba hivi visiwa vingi vidogo vidogo hatutaweza kujenga *cable* kwa kila kisiwa, ila umeme watakaoupata ni umeme wa jua.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Nassoro.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kuhusu mpango wa umeme vijijini. Mimi nina kata 15 lakini nina kata tatu ambazo zimepata umeme na ni vijiji vitatu vimepata umeme, je, Kata zifuatazo zitapata umeme katika mpango huu? Kata ya Bukwimba, Nyugwa, Busolwa, Shabaka, Nyijundu, Nyabulanda, Kafita, Kakola, Mwingilo, Kaboha, Nyabulanda na Izunya, je, serikali katika mpango wake wa mwaka huu tutapata umeme katika Jimbo la Nyang'hwale Kata zote hizo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika Jimbo la Nyang'hwale ni kata tatu tu ambazo zimepata umeme kwa mpango wa *REA* Awamu ya Pili, lakini *REA* Awamu ya Tatu pamoja na tathmini inayofanyika sasa katika REA Awamu ya Pili, vijiji vyote na kata zote

zilizobaki za Nyang'hwale pamoja na vijiji alivyovitamka vimeingizwa kwenye mpango wa *REA* unaoendelea utakaonza mwezi Julai mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kadhalika kama nilivyosema bado *TANESCO* wanaendelea na kazi za kuunganisha umeme katika maeneo yote na maeneo ya Nyang'hwale ambayo hayatapitiwa yataingizwa kwenye mpango wa *TANESCO* ili vijiji vyote na kata zote za Nyang'hwale zipate umeme mwaka 2017/2018.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.Ningependa kupata jibu, kwakuwa masuala ya madini hasa yale ambayo si ya kawaida yapo hata katika Mkoa wa Songwe; tuna migodi ya marumaru hususan Mbozi, Ileje, Chunya, yote haya bado hayajaendelezwa kwa kiasi ambacho yangeweza kuleta tija, je, Wizara ya Nishati na Madini itafanya lini utafiti wa kuja kutuletea na sisi uchimbaji wa migodi hii kwa sababu ina faida sana. Badala ya kuagiza *tiles* nje tungeweza kutumia za kwetu na ubora wake ni mzuri kuliko ule wa nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile, je, mgodi wa Kiwira ambao uko Ileje na haujawahi kuifaidia Ileje utazinduliwa lini? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika Mkoa wa Mbeya pamoja na maeneo ya Songwe na Ileje kuna madini ya aina nyingi sana mbali na dhahabu. Na madini mengi yaliyoko katika maeneo yale ni madini ya viwandani. Kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi, madini ya *niobium* yanapatikana kwenye Mkoa wa Mbeya na hasa kwenye maeneo ya Songwe karibu na Gereza la Songwe. Madini haya ya *niobium* ni adimu sana, na ni madini ya kwanza kupatikana kwa Tanzania na Afrika Mashariki. Kama nilivyosema madini haya yatatumika sana kwa shughuli za viwandani na hasa baadaye kwa kutengeneza *computer*, *engine* za ndege pamoja na *rocket,*, kwa hiyo ni madini ambayo yanapatikana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti niongeze tu, kwamba sasa madini mengine yaliyoko pale utafiti unafanyika. Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* linaendelea na kufanya utafiti ili kubaini madini mengine ambayo yanapatikana kwenye maeneo ya Songwe, Mbeya Vijijini pamoja na Ileje ili na yenyewe yaweze kuchimbwa kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye mgodi wa Kiwira. Kama mnavyojua Mgodi wa Kiwira unatarajiwa kabisa kwa kuanza kuzalisha umeme, lakini kwa shughuli za uchimbaji wa Mgodi wa Kiwira sasa hivi kinachofanyika ni kukamilisha *detail design* na taratibu za kumpata mkandarasi. Na kwa

utaratibu ambao kwenye bajeti yetu tutakayoisoma Alhamisi wiki hii tutawaeleza, taratibu za kuanza ujenzi huu zitaanza mwaka 2018 na mgodi huu utachukua takribani miaka 20 na kuendelea.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Selemani Kakoso.

Na. 171

Hitaji la Umeme – Mpanda Vijijini

MHE. MOSHI S. KAKOSO aliuliza:-

Vijiji vingi katika Jimbo la Mpanda Vijijini havina huduma ya umeme.

Je, ni lini Serikali itapelekea huduma ya umeme katika vijiji hivyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya REA awamu ya kwanza nay a pili haikuhusisha Jimbo la Mpanda Vijijini. Katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Mpanda wanapata umeme wa uhakika Serikali inatarajia sasa kuvipatia umeme vijiji 49 vya Mpanda Vijijini pamoja na Ofisi za Wilaya kupitia Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu unaotarajiwa kuanza mwezi Juni, mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme katika Jimbo la Mpanda Vijijini itahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *kilovolt* 0.4 yenye urefu wa kilometa 280. Lakini pia ufungaji wa transfoma 64 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 2,452. Gharama ya kazi hii ni shilingi bilioni 9.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi kupitia Mradi wa *ORIO* itafunga mitambo mipya ya kuzalisha umeme wa *megawatts* 2.5 katika Mji wa Mpanda itakayowezesha maeneo mengi kupata umeme wa uhakika. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2016 na kukamilika mwezi Julai, 2017.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, mradi wa *ORIO* ulikuwepo toka mradi wa umeme vijijini *Phase II* ambao ulihusisha vijiji vitano, vya Kabungu, Ifukutwa, Igalula na Majalila. Mradi huu ulikwama kwa sababu

ya ukosefu wa fedha, Serikali ilishindwa kuwekeza fedha ambazo zinge-*support* kampuni ya *ORIO*. Je, Serikali ina majibu yapi sahihi ambayo yatawezesha miradi hii iweze kukamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nilikuwa nataka kufahamu uwiano wa miradi hii ya umeme vijijini. Yapo maeneo mengine ambayo sasa hivi yana asilimia mpaka 80, yamepata miradi hii, maeneo mangine bado hayajakuwa na fedha zinazopelekwa kwenye maeneo husika kama Jimbo la Mpanda Vijijini. Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya mgawanyo wa fedha zinazofadhili Mradi wa Umeme Vijijini?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba mradi wa *ORIO* ni wa Uholanzi. Ni kweli kwamba sisi tulikuwa hatujalipa fedha, lakini sasa fedha zimelipwa na hiyo mitambo imetengenezewa Ubeligiji na itafungwa. Ndio maana *engine* nyingine ambazo zilikuwa Ngara na kwingine tutahamisha, kwa sababu *engine* zinakuja zimeshatoka na wanazifunga kule; kwa hiyo mradi huo utatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la nyongeza juu ya uwiano, ni kweli napenda kukiri, kwanza Awamu ya Kwanza ya Umeme Vijijini, ilikuwa ni ya majaribio, ilifanyika ndani ya mkoa mmoja tu, Awamu ya Pili, tumejaribu kwenda nchi nzima. Lakini ukweli ni kwamba uwiano sio mzuri, na ndiyo maana Awamu ya Tatu tumekubaliana kwamba itabidi tufanye tathimini mkoa kwa mkoa, tuone mikoa ambayo imefaidika kwa kupata umeme Awamu ya Kwanza na ya Pili, safari hii watapata vijiji vichache kusudi vijiji ambavyo havijapata umeme vipewe kipaumbele.

Ninapenda kukiri kwamba mikoa ambayo kusema ukweli hawajapewa umeme sana ni mikoa ya Kusini Magharibi mwa Tanzania na *REA* Awamu ya Tatu inaweka mkazo hapo.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka mwezi Machi, *REA* walikuwa wamepata karibia asilimia 40 tu ya fedha za kwenda kumalizia katika *REA* ya Awamu ya Pili. Nilitaka kujua, mpaka sasa hivi Wizara yako imepokea kiasi gani ili vijiji vyangu ambavyo vilikuwa viporo kabla ya hii *REA* ya Awamu ya Tatu, kama Kunzugu, Mihale, Nyamatoke, Bukole, Kamkenga, Kangetutya, Rwagu na maeneo mengine yapate umeme katika ule ule mpango wa *REA* ya Pili na huu wa *REA* ya Tatu?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba tulikuwa asilimia 40, lakini kwa sasa hivi tuko zaidi ya asilimia 75, kwa hiyo jinsi ambavyo tunakusanya fedha na ndivyo jinsi ambavyo Hazina inatupatia fedha. Kwa hiyo, kwa mipangilio inavyokwenda na wakandarasi tumewaambia huu mwezi Mei tutafanya tena tathmini kwa kila mkandarasi amefanya kazi kiasi gani, nadhani hadi kufikia mwezi Mei tutakuwa tumefika karibu asilimia 80. Mheshimiwa Mbunge nataka kukuhakikishia na ndiyo maana tumekubaliana na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kama miradi yako ya *REA* Awamu ya Pili haikukamilika ni lazima itapewa kipaumbele kwenye *REA* Awamu ya Tatu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kigola.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Katika Mpango wa *REA* kwamba itapeleka umeme vijijini, kuna vijiji vya Jimbo la Mufindi Kusini vyapata karibu 30 havijapata umeme, kuna nguzo zilipelekwa kule na baadaye zile nguzo zikaenda kuhamishwa na wananchi wana wasiwasi. Mheshimiwa Waziri naomba uwathibitishie wananchi kwamba kwenye mpango huu wa tatu wanaweza kupata huo umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika maeneo ya Mufindi kuna nguzo zilipelekwa na mashimo yakachimbwa, lakini kutokana na *scope* ya kazi ile ilionekana kwamba mashimo yalikuwa yamechimbwa maeneo ambayo siyo yenyewe. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu, tumeshakaa na Mheshimiwa Mbunge, tumetathmini vijiji vyake vyote vya Mufindi Kusini na vyote alivyoviorodhesha vitaingia kwenye *REA III* na vitapatiwa umeme kwenye *REA III* inayoanza mwezi Julai mwaka huu. *(Makofi)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa pesa ambazo *MCC* walikuwa waipatie Tanzania zingeshiriki kutatua tatizo kubwa na kero kubwa ya umeme na sasa wamesitisha kutoa pesa hizo. Je, Serikali inaweza kutuambia ni athari gani zinaweza kupatikana kwa wananchi kwa kukosa msaada huo wa *MCC? (Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wasikilize kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna hata dola moja, hata senti moja ya *MCC* ilikuwa iko kwenye Miradi ya Umeme Vijijini. Hiyo hawezi kunibishia Mheshimiwa Msigwa kwa sababu mimi mwenyewe ndiyo nimeenda kukaa na

watu wa *MCC*, nimekaa na Waziri wa Nishati na wa Fedha wa Marekani, hizo fedha zilikuwa haziji Bungeni hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *MCC* halafu fedha zote za *MCC* hazikuwa za umeme vijijini. Hilo nalo ni kosa lingine ambalo lazima watu waelewe, kuna fedha za barabara halafu kuna fedha za maji na vitu vingi sana, katika zile fedha za *MCC* zilizokuwa za umeme hazivuki theluthi moja. Waheshimiwa Wabunge na Watanzania ni kwamba mimi tunaongea kwa takwimu, siyo ubishi, ni takwimu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wote naomba hili jambo tulielewe hivi, mimi hapa ninataka kulima heka nane za mahindi, ndugu yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango anasema Mheshimiwa Muhongo kwa nini ulime heka nane? Mimi naomba nikuongezee heka mbili, ili zitimie ziwe kumi na mimi nasema ahsante ndugu yangu nipatie. Kwa hiyo, asiponipatia hizo heka mbili mimi bado za kwangu nane nitalima. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea muda wetu umekwenda. Wizara hiyo Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa.

Na. 172

Kuwawezesha Wananchi Kupata Umeme wa Bei Nafuu

MHE. GODFREY W. MGIMWA aliuliza:-

Licha ya Serikali kupeleka umeme vijijini kwa kasi kupitia mradi wa *REA*, bado kuna changamoto za kuunganisha umeme kwa wananchi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuwawezesha wananchi kupata umeme kwa bei nafuu?

(b) Nguzo za umeme zinasimikwa kwenye njia kuu tu; je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha nguzo hizi zinapelekwa kwenye vitongoji?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha wananchi kupata umeme kwa gharama nafuu, Serikali kupitia mradi kabambe wa kusambaza umeme vijijini

(REA) inaunganisha umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 tu na hii ikiwa ni Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Umeme Nchini *(TANESCO)* imepunguza gharama za umeme kwa kuondoa gharama za malipo ya maombi ya kufungiwa umeme yaani shilingi 5,000 pamoja na malipo ya huduma ya kila mwezi *(service charge)* ambayo ni shilingi 5,520 kwa wateja wote wa majumbani; hatua hii imeanza tangu tarehe 1 Aprili, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuwekeza zaidi katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo vya gesi asilia, joto-ardhi, jua, maji na makaa ya mawe pamoja na tungamotaka, ili kupunguza gharama za umeme zaidi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, nguzo nyingi zimesimikwa kwenye njia kuu, hata hivyo katika Mpango wa *REA* Awamu ya Tatu utakaoanza bada ya bajeti yetu kupita mwezi Julai mwaka huu, maeneo mengi ya vitongoji yatafikiwa kwa kupewa huduma ya umeme, ili kurahisisha shughuli za uchumi za wananchi wa maeneo ya Kalenga.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la umeme hasa kwenye uunganishaji limekuwa ni tatizo kubwa hasa kwenye maeneo ya mita. Wananchi wengi na wateja wengi wamekuwa wakilalamika kwamba mita ambazo wanafungiwa zinaharibika baada ya muda mfupi. Ningependa kujua kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba je, analifahamu hili na kama analifahamu, hatua gani zitachukuliwa, ili kuhakikisha kwamba, utaratibu huu mbovu unasitishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Jimbo la Kalenga limekuwa lina changamoto kubwa katika masuala haya ya umeme na nina vijiji kadhaa ambavyo mpaka dakika hii viko gizani na vinahitaji umeme. Kijiji cha Lupalama katika Kata ya Nzii, Kijiji cha Kipera, Kijiji cha Itagutwa, Kijiji cha Magunga na Lyamgungwe; ningependa kusikia *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, je, ana utaratibu gani na mpango gani kuhakikisha kwamba, vijiji hivi vinapata umeme? Na kama je, yuko tayari kuungana na mimi kwenda moja kwa moja Kalenga ili kuweza kuwapa hamasa wananchi wangu? Nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, wakati *REA* wanapofunga umeme ni mara nyingi sana imekuwa ikitokea kwamba zile mita inaonekana

kama hazina nguvu, tatizo siyo kwamba mita ni mbovu, tatizo tu ni kwamba umeme unaokuja ni wa *low voltage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni vizuri tukawaeleza baada ya *REA* kuunganisha umeme sasa, umeme tunaotumia ni wa *low voltage* ambao ni *kilovolt* 30 na mwingine 11 zaidi ni 132. Kuanzia Julai mwaka huu kuna mradi sasa wa kuongeza nguvu za umeme ambao ni *kilovolt* 400 utapita kwenye maeneo ambayo tuliyataja. *Kilovolt* 400 zitakapoingia na kuanza matatizo ya kukatika kwa umeme kwenye tatizo la mita yatakoma mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na vijiji alivyotaja Mheshimiwa Mgimwa, vijiji vitano vya Lupalama, Lupelo, Magunga na vingine ni kweli kabisa havijapata umeme na tulishavitembelea, kwa sasa tumezungumza na Mheshimiwa Mgimwa, kati ya vijiji vitakavyoanza kupatiwa umeme kwenye Jimbo lake tutaanza na hivi vijiji vitano ambavyo Mheshimiwa Mgimwa amevitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ameomba sana tupate fursa ya kutembelea kule mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukitembelea sana maeneo ya Morogoro, hata hivyo, bado tumhakikishie baada ya Bunge lako Tukufu kuisha mimi na Mheshimiwa Mbunge bado tutakwenda kutembelea zaidi, hata akisema mara tano bado tutakwenda kuhakikisha wananchi wanapata umeme.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa muda wetu umekwisha.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu linaelekea kwa Naibu Waziri. Katika mikoa ya Mtwara na Lindi tuna tatizo kubwa sana la usambazaji wa umeme kwa kuwa haikuwahi kupata *Phase I* ya *REA* wala fedha za *MCC*. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akalithibitishia Bunge hili kwamba, katika awamu hii ya tatu ya *REA* vijiji vyote vitapewa umuhimu wa kupewa umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kabisa Mtwara na Lindi yamekuwa ni maeneo ambayo kwa miaka mingi hayapati umeme, lakini baada ya ugunduzi wa gesi miaka miwili iliyopita, kati ya maeneo ambayo tuliyapa vipaumbele kuyapatia umeme wa gharama nafuu ni pamoja na Mtwara na Lindi. Hii ni kwa sababu tulianza sasa kutumia umeme wa gesi kwa mikoa yote hiyo miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu kwa mikoa hii miwili tuliwatengea kisima ambacho kwa ujumla wake kinapata *megawatt* 18 za umeme wa gesi. Kwa hiyo, watu wa Mtwara na Lindi wanaweza kupata umeme na tena wa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kwenye *REA* Awamu ya Tatu inayokuja kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha kwamba vijiji vyote vya Mtwara na Lindi ambavyo vimebaki kutopata umeme kwenye *REA* Awamu ya Kwanza kwa sababu haikuwepo na Awamu ya Pili ambayo imekwenda kwa kiwango kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahakikisha vijiji vyote vya Mtwara na Lindi ambavyo vimeingia kwenye mpango huu wa *REA* Awamu ya Tatu vitapata umeme wa uhakika.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge muda umekwenda sana tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kwa niaba yake.

Na. 173

Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani – Bagamoyo kwa Kiwango cha Lami

MHE. SAUMU H. SAKALA (K.n.y. MHE. MUSSA B. MBAROUK) aliuliza:-

Awamu zote za Serikali zilizopita Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne ziliahidi kujenga barabara ya Tanga – Pangani – Saadani hadi Bagamoyo kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, ni lini Serikali itaamua kujenga barabara ya Tanga – Pangani kwa kiwango cha lami?

(b) Kupitia Bunge la Kumi na Moja, je, Serikali inaahidi nini kuhusu ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, lenge kipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tanga – Pangani – Saadani hadi Bagamoyo, yenye urefu wa kilometa 178 ni sehemu ya mradi wa Kikanda wa barabara ya Malindi – Mombasa – Lungalunga – Tanga hadi Bagamoyo. Mradi huu wa Kikanda unaratibiwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani – Bagamoyo kwa kiwango cha lami ilianza mwezi Januari, 2011 na kukamilika mwezi Novemba, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea na…

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea kwa sauti ndani ya Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa, naomba utulivu ndani ya Bunge.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kutoka kwa washirika wa maendeleo. Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* tayari imeonesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa barabara hii. Taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii ya Tanga – Pangani – Saadani hadi Bagamoyo zitaanza baada ya kupatikana kwa fedha za ujenzi. Aidha, zoezi la uhakiki wa taarifa za uthamini wa mali za wananchi watakaoathirika na ujenzi wa barabara hii linaendela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imedhamiria kuijenga barabara hii ya Tanga – Pangani – Saadani hadi Bagamoyo kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa! Kwa niaba ya Mheshimiwa Mabrouk!

MHE. SAUMU H. SAKALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Anaitwa Mussa Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii ambayo ina kivutio cha pakee ambacho imeunganika na mbuga pamoja na bahari. Je, Serikali kwa kuendelea kuchelewa kuitengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami, haioni kuwa inapoteza mapato mengi ya kiutalii kutokana na kivutio hiki? *(Makofi)*

Swali la pili, Wakazi wa Wilaya ya Pangani ambao wako pembezoni mwa barabara ile wamewekewa alama ya "*X*" nyumba zao, lakini bado

wanaendelea kuishi na hawajui ni lini watalipwa fidia zao ili waendelee na maisha yao sehemu nyingine.

Je, Serikali ipo tayari kutoa ahadi kwamba ni lini itawalipa wakazi hawa fidia zao? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano inapotoa ahadi inatekeleza; barabara hii imeanza kufanyiwa usanifu na itakapokamilika maadam tumeshaona mtu anayetoa fedha tayari amepatikana kwa vyovyote vile ujenzi utafanyika kwa haraka itakavyowezekana ili mapato haya ya kitalii yaanze kuingia katika Mfuko wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la pili, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hizo alama za "*X*" anazoziona ndiyo sehemu ya utaratibu wa kufanya fidia. Ni hatua ya kwanza, baada ya hapo wanamalizia hatua inayofuata na mara utaratibu wa kufanya uthamini utakapokamilika suala la ulipaji wa fidia litashughulikiwa.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea muda umekwisha. Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Immaculate Sware Semesi aulize swali lake.

Na. 174

Usafirishaji wa Magogo Nje ya Nchi

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI aliuliza:-

(a) Je, Serikali inasafirisha nje ya nchi mbao na magogo kiasi gani kwa mwaka?

(b) Je, ni nchi gani inaongoza kwa kununua mbao na magogo kutoka Tanzania?

(c) Je, ni fedha za kigeni kiasi gani zimepatikana kutokana na mauzo ya magogo na mbao nje ya nchi kwa kipindi cha mwaka 2010 - 2015?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 50 ya Kanuni za Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002, inakataza usafirishaji wa magogo kwenda nje ya nchi. Aidha, Kanuni hiyo hairuhusu uuzaji nchi za nje wa mbao zenye unene unaozidi inchi sita. Kanuni hii na sheria vinaweka zuio ili kutoa fursa ya kukuza viwanda vya ndani ya nchi na ajira kwa Watanzania katika kupasua mbao na utengenezaji wa samani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 jumla ya mita za ujazo 333,404.91 za mbao chini ya inchi sita ziliuzwa na kusafirishwa kwenda nchi za nje.

Aidha, kwa mujibu wa takwimu nchi ya India inaongoza kwa kununua mbao kutoka Tanzania ambapo katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 jumla ya meta za ujazo 210,968.07 zilisafirishwa kwenda India, ikifuatiwa na nchi ya China ambayo ilinunua mita za ujazo 68,337.04.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi 269,985,300,000 kutokana na mauzo ya mbao nchi za nje. Aidha, hakuna kiasi cha fedha kilichopatikana kutokana na mauzo ya magogo kwa kuwa biashara ya magogo kwa mujibu wa sheria haikufanyika.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kumekuwa na uvunaji holela wa mikoko katika eneo la Rufiji na mikoko hii ikiwa inasafirishwa kwenda Zanzibar kwa kutumia bandari bubu. Je, Serikali inajua kuhusu suala hili na je, itachukua hatua gani?

Swali la pili, kumekuwa kuna uvunaji na utoaji holela wa mbao au mazao ya misitu katika maeneo ambayo hayana hata hiyo *management plan* au *strategy* ya uvunaji wa rasilimali hii. Je, Serikali ina mpango gani kupambana na hii hali? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya maliasili na utalii kwa ujumla viko vitendo ambavyo kwa ujumla wake vinaitwa ujangili na ujangili hauishii kwa wanyamapori tu peke yake na bidhaa zao, ujangili pia unahusisha bidhaa za misitu na misitu yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vyote ambavyo vimekuwa vikifanyika vya ujangili ni kinyume cha sheria na Wizara au Serikali kwa ujumla imejipanga vizuri zaidi sasa hivi kuweza kudhibiti vitendo vyote vya ujangili kwa kuimarisha ulinzi kwenye maeneo yanayohusika, kuboresha vikosi vya askari na kuwawezesha askari kuwa na vitendea kazi bora zaidi katika kufuatilia vitendo vya ujangili na kuchukua hatua mara moja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha, tuliongeza muda kwa sababu kulikuwa na hati za kuwasilisha na vilevile kulikuwa na maswali muhimu ya *REA* ambayo Wabunge walitaka kupata majibu. Nampongeza Waziri wa Nishati kwa kutoa majibu sahihi na mazuri. *(Makofi)*

Wageni waliopo jukwaa la Spika, wageni 20 wa Mheshimiwa Spika ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wageni 21 wa Mheshimiwa Charles Kitwanga, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni Agness Kitwanga, mtoto wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Joel Chacha, mkwe wa Mheshimiwa Waziri.

Wageni wengine wa Mheshimiwa Charles Kitwanga Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Meja Jenerali Projest Rwegasira - Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Balozi Simba Yahya - Naibu Katibu Mkuu, Ernest Mangu - Inspekta Jenerali wa Polisi, Ndugu John Minja - Kamishna wa Magereza, Ndugu Thobias Andengenye - Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, Ndugu Victoria Lembeli - Kaimu Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Modestus Kipilimba - Kaimu Mkurugenzi Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*, Ndugu Hamdan Makame - Kamishna wa Polisi Zanzibar, Ndugu Johari M. Sururu - Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Ndugu Hassan Hassan Mkurugenzi wa *NIDA* Zanzibar, Ndugu Athumani Diwani -Kamishna wa Upelelezi na Makosa ya Jinai, Ndugu Haji Janabi - Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango, Ndugu Rogatius P. Kipali - Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji Operesheni, Ndugu Gastom K. Sanga - Kamishna wa Magereza Fedha na Utawala, Ndugu Albert Jamhanga -Kamishna wa Polisi Fedha na *Logistic*, Makamishna, Wakurugenzi na viongozi wengine waandamizi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Godbless Lema, Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni ndugu Neema Godbless Lema - mke wake, Haleluya Natali mdogo wake, Patrobas Katambi - Mwenyekiti wa Vijana Taifa CHADEMA. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni sita wa Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum ambao ni watoto wake, wakiongozwa na ndugu Maxwell Mugaya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ambao ni Ndugu Andrew Charles.

Kuna wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Mariam Ditopile ambao ni wanafunzi 50 kutoka shule ya sekondari Rubi kutoka Jimboni kwakwe, wameambatana na walimu wanne wakiongozwa na Katibu wa UVCCM Wilaya ya Mpwapwa ndugu Jumanne Ali Kimtende. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni nane wa Mheshimiwa Pascal Haonga, Mbunge Jimbo la Mbozi, ambao ni Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji kutoka Jimboni kwake wakiongozwa na Ndugu Aidan Nzowa - Diwani. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Harisson Mwakyembe, ambao ni wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wanaosoma Shahada ya Ualimu, Sera, Mipango na Utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mkuchika anaomba kumtangaza mgeni wake ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Mwanza, Ndugu Haufi Maarifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la Kikao cha Kamati, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 16 Mei, saa saba mchana, kutakuwa na kikao kitakachofanyika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Venance Mwamoto, Kocha wa *Bunge Sports Club* anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanaopenda kujiunga na timu ya Bunge ya mpira wa wavu na mpira wa kikapu kwamba waonane na ndugu Chacha Nyakega chumba namba 329, Jengo la Utawala kwa ajili ya kujiandikisha. Utaratibu huu unaandaliwa kwa ajili ya kuanza mazoezi ya michezo.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi ya leo kuna taarifa zimewekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5), miongoni mwa taarifa hizi ni taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Nimezipitia taarifa hizo na kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za leo hususani mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, naamini kuna umuhimu wa Kamati ya Kanuni za Bunge kukutana na kujiridhisha kuwa maudhui ya taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yanakidhi masharti ya Kikanuni. *(Makofi)*

Hivyo basi, naelekeza Kamati ya Kanuni ya Bunge, ikutane mara moja katika Ukumbi wa Spika, aidha naelekeza Mheshimiwa Godbless Lema ambaye ndiye Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, naye ahudhurie kikao hicho pamoja na Mheshimiwa Freeman Mbowe ambaye ni Mjumbe wa Kamati hii lakini ndiye Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na shughuli kama zilivyopangwa katika *Order Paper* na iwapo itafika zamu ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuwasilisha taarifa yake wakati wa Kamati ya Kanuni haijamaliza kazi yake nitatoa mwongozo utakaofuata.

Kwa hiyo, sasa naagiza Kamati ya Kanuni, Mheshimiwa Lema na Wajumbe wa Kamati ya Kanuni pamoja na Mheshimiwa Mbowe ambaye ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani...

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu naomba unifafanulie tena, sijaelewa.

MWENYEKITI: Mheshimwa Lema, mimi nikisimama wewe hutakiwi kusimama na kwa mujibu wa Kanuni huwezi kusema mpaka nikuruhsu. Kwa Kiswahili cha kawaida, naagiza Kamati ya Kanuni ikutane na Mheshimiwa Lema na Wajumbe wote mkaipitie taarifa ya Kambi ya Upinzani iweze kukidhi matakwa ya Kanuni za Kibunge, na pale ambapo shughuli za Bunge zinaendelea ikifika wakati wa Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Kamati ya Kanuni haijamaliza muda wake nitatoa mwongozo kitakachofuata. Katibu.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68 (7), naomba nisiisome kwa sababu ya muda. Kumekuwepo na *video* inayozunguka kwenye mitandao mingi ya kijamii, ambayo inaonesha udhalilishaji mkubwa sana wa wanawake, udhalilishaji wa utu, udhalilishaji wa ubinadamu pamoja na udalilishaji mkubwa sana wa mila na desturi za Kitanzania. Naomba Mwongozo wako, naomba tamko la Serikali ni hatua gani imechukua kuhusiana na watu waliofanya udhalilishaji mkubwa wa mwanamke huyo. Nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesikitishwa sana na tukio lililotokea eneo la Wami, Dakawa ambapo binti wa Kitanzania amedhalilishwa, kwanza, kwa kuvuliwa nguo, pili, kwa kulazimishwa kufanya mapenzi na wanaume wawili,

tatu, kwa kurekodiwa hilo tukio na nne, video hiyo kusambazwa katika mitandao mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa na dhamana ya maendeleo ya wanawake na jinsia ninakemea kwa nguvu zangu zote tukio hilo na hatua ambazo Serikali imechukua, jana tumewasiliana na Waziri wa Mambo ya Ndani na *IGP*, wahusika wamekamatwa. Ni matumaini yangu kwamba wahusika watapelekwa mahakamani haraka iwezekanavyo ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa rai kwa jamii hasa wanaume kuwaheshimu na kuwathamini wanawake. Wanawake ni mama zenu, ni dada zenu, ni shangazi zenu na ni mabinti zenu. Suala hili hatuwezi kulivumilia na niombe wanaosambaza wasiendelee kusambaza hiyo video, ni udhalilishaji mkubwa uliopitiliza dhidi ya wanawake na wasichana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Msigwa.

MHE. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naheshimu maagizo uliyoyatoa kama Mwenyekiti, nasimama hapa kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Kambi tunapoandaa hotuba, hii hotuba siyo ya Mheshimiwa Godbless Lema ni hotuba ya Kambi ya Upinzani na kwa mara ya kwanza katika Bunge tunaona kwamba Kambi sasa inataka iambiwe nini cha kuleta mezani. Kanuni hazisemi hivyo, sisi tunaandaa kama Kambi na kile tunachoona kinaweza kuishauri Serikali ndicho tunachokileta mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tupate ufafanuzi haya yanatoka wapi kwamba Kamati ya Maadili ikae ianze ku-*filter* na kama kuna udhaifu kwenye hotuba yetu ndiyo udhaifu wa Kambi ambao Serikali wanatakiwa watu-*challenge* wanapojibu. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKTI: Mheshimiwa Msigwa, nafikiri wewe unajua Kiswahili vizuri sana. Nimesema Kamati ya Kanuni na Mheshimiwa Lema na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani wakutane. Sijasema Kamati ya Kanuni ikaandae taarifa ya Upinzani. Nawaomba Mheshimiwa Lema mpaka sasa hivi nilitegemea muwe mmeshaondoka humu ndani pamoja na Kamati ya Kanuni. Mheshimiwa Aeshi.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate Mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68(7) kuhusiana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya katika kipindi cha maswali na majibu, alipokuwa akimjibu Mheshimiwa Susan Lyimo kwenye swali Na. 167, swali lake la nyongeza akisema kwamba vituo vile vya afya vilivyojengwa ndani ya mkoa wa Rukwa na maeneo mengine, sasa mimi nitaongelea mkoa wa Rukwa tu kwamba mpaka leo

majengo yale yameshindwa kufunguliwa kutokana na taratibu za makabidhiano hazijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuomba Mwongozo wako kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya amesema uongo mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kupata Mwongozo wako kwa sababu nijuavyo mimi na mbele yangu pale yupo Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya akiwa Mkuu wa Mkoa alikabidhiwa majengo haya miaka miwili iliyopita. Nataka Mwongozo wako ikiwa Waziri amesema uongo ni hatua ipi inatakiwa ichukuliwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aeshi kwa mujibu wa Kanuni Mwongozo huo nitakujibu baadaye. Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Juzi tarehe saba limetokea tukio la ajabu sana Tarime...

MWENYEKITI: Soma hiyo Kanuni Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7) inasema hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi…

MWENYEKITI: Jambo lako limetokea lini? Tarehe saba, leo tarehe ngapi?

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ungeniacha kwanza niseme kwa sababu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa usibishane na Kiti, sasa wewe sema nikuruhusu tu lakini upo nje, sawa sema.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Juzi tarehe saba kuna tukio limetokea ambalo halijawahi kutokea kwenye nchi yetu, ambapo askari polisi walikwenda kwenye Kituo cha Afya cha Nyamongo kinaitwa Sungusungu, wakapiga risasi nyingi za kutosha na wagonjwa wawili wakapigwa risasi na jana nimeona taarifa ya Mkuu wa Mkoa anasema kwamba ni wahuni waliopigwa risasi pale. Tukio ambalo pale hospitali watu

walikuwa wanafanyiwa *operation,* unajua kuna watu wana *pressure* pale na watu wanaumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo limesikitisha sana na Tarime kuna *tension* kubwa, naomba Mwongozo wako ni nini kifanyike kwa sababu kama Mkuu wa Mkoa anasema watu wa Tarime ni wahuni na anahamu ya damu za watu, mimi nitampelekea watu zaidi ya laki moja aue afanye *massacre* na tuone kama wahuni wa Tarime wote wataisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Ahsante, Mwongozo huo nitaujibu baadaye kwa sababu unahitaji vilevile uchambuzi wa kina na taarifa rasmi ambazo Bunge ilitakiwa izipate haijazipata.

MHE. GODFERY W. MGIMWA: Mwongozo Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mgimwa.

MHE. GODFERY W. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7), wakati nilipokuwa nauliza swali langu la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri ali-*refer* jina langu na Jimbo langu kama natoka Morogoro, kwa hiyo ningeomba ifutwe katika *Hansard* ili iweze kurudi katika uhalisia wake ionekane kwamba natoka katika Jimbo la Kalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mgimwa soma Kanuni, Kanuni ya 45(3) ndiyo utapata jibu lake na mimi nalichukua nitalipangia siku nyingine.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Hamna Mwongozo tena, tuendelee Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali, kwamba Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

MWENYEKITI: Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia muda naomba hotuba yangu yote kama ilivyo kwenye kitabu cha hotuba iingie kwenye *Hansard. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mapema leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na kwa masikitiko makubwa naomba kuchukua nafasi hii kutoa rambirambi na salamu zangu za pole kwa familia na wananchi wa mikoa mbalimbali ya Tanzania kutokana na mvua kubwa iliyonyesha katika kipindi tofauti mwaka huu na kusababisha mafuriko na hivyo kuleta adha kubwa kwa wananchi ikiwemo vifo, uharibifu wa mali na miundombinu. Aidha, nawapa pole ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha yao kutokana na matukio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutumia fursa hii kutoa masikitiko yangu kwa familia na wananchi kwa ujumla kutokana na vifo, ulemavu, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu vilivyosababishwa na ajali za barabarani, angani, majini na nchi kavu katika kipindi chote tokea mwezi Julai, 2015. Aidha, nawapa pole ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha katika matukio hayo, naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahala pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge kwa kuteuliwa na hatimaye kupitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha imani kubwa kwangu na kunipa dhamana ya kuongoza Wizara hii, naahidi kutumia uwezo wangu wote kufanya kazi hii kwa uaminifu na uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa umuhimu mkubwa naomba niwashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa maelekezo yao mbalimbali yanayohusu Wizara yangu na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhimiza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake aliyoitoa mapema katika Mkutano huu wa Bunge ambapo pamoja na mambo mengine imetoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Jimbo la Muheza kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya ulinzi na usalama ya mwaka wa fedha wa 2015/2016 na Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Ninaishukuru pia Kamati hiyo kwa maelekezo na ushauri wao wenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kurekebisha wafungwa, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwezesha na kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutekeleza programu ya huduma kwa jamii, kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini na kutoa vitambulisho vya Taifa. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Uhamiaji, Idara ya Huduma kwa Jamii, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama nchini; kwa ujumla hali ya usalama nchini ni ya kuridhisha. Napenda kuvipongeza vyombo vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano wao na vyombo vingine vya dola kwa kutoa mchango mkubwa katika kudumisha amani na utulivu nchini katika kipindi cha mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uhalifu na makosa ya jinai; katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, makosa makubwa ya jinai 53,201 yaliripotiwa polisi kote nchini ikilinganishwa na makosa 47,942 yaliyoripotiwa kipindi kama hiki mwaka 2014/2015, ikiwa ni ongezeko la makosa 5,259 sawa na asilimia 11.

Katika mwaka 2015/2016 kumekuwa na matukio ya kuvamiwa kwa vituo vya polisi, kuua askari pamoja na kuporwa silaha na risasi. Matukio ya uvamizi ya vituo vya polisi yamepungua kutoka nane kwa mwaka 2014/2015 hadi kufikia matukio sita kwa mwaka 2015/2016. Katika matukio hayo, askari wanne, raia mmoja waliuawa, silaha 22 na risasi 273 ziliporwa. Jeshi la Polisi limefanikiwa kuwakamata watuhumiwa 17 waliohusika na uvamizi huo na kupata silaha zote zilizoporwa katika vituo vya Stakishari, Tanga na Ikwiriri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la biashara haramu na matumizi ya dawa za kulevya limeendelea kuwepo hapa nchini. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Jeshi la Polisi limeendelea kufanya doria, misako na *operation* maalum katika maeneo mbalimbali nchini ili kukabiliana na tatizo hili. Juhudi za kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya zitaendelea na Serikali haitakuwa na msamaha wala suluhu kwa wahusika wote. Natoa rai kwa watu wote kutojihusisha na uuzaji, utumiaji na usafirishaji wa dawa hizi.

Narudia tena, Serikali haitakuwa na msamaha wala suluhu kwa wahusika wote, natoa rai kwa watu wote kutojihusisha na uuzaji, utumiaji na usafirishaji wa dawa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama barabarani; ajali za barabara zimeendelea kupungua, takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 ajali za barabarani 6,980 zilitokea na kupoteza maisha watu 2,577 na wengine 7,503 walijeruhiwa ikilinganishwa na ajali 8,072 zilizotokea mwaka 2014/2015 na kusababisha vifo vya watu 2,883 na kujeruhi 9,370. Upungufu huu wa ajali ni sawa na asilimia 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na makosa ya usalama barabarani kuwa tishio kwa usalama wa wananchi, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine limeendelea kuchukua hatua za kuzuia na kudhibiti vyanzo vya ajali za barabarani. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu ya kuzingatia sheria za usalama barabarani kwa watumiaji wa barabara wakiwemo madereva wa bodaboda, kufanya doria za masafa mafupi na marefu katika barabara kuu, kufanya ukaguzi wa magari makubwa na madogo na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria askari wanaojihusisha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016 na malengo ya mwaka 2016/2017. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika mwaka wa 2015/2016 ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Serikali shilingi 178,969,264,691; hadi kufikia tarehe 31 Machi mwaka huu, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 148,273,978,722 sawa na asilimia 83 ya lengo la mwaka. Katika mwaka 2016/2017 Wizara imelenga kukusanya shilingi 289,969,630,604 nguvu zaidi zitaelekezwa katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato, hususani

katika kuimarisha na kuboresha matumizi ya benki na mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kufanya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara iliidhinishiwa shilingi 872,703,062,000 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 shilingi 685,860,659,133 zilikuwa zimetumika, sawa na asilimia 78.59 ya bajeti ya mwaka mzima ambapo shilingi 348,938, 631,450 ni mishahara, na matumizi mengine ya shilingi 332, 296, 027, 680 na fedha za maendeleo zilikuwa ni shilingi 4,626,000,000. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara inategemea kutumia shilingi 864,106,290,105 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi; udhibiti wa uhalifu nchini. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 Jeshi la Polisi liliendelea kulinda na kudumisha amani na utulivu uliopo nchini. Kwa namna ya pekee napenda kutumia fursa hii kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kufanya kazi kwa weledi, wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge, Wawakilishi, na Madiwani mwezi Oktoba, 2015 na mwezi Machi, 2016 na kuliletea Taifa letu heshima kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Jeshi la Polisi litaanza rasmi utekelezaji wa Mpango Matokeo Makubwa Sasa katika Mkoa wa Kipolisi Kinondoni kama sehemu ya kuboresha utendaji na kuimarisha usalama wa nchi, inatarajiwa kuwa mpango huu utatekelezwa nchi nzima baada ya kubaini changamoto zitakazotokana na utekelezi huo katika Mkoa wa kipolisi Kinondoni. Nitumie fursa hii kuomba ushirikiano wa wadau mbalimbali hasa wananchi wa Kinondoni ili kazi hii iweze kuleta mafanikio yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali itakamilisha taratibu za kuanzisha mfumo wa ulinzi wa raia na mali zao kwa njia ya mtandao wa kamera za usalama yaani *CCTV cameras* katika Mkoa wa Dar es Salaam kisha kuenea katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2016/2017 Jeshi la Polisi litaendelea kupambana na makosa yanayovuka mipaka hususani ni ugaidi, uharamia, biashara ya dawa za kulevya, biashara haramu ya kusafirisha binadamu, wizi wa vyombo vya moto hususani magari, wizi wa kutumia mitandao ya TEHAMA, bidhaa bandia, biashara haramu ya silaha na uchafuzi wa mazingira. Aidha, Jeshi la Polisi litaimarisha doria, misako na *operation* maalum za nchi kavu na majini ili kupunguza matishio ya uhalifu, makosa makubwa ya jinai hususani wizi wa aina zote na unyang'anyi wa kutumia silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji ya wanawake, wazee na watu wenye ualbino. Suala la mauaji ya wanawake, wazee na watu wenye ualbino wanaokatwa viungo kwa sababu ya imani ya kishirikina vimeendelea kulitia doa Taifa letu. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 jumla ya matukio

222 ya mauaji ya wanawake na wazee, yalijitokeza. Katika matukio hayo wanawake 157 na wanaume 71 waliuawa, mchanganuo wa matukio hayo kwa Mkoa ni kama inavyooneshwa katika ukurasa wa 17 aya ya 31 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia matukio hayo, watuhumiwa 135 walikamatwa na kufikishwa mahakamani, ambapo 20 walifungwa, 15 waliachiwa huru, 65 walishinda kesi kwa kukosekana ushahidi na watuhumiwa 35 kesi zao zinaendelea. Katika kuhakikisha kuwa vitendo hivi vinakomeshwa Wizara yangu imeunda kikosi kazi maalum, kinachojumuisha vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi nyingine za haki jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vitendo vya ukatili dhidi ya ndugu zetu wenye ualbino, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, zipo dalili za kupungua kwa kiasi kikubwa kwa matukio hayo kwa miaka ya hivi karibuni. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 hakukuwa na tukio lolote la mauaji lililoripotiwa. Aidha, matukio mawili ya kujeruhiwa kwa watu wenye ualbino yalitoka Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Tanga. Mtuhumiwa mmoja alikamatwa mkoani Tanga na kufikishwa mahakamani na katika matukio ya siku za nyuma kesi tano za mauaji na mbili za kujeruhi upelelezi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na vitendo hivi dhalimu katika mwaka 2016/2017 Serikali itahakikisha kuwa inaendelea kushirikiana na raia wema Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi zinazoratibu shughuli za waganga wa jadi, kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha mahakamani waganga wanaothibitika kupiga ramli chochezi. Wahalifu wanaokodishwa kufanya mauaji na watu wanaotoa fedha kwa waganga wa jadi na kupewa masharti ya kuua na ndugu zao, wazee, wanawake na watu wenye ualbino ili wapate utajiri wa haraka. Aidha, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha Kamisheni mpya ya Intelijensia ya Jinai ili kujenga uwezo wa kupata taarifa za uhalifu mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa dawa za kulevya. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 jumla ya kilo 141.27 za dawa ya kulevya ya viwandani ambayo ni *heroin, cocaine, cannabis* na *mandrax* zilikamatwa na watuhumiwa 719 kufikishwa mahakamani. Aidha, kilo 18,513 na *gram* 415 za bangi na kilo 15,402 za mirungi zilikamatwa ambapo watuhumiwa wanaume 9,935 na wanawake 1,020 walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadilishanaji wa taarifa za wahalifu na uhalifu. Jeshi la Polisi limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuzuia uhalifu unaovuka mipaka usitokee ndani ya ardhi ya Tanzania. Ili kufikia azma hiyo na kwa ushirikiano na vyombo hivyo umeanzishwa mkakati wa kupambana na uhalifu katika maeneo ya

mipaka ya Tunduma, Kasumulu na Namanga. Aidha, mkakati huo utaendelezwa katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushughulikia uhalifu katika shughuli za kisiasa na kijamii. Katika mwaka 2015/2016 Jeshi la Polisi liliendelea kuimarisha usalama katika kipindi chote cha kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu Oktoba 2015. Uchaguzi wa marudio Zanzibar Machi, 2016. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza wajibu wake wa ulinzi na usalama, kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi. Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi na jamii yote ya Tanzania kwa ujumla, kuzingatia umuhimu wa amani na usalama katika shughuli zote za kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira; kwa sasa uwiano wa askari kwa raia nchini ni askari mmoja kwa raia 1,071 kiwango ambacho hakijafikia kiwango cha uwiano wa Kimataifa ambacho ni askari mmoja kwa raia 450. Katika juhudi za kufikia kiwango hicho, katika mwaka wa fedha 2015/2016, askari polisi wapya 3,882 waliajiriwa na katika mwaka wa fedha 2016/2017 wanatarajiwa askari polisi wapya 3,700 kuajiriwa. Aidha, Serikali imeendelea kuhuisha viwango vya mishahara na posho mbalimbali ikiwemo posho ya chakula ambayo iliongezwa kutoka shilingi 180,000 hadi kufikia shilingi 300,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendea kazi na makazi kwa askari polisi. Ili kukabiliana na changamoto ya uchache wa miundombinu na makazi kwa askari polisi, Serikali kupitia mkopo kutoka Serikali ya China inakusudia kujenga nyumba 4,136. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa miradi iliyoanzishwa siku za nyuma, miradi hiyo ni nyumba za makazi ya askari na vituo vya polisi kama ilivyoainishwa katika aya ya 37 ukurasa wa 25, wa kitabu cha hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza; juhudi za kuwasindikiza mahabusu kwenda mahakamani na kurudi gerezani zinaendelea kutekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Wilaya ya Arusha Mjini na Wilaya ya Dodoma Mjini. Utaratibu huu umesaidia mahabusu kusikilizwa kesi zao na kupata haki ya kisheria kwa wakati. Katika mwaka 2016/2017 Serikali itaendelea kuboresha huduma za usafirishaji wa mahabusu kwenda mahakamani na kurudi magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya urekebishaji wa wafungwa; Jeshi la Magereza, limeendelea kutekeleza programu za kurekebisha wafungwa magerezani kwa kuwapa stadi katika kilimo, ufugaji, viwanda vidogo vidogo na ujenzi. Kwa upande wa kilimo urekebishaji huo unaenda sambamba na utumiaji wa zana bora za kilimo, matumizi bora ya ardhi na pembejeo. Malengo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kuendeleza mafunzo ya kilimo cha kisasa, katika magereza yote ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi na ukamilishaji ukarabati wa ujenzi wa mabweni ya wafungwa. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 lengo lilikuwa ni kuendeleza ujenzi wa jiko na bweni moja la wafungwa Gereza la Segerea - Dar es Salaam, ambalo ujenzi wake upo katika hatua za msingi. Kazi nyingine ilikuwa ni kukamilisha ujenzi wa hospitali iliyopo Gereza la Segerea, na ujenzi wa Gereza Maalum Isanga ili lianze kutumika. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 nguvu zitaelekezwa katika ujenzi wa mabweni 16 ya wafungwa, kuendelea na ukamilisha wa ujenzi wa mabweni saba, ukarabari wa mabweni 59 ya wafungwa na kuanza ujenzi wa jengo la utawala katika Gereza la Chato, mkoa wa Geita. Mchanganuo wa magereza yatakayohusika umeainishwa katika aya ya 46 ukurasa wa 31 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Magereza limeendelea na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo na viwanda vidogovidogo, kwa upande wa kilimo, eneo la hekari 4,750 limelimwa kwa matarajio ya kuvuna tani 5,557.5 za mazao mbalimbali sawa na ongezeko la asilimia Saba ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, shirika kupitia kikosi cha ujenzi cha Jeshi la Magereza, limeendelea kufanya kazi mbalimbali za ujenzi na ukarabati wa majengo ya watu binafsi na taasisi za Serikali. Matarajio ya mwaka wa fedha 2016/2017 ni kuongeza shughuli za uzalishaji kwa kuingia ubia na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kupata mtaji wa kutosha kuweza kukidhi soko la bidhaa zitokanazo na shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya nishati mbadala magerezani. Katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na matumizi makubwa ya kuni magerezani, Jeshi la Magereza limechukua hatua za kuanza matumizi ya *biogas* na majiko banifu katika nishati mbadala kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa magerezani. Matumizi ya *biogas* yanaendelea katika Gereza la Ukonga na gesi asili katika Gereza la Keko. Kwa sasa Jeshi limeanza kutumia majiko yanayotumia kuni kidogo yaani *energy saving stove* katika Gereza la Karanga na Mwanga - Kilimanjaro, Kibondo na Bangwe - Kigoma na Gereza la Sumbawanga - Rukwa. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi litaendelea kueneza matumizi ya majiko banifu na gesi asilia katika magereza mengine yenye matumizi makubwa ya kuni kadri uwezo wa fedha utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Idara ya Uhamiaji iliendelea kutoa huduma kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini. Katika kipindi hicho wageni 1,187,490 waliingia ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo wageni 1,005,652 waliingia nchini ikiwa ni ongezeko la asilimia 18. Aidha, wageni 1,199,995 walitoka nje ikilinganishwa na wageni 892,614 waliotoka nchini mwaka uliopita likiwa ni ongezeko la asilimia 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misako ya doria na ukaguzi. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Idara ya Uhamiaji iliendelea kufanya misako, doria na ukaguzi katika maeneo mbalimbali ili kudhibiti wahamiaji haramu na biashara haramu ya usafirishaji binadamu. Jumla ya watuhumiwa wa uhamiaji haramu 6,600 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikilinganishwa na wahamiaji haramu 3,944 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka 2014/2015. Aidha, vinara tisa raia wa kigeni wanaojihusisha na mtandano wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu walikamatwa, kuchukuliwa hatua za kisheria na hatimaye kufukuzwa nchini. Pia Watanzania saba wanaojihusisha na mtandao huo kesi zao ziko mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vilivyotolewa kwa wageni wakaazi; Idara ya Uhamiaji imetoa vibali vya ukaaji kwa wageni wawekezaji na wengine waliopata ajira katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya wageni 12,584 wamepewa vibali vya ukaazi kama vinavyoainishwa katika ukurasa wa 37 aya ya 54 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *passport* na hati nyingine za safari; Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi 2016, Idara ya Uhamiaji imetoa jumla ya *passport* 85,758 kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali, mchanganuo wa *passport* hizo unaainishwa katika ukurasa wa 37 aya 55 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 02 Machi, 2016 viongozi wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walizindua *passport* za kielektroniki za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, zenye ubora unaokidhi viwango vya Kimataifa na zitatumika kusafiria duniani kote tofauti na *passport* za Afrika Mashariki zilizopo sasa. *Passport* hizo zinakusudiwa kuanza kutumika rasmi tarehe 01 Januari, 2017, *passport* zinazotumika sasa za nchi wanachama zitafikia ukomo wa kutumika mwezi Disemba, 2018. Aidha, Serikali itakamilisha taratibu za kuanzisha mfumo wa utoaji wa huduma ya uhamiaji kwa njia ya mtandao yaani *e-immigration*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wageni walioomba kupewa uraia Tanzania, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 wageni 405 walipewa uraia wa Tanzania. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, Watanzania 44 walipata uraia wa mataifa mengine na kupoteza sifa za kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia, Sura 357 Rejeo la mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira na mafunzo; katika mwaka wa fedha 2015/2016 Idara ya Uhamiaji imepata kibali cha kuajiri askari wapya 1,000 ambapo askari 298 wapo katika mafunzo ya awali ya uhamiaji katika Chuo cha Polisi Moshi wakati linaendelea na utaratibu wa kuajiri askari wapya 702.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendea kazi, majengo na ofisi na makazi ya askari; Idara ya Uhamiaji imeendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi ambapo upo katika hatua mbalimbali katika mikoa ya Manyara, Pwani, Geita, Mtwara na Lindi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Idara ya Uhamiaji inatarajia kuanza ujenzi wa ofisi katika Wilaya ya Ileje, Mkoa wa Songwe, kituo cha Kilongwe - Wilayani Rorya, Mkoa wa Mara na kufanya ukarabati wa majengo ya Chuo cha Uhamiaji Moshi na jengo la Makao Makuu Dar es Salaam, pia ujenzi wa nyumba za makazi ya askari katika eneo la Ndugukitu - Chakechake, Pemba na nyumba za viongozi mikoani Kigoma na Mwanza. Aidha, ukarabati unaendelea katika ofisi za Uhamaji Mkoa wa Kaskazini Unguja, Wilaya ya Micheweni Pemba na Kaskazini Pemba. Aidha, Ofisi ya Mjini Magharibi ukarabati umekamilika.

Aidha, katika wa mwaka wa fedha 2016/2017, Idara ya Uhamiaji itamalizia ujenzi wa nyumba ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji na kuanza ujenzi wa nyumba za askari Kisongo Arusha na kukarabati nyumba za watumishi mkoani Tabora. Katika kujiimarisha kiutendaji Idara ya Uhamiaji imekamilisha taratibu za kununua magari 16 na pikipiki 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kufanya ukaguzi wa tahadhari na majanga ya moto kwenye maeneo mbalimbali, kuzima moto, kuokoa maisha na mali kwenye majanga ya moto na majanga mengineyo. Kuelimisha umma juu ya tahadhari ya moto, kinga ya moto na majanga mengineyo ambayo yanaweza kulikumba Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Ukoaji linahitaji jumla ya vituo 152 Tanzania, lakini kwa sasa lina vituo 57, kati ya hivyo, 32 viko katika miji na 19 viko katika viwanja vya ndege, huu ni upungufu wa vituo 95 hali inayosababisha maeneo mengi kukosa huduma za zimamoto na uokoaji. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi linategemea kujenga kituo kimoja Kigamboni Dar es Salaam na kuendelea na ujenzi wa Jengo la Makao Makuu lililoko *TAZARA,* Jiji Dar es Salaam. Aidha, Jeshi lina magari ya kuzima moto 56 yenye ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi linatarajia kununua magari mawili ya kuzima moto ili kuendelea kuboresha huduma ya zimamoto na uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya moto na majanga mengine, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuanzia Julai, 2015 hadi kufikia Machi, 2016 limeshiriki kuzima moto katika matukio 517 Tanzania Bara ikiwemo moto katika shule ya sekondari Iyunga, mkoani Mbeya na soko Wilayani Masasi. Vilevile Jeshi limefanya maokozi katika matukio 245 kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kushiriki katika maokozi ya watu watano waliofukiwa kifusi katika mgodi wa Nyangarata Wilayani Kahama, maokozi ya watu 554 katika kijiji cha Pawaga na watu 104 katika kijiji cha Mbuyuni katika mafuriko Mkoani Iringa. Aidha,

kulifanyika maokozi ya watu na mali zao katika ajali za kuzama kwa kivuko katika Mto Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma kwa wakimbizi, nchi yetu kwa miaka ya karibuni ilishuhudia kupungua kwa idadi ya wakimbizi hata kufikia hatua ya kubaki na kambi moja tu ya wakimbizi ya Nyarugusu. Hata hivyo, kuanzia mwezi Aprili, 2013 tulianza tena kupokea wakimbizi kutoka Burundi baada ya kuzuka mgogoro wa kisiasa nchini humo. Kutokana na ujio wa wakimbizi hao, Serikali ilianzisha upya kambi tatu za wakimbizi ambazo ni Nduta iliyoko Wilayani Kibondo, Mtendeli na Kalongo zilizoko katika Wilaya ya Kakonko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike kuwa miongoni mwa watu waliokimbilia nchini kutafuta hifadhi ya ukimbizi ni pamoja na wapiganaji ambao walikuwa wanaendesha harakati katika nchi zao za asili. Wale wanaobainika kuwa walikuwa ni wapiganaji wamekuwa wanatengwa na kupelekwa kwenye kituo maalum kilichoanzishwa kwa ajili hiyo ambacho ni Gereza la Mwisa lililopo Kitengule, Karagwe, mkoani Kagera. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 kulikuwa na wakimbizi wa aina hiyo 58 gerezani hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya hatua zinazochukuliwa kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la idadi kubwa ya wakimbizi nchini ni kuhamishia katika nchi ya tatu, katika kutekeleza suala hilo Serikali yetu na Serikali ya Marekani zinaendelea kutekeleza mpango maalum wa kuwahamishia nchini Marekani wakimbizi wenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo wapatao 32,000. Kwa takwimu mpya nilizozipata asubuhi hii ni wakimbizi 50,000 wanaoishi katika kambi ya Nyarugusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; Serikali itaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanasajiliwa na kutambuliwa ili kupatiwa vitambulisho vya Taifa mapema iwezekanavyo. Aidha, kutokana na umuhimu wa vitambulisho vya Taifa Serikali itaendelea kuiwezesha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kwa kadri iwezekanavyo ili iweze kukamilisha jukumu hilo. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeendelea na zoezi la usajili na utambuzi wa watu katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Ruvuma na mikoa yote ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika mwaka 2016/2017 inalenga kuwasajili Watanzania milioni 22 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na kupewa vitambulisho vya Taifa kuendelea kuelimisha Umma juu ya umuhimu wa vitambulisho vya Taifa na matumizi yake ya kila siku katika dhana nzima ya utambuzi, kukamilisha Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, kupata vitendea kazi vya kutosha ikiwemo magari 30 maalum kwa ajili ya kusajili, vifaa vya

kugawiwa vitambulisho, vifaa vya kusomea vitambulisho 700 na kompyuta 302 kwa ajili ya ofisi 150 za usajili katika Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vita dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu; baada ya ripoti mbalimbali za kitaifa na kimataifa kuitaja nchi yetu kama mojawapo ya wahanga wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, Wizara yangu ilianzisha sekretarieti ya kupambana na kudhibiti biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kwa lengo la kudhibiti biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 Sekretarieti ya Kupambana na Kudhibiti Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu ilifanya ufuatiliaji katika makampuni yanayofanya biashara ya starehe za usiku yaani *night clubs* na *cassino* ambazo huingiza wasichana kutoka nje ya nchi ili kudhibiti biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Katika ufuatiliaji huo, wamiliki wa makampuni matano na wasichana 57 walihojiwa bila kupatikana na dosari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa vyama vya kijamii na vya kidini; Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imeendelea na jukumu la usajili na uhakiki wa vyama vya kijamii na kidini. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 maombi 472 ya usajili wa vyama yalipokelewa ambapo kati ya hayo maombi 370 ni ya vyama vya kijamii na maombi 102 ni ya vyama vya kidini. Katika kipindi hicho vyama 404 vilisajiliwa, kati ya hivyo 378 ni vyama vya kijamii na 26 ni vyama kidini. Aidha, maombi ya vyama 55 bado yanashughulikia na maombi ya vyama 13 yamekataliwa kutokana na kukosa sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani, kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 katika kutimiza malengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za dhati ziwaendee Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Jimbo la Muheza kwa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za kipekee nazitoa kwa viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mheshimiwa mhandisi Hamad Masauni Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Meja Jenerali Projest A. Rwegasira - Katibu Mkuu; Balozi Simba Yahaya - Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Ernest Jumbe Mangu -Inspekta Jenerali wa Polisi; Ndugu John Minja - Kamishna Jenerali wa Magereza; Ndugu Thobias Andengenye - Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji; Ndugu Pius Nyambacha -

Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji Mstaafu; Ndugu Victoria Lembeli - Kaimu Kamishna Jenerali wa Uhamiaji; Dkt. Modestus Kipilimba - Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wote wa Idara na Vitengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua pia fursa hii kuwashukuru washirika wa maendeleo walioendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza programu za mipango. Washirika hao ni pamoja na Australia, China, Japan, Korea, Marekani, Misri, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uturuki na taasisi za Kimataifa zikiwemo *INTERPOL, IOM, EU, UNHCR, DFID, USAID, UNICEF, WFP* na *Pharm Access* pamoja na wadau wengine wote kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ingawa siyo kwa umuhimu ninamshukuru sana mke wangu Matilda, watoto wangu… *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa omba pesa, kuanzia ukurasa wa 63.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuiwezesha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa 2016/2017 naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ya jumla ya shilingi 864,106,290,105. Kati ya fedha hizo shilingi 316,126,377,000 ni za matumizi mengineyo, shilingi 500,056,492,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 47,923,421,105 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mchanganuo kama ufuatao:-

Fungu 14 – Jeshi la Ukoaji ni shilingi 31,967,579,000.00; Fungu 28 – Jeshi la Polisi ni shilingi 535,211,306,105.00; Fungu 29 – Jeshi la Magereza shilingi 194,997,817,000.00; Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani na *NIDA* shilingi 49,371,988,000.00; Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji shilingi 52,557,600,000.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe, Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi wengine wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imeungwa mkono.

HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI, MHESHIMIWA CHARLES M. KITWANGA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

I. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mapema leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote na kwa masikitiko makubwa naomba kuchukua nafasi hii kutoa rambirambi na salamu zangu za pole kwa familia na wananchi wa mikoa mbalimbali ya Tanzania kutokana na mvua kubwa iliyonyesha katika vipindi tofauti mwaka huu na kusababisha mafuriko na hivyo kuleta adha kubwa kwa wananchi ikiwemo vifo na uharibifu wa mali na miundombinu. Aidha, nawapa pole ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha yao kutokana na matukio hayo.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kutumia fursa hii kutoa masikitiko yangu kwa familia na wananchi kwa ujumla kutokana na vifo, ulemavu, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu vilivyosababishwa na ajali za barabarani, angani, majini na nchi kavu katika kipindi chote toka mwezi Julai, 2015. Aidha, nawapa pole ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha katika matukio hayo. Namuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee napenda kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb) kwa kuteuliwa na hatimaye kupitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha imani kwangu na kunipa dhamana ya kuongoza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nami naahidi kufanya kazi kwa uaminifu.

6. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, kwa umuhimu mkubwa naomba niwashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa maelekezo yao mbalimbali yanayohusu Wizara yangu na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhimiza utekelezaji wake.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoitoa mapema katika mkutano huu wa Bunge ambayo pamoja na mambo mengine imetoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mbunge wa Jimbo la Muheza, kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya Ulinzi na Usalama ya mwaka wa fedha 2015/16 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2016/2017. Ninaishukuru pia Kamati hiyo kwa maelekezo na ushauri wao wenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara yangu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya msingi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwezesha na kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutekeleza Programu ya Huduma kwa Jamii, kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini na kuandaa na kutoa vitambulisho vya Taifa. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Uhamiaji, Idara ya Huduma kwa Jamii, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

II. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM KATIKA KIPINDI CHA 2015/2016

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina malengo 5 ya kutekeleza yanayotokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Taarifa ya utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

a) Kuendeleza Utawala Bora na Demokrasia

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za utawala bora. Maeneo husika ni pamoja na uzingatiaji wa haki za binadamu, ulinzi na huduma kwa wafungwa na mahabusu, wakimbizi na watafuta hifadhi, matumizi ya

adhabu mbadala wa vifungo, usajili wa vyama vya kijamii na kidini, kupiga vita biashara haramu ya binadamu na vilevile utoaji wa Vitambulisho vya Taifa kwa raia, wageni wakaazi na wakimbizi.

b) Kuviimarisha Vyombo vya Ulinzi na Usalama

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inaendelea kujenga uwezo wa watendaji katika vyombo vya Ulinzi na Usalama ikiwemo kutoa mafunzo, ujenzi wa ofisi na makazi kwa askari na watumishi pamoja na kuwapatia zana za kisasa za kufanyia kazi. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 askari 12,844 kutoka Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji wamepatiwa mafunzo katika fani mbalimbali ambapo Polisi ni 8,894 Magereza 3,076, Zimamoto na Uokoaji 505 na Uhamiaji 369. Aidha, Chuo cha Maafisa Magereza Ukonga kimefanikiwa kupata usajili wa kudumu kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*National Council for Technical Education – NACTE*) na sasa ni Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji ambacho kina mamlaka kamili ya kujiendesha (*Autonomous*). Kuwepo kwa Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji kutasaidia kutoa elimu stahiki ya Urekebishaji itakayotambulika ndani na nje ya Nchi. Elimu hii itaongeza weledi wa askari wetu watakaopitia kwenye Chuo hiki. Aidha, mpango huu wa vyuo kujiendesha upo pia katika vyuo vya Polisi na baadae utaanzishwa katika Chuo cha Uhamiaji.

c) Kujenga Uwezo wa Kukabili Majanga

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeajiri askari wapya 481 na kuwapatia mafunzo ya namna ya kukabiliana na majanga ya moto pamoja na majanga mengine. Aidha, askari 157 wanaendelea kupatiwa mafunzo ya namna ya kukabiliana na majanga mbalimbali katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo- Handeni, mkoani Tanga.

d) Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya

14. ***Mheshimiwa Spika,*** mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya yaliendelezwa. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Jeshi la Polisi liliendelea kuzifanyia kazi taarifa za wananchi zilizolenga kuwadhibiti wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Aidha doria, misako na operesheni maalum zilifanyika nchi nzima ikiwemo katika bahari ya Hindi, viwanja vya ndege, stendi za mabasi yaingiayo na kutoka nchini pamoja na maeneo yenye magenge ya vijana ili kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya nchini.

e) Usalama kwa Makundi Maalum

15. ***Mheshimiwa Spika,*** makundi haya yanajumuisha watu wenye ualbino, wazee, walemavu wa viungo, watoto na wanawake. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Jeshi la Polisi liliendesha operesheni kabambe ili kuimarisha usalama wa makundi maalum nchi nzima. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya watuhumiwa 135 walikamatwa na kufikishwa mahakamani ambapo kesi hizo zipo katika hatua mbalimbali. Kwa nafasi hii kupitia Bunge lako tukufu nitoe rai kwa wananchi waache tabia ya kuyasakama makundi haya kwa sababu mbalimbali ikiwemo ya ushirikina. Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali mkiwemo ninyi waheshimiwa wabunge ili kukomesha tatizo hili.

III. HALI YA USALAMA NCHINI

16. ***Mheshimiwa Spika***, wajibu wa kwanza wa Serikali ni kulinda usalama wa raia na mali zao na kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu. Napenda kuvishukuru vyombo vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano wao na vyombo vingine vya dola kwa kutoa mchango mkubwa katika kudumisha amani na utulivu nchini katika kipindi cha mwaka 2015/2016. Changamoto zinazokabili utekelezaji wa majukumu haya ni pamoja na kuendelea kuwepo kwa makosa ya usalama barabarani, kuongezeka kwa mbinu za uhalifu, biashara ya madawa ya kulevya, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, migogoro ya kijamii, msongamano magerezani, majanga mbalimbali na uhamiaji haramu.

Hali ya Uhalifu na Makosa ya Jinai

17. ***Mheshimiwa Spika***, kimsingi hali ya usalama nchini ilikuwa ya kuridhisha, takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 jumla ya makosa makubwa ya jinai 53,201 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi kote nchini ikilinganishwa na makosa 47,942 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2014/2015 ikiwa ni ongezeko la makosa 5,259 sawa na asilimia 11. Ongezeko la makosa haya yaliyoripotiwa limetokana na kusogezwa kwa huduma za kipolisi hadi ngazi ya Kata/Shehia na kuongezeka kwa elimu ya Usalama wa Raia kwa wananchi ambao wameelewa umuhimu wa kutoa taarifa za uhalifu kwa vyombo vya dola. Jeshi la Polisi litaendelea kuongeza juhudi katika kukabiliana na uhalifu nchini.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 kumekuwa na matukio ya kuvamiwa kwa vituo vya polisi, kuua askari pamoja na kuporwa silaha na risasi. Matukio ya uvamizi wa vituo vya polisi yamepungua kutoka 8 mwaka 2014/2015 hadi kufikia matukio 6 mwaka 2015/2016 ambapo jumla ya askari 4 na raia mmoja waliuawa ambapo silaha 22 na risasi 273 ziliporwa. Jeshi la Polisi

limefanikiwa kuwakamata watuhumiwa 17 waliohusika na uvamizi wa vituo na kupata silaha zote zilizoporwa katika vituo vya Stakishari, Tanga na Ikwiriri. Katika tukio la Stakishari silaha 14 zilizoporwa zilikamatwa ambapo watuhumiwa 13 walifikishwa mahakamani. Katika tukio la Tanga silaha mbili zilizoporwa zote zilikamatwa. ambapo mtuhumiwa mmoja alikamatwa na kufikishwa mahakamani. Aidha, katika tukio la Ikwiriri silaha 6 na risasi 273 zilizoporwa zote zilikamatwa na watuhumiwa watatu walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inakemea tabia hii ya kuvamia vituo vya polisi ambayo inaambatana na dalili za vimelea vya ugaidi na kuomba jamii iwafichue waovu wanaotenda vitendo hivi ili kudumisha hali ya ulinzi na usalama nchini.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** tatizo la biashara haramu na matumizi ya dawa za kulevya limeendelea kuwepo hapa nchini. Katika kukabiliana na biashara hiyo Jeshi la Polisi kwa mwaka wa fedha 2015/16 limeendelea kufanya doria, misako na operesheni maalum nchi nzima ikiwemo katika bahari ya Hindi na fukwe zake, mipakani, magenge ya vijana, viwanja vya ndege na stendi za mabasi yaingiayo na kutoka nchini. Hatua hizo zililenga kudhibiti uingizaji, usafirishaji, uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** juhudi za kupambana na biashara haramu ya madawa ya kulevya zinaendelea na Serikali haitakuwa na msamaha wala suluhu kwa wahusika wote. Natoa rai kwa watu wote kutojihusisha na uuzaji, utumiaji na usafirishaji wa madawa haya.

Hali ya Usalama Barabarani

21. ***Mheshimiwa Spika,*** ajali za barabarani zimeendelea kupungua. Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 jumla ya ajali za barabarani 6,984 zilitokea katika maeneo mbalimbali ambapo watu 2,577 walipoteza maisha na wengine 7,503 walijeruhiwa ikilinganishwa na ajali 8,072 zilizotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015 na kusababisha vifo vya watu 2,883 na majeruhi 9,370. Upungufu huu wa ajali ni sawa na asilimia 13. Ajali hizi zimeendelea kuleta madhara makubwa kwa wananchi kwani idadi ya majeruhi na vifo bado ni kubwa. Ajali nyingi kati ya hizo zimesababishwa na uzembe wa madereva kutozingatia Sheria za Usalama Barabarani ikiwa ni pamoja na mwendo kasi, ulevi, ubovu wa magari na miundombinu na pia kuendesha magari bila kujali watumiaji wengine wa barabara .

22. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na makosa ya usalama barabarani kuwa tishio kwa usalama wa wananchi, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine kama vile SUMATRA, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), TANROADS na Shule za Udereva zilizosajiliwa limeendelea kuchukua hatua za kuzuia na kudhibiti vyanzo vya ongezeko la ajali za barabarani. Hatua hizo ni pamoja na

kutoa elimu ya kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani kwa watumiaji wa barabara wakiwemo madereva wa bodaboda, kufanya doria za masafa mafupi na marefu katika barabara kuu, ukaguzi wa magari makubwa na madogo, kutumia kamera (tochi) za kutambua madereva wanaoendesha mwendo kasi, kusimamia zoezi la utoaji wa leseni mpya za udereva, kuwahamasisha abiria kutoa taarifa mapema za madereva wanaokiuka Sheria za Usalama Barabarani, kuwaelekeza wamiliki wa mabasi kubandika kwenye mabasi yao namba za simu za viongozi wa Polisi, kuwafikisha mahakamani madereva wazembe na kuwachukulia hatua za kinidhamu askari wanaojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa toka kwa madereva. Aidha, mifumo mipya ya udhibiti wa makosa ya usalama barabarani ikiwemo tozo za papo kwa papo kwa kutumia mashine za kielektroniki umeweza kusaidia kudhibiti ajali za barabarani. Hata hivyo, katika mwaka 2016/17 Jeshi lina mpango wa matumizi ya mfumo wa pointi na ufungaji wa kamera za kudumu za barabarani ili kusaidia udhibiti wa ajali za barabarani.

23. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali itakamilisha taratibu za kuanzisha ukaguzi wa lazima wa magari yote nchini (*Mandatory Vehicle Inspection*) pamoja na taratibu za ufuatiliaji wa magari yaendayo mikoani kwa njia ya TEHAMA. Taratibu hizi zitasaidia kupunguza ajali za barabarani pamoja na kuondoa magari chakavu ili kuweka mazingira salama.

IV. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2015/2016 NA MALENGO YA MWAKA 2016/2017

MAPATO NA MATUMIZI

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika mwaka 2015/2016 ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Serikali ya jumla ya shilingi 178,969,264,691. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 148,273,978,722.00 sawa na asilimia 83 ya lengo la mwaka. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imelenga kukusanya mapato ya shilingi 289,966,630,604. Nguvu zaidi zitaelekezwa katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato hususani katika kuimarisha na kuboresha matumizi ya benki na mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kufanya malipo ya huduma zitolewazo na taasisi za Wizara.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 872,703,062,000 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 jumla ya shilingi 685,860,659,133 zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 78.59 ya bajeti ya mwaka mzima, ambapo shilingi 348,938,631,450 zimetumika kulipia mishahara, matumizi mengineyo zimetumika shilingi 332,296,027,683 na fedha za maendeleo zimetumika shilingi 4,626,000,000. Katika mwaka 2016/2017, Wizara

inategemea kutumia shilingi 864,106,290,105 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

JESHI LA POLISI

26. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Jeshi la Polisi ni kulinda raia na mali zao kwa kuhakikisha nchi inakuwa na amani na utangamano, kubaini, kupeleleza na kuzuia uhalifu, kuwakamata na kuwashitaki wahalifu pamoja na kusimamia Sheria nyingine kama vile za usalama barabarani.

Udhibiti wa Uhalifu Nchini

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2015/16 Jeshi la Polisi liliendelea kulinda na kudumisha amani na utulivu uliopo nchini kwa manufaa ya ustawi wa Nchi yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa. Usalama wa raia na mali zao umeendelea kudumishwa na kutambuliwa kama miongoni mwa misingi ya ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na maendeleo binafsi ya wananchi mijini na vijijini. Kwa namna ya pekee, napenda kutumia fursa hii kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kufanya kazi kwa weledi wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani mwezi Oktoba, 2015 na mwezi Machi, 2016 na kuliletea Taifa letu heshima duniani kwa kufanya uchaguzi wa haki, huru na wa kidemokrasia. Hali hii iliwezekana kwa sababu ya uwepo wa hali ya usalama na utulivu.

28. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, Jeshi la Polisi litaanza rasmi kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) katika Mkoa wa Kipolisi Kinondoni kama sehemu ya kuboresha utendaji na kuimarisha Usalama wa nchi. Inatarajiwa kuwa mpango huu utatekelezwa nchi nzima baada ya kubaini changamoto zitakazotokana na utekelezaji huo katika Mkoa wa Kipolisi Kinondoni. Nitumie fursa hii kuomba ushirikiano mkubwa wa wadau mbalimbali hasa wananchi ili kazi hii hatimaye iweze kuleta mafanikio yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali itakamilisha taratibu za kuanzisha mfumo wa ulinzi wa raia na mali zao kwa njia ya mtandao wa kamera za usalama (*CCTV Camera*).

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017 Jeshi la Polisi litaendelea kuwapatia wananchi elimu ya ulinzi shirikishi ili waweze kuongeza ushirikiano na Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa jukumu la kupambana na uhalifu. Aidha wananchi wataendelea kuhamasishwa kuchangia juhudi za Jeshi la Polisi katika kupambana na uhalifu.

30. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, Jeshi la Polisi litaendelea kupambana na makosa yanayovuka mipaka hususani ugaidi, uharamia, biashara ya dawa za kulevya, biashara haramu ya kusafirisha binadamu, wizi wa vyombo vya moto hususani magari, wizi wa kutumia mitandao ya TEHAMA,

bidhaa bandia, biashara haramu ya silaha na uchafuzi wa mazingira. Aidha, Jeshi la Polisi litaimarisha doria, misako na operesheni maalum za nchi kavu na majini ili kupunguza matishio ya uhalifu, makosa makubwa ya jinai hususani wizi wa aina zote na unyang'anyi wa kutumia silaha. Jeshi pia litaendelea kusimamia utekelezaji wa sheria za usalama barabarani ili kupunguza idadi ya majeruhi na vifo vinavyotokana na ajali hizo.

Mauaji ya Wanawake, Wazee na Watu Wenye Ualbino

31. ***Mheshimiwa Spika,*** suala la mauaji ya wanawake, wazee na watu wenye ualbino, pamoja na kukatwa viungo kwa sababu ya imani za kishirikina vimeendelea kulitia doa Taifa letu na kutoa taswira mbaya kwa nchi yetu kitaifa na kimataifa. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 jumla ya matukio 222 ya mauaji ya wanawake na wazee yalijitokeza. Katika matukio hayo wanawake 157 na wanaume 71 waliuawa. Matukio hayo yalitokea mikoa ya; Tabora (69), Mbeya (29), Shinyanga (22), Dodoma (11), Rukwa (12), Lindi (9), Geita (13), Simiyu (8), Katavi (7), Morogoro (7), Kigoma (5), Pwani (5), Mara (4), Kagera (3), Mwanza (3), Singida (2), Arusha (8), Songwe (2), Njombe (2) na Ilala (1). Kufuatia matukio hayo watuhumiwa 135 walikamatwa na kufikishwa mahakamani kati ya hao waliofungwa 20, walioachiwa huru 15, walioshinda kesi 65 na kesi zinazoendelea 35. Katika kuhakikisha kuwa vitendo hivi vinakomeshwa Wizara yangu imeunda Kikosi Kazi Maalum kinachojumuisha vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi nyingine za haki jinai.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa vitendo vya ukatili dhidi ya ndugu zetu wenye ualbino napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa zipo dalili za kupungua kwa kiasi kikubwa kwa matukio hayo kwa miaka ya hivi karibuni. Katika kipindi cha mwaka 2015/16 hakukuwa na tukio lolote la mauaji lililoripotiwa. Aidha, matukio mawili (2) ya kujeruhiwa kwa watu wenye ualbino yalitokea katika mikoa ya Pwani (1) na Tanga (1) na mtuhumiwa mmoja (1) alikamatwa mkoani Tanga na kufikishwa mahakamani. Aidha, katika matukio ya siku za nyuma, kesi tano (5) za mauaji na mbili (2) za kujeruhi upelelezi unaendelea. Kimsingi matukio haya yanaifedhehesha nchi na hivyo tunaiomba jamii yote ione kuwa tatizo hili ni la kwetu sote na pia tunawaomba tushirikiane ili kukomesha na kuondokana kabisa na tabia hii ovu.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na vitendo hivi dhalimu dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi na mauaji ya wanawake na wazee, mwaka 2016/17 Serikali itahakikisha inafanya yafuatayo:-

i) Kuendelea kushirikiana na raia wema, Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi zinazoratibu shughuli za waganga wa jadi, kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani waganga wanaothibitika kupiga ramli chochezi na kusababisha mauaji ya wazee, wanawake na watu wenye ulemavu wa ngozi.

ii) Kuendelea kushirikiana na raia wema na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani wahalifu wanaokodishwa kufanya mauaji ya wazee, wanawake na watu wenye ulemavu wa ngozi na ukataji wa viungo vyao kwa imani potofu.

iii) Kuendelea kutumia taarifa za kiintelijensia kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani wanaotuhumiwa kutoa fedha kwa waganga wa jadi kwa lengo la kuambiwa waue ndugu zao kama mbinu na masharti ya kupata utajiri wa haraka;

iv) Kuendelea kuiimarisha Kamisheni mpya ya Intelijensia ya Jinai kwa kuongeza rasilimali watu na vitendea kazi kuanzia ngazi ya Makao Makuu hadi ngazi ya Kata/Shehia ili kujenga uwezo wa kupata taarifa za uhalifu mapema.

Udhibiti wa Madawa ya Kulevya

34. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 jumla ya kilo 141.27 za dawa za kulevya za viwandani ambazo ni *Heroin, Cocain, Cannabis resin, morphine* na *mandrax* zilikamatwa na jumla ya watuhumiwa 719 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Kati ya hao wanaume walikuwa 644 na wanawake walikuwa 75. Aidha, kilo 18,513 na gramu 415 za bhangi na kilo 15,402 za mirungi zilikamatwa ambapo watuhumiwa wanaume 9,935 na wanawake 1,020 walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi katika mwaka 2016/17 litaendeleza mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya kwa kubaini mtandao wa wahalifu wa ndani na nje ya nchi unaojihusisha na uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini kwa kushirikiana na Shirika la Polisi la Kimataifa (INTERPOL) na mashirikisho ya kipolisi ya Kanda za Kusini na Mashariki mwa Afrika (SARPCCO na EAPCCO). Pia Jeshi litaendelea kutafuta taarifa za kiintelijensia kuhusu wasafirishaji wa dawa za kulevya. Aidha, Kikosi cha kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya kitaendelea kuimarishwa kwa kukiongezea rasilimali watu na vitendea kazi, ili kiweze kuwa na uwezo wa kutosha kupambana na uhalifu huu wenye sura ya kimataifa.

Ubadilishanaji wa Taarifa za Wahalifu na Uhalifu

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuzuia uhalifu unaovuka mipaka usitokee ndani ya ardhi ya Tanzania. Ili kufikia azma hiyo na kwa ushirikiano wa vyombo hivyo, kumeanzishwa mkakati wa kupambana na uhalifu katika maeneo ya mipaka ya Tunduma, Kasumulu na Namanga. Aidha, mkakati huo utaendelezwa katika maeneo yote nchini. Katika kudhibiti usalama mipakani mbwa 350 na farasi 30 wapo kwenye vituo mbalimbali nchini ikiwemo

Himo, Rusumo, Kabanga, Mtukula, Tunduma na Namanga. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuzuia uhalifu unaovuka mipaka usitokee ndani ya ardhi ya Tanzania. Aidha, katika mipaka ya maji ikiwemo bandari na Maziwa huduma ya ulinzi wa Polisi umerudishwa ili kuboresha ulinzi na usalama katika eneo hilo muhimu kwa ustawi wa Taifa letu.

Kudhibiti Uvunjifu wa Amani unaotokana na Migogoro ya Ardhi

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi limeendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ili kuzuia mauaji, majeruhi na uharibifu wa mali unaosababishwa na migogoro ya ardhi. Kwa kushirikiana na mamlaka husika kumefanyika utafiti katika mikoa miwili Morogoro na Tanga juu ya kuimarisha usalama katika matumizi sahihi ya ardhi na jinsi ya kuigawa kwa wakulima na wafugaji. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kuzuia mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali unaosababishwa na migogoro ya ardhi.

Kushughulikia Uhalifu katika Shughuli za Kisiasa na Kijamii

38. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016 Jeshi la Polisi liliendelea kufanya kazi za ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini. Hatua hii imewezesha kuwepo kwa hali ya utulivu na Usalama katika kipindi chote cha michakato ya kisiasa kama mikutano ya vyama vya siasa na hatimaye wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015 na Uchaguzi wa Marudio Zanzibar Machi, 2016. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza wajibu wake wa ulinzi na usalama kwa ukamilifu kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi. Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi na jamii yote ya Tanzania kwa ujumla kuzingatia umuhimu wa kuwepo amani na usalama katika hatua zote. Vilevile, linawasihi viongozi na wananchi wote kujiepusha na vitendo vya aina yoyote ya uvunjifu wa amani na kushirikiana na Jeshi kwa kutoa taarifa sahihi pale dalili, viashiria au vitendo viovu vinapojitokeza.

Ulinzi wa Amani Nje ya Nchi

39. ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2015/2016 Jeshi la Polisi liliendelea kutoa mchango wake katika Operesheni za Ulinzi wa Amani *(Peace Keeping Missions)* nje ya nchi ambapo jumla ya askari 94 wa vyeo mbalimbali kati yao wanaume 78 na wanawake 16 waliruhusiwa kwenda misheni za ulinzi wa amani katika nchi za Sudan, Lebanon na Sudani Kusini. Ushiriki huu endelevu wa askari katika kazi za ulinzi wa amani nje ya nchi ni ishara na ushahidi kwamba askari wetu wanao weledi na nidhamu inayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu kupitia vyombo vya usalama

vya ndani ya Wizara itaendelea kuwaruhusu maafisa, wakaguzi na askari kutegemea ufaulu wa mitihani maalum itakayowawezesha kushiriki katika Operesheni za Ulinzi wa Amani ndani na nje ya nchi.

Ajira, Mafunzo na Upandishwaji Vyeo Askari Polisi

36. ***Mheshimiwa Spika***, kwa sasa uwiano wa askari kwa raia nchini ni askari mmoja kwa raia 1,071 kiwango ambacho hakijafikia viwango vya uwiano wa kimataifa ambavyo ni askari mmoja kwa raia 450, hali inayopelekea kuwepo haja ya kuajiri askari wapya. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 jumla ya askari polisi wapya 3,882 waliajiriwa. Aidha, jumla ya askari, wakaguzi na maafisa 4,065 wa vyeo mbalimbali walipandishwa vyeo kwa kufuata utaratibu wa ajira. Kuhusu mafunzo, jumla ya askari na maafisa 8,894 wamepatiwa mafunzo katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Jeshi la Polisi limepanga kuajiri askari wapya 3,700 na kuwapandisha vyeo askari 7,140, wakaguzi 1,325 na maafisa 991. Aidha, Serikali imeendelea kuhuisha viwango vya mishahara na posho mbalimbali ikiwemo posho ya chakula ambayo iliongezwa kutoka Shilingi 180,000/- hadi kufikia Shilingi 300,000/- kwa mwezi.

Vitendea Kazi na Makazi Kwa Askari Polisi

37. **Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto ya uchache wa miundombinu ya makazi kwa askari Polisi, Serikali kupitia mkopo kutoka Serikali ya China inakusudia kujenga nyumba 4,136 chini ya usimamizi wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi (*Tanzania Police Force Corporation Sole*). Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa miradi iliyokwishaanzishwa siku za nyuma, miradi hiyo ni nyumba za makazi ya askari Mabatini - Mwanza za familia 24, Buyekera - Kagera familia 12, Musoma - Mara familia 24 na Ludewa - Njombe familia 12. Jengo la ofisi ya Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, ujenzi wa kituo cha Polisi Mkokotoni – Zanzibar, kituo cha Polisi Mtambaswala – Mtwara na kituo cha polisi Ludewa – Njombe. Serikali imeendelea kuliongezea Jeshi la Polisi vitendea kazi yakiwemo magari, pikipiki na vyombo vya mawasiliano ili kuongeza ufanisi.

Usimamizi wa Nidhamu za Askari

38. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/2016 hatua za kinidhamu ziliendelea kuchukuliwa kwa maafisa, wakaguzi na askari polisi waliobainika kujihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili mema ya Jeshi la Polisi. Jumla ya askari na maofisa 207 walishtakiwa kijeshi, 118 walipewa adhabu ya kufukuzwa kazi na 19 walifikishwa mahakamani. Aidha, maofisa 24, wakaguzi 11 na askari 54 wa vyeo mbalimbali waliandikiwa barua za onyo. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Jeshi la Polisi litaongeza umakini katika kusimamia nidhamu kwa askari wake na kufanya uchambuzi wa kina (vetting) kwa

kuchukua vijana waliomaliza mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa wanaoomba kujiunga na Jeshi la Polisi ili kuwa na askari wenye nidhamu na moyo wa dhati wa kulitumikia Taifa kwa ujumla.

Tuzo na Zawadi kwa Askari

39. ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi liliendelea kutoa tuzo, motisha na zawadi kwa askari waliotekeleza majukumu yao kwa umahiri mkubwa. Katika mwaka 2015/2016 Jeshi la Polisi limetoa tuzo na zawadi kwa watumishi 201 walioonyesha ubunifu, ujasiri, uadilifu, uaminifu na utendaji mzuri wakiwemo askari 152, wakaguzi 17, maofisa 12, watumishi raia 10 na wadau wengine 10. Jeshi la Polisi litaendelea kuwatambua maafisa, wakaguzi, askari na watumishi raia wanaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa na kuwapa tuzo na zawadi stahiki.

JESHI LA MAGEREZA

40. ***Mheshimiwa Spika***, jukumu la msingi la Jeshi la Magereza ni kuwahifadhi wafungwa na mahabusu wa aina zote pamoja na kuwarekebisha tabia waliohukumiwa vifungo. Urekebishaji wa tabia za wafungwa unafanyika kupitia programu za mafunzo kwa njia ya vitendo katika miradi ya kilimo, ufugaji, viwanda vidogo vidogo na ujenzi.

Usafirishaji wa Mahabusu kwenda Mahakamani na Kurudi Magerezani

41. ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu la kuwasindikiza mahabusu kwenda mahakamani na kurudi Gerezani linaendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Wilaya ya Arusha mjini na Wilaya ya Dodoma mjini. Utaratibu huu umesaidia mahabusu kusikilizwa kesi zao na kupata haki za kisheria kwa wakati. Katika mwaka 2016/2017 Serikali itaendelea kuboresha huduma za usafirishaji wa mahabusu kwenda mahakamani na kurudi magerezani.

Programu za Urekebishaji wa Wafungwa

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza limeendelea kutekeleza programu za urekebishaji wa wafungwa magerezani kwa kuwapa stadi katika kilimo, ufugaji, viwanda vidogo vidogo na ujenzi. Kwa upande wa kilimo urekebishaji huo unaenda sambamba na utumiaji wa zana bora za kilimo, matumizi bora ya ardhi na pembejeo. Aidha, yalifanyika matengenezo ya matrekta katika Magereza ya Babati – Manyara, Ushora – Singida, Karanga – Kilimanjaro, Ngwala – Mbeya, Nachingwea – Lindi, Kongwa – Dodoma na Matongo – Simiyu. Malengo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kuendeleza mafunzo ya kilimo cha kisasa katika Magereza yote ya kilimo nchini.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Jeshi la Magereza liliendelea na jukumu la urekebishaji wa wafungwa kwa kuwapa stadi mbalimbali kupitia ufugaji wa ng'ombe wa nyama 8,830 na ng'ombe wa maziwa 2,573 pamoja na mifugo mingine. Huduma mbalimbali za mifugo ziliboreshwa kama vile chanjo na dawa za tiba na huduma za kuogeshea mifugo kwenye Magereza yote yaliyo na mifugo. Aidha, huduma za uhamilishaji (artificial insermination) wa mifugo ziliendelea kuboreshwa kwenye Magereza ya Ubena – Pwani, Kingolwira na Mbigiri – Morogoro, King'ang'a – Dodoma, Mugumu – Mara, Kitengule - Kagera, Kilimo Urambo – Tabora na Gereza Arusha. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Jeshi la Magereza linatarajia kuhudumia jumla ya ng'ombe wa nyama 9,500 na ng'ombe wa maziwa 3,200, mbuzi 3,400 pamoja na wanyama wengine wadogo wadogo kwa lengo la kutekeleza jukumu la msingi la urekebishaji wa wafungwa.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha shughuli za viwanda vidogo vidogo magerezani, Jeshi linakamilisha kazi ya kufunga mashine moja (1) ya ukamuaji wa mafuta ya mawese katika Kiwanda cha Mafuta Kambi Kimbiji - Dar es Salaam pamoja na kufanya ukarabati wa pampu ya maji katika Kiwanda cha Chumvi kilichopo Gereza la Lindi.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Jeshi la Magereza litaendelea na uimarishaji wa viwanda vidogo vidogo vya useremala, ushonaji, utengenezaji wa mazulia, ufumaji n.k vilivyopo katika Magereza mbalimbali nchini kwa kuvipatia nyenzo na malighafi ili viendelee kutekeleza jukumu la msingi la kuwarekebisha wafungwa endapo hali ya raslimali fedha itaruhusu.

Mafunzo kwa Maafisa, Askari na Watumishi Raia

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Jeshi la Magereza limeendelea pia kutoa mafunzo mbalimbali ndani na nje ya Jeshi kwa ajili ya maafisa, askari na watumishi raia. Mafunzo hayo ni yale yanayohusu uendeshaji wa Magereza na yale yanayohusu taaluma mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukihuisha Chuo cha Maafisa wa Magereza Ukonga kuwa Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji. Kwa upande wa mafunzo, jumla ya maafisa, askari na watumishi raia 3,076 wanaendelea na mafunzo katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya vyuo vya Magereza. Mafunzo haya yataongeza weledi na kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi hao kiasi cha kuwezesha kuboresha utendaji wa Jeshi la Magereza katika utoaji wa huduma kwa wananchi na pia kusimamia vema programu za urekebishaji wa wafungwa magerezani. Mwaka wa fedha 2016/2017, Jeshi la Magereza linatarajia kutoa mafunzo kwa maafisa na askari 4,975 katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na yale ya Taaluma ya Urekebishaji.

Upanuzi, Ukamilishaji, Ukarabati na Ujenzi wa Mabweni ya Wafungwa

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016, lengo lilikuwa ni kuendeleza ujenzi wa jiko na bweni moja la wafungwa Gereza Segerea – Dar es Salaam ambalo ujenzi wake upo katika hatua za msingi. Kazi nyingine ilikuwa ni kukamilisha ujenzi wa Hospitali iliyopo Gereza la Segerea na pia kukamilisha ujenzi wa Gereza Maalum Isanga ili lianze kutumika. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, nguvu zitaelekezwa katika ujenzi wa mabweni 16 ya kulala wafungwa katika Magereza ya Mahabusu Sumbawanga – Rukwa, Nzega – Tabora, Ushora – Singida, Biharamulo – Kagera, Babati – Manyara, Ngudu – Mwanza, Tarime – Mara, Mahabusu Shinyanga, Kahama Shinyanga, Segerea - Dar es Salaam na Ruanda - Mbeya. Kuanza ujenzi wa jengo la utawala Gereza Chato – Geita, kufanya ukarabati wa mabweni 59 ya wafungwa katika Magereza ya Karanga – Kilimanjaro, Mahabusu Morogoro, Mahabusu Tabora – Tabora, Handeni – Tanga, Lindi na Kilosa – Morogoro, kukamilisha ujenzi wa Hospitali iliyopo Gereza Segerea – Dar es Salaam pamoja na kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa mabweni saba (07) ya kulala wafungwa katika Magereza ya Chato – Geita, Biharamulo – Kagera, Mpwapwa – Dodoma, Kambi Mkoka – Dodoma, Mahabusu – Urambo, Rombo – Kilimanjaro na Mkuza – Pwani.

Kilimo cha Umwagiliaji

47. ***Mheshimiwa Spika***, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 sehemu kubwa ya mradi wa umwagiliaji Gereza Idete – Morogoro imekamilika. Hata hivyo, ukamilishaji wa mradi huu ulikwama baada ya mfereji mkuu kuharibiwa na mvua kubwa. Tayari marekebisho yamefanyika na sasa mradi huo utakamilika katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa kuanza umwagiliaji katika eneo la ekari 2,500.

Shirika la Magereza

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Magereza limeendelea na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo na viwanda vidogo vidogo. Kwa upande wa kilimo, eneo la ekari 4,750 limelimwa kwa matarajio ya kuvuna tani 5,557.5 za mazao mbalimbali, sawa na ongezeko la asilimia 7 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, Shirika kupitia Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Magereza limeendelea kufanya kazi mbalimbali za ujenzi wa majengo ya watu binafsi na Taasisi za Serikali zikiwemo maandalizi ya ujenzi wa Ofisi ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ufundi - Dodoma, ukarabati wa baadhi ya majengo yaliyopo katika eneo la Bunge – Dodoma, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Wizara ya Maliasili na Utalii – Dar es Salaam pamoja na paa la jengo la kuhifadhi vifaa lililopo Polisi Kilwa Road – Dar es Salaam. Matarajio ya mwaka wa fedha 2016/2017 ni kuongeza shughuli za uzalishaji kwa kuingia ubia na wawekezaji wa

ndani na nje ya nchi ili kupata mtaji wa kutosha kuweza kukidhi soko la bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo, samani za ofisi, samani za nyumbani, bidhaa za ngozi na shughuli za ujenzi ambazo zinaendelea kupanuka.

Matumizi ya Nishati Mbadala Magerezani

49. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na matumizi makubwa ya kuni Magerezani na hivyo kuweko na uharibifu wa mazingira, Jeshi la Magereza limeendelea kuchukua hatua za kuanza matumizi ya gesi itokanayo na tungamotaka *(biogas)* na majiko banifu kama nishati mbadala kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa magerezani. Matumizi ya gesi itokanayo na tungamotaka yanaendelea katika Gereza Ukonga na gesi asilia (natural gas) katika Gereza Keko. Kwa sasa, Jeshi limeanza kutumia majiko yanayotumia kuni kidogo (energy saving stoves) ambayo yameanza kutumika katika Gereza Karanga na Mwanga – Kilimanjaro, Kibondo na Bangwe – Kigoma na Sumbawanga – Rukwa. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Jeshi litaendelea kueneza matumizi ya majiko banifu na gesi asilia katika Magereza mengine yenye matumizi makubwa ya kuni kadri uwezo wa fedha utakavyoruhusu.

Utunzaji na Hifadhi ya Mazingira

50. ***Mheshimiwa Spika,*** utunzaji wa mazingira ni miongoni mwa shughuli za kila siku za Jeshi la Magereza. Shughuli za kuandaa vitalu vya miche na upandaji miti zinaenda sambamba na maandalizi ya msimu wa kilimo kwa kila kituo. Katika kuadhimisha siku ya upandaji miti kitaifa tarehe 1 Aprili, 2015 ilipandwa jumla ya miti 223,160 katika Magereza yote nchini. Aidha, Mradi wa Hifadhi ya Mazingira na Upandaji Miti ambao unatekelezwa na Jeshi la Magereza kwa ufadhili wa *Tanzania Forest Fund* katika Magereza ya Mgagao na Isupilo – Iringa, Kambi Ihanga – Njombe na Mkwaya – Ruvuma una jumla ya miti 1,000,000. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, lengo litakuwa ni kuendeleza juhudi zaidi za upandaji miti katika Magereza mengine yaliyoingizwa katika mpango huo ambayo ni Magereza ya Msalato - Dodoma, miti 100,000 Bariadi - Simiyu miti 323,451 na Ngudu – Mwanza miti 157,178 kwa nia ya kuhifadhi mazingira. Magereza mengine nchini yataendelea kupanda miti kwa njia ya kujitegemea kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

IDARA YA UHAMIAJI

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji ina jukumu la msingi la kudhibiti uingiaji na utokaji wa raia na wageni ili kuhakikisha usalama unadumishwa na maslahi ya Taifa kijamii, kisiasa na kiuchumi yanazingatiwa pamoja na kuratibu maombi ya uraia kwa wageni wanaoomba uraia wa Tanzania.

Hali ya Ulinzi na Usalama Mipakani

52. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi, 2016 Idara ya Uhamiaji iliendelea kutoa huduma kwa kufuata sheria na kanuni za kiuhamiaji kwenye mipaka kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya wageni 1,187,490 waliingia ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo wageni 1,005,652 waliingia nchini ikiwa ni ongezeko la asilimia 18. Katika kipindi hicho jumla ya wageni 1,199,995 walitoka nchini ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo wageni 892,614 walitoka nchini ikiwa ni ongezeko la asilimia 34.

Misako, Doria na Ukaguzi

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki cha Julai 2015 hadi Machi, 2016 Idara ya Uhamiaji iliendelea kufanya misako, doria na ukaguzi katika sehemu mbalimbali kama vile mipakani, migodini, viwandani, mahotelini, kwenye mashamba makubwa na kwingineko kwa lengo la kudhibiti wahamiaji haramu nchini na biashara haramu ya usafirishaji binadamu. Jumla ya watuhumiwa wa uhamiaji haramu 6,600 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria, ikilinganishwa na wahamiaji haramu 3,944 waliokamatwa katika kipindi hiki mwaka jana. Aidha, vinara tisa (9) raia wa kigeni wanaojihusisha na mtandao wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu walikamatwa, kuchukuliwa hatua za kisheria na hatimaye kufukuzwa nchini na Watanzania saba (7) wanaojihusisha na mtandao huo kesi zao zipo mahakamani. Aidha, katika kipindi hiki Watanzania waliokwenda nje ya nchi kinyume na Sheria za Uhamiaji (stowaways) 120 walirudishwa nchini toka nchi mbalimbali.

Vibali Vilivyotolewa kwa Wageni Wakaazi

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji imetoa vibali vya ukaazi kwa wageni wawekezaji na wengine waliopata ajira katika makampuni mbalimbali na walioingia nchini kwa malengo mbalimbali kwa kufuata sheria na taratibu za kiuhamiaji kulingana na madhumuni ya ukaazi wao nchini. Jumla ya wageni 12,584 wamepewa vibali vya ukaazi kwa mchanganuo ufuatao: - Kibali Daraja "A"1152, Kibali Daraja "B" 7,709 na Kibali Daraja "C" 3,723. Aidha, katika kipindi hiki jumla ya Hati za Mfuasi 1,896 na Hati za Msamaha 3,162 zilitolewa.

Pasipoti na Hati nyingine za Safari

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016, Idara ya Uhamiaji imetoa jumla ya pasipoti 85,758 kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali. Kati ya hati hizo, Pasipoti za kawaida 84,380, Afrika Mashariki 752, Pasipoti za Kibalozi 410, Pasipoti za Kiutumishi 216 na Hati za Dharura 89,565.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mnamo tarehe 02 mwezi Machi mwaka 2016 Viongozi Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walizindua pasipoti za kielektroniki za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zenye ubora unaokidhi viwango vya Kimataifa na zitatumika kusafiria duniani kote tofauti na pasipoti za Afrika Mashariki zilizopo sasa. Pasipoti hizo zinakusudiwa kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Januari, 2017. Pasipoti zinazotumika sasa za nchi wanachama zitafikia ukomo wa matumizi mwezi Disemba, 2018. Aidha, Serikali itakamilisha taratibu za kuanzisha mfumo wa utoaji wa huduma za uhamiaji kwa njia ya mtandao (*e-immigration*).

Wageni Walioomba na kupewa Uraia wa Tanzania

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 wageni 405 walipewa uraia. Wageni waliopewa uraia ni kutoka India (238), Kenya (22), Somalia (11), Uingereza (6), Italia (1), Rwanda (4), Yemeni (49), Burundi (11), Congo (4), China (1), Ujerumani (1), Zambia (1), Pakistani (28), Uganda (2), Saudi Arabia (6), Iran (1), Belarus (3), Afrika ya Kusini (1), Sierra-Leone (1), Australia (1), Zimbabwe (1), Lebanon (1), Marekani (1) na watu wasiokuwa na Utaifa (10).

Watanzania waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Watanzania 44 waliukana uraia baada ya kujipatia Uraia wa Mataifa mengine kama ifuatavyo; Ujerumani (18), Australia (1), Norway (9), Afrika ya Kusini (3), Zambia (1), Namibia (2), Sweden (1), Kenya (1), Canada (2), Denmark (2) na Uingereza (4) hivyo kupoteza hadhi ya kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Sura ya 357 Rejeo la 2002.

Ajira na Mafunzo

58. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Idara ya Uhamiaji imepata kibali cha kuajiri askari wapya 1,000 ambapo askari 298 wapo katika mafunzo ya awali ya Uhamiaji katika Chuo cha Polisi Moshi wakati inaendelea na utaratibu wa kuajiri askari wapya 702. Kadhalika, Idara imeajiri watumishi raia 72. Katika kuwajengea uwezo watumishi askari 156 na watumishi raia 20 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi wakati askari 193 na watumishi raia 16 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi.

Vitendea kazi, Majengo ya Ofisi na Makazi ya Askari

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji inaendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi ambapo upo katika hatua mbalimbali katika mikoa ya

Manyara, Pwani, Geita, Mtwara na Lindi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Idara ya Uhamiaji inatarajia kuanza ujenzi wa ofisi katika Wilaya ya Ileje - Mbeya na Kituo cha Kirongwe wilayani Rorya mkoani Mara. Aidha, Idara ya Uhamiaji inatarajia kufanya ukarabati wa majengo ya Chuo cha Uhamiaji – Moshi na jengo la Makao Makuu – Dar es Salaam. Kwa upande wa Zanzibar Idara ya Uhamiaji inaendelea na ujenzi wa nyumba za makazi ya askari katika eneo la Ndugukitu – Chakechake Pemba na ukarabati unaendelea katika Afisi za Uhamiaji Mkoa wa Kaskazini unguja, Wilaya ya Micheweni Pemba, Kaskazini Pemba na katika Afisi ya Mjini Magharibi ukarabati umekamilika. Katika kujiimarisha kiutendaji Idara ya Uhamiaji imekamilisha taratibu za kununua magari 16 na pikipiki 57.

Makazi ya Askari

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Idara ya Uhamiaji imeendelea na ujenzi wa nyumba za viongozi katika mikoa ya Kigoma na Mwanza. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/17 Idara ya Uhamiaji itamalizia ujenzi wa nyumba ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji na kuanza ujenzi wa nyumba za makazi ya askari huko Kisongo mkoani Arusha na ukarabati wa nyumba za makazi ya watumishi mkoani Tabora.

JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kufanya ukaguzi wa tahadhari na majanga ya moto kwenye maeneo mbalimbali, kuzima moto, kuokoa maisha na mali kwenye majanga ya moto na majanga mengineyo, pamoja na kuelimisha umma juu ya tahadhari ya moto na kinga ya moto na majanga mengineyo ambayo yanaweza kulikumba Taifa letu.

Hali ya vituo vya Zimamoto na Uokoaji Nchini

62. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na uokoaji linahitaji jumla ya vituo 152 Tanzania Bara. Kwasasa Jeshi lina vituo 57, kati ya vituo hivyo 38 vipo katika miji na 19 vipo katika viwanja vya ndege. Huu ni upungufu wa vituo 95 hali inayosababisha maeneo mengi kukosa huduma za zimamoto na uokoaji. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Jeshi linategemea kujenga kituo 1 cha zimamoto na uokoaji katika eneo la Kigamboni Jiji la Dar es Salaam na kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu lililopo TAZARA - Mchicha jijini Dar es Salaam. Aidha, Jeshi lina magari ya kuzima moto 56 yenye ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Jeshi linatarajia kununua magari mawili (2) ya kuzimia moto ili kuendelea kuboresha huduma za zimamoto na Uokoaji nchini. Jeshi litaendelea kununua magari ya zimamoto kadri hali ya bajeti itakavyoruhusu.

Ukaguzi wa Tahadhari na Kinga Dhidi ya Moto na Majanga

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limefanya ukaguzi wa jumla ya maeneo 39,697 kati ya lengo la ukaguzi wa maeneo 63,500. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepanga kukagua jumla ya maeneo 101,920 Tanzania Bara katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha.

Matukio ya Moto na Majanga Mengine

64. ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuanzia Julai, 2015 hadi kufikia Machi, 2016 limeshiriki kuzima moto katika matukio 517 Tanzania Bara, ikiwemo moto uliotokea hivi karibuni katika Shule ya Sekondari Iyunga mkoani Mbeya pamoja na moto uliotokea katika soko wilayani Masasi. Vile vile, Jeshi limefanya maokozi katika matukio 245 kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kushiriki katika maokozi ya watu 5 waliofukiwa na kifusi katika mgodi wa Nyangarata, Wilaya ya Kahama, maokozi ya watu 554 katika Kijiji cha Pawaga na watu 104 katika Kijiji cha Mbuyuni katika mafuriko mkoani Iringa. Aidha, kulifanyika maokozi ya watu na mali zao katika ajali ya kuzama kwa kivuko katika mto Kilombero.

Mafunzo

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na juhudi mbalimbali ya kuwapatia mafunzo askari na maafisa wake kwa lengo la kuboresha utendaji katika majukumu yake. Katika mwaka wa fedha 2015/16 askari na watumishi raia wamepatiwa mafunzo katika maeneo mbalimbali ikiwemo mafunzo ya ndani na nje ya nchi. Katika mafunzo ya ndani ya nchi, askari na watumishi raia 24 wamepatiwa mafunzo kama ifuatavyo; Stashahada 7, Shahada 8 na Shahada ya Uzamili 8 na katika mafunzo ya nje ya nchi, afisa mmoja anapatiwa mafunzo ya namna ya kufanya uchunguzi wa moto nchini Uingereza. Aidha, askari 481 walioajiriwa mwezi Januari, 2016 walipatiwa mafunzo ya uaskari na namna ya kukabiliana na majanga ya moto pamoja na uokoaji. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Jeshi litaendelea kutoa mafunzo kwa askari na watumishi raia mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi.

Chuo cha Zimamoto na Uokoaji

66. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupata ufanisi wa mafunzo ya zimamoto na uokoaji Jeshi lilipewa eneo iliyokuwa Kambi ya Wakimbizi Chogo, wilayani Handeni mkoani Tanga na hivyo kuhamisha Chuo chake kilichokuwa Dar es Salaam. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/16, askari 157 wamepelekwa katika chuo hicho kuhudhuria mafunzo ya uongozi. Katika mwaka wa fedha

2016/17 Jeshi linalenga kuimarisha miundombinu ya Chuo hicho ili kiweze kukidhi mahitaji ya mafunzo.

Kuimarisha Vitendea Kazi

67. ***Mheshimiwa Spika,*** mahusiano mazuri kati ya nchi yetu na nchi mbalimbali yamepelekea Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupata misaada mbalimbali ikiwemo vitendea kazi na mafunzo. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Jeshi limepata msaada wa jumla ya magari ya kuzima moto na maokozi 24. Kati ya hayo Japan imetoa magari 23 yakiwemo magari makubwa manne ya kuzima moto na magari mengine 19 *pumper* kwa ajili ya kuzimia moto mahali palipo na visima (fire hydrants). Aidha, Ujerumani imetoa gari moja la maokozi. Pia, Jeshi limepata msaada wa vifaa mbalimbali vya kuzimia moto pamoja na boti 3 kwa ajili ya maokozi kutoka Austria. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara itaendeleza juhudi za kuimarisha na kuboresha huduma za zimamoto na uokoaji.

Elimu kwa Umma

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna ya kukabiliana na majanga mbalimbali ya moto katika masoko, Taasisi za Elimu na kupitia vyombo vya habari ikiwemo luninga, redio, magazeti na matangazo kupitia magari ya Zimamoto na Uokoaji. Katika mwaka wa fedha, 2016/2017 Jeshi la Zimamoto litaendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa lengo la kupunguza majanga ya moto nchini.

HUDUMA KWA JAMII

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Probesheni na Huduma kwa Jamii ambayo inasimamia utekelezaji wa adhabu mbadala wa kifungo gerezani, chini ya Sheria ya Probesheni Sura ya 247 na Sheria ya Huduma kwa Jamii Sura ya 291 hivi sasa inatekeleza Programu hizo kwenye Wilaya 63 za Mikoa 21 ya Tanzania Bara. Kuanzia Julai, 2015 hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya Taarifa za Uchunguzi wa Kijamii 1,601 ziliandaliwa na kuwezesha wafungwa 1,253 kuingizwa kwenye programu hii ambapo wanaume ni 1,117 na wanawake ni 136. Miongoni mwa wafungwa hao, 71 wametumikia adhabu ya Probesheni na wafungwa 1,182 wametumikia adhabu ya Huduma kwa Jamii kwa kufanya kazi za kijamii, hivyo kupunguza msongamano katika magereza na gharama za uendeshaji katika magereza na vile vile taasisi wanazofanyia kazi. Aidha, wafungwa 656 wamemaliza adhabu zao katika kipindi hicho. Pamoja na changamoto zilizojitokeza, bado azma ya Wizara ya kuongeza mikoa miwili iko palepale kwa mwaka wa fedha 2016/17. Lengo ni kuendelea kuimarisha

matumizi ya adhabu mbadala wa kifungo nchini ili kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani.

HUDUMA KWA WAKIMBIZI

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Huduma kwa Wakimbizi ina jukumu la msingi la kuwapokea, kuwahifadhi, kuratibu huduma kwa wakimbizi wawapo nchini na kushiriki juhudi za kupata suluhisho la kudumu la tatizo la wakimbizi. Utekelezaji wa jukumu hili la kuhudumia wakimbizi wawapo nchini hushirikisha vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na wadau wengine wa kimataifa wakiongozwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR).

71. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu kwa miaka ya karibuni ilishuhudia kupungua kwa idadi ya wakimbizi hata kufikia hatua ya kubakia na kambi moja tu ya Wakimbizi ya Nyarugusu. Hata hivyo, kuanzia mwezi Aprili, 2015 tulianza tena kupokea wimbi jipya la wakimbizi kutoka Burundi baada ya kuzuka mgogoro wa kisiasa nchini humo. Kutokana na ujio wa wakimbizi hao Serikali ilianzisha upya kambi tatu za wakimbizi ambazo ni Nduta iliyoko wilayani Kibondo, Mtendeli na Karago zilizoko wilayani Kakonko, mkoani Kigoma.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** awali wakimbizi wote wa Burundi walikuwa wanahifadhiwa kwa muda katika kambi ya Nyarugusu, ila kwa sasa wanahamishiwa katika kambi za Nduta na Mtendeli wakati utaratibu wa kujenga miundombinu ya kambi ya Karago unaendelea. Aidha, idadi ya wakimbizi inazidi kuongezeka siku hadi siku, na kupelekea kuwa na idadi ya wakimbizi wote ambao wanahifadhiwa nchini hadi tarehe 31 Machi, 2016 kufikia 232,215 kama inavyonyeshwa katika majedwali Na. 1 na Na. 2 ya Hotuba hii.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** ifahamike kuwa miongoni mwa watu waliokimbilia nchini kutafuta hifadhi ya ukimbizi ni pamoja na wapiganaji ambao walikuwa wanaendesha harakati katika nchi zao za asili. Wale wanaobainika kuwa walikuwa ni wapiganaji wamekuwa wanatengwa na kupelekwa kwenye kituo maalum kilichoanzishwa kwa ajili hiyo ambacho ni Gereza Mwisa lililoko Kitengule- Karagwe mkoani Kagera. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 kulikuwa na wakimbizi wa aina hiyo 58 katika Gereza Mwisa.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeimarisha taratibu za upekuzi wa wakimbizi wapya ili kuzuia uwezekano kwa wapiganaji hao kupenyeza silaha na milipuko. Aidha, ulinzi umeimarishwa katika kambi za wakimbizi na katika maeneo yanayozunguka kambi hizo, ikiwa ni pamoja na kufanya doria za mara kwa mara kwenye barabara kuu za maeneo hayo. Lengo ni kuzuia vitendo vya kihalifu, kuzagaa kwa silaha na wakimbizi kwenye vijiji vinavyozunguka makambi ya wakimbizi. Hivyo basi, wananchi na viongozi wanaoishi maeneo ya mipakani hususani kwenye mpaka wa Burundi wanaaswa kutoa taarifa za uwepo wa

wageni ama wakimbizi ili Serikali ifanye taratibu muafaka za kuwapeleka kwenye maeneo yaliyotengwa kwa madhumuni hayo au kuchukua hatua stahiki dhidi yao.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** kama inavyofahamika, ujio wa wimbi kubwa la wakimbizi nchini unasababisha uharibifu wa mazingira kwani wakimbizi hao wanalazimika kukata miti kwa ajili ya kupata fito za kujengea na kutumia kuni kama nishati ya kupikia. Serikali ilichukua hatua mbalimbali ili kuhifadhi mazingira kwa kuainisha na kuratibu shughuli za ukataji miti na upatikanaji wa kuni, kuhamasisha upandaji wa miti na utunzaji wa mazingira, na kusisitiza matumizi ya majiko sanifu. Pamoja na hatua hizo, Serikali imeiomba Jumuiya ya Kimataifa kupitia UNHCR kufanya jitihada za makusudi kuwezesha kupatikana nishati mbadala ya kupikia badala ya matumizi ya kuni. UNHCR imeahidi kuisaidia Serikali ya Tanzania katika suala hili. Wakimbizi kwa upande wao, wanaelekezwa kutunza mazingira yaliyomo ndani ya kambi na maeneo yanayozunguka kambi hizo. Serikali itachukua hatua kwa wale watakaobainika kuharibu mazingira ama kuvamia maeneo ya hifadhi yaliyotengwa ambayo yanapakana na kambi zao.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya hatua zinazochukuliwa kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la idadi kubwa ya wakimbizi nchini ni kuwahamishia watu hao katika nchi ya tatu. Katika kutekeleza suala hilo, Serikali yetu na Serikali ya Marekani zinaendelea kutekeleza mpango maalum wa kuwahamishia nchini Marekani wakimbizi wenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wapatao 32,000 wanaoishi katika kambi ya Nyarugusu ambako kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2015 hadi tarehe 31 Machi, 2016 wakimbizi 2,284 walikuwa wameshapelekwa nchini humo. Wapo pia wakimbizi 242 waliohamishiwa kwenye nchi za Australia, Kanada, Uingereza, Sweden, Ubeligiji na Ireland. Aidha, ujenzi wa kituo kitakachotumika katika kufanikisha mradi wa kuwapeleka wakimbizi nchini Marekani katika kijiji cha Makere, Kasulu unaendelea.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa utangamanisho (*local integration*) wa raia zaidi ya 162,000 wenye asili ya Burundi waliokuwa wakimbizi na ambao wameruhusiwa kuishi kwenye maeneo ya Katumba, Mishamo na Ulyankulu. Awali, Benki ya Dunia iliishauri Serikali ya Tanzania kuchukua mkopo toka Taasisi hiyo ili utumike kutekeleza baadhi ya miradi itakayoanzishwa kwa kusudio hilo. Kwa sasa Serikali inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia kuhusu ushauri huo. Hata hivyo, Serikali inaiomba Jumuiya ya Kimataifa kutimiza wajibu wake wa kuchangia rasilimali (*principle of burden sharing*) zinazohitajika kuwawezesha raia hao kuwa sehemu ya jamii inayowazunguka. Baadhi ya Mashirika ya Kimataifa chini ya mwamvuli wa *Solution Alliance* yameonesha nia ya kuchangia katika eneo hilo, na Wizara yangu inaendelea kuratibu juhudi hizo.

MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inalo jukumu la kuwatambua, kuwasajili na kuwapa Vitambulisho vya Taifa raia, wageni wakaazi na wakimbizi wanaostahili, pamoja na kutunza kanzidata kwa ajili ya matumizi ya taarifa hizo katika huduma mbalimbali za mipango ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii, ulinzi na usalama.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanasajiliwa na kutambuliwa ili kupatiwa Vitambulisho vya Taifa mapema iwezekanavyo. Aidha, kutokana na umuhimu wa mradi huu wa Vitambulisho vya Taifa, Serikali itaendelea kuiwezesha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kwa kadri iwezekanavyo ili iweze kukamilisha jukumu hilo muhimu kwa wakati.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/16 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, imefanikiwa kutekeleza kazi muhimu zilizopangwa ikiwemo kuendelea na zoezi la kusajili na kutambua wananchi katika mikoa ambayo imefungua ofisi. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Ruvuma na Mikoa yote ya Zanzibar. Mamlaka imeandaa mpango kazi wa kukamilisha lengo la Usajili na Utambuzi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar ifikapo mwishoni mwa mwezi Disemba, 2016.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeanza ujenzi wa kituo kikuu cha uchakataji, uzalishaji na utunzaji wa kumbukumbu katika Mkoa wa Pwani na ujenzi wa kituo cha kujikinga na majanga mkoani Morogoro, sambamba na ujenzi wa ofisi za usajili katika Wilaya za Temeke, Ilala, Kinondoni, Morogoro Mjini, Nyamagana, Ilemela, Kwimba, Magu, Arusha Mjini, Arumeru na Longido kwa Tanzania Bara na Dunga kwa upande wa Zanzibar. Ujenzi huu unafanywa kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Korea Kusini.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuipunguzia gharama Serikali, Wizara yangu imeomba na kupewa vifaa vya usajili (BVR) 5,000 vilivyotumiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wakati wa uboreshaji na uandikishaji wa wapiga kura ili viweze kutumiwa na NIDA katika kufanya usajili na utambuzi wa wananchi katika mikoa yote ambayo wananchi wake hawajasajiliwa. Vilevile itatumia kanzidata ya NEC yenye taarifa za wananchi wapatao milioni 22 katika mchakato wa awali wa kuandaa Vitambulisho vya Taifa. Hatua hii itasaidia kuongeza kasi ya kazi ya usajili na utambuzi na hivyo kukamilisha zoezi kwa muda mfupi.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika mwaka 2016/17 inalenga kuwasajili Watanzania milioni 22 katika

mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na kupewa Vitambulisho vya Taifa, kuhakikisha kwamba mtandao wa mawasiliano kati ya ofisi za Wilaya na Makao Makuu unakamilika ili kurahisisha utumiaji wa taarifa za wananchi kutoka Wilayani, kuendeleza ujenzi wa kituo cha Uchakataji, Uzalishaji na Utunzaji Kumbukumbu (*Data Center*), Kituo cha Uokozi wa Majanga (*Disaster Recovery Center*) na ofisi za usajili za wilaya, kuendelea kuelimisha umma juu ya umuhimu wa Vitambulisho vya Taifa na matumizi yake ya kila siku katika dhana nzima ya utambuzi, kukamilisha Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, kupata vitendea kazi vya kutosha ikiwemo magari 30 maalum kwa ajili ya usajili, vifaa vya kugawia vitambulisho (Portable Card Issuance Device) 500, vifaa vya kusomea vitambulisho 700 na kompyuta 302 kwa ajili ya ofisi 151 za usajili katika wilaya zote nchini.

UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya watumishi ndani ya vyombo vya Wizara pamoja na wananchi wanaolalamikia utendaji wa vyombo hivyo. Aidha, Wizara inayafanyia uchunguzi malalamiko hayo ili kuhakikisha inayapatia ufumbuzi kwa wakati.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Wizara kupitia Idara ya Kushughulikia Malalamiko ilipokea jumla ya malalamiko 238 yanayohusu utendaji kazi wa vyombo vya kijeshi ndani ya Wizara kutoka kwa wananchi kupitia njia ya barua, simu, barua pepe, nukushi pamoja na mahojiano ya ana kwa ana. Kati ya malalamiko hayo, 138 yalipatiwa ufumbuzi na wahusika kujulishwa na mengine 100 yako katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara itaendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi na watumishi wa Wizara pamoja na kufanya uchunguzi wa kina.

VITA DHIDI YA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI WA BINADAMU

86. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya ripoti mbalimbali za kitaifa na kimataifa kuitaja Tanzania kama chanzo (*origin*), njia ya kupitishia (*transit*) na kituo cha mwisho (*destination*) kwa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, Wizara yangu ilianzisha Sekretarieti ya Kupambana na Kudhibiti Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu kwa lengo la kudhibiti biashara hii.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekretarieti ya Kupambana na Kudhibiti Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu ilifanya ufuatiliaji katika makampuni yanayofanya biashara za starehe za usiku (*night clubs/casinos*) ambazo huingiza wasichana kutoka nchi za India, Nepal na Pakistani ili kudhibiti biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Katika

ufuatiliaji huo, wamiliki wa makampuni 5 na wasichana 57 walihojiwa bila kubaini dosari yoyote. Hata hivyo, uchunguzi unaendelea ili kujiridhisha na uhalali wa ajira zao. Kwa upande wa Watanzania wasichana 31 walizuiliwa Hati na Nyaraka zao za kusafiria kwa lengo la kufanya uchunguzi ili kubaini mtandao wa wasafirishaji haramu wa binadamu. Aidha, msichana mmoja aliteremshwa kutoka ndani ya ndege akiwa tayari kwenda Uarabuni kufanya kazi za ndani baada ya kupata taarifa kwamba anasafirishwa kinyume cha utaratibu.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/2017 Sekretarieti, imejipanga kufanya ufuatiliaji *(monitoring)* na uchunguzi wa wazi *(public inquiries)* juu ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu na utoaji wa elimu kwa umma kwenye mikoa ya Singida, Dodoma na Iringa maeneo yanayotoa wasichana wengi zaidi katika ufanyaji kazi za ndani.

USAJILI WA VYAMA VYA KIJAMII NA VYA KIDINI

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imeendelea na jukumu la usajili na uhakiki wa Vyama vya Kijamii na Kidini kwa lengo mahususi la kuhakikisha amani na utulivu inakuwepo katika jamii. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 jumla ya maombi 472 ya kusajili vyama yalipokelewa ambapo kati ya hayo maombi 370 ni ya vyama vya kijamii na maombi 102 ni vyama vya kidini. Katika kipindi hicho vyama 404 vilisajiliwa, kati ya hivyo 378 ni vya kijamii na 26 ni vya kidini. Aidha, maombi ya vyama 55 bado yanashughulikiwa na maombi ya vyama 13 yamekataliwa kutokana na kukosa sifa.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** uhakiki wa vyama umeendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na kuboresha kanzidata ya vyama ili kuwa na kumbukumbu sahihi kwa vyama vyote vilivyosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama, Sura 337 ambavyo vinakidhi vigezo vya kuendelea kuwepo kwenye daftari la usajili wa vyama. Vilevile, hatua mbalimbali zimechukuliwa za kutoa kusudio la kuvifutia usajili vyama visivyotekeleza wajibu wao kulingana na Sheria ya Vyama, Sura 337 na kanuni zake. Hadi sasa vyama 1,481 tayari vimefutiwa usajili na vilevile hatua za uhakiki kwa vyama vingine visivyokidhi matakwa ya Sheria unaendelea. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara itaendelea kusajili vyama, kusimamia vyama na kufanya uhakiki wa vyama vilivyo hai na kufanya ukaguzi katika Mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

KUBORESHA SERA, SHERIA, KANUNI, MIKAKATI NA USIMAMIZI WAKE

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imeendelea na hatua za kuboresha sera, sheria, kanuni na mikakati mbalimbali ili kuimarisha utendaji kazi na huduma inazozitoa. Rasimu 3 za sera zimeandaliwa, sera moja ipo katika mapitio, rasimu 3 za sheria zipo katika hatua

mbalimbali za maandalizi. Aidha, kanuni mbalimbali za sheria zimeandaliwa na kuidhinishwa. Katika mwaka 2016/17 Wizara itaendelea kukamilisha kuandaa sera, sheria, kanuni na mikakati mbalimbali ili kuidhinishwa na kuanza kutumika. Aidha, Wizara itaendelea kufanya kazi kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na kuzingatia utawala bora.

MAPAMBANO DHIDI YA VVU/UKIMWI NA MAGONJWA SUGU YASIYOAMBUKIZWA

92. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI, Wizara yangu imendeleza juhudi mbalimbali za kuimarisha mapambano hayo kwa kutoa mafunzo ya elimu rika kwa askari, watumishi, familia za askari na wafungwa ikiwa ni pamoja na kuhamasisha upimaji wa hiari. Pamoja na hayo, Wizara iliendelea kuwapatia fedha kila mwezi askari na watumishi raia wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa ajili ya kuimarisha afya zao dhidi ya magonjwa nyemelezi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, mkazo zaidi utakuwa katika kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya kwa askari na watumishi raia sambamba na upimaji wa afya zao.

USHIRIKISHWAJI WA WAFANYAKAZI

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara iliwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi mbalimbali yanayohusu utendaji kazi wa Wizara kupitia Mabaraza ya Wafanyakazi. Aidha, vikao viwili vya kisheria vya Baraza la Wafanyakazi vilifanyika na maamuzi mbalimbali yalifikiwa. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara itaendelea kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi yanayofikiwa kwa mujibu wa sheria.

MAFUNZO, AJIRA MPYA NA KUPANDISHWA VYEO WATUMISHI

94. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea na jitihada za kuwaendeleza kitaaluma watumishi wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo elekezi watumishi 30, na kuwawezesha watumishi 17 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu katika kozi mbalimbali zikiwemo za shahada, stashahada na cheti. Vilevile, watumishi 3,689 walipandishwa vyeo katika kada mbalimbali na watumishi 25 waliajiriwa kwa kada mbalimbali kufanya kazi ndani ya Wizara. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara inatarajia kupeleka watumishi 20 katika mafunzo ya muda mfupi na watumishi 15 katika mafunzo ya muda mrefu katika programu mbalimbali, kuwapandisha vyeo watumishi kutokana na sifa kulingana na miundo yao ya kiutumishi pamoja na kuajiri watumishi wapya ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na watumishi kufariki, kustaafu na kuacha kazi.

V. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA AHADI ZA SERIKALI BUNGENI 2015/16

95. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Serikali Bungeni katika mwaka wa fedha 2015/2016 umeelezwa katika **Kiambatisho Na.1** cha Hotuba hii. Ahadi hizo zipo katika maeneo ya vitendea kazi, ajira na mafunzo, misako na doria, ujenzi na ukarabati wa ofisi, vituo, nyumba na magereza, zoezi la utambuzi na usajili wa watu na kuwarejesha wakimbizi kwao.

VI. SHUKRANI

96. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 katika kutimiza malengo yetu. Shukrani za dhati ziwaendee wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mbunge wa Jimbo la Muheza, kwa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** shukrani za kipekee nazitoa kwa viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mheshimiwa mhandisi Hamad Masauni Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Meja Jenerali Projest A. Rwegasira, Katibu Mkuu; Balozi Simba Yahaya, Naibu Katibu Mkuu; Bwana Ernest Mangu, Inspekta Jenerali wa Polisi; Bwana John Minja, Kamishna Jenerali wa Magereza; Bwana Thobias Andengenye, Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji; Bwana Pius Nyambacha Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji mstaafu; Bibi Victoria Lembeli, Kaimu Kamishna Jenerali wa Uhamiaji; Dkt. Modestus Kipilimba, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Makamanda, Askari pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao wamesaidia maandalizi ya hotuba kwa namna moja au nyingine na vilevile kwa kuweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

98. ***Mheshimiwa Spika***, nachukua pia fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo walioendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza progamu na mipango ya Wizara Washirika hao ni pamoja na Austria, China, Japan, Korea Kusini, Marekani, Misri, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uturuki na taasisi za kimataifa zikiwemo INTERPOL, IOM, EU, UNHCR, DFID, USAID, UNICEF, WFP na Pharm Access pamoja na wadau wengine wote kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho ingawa sio mwisho kwa umuhimu ninamshukuru mke wangu pamoja na watoto wangu kwa kunivumilia pale ambapo wananihitaji na nashindwa kuwa nao, kutokana na kuwa katika utekelezaji wa majukumu ya kitaifa.

VII. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

100. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuiwezesha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2016/17, naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ya jumla ya shilingi 864,106,290,105. Kati ya fedha hizo shilingi 316,126,377,000 ni za matumizi mengineyo, Shilingi 500,056,492,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 47,923,421,105 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

a. Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

(i) Matumizi Mengineyo Shilingi 11,186,151,000.00
(ii) Mishahara Shilingi 17,281,428,000.00
(iii) Matumizi ya maendeleo Shilingi 3,500,000,000.00
Jumla 31,967,579,000.00

b. Fungu 28 – Jeshi la Polisi

(i) Matumizi Mengineyo Shilingi 187,429,446,000.00
(iii) Matumizi ya Mishahara Shilingi 342,411,819,000.00
(iii) Matumizi ya maendeleo Shilingi 5,370,041,105.00
Jumla 535,211,306,105.00

c. Fungu 29 – Jeshi la Magereza

(i) Matumizi Mengineyo Shilingi 87,630,603,000.00
(iii) Mishahara Shilingi 104,313,834,000.00
(iii) Matumizi ya maendeleo Shilingi 3,053,380,000.00
Jumla 194,997,817,000.00

d. Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na NIDA

(i)Matumizi Mengineyo Shilingi 15,041,937,000.00
(iii) Mishahara Shilingi 4,330,051,000.00
(iii) Matumizi ya maendeleo Shilingi 30,000,000,000.00
Jumla 49,371,988,000.00

e. Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji

(i)Matumizi Mengineyo	Shilingi 14,838,240,000.00
(iii) Mishahara	Shilingi 31,719,360,000.00
(iii) Matumizi ya maendeleo	Shilingi 6,000,000,000.00
	Jumla 52,557,600,000.00

Jumla Kuu 864,106,290,105.00

101. ***Mheshimiwa Spika***, nakushukuru wewe, Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi wengine wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; www.moha.go.tz.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB- MWENYEKITI KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuwa hapa, Pili, ningependa kuwashukuru Wanamuheza ambao wanaendelea kuniamini kwa kuniingiza hapa Bungeni. Tatu, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa taarifa ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kwa heshima kubwa kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 6(3)(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati hii inalo jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeainisha uchambuzi wa bajeti ya Wizara kuwa ni jukumu la Kamati za kisekta, Kamati hii ikiwa ni mojawapo. Vilevile Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti la Kamati za kisekta, ikiwemo Kamati hii,

kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka unaoshia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inahusisha Mafungu Matano ya kibajeti kama ifuatavyo:-

Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 28 – Jeshi la Polisi, Fungu 29 – Jeshi la Magereza, Fungu 51- Wizara (Makao Makuu) ikiwemo *NIDA* na Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo ya awali, Taarifa hii inafafanua mambo manne yafuatayo:-

(i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

(ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:-

Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) na kufanya ziara za ukaguzi wa miradi kuanzia tarehe 29 Machi hadi 04 Aprili, 2016. Kamati ilitembelea na kukagua miradi nane kati ya miradi 15 iliyoidhinishiwa fedha chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 29

(i) Mradi uliohusu kuboresha mashamba ya mifugo;
(ii) Mradi uliohusu ukamilishaji wa majengo ya Magereza;
(iii) Mradi uliohusu ukamilishaji wa nyumba za askari; na
(iv) Mradi uliohusu ukarabati wa majengo na miundombinu ya Magereza yenye ulinzi mkali.

(b) Fungu 93

(i) Mradi uliohusu ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji Mikoani na nyumba za watumishi; na
(ii) Mradi uliohusu ukarabati wa Chuo cha Uhamiaji, Jengo la Makao Makuu na Nyumba za Watumishi.

(c) Fungu 51

(i) Mradi uliohusu ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi; na
(ii) Mradi uliohusu Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi kuhusiana na ukaguzi wa miradi hiyo inaonesha kwamba mwenendo wa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha kutokana na kiasi kidogo cha fedha kilichopokelewa. Hadi kufikia Machi 2016, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi 5,984,023,924 tu kati ya shilingi 79,689,945,000 zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 7.5 ya bajeti yote ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo ya ukaguzi; baada ya kukagua miradi ya maendeleo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu hali ya utekelezaji katika miradi hiyo. Naomba nianze taarifa hiyo kwa kueleza kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ulikuwa ni jambo muhimu kwa ukamilishaji wa miradi hiyo. Kwa sababu hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi umegawanyika katika makundi matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la kwanza ni miradi ambayo haikutekelezeka kabisa. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi hii hazikupatikana. Mfano wa miradi hiyo ni mradi Namba 6306, Namba 6307 na Namba 6308 inayohusu ukamilishaji wa majengo, ujenzi wa nyumba za askari na uboreshaji wa mashamba ya Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la pili ni miradi ambayo ilitekelezwa kwa kiwango kisichokamilika, sababu iliyoelezwa ni kutolewa kwa fedha pungufu ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Mfano wa miradi hiyo ni mradi wa Vitambulisho vya Taifa unaosimamiwa na *NIDA*. Kamati ilijulishwa kuwa bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya mradi huu kwa mwaka 2015/2016 ni shilingi bilioni 47.7. Hata hivyo, taarifa ilionesha kuwa hadi mwisho wa robo ya tatu ya mwaka wa fedha kiasi cha shilingi bilioni mbili tu zilipokelewa ikiwa ni sawa na asilimia 4.26.

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni miradi iliyopatiwa fedha zote zilizoidhinishwa na utekelezaji wake ulikamilika. Mfano wa miradi hiyo ni mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za Uhamiaji mkoani Singida na mradi wa ukamilishaji wa nyumba za Makamishna wa Uhamiaji Mtoni Kijichi ambao umekamilika kwa asilimia 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni kuhusu miradi ya maendeleo, kutokana na hali ya miradi ya maendeleo kama ilivyobainika wakati wa ziara za ukaguzi, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Kutokupatikana kwa fedha kutoka Hazina kumesababisha miradi isitekelezwe kama ilivyokusudiwa;

(ii) Upatikanaji wa fedha pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa unadhorotesha ukamilishaji wa miradi ya maendeleo;

(iii) Mwenendo mzima wa utekelezaji wa bajeti kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo unahitaji kuboreshwa ipasavyo; na

(iv) Uzuri wa matokeo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na manufaa ya miradi hiyo hutegemea kukamilishwa kwa miradi. Jambo hili linawezekana endapo fedha zinazoidhinishwa na Bunge zitapatikana kwa wakati na kwa kiwango kilichoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016; katika kuchambua mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilizingatia ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha na lengo lililokusudiwa, upatikanaji wa fedha za Matumizi Mengineyo *(OC)* na fedha za Miradi ya Maendeleo. Aidha, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwa kipindi cha Februari na Machi, 2016 na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi 179,471,819,800; lakini hadi kufikia mwezi Machi 2016, kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni shilingi 132,836,141,280, hii ni sawa na asilimia 74 ya makadirio ya makusanyo katika kipindi husika. Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mafungu yote ni mzuri kwani hadi kufikia mwisho wa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2015/2016, wastani wa makusanyo ulikuwa ni takribani asilimia 75 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ulinganisho wa ukusanyaji wa maduhuli baina ya mafungu na kubaini kwamba Fungu 29 – Jeshi la Magereza liliongoza katika ukusanyaji kwa kufikia asilimia 86.7 ya lengo, wakati Fungu 51 – Wizara (Makao Makuu) lilikuwa la mwisho kwa kukusanya asilimia 67.29 tu ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Serikali umeendelea kuwa changamoto kwa Wizara hii. Kwa kuzingatia jambo hilo Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mipango ya bajeti, kwa kulinganisha fedha zilizopatikana hadi Machi 2016 na kiasi kilichoidhinishwa. Hadi kufikia Machi, 2016 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 660,333,375,957 kati ya shilingi 816,080,198,000 zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ulinganisho na kubaini kuwa kati ya fedha zote zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya Wizara, mishahara ilikuwa asilimia 52 wakati matumizi mengineyo ilikuwa asilimia 47. Aidha, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, uchambuzi ulibaini kuwa fedha zilizopatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ilikuwa ni asilimia moja tu ya kiasi cha fedha kilichopokelewa. Ili kupata picha halisi ya uwiano wa upatikanaji wa fedha za mishahara, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ililinganisha kasma za matumizi hayo kwa kuangalia mafungu yote matano ya Wizara na kulinganisha kama inavyoonekana katika chati ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati ikichambua mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2015/2016, iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, ilitoa mapendekezo 12 kwa ajili ya kuzingatiwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kati ya mapendekezo yaliyotolewa ni moja tu ndilo limetekelezwa kikamilifu, nalo linahusu kuongezwa kwa kiwango cha posho ya chakula kwa askari polisi kutoka shilingi 6,000 hadi shilingi 10,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliarifiwa kwamba Wizara inaendelea na utekelezaji wa baadhi ya maoni, na mengine bado utekelezaji wake haujaanza. Miongoni mwa maoni ambayo utekelezaji wake unaendelea ni lile lililoitaka Serikali iwezeshe kutumika kwa Sheria ya *Community Service* katika mikoa yote 25 ya Tanzania Bara badala ya 19 ya sasa ili wahalifu waliotiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo kutokana na makosa madogo, watumikie adhabu hiyo nje ya magereza. Utekelezaji umeendelea kufanyika ambapo kwa

sasa sheria hiyo inatumika katika mikoa 21 na utaratibu wa kuifikia mikoa iliyosalia unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka 2016/2017; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yenye mafungu matano imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 864,106,290,105 kutoka vyanzo mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba makadirio hayo ya makusanyo ya maduhuli yameongezeka kwa asilimia 38 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2015/2016 ambayo yalikuwa shilingi 179,471,819,800; hayo yalikuwani makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi; katika mwaka wa fedha 2016/2017 bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwa kwa mafungu yote matano ni shilingi 864,106,290,105; inawezekana labda *addendum* ya marekebisho hayo hayajafanyika kufuatana na taarifa yangu ambayo ipo kwenye vitabu. Lakini taarifa ninayoisoma hapa sasa hivi ndiyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; ni dhahiri kuwa, amani na utulivu katika nchi yetu ni vipaumbele vya awali, hivyo vyombo vyenye dhamana ya ulinzi na usalama vinapaswa kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kwa upande mwingine ili vyombo hivyo viweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, ni lazima vipewe bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inafahamu kwamba matarajio ya walio wengi ni kusikia Kamati hii inazungumzia suala la mitambo ya kuchukulia alama za vidole *(Automated Fingerprint Intergrated System - AFIS)* zilizoagizwa au kununuliwa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati inatambua uzito na umuhimu wa suala hili. Hata hivyo, kwa kuwa suala hilo ni hoja iliyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG);* na kwa kuwa kifungu cha 14 (a) kikisomwa pamoja na kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kimeipa jukumu Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali yalioainishwa katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuwa suala hili tayari linashughulikiwa na Kamati ya *PAC;* hivyo basi, ni vyema Kamati ya Hesabu za Serikali ikaachwa ikaendelea kushughulikia hoja ya *CAG* kwa utaratibu wa uendeshaji shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kupitia na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye vikao vya Kamati katika kipindi cha Machi hadi Aprili, 2016, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ihakikishe kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, pamoja na zile za maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017 zinatolewa kwa ukamilifu na kwa wakati ili kuwezesha majukumu na miradi iliyopangwa kutekelezwe kikamilifu.

(ii) Wizara kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake ibuni mbinu za kuongeza uzalishaji ili kujiongezea kipato hususan kupitia Jeshi la Magereza katika fani za kilimo, ushonaji na ufugaji.

(iii) Hatua za makusudi zichukuliwe kuhusu ujenzi wa nyumba katika Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji ili kupunguza uhaba wa makazi kwa wafanyakazi wa ngazi za chini, badala ya kuweka kipaumbele na kutumia gharama kubwa katika ujenzi wa nyumba chache za viongozi. Hali ya fedha itakapoimarika, ujenzi wa nyumba za viongozi uendelee.

(iv) Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi, wazabuni na makandarasi katika mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kuondoa adha wanayokumbana nayo kutoka kwa wadeni wao.

(v) Serikali iruhusu fedha zinazokusanywa na mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kutokana na tozo mbalimbali zitumiwe na mafungu hayo kuboresha utendaji na kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo.

(vi) Jeshi la Polisi liongeze usimamizi wa Sheria za Usalama Barabarani ili kupunguza ajali, vifo na majeruhi. Aidha, ni vizuri mapendekezo yaliyowahi kutolewa na Kamati mbalimbali kuhusu usimamizi wa Sheria za Usalama Barabarani yakazingatiwa ili yatumike kushauri namna ambavyo zitaweza kupunguza ajali, sambamba na hilo askari wa usalama barabarani ambao wamelalamikiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa wachukuliwe hatua stahiki.

(vii) Serikali itoe fedha kwa Jeshi la Polisi kugharamia Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa yaani *Big Results Now (BRN)* unaolenga kuzuia uhalifu, ufanyaji wa doria na operesheni za mara kwa mara, mpango huu tunaamini utalifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa.

(viii) Jeshi la Polisi lifuatilie na kudhibiti vitendo vya kigaidi vinavyotaka kujitokeza hapa nchini. Aidha, kesi za dawa za kulevya na mauaji zipelelezwe kwa makini na haraka kuepusha watuhumiwa kukaa magerezani kwa muda mrefu.

(ix) Ili kupunguza msongamano katika Magereza haya hapa nchini, Kamati inashauri Serikali ijiandae kujenga Magereza katika Wilaya mpya. Wakati Serekali ikijiandaa kwa mpango huo wa muda mrefu, ijielekeze katika matumizi ya adhabu mbadala kwa wafungwa kama vile kifungo cha nje, Mpango wa *Parole* na huduma za jamii. Aidha, Kamati za Kusukuma Kesi *(Case flow Management Committee),* ziongeze kasi ya kupitia kesi zote zilizokaa zaidi ya siku 60 bila ya kuwa na ushahidi unaojitosheleza na kushauri zifutwe. Vilevile Wizara iwe na mpango maalum wa Wakuu wa Upelelezi pamoja na Mawakili wa Serikali kutembelea magereza mara kwa mara kwa lengo la kusikiliza malalamiko ya mahabusu.

(x) Serikali itoe fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi kwa Jeshi la Magereza ili kuliwezesha kuwafikisha mahabusu mahakamani kwa wakati na hivyo kutoathiri mwenendo wa kesi zao.

(xi) Serikali itoe fedha za kukamilisha miradi ya maendeleo iliyoathiriwa kwa kutopewa fedha hizo kwa mwaka wa fedha 2015/2016, hususan fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa jengo la bweni, jiko na hospitali katika Gereza la Segerea na ukamilishaji wa nyumba za askari kwa magereza yote. Fedha hizi zitolewe kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha kama inawezekana.

(xii) Serikali itoe fedha kwa Jeshi la Magereza kwa ajili ya kununua vifaa vya kilimo vya kisasa ili liweze kujiendesha lenyewe. Aidha, Serikali itoe kipaumbele kwa kutoa mtaji kwa Jeshi la Magereza ili liweze kuanzisha na kuimarisha viwanda vya viatu na viwanda vya kushona sare kwa ajili ya kuhudumia mahitaji ya sare ya majeshi yote nchini.

(xiii) Serikali ilitolee ufumbuzi suala la adhabu ya kifo ambayo haijatekelezwa kwa kipindi kirefu na hivyo kusababisha wafungwa waliohukumiwa adhabu hiyo kuongezeka magerezani na kuleta msongamano.

(xiv) Serikali itenge fedha za kutosha ili kukamilisha Mradi wa Vitambulisho vya Taifa ifikapo Disemba, 2016 kama ilivyoahidiwa.

(xv) Serikali iandae mpango wa kuwarudisha makwao wahamiaji haramu walioko magerezani ili kupunguza gharama za kuwahudumia na kupunguza msongamano magerezani. Aidha, Serikali iimarishe udhibiti wa mipaka ili kuzuia uingiaji wa wahamiaji haramu.

(xvi) Serikali iangalie upya namna ya kuwaongezea fedha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili liweze kuwa la kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa

Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao ushirikiano wao, maoni yao na ushauri wao vimewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Wajumbe wote 24 nawashukuru na kwa sababu ya muda naomba niwatambue tu sitawataja kwa majina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe pia wa Kamati yangu napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Charles Kitwanga, (Mb); Naibu Waziri - Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni (Mb); Katibu Mkuu Meja - Jenerali Projest Rwegasira, Naibu Katibu Mkuu - Balozi Yahya Simba pamoja na watendaji wote wa Wizara wakiwemo Inspekta Jenerali wa Polisi, Kamishna Mkuu wa Magereza, Kamishna Mkuu wa Uhamiaji, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Mkuu wa Zimamoto na wengineo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuratibu vema shughuli za Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein na Makatibu wa Kamati hii ambao wamefanya kazi kubwa sana akiwemo ndugu Ramadhani Issa Abdallah, ndugu Grace Bidya na Ndugu Hamisi Mwinyimkuu, wakisaidiwa na Ndugu Rehema Kimbe kwa kuratibu taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante.

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016,

pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 Fasili ya 3 (c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati hii inalo jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeainisha uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kuwa ni jukumu la Kamati za kisekta, Kamati hii ikiwa ni mojawapo. Vile vile, Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti la Kamati za kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka unaoshia.

Naomba kutoa Taarifa kuwa kamati ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inahusisha mafungu matano ya kibajeti kama ifuatavyo:- Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 28 – Jeshi la Polisi, Fungu 29 – Jeshi la Magereza, Fungu 51- Wizara (Makao Makuu) ikiwemo NIDA, na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Kwa maelezo hayo ya awali, Taarifa hii inafafanua mambo manne (4) yafuatayo:-

(v) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

(vi) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016;

(vii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017; na

(viii) Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) na kufanya ziara za ukaguzi wa miradi kuanzia tarehe 29 Machi hadi 04 Aprili, 2016. Kamati ilitembelea na kukagua miradi Nane (8) kati ya Kumi na Tano (15)

iliyoidhinishiwa fedha chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

a) Fungu 29

· Mradi Namba 4428 uliohusu kuboresha mashamba ya mifugo;

· Mradi Namba 6306 uliohusu ukamilishaji wa majengo ya Magereza;

· Mradi Namba 6307 uliohusu ukamilishaji wa nyumba za askari; na

· Mradi Namba 6308 uliohusu ukarabati wa majengo na miundombinu ya Magereza yenye ulinzi mkali.

b) Fungu 93

· Mradi Namba 6301 uliohusu ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji Mikoani na nyumba za watumishi; na

· Mradi Namba 6339 uliohusu ukarabati wa Chuo cha Uhamiaji, Jengo la Makao Makuu na Nyumba za Watumishi.

c) Fungu 51

· Mradi Namba 6327 uliohusu Ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi; na
· Mradi Namba 6501 uliohusu Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hali halisi kuhusiana na ukaguzi wa miradi hiyo inaonesha kwamba, mwenendo wa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha kutokana na kiasi kidogo cha fedha kilichopokelewa. Hadi kufikia Machi 2016, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi 5,984,023,924** tu kati ya s**hilingi 79,689,945,000.00** zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 7.5 ya bajeti yote ya maendeleo.

2.2 Matekeo ya Ukaguzi

Mheshimwia Spika, baada ya kukagua Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu hali ya utekelezaji katika Miradi hiyo. Naomba nianze taarifa hiyo kwa kueleza kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ulikuwa ni jambo muhimu kwa ukamilishaji wa Miradi. Kwa sababu hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa Miradi umegawanyika katika makundi matatu.

Mheshimiwa Spika, kundi la kwanza ni Miradi ambayo haikutekelezwa kabisa. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi hii hazikupatikana. Mfano wa miradi hiyo ni mradi Na. 6306, 6307 na 6308 inayohusu ukamilishaji wa majengo, ujenzi wa nyumba za askari na uboreshaji wa mashamba ya Magereza.

Mheshimiwa Spika, Kundi la pili ni Miradi ambayo ilitekelezwa kwa kiwango kisichokamilika. Sababu iliyoelezwa ni kutolewa kwa fedha pungufu ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Mfano wa Miradi hiyo ni Mradi wa vitambulisho vya taifa unaosimamiwa na NIDA. Kamati ilijulishwa kuwa bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya mradi huu kwa mwaka 2015/2016 ni **ShT**. Bilioni 47.7. Hata hivyo, taarifa ilionesha kuwa hadi mwisho wa robo ya tatu ya mwaka wa fedha (mwezi Machi 2016), kiasi cha **ShT**. Bilioni 2 tu zilipokelewa ikiwa ni sawa na asilimia 4.26.

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni miradi iliyopatiwa fedha zote zilizoidhinishwa na utekelezaji wake ulikamilika. Mfano wa miradi hiyo ni Mradi wa ujenzi wa Jengo la ofisi za Uhamiaji Mkoani Singida, na Mradi wa ukamilishaji wa nyumba za Makamishna wa Uhamiaji Mtoni kijichi ambao umekamilika kwa asilimia 90.

2.3 Maoni kuhusu Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya miradi ya maendeleo kama ilivyobainika wakati wa ziara za ukaguzi, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Kutopatikana kwa fedha kutoka Hazina kumesababisha miradi isitekelezwe kama ilivyokusudiwa;

(ii) Upatikanaji wa fedha pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa unazorotesha ukamilishaji wa miradi ya maendeleo;

(iii) Mwenendo mzima wa utekelezaji wa bajeti kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo unahitaji kuboreshwa ipasavyo; na

(iv) Uzuri wa matokeo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na manufaa ya miradi hiyo hutegemea kukamilishwa kwa miradi. Jambo hili linawezekana endapo fedha zinazoidhinishwa na Bunge zitapatikana kwa wakati na kwa kiwango kilichoidhinishwa.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilizingatia ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha na lengo lililokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwa kipindi cha Februari na Machi, 2016, na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

3.2 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya **shilingi 179,471,819,800/=.** Hadi kufikia mwezi Machi 2016, kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni **shilingi 132,836,141,280/=** sawa na asilimia 74 ya makadirio ya makusanyo katika kipindi husika.

Mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mafungu yote ni mzuri kwani hadi kufikia mwisho wa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2015/2016, wastani wa makusanyo ulikuwa ni takribani asilimia 75 ya lengo. Kamati ilifanya ulinganisho wa ukusanyaji wa Maduhuli baina ya Mafungu na kubaini kwamba, Fungu 29 – Jeshi la Magereza liliongoza katika ukusanyaji kwa kufikia asilimia 86.7 ya lengo, wakati Fungu 51 – Wizara (Makao Makuu), lilikuwa la mwisho kwa kukusanya asilimia 67.29 tu ya lengo.

3.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka hazina

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Serikali umeendelea kuwa changamoto kwa Wizara hii. Kwa kuzingatia jambo hilo Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Mipango ya Bajeti, kwa kulinganisha fedha zilizopatikana hadi Machi 2016, na kiasi kilichoidhinishwa. Hadi kufikia Machi, 2016 Wizara ilikuwa imepokea **shilingi 660,333,375,957/=** kati ya **Shilingi 816,080,198,000.00 /=** zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo**.** Kamati ilifanya ulinganisho na kubaini kuwa, kati ya fedha zote zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya Wizara, mishahara ilikuwa asilimia 52 wakati matumizi mengineyo ilikuwa asilimia 47. Aidha, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, uchambuzi ulibaini kwamba, fedha zilizopatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ilikuwa ni **asilimia moja tu** ya kiasi cha fedha kilichopokelewa.

Ili kupata picha halisi ya uwiano wa upatikanaji wa fedha za mishahara, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ililinganisha kasma za matumizi hayo kwa kuangalia mafungu yote matano ya Wizara na kulinganisha kama inavyoonekana katika Chati Na. 1

Chati Na. 1. Uwiano wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2015/2016



Chanzo- Randama ya Wizara 2015/2016

3.4 Mapitio ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama

Mheshimiwa Spika, wakati ikichambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2015/2016, iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, ilitoa mapendekezo 12 kwa ajili ya kuzingatiwa na Wizara. Nasikitika kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kati ya mapendekezo yaliyotolewa ni moja tu ndilo limetekelezwa kikamilifu, nalo linahusu kuongezwa kwa kiwango cha posho ya chakula kwa Askari Polisi kutoka **shilingi 6,000** hadi **shilingi 10,000** kwa siku.

Kamati iliarifiwa kwamba, Wizara inaendelea na utekelezaji wa baadhi ya maoni, na mengine bado utekelezaji wake haujaanza. Miongoni mwa maoni ambayo utekelezaji wake unaendelea ni lile lililoitaka Serikali iwezeshe kutumika kwa Sheria ya "*Community Service*" katika Mikoa yote 25 ya Tanzania Bara badala ya 19 ya sasa ili Wahalifu waliotiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo kutokana na makosa madogo, watumikie adhabu hiyo nje ya Magereza. Utekelezaji umeendelea kufanyika ambapo kwa sasa Sheria hiyo inatumika katika Mikoa 21 na utaratibu wa kuifikia mikoa iliyosalia unaendelea.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2016/2017

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yenye Mafungu Matano imepangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 289,966,630,604/=** kutoka vyanzo mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao:-

Jedwali Na.1: MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI

Fungu na Taasisi husika	**Kiasi**
Fungu 14 - Zimamoto na uokoaji	35,500,003,000
Fungu 28 - Jeshi la Polisi	70,915,650,000
Fungu 29 - Jeshi la Magereza	2,619,336,504
Fungu 51 – Wizara	226,601,100
Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji	180,705,040,000
Jumla	**289,966,630,604**

Chanzo: Randama ya Wizara 2016/2017

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, makadirio hayo ya makusanyo ya Maduhuli yameongezeka kwa asilimia 38 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2015/2016 ambayo yalikuwa **shilingi 179,471,819,800/=**.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mhesimiwa Spika, Katika mwaka wa Fedha 2016/2017, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwa kwa mafungu yote matano ni **shilingi 350,837,478,000/=.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 263,913,957,000/=** ni fedha maalum, **shilingi 42,423,519,578/=** ni matumizi mengineyo na **shilingi 44,500,000,000/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**.** Bajeti hii imepungua kwa takribani asilimia 57 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2015/2016 ambayo ilikuwa **shilingi 816,080,198,000.00/=.**

Uchambuzi wa Kamati kuhusiana na upungufu huo umebaini kwamba, upande wa fedha za matumizi mengineyo (OC) umeathirika zaidi kwani bajeti yake imepungua kwa takribani asilimia 68 ikilinganishwa na bajeti ya OC kwa mwaka 2015/2016. Aidha, bajeti ya maendeleo imepungua kwa takribani asilimia 40 ikilinganishwa na bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, upungufu huu wa bajeti utaathiri utekelezaji wa shughuli kwa mafungu yote. Kwa mfano; Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, halijatengewa fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa za kuzimia moto. Kamati inajiuliza ni utaratibu gani utatumika pale yatakapozuka majanga ya moto na Jeshi hilo kutakiwa kushiriki katika uzimaji? Aidha, Kamati inajiuliza ni vipi Majeshi ya Magereza na Polisi yatamudu kutekeleza majukumu yao kwa ufinyu huu wa bajeti hasa kwa kuzingatia kwamba Serikali ina azma ya kuboresha vyombo hivi ili viweze kuwa vya kisasa zaidi na viendane na mabadiliko ya kiteknolojia yaliyopo?

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa, amani na utulivu katika nchi yetu ni vipaumbele vya awali, hivyo vyombo vyenye dhamana ya ulinzi na usalama vinapaswa kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kwa upande mwingine ili vyombo hivyo viweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, ni lazima vipewe bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya walio wengi ni kusikia Kamati hii inazungumzia suala la mitambo ya kuchukulia alama za vidole- AFIS *(Automated Fingerprint Intergrated System)* zilizoagizwa/ kununuliwa na Jeshi la Polisi.

Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati inatambua uzito na umuhimu wa suala hili. Hata hivyo, kwa kuwa suala hilo ni hoja iliyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), na kwa kuwa kifungu cha 14 (a) kikisomwa pamoja na kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeipa jukumu Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Wizara za Serikali yalioainishwa katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), na kwa kuwa suala hili tayari linashughulikiwa na Kamati ya PAC; hivyo basi, ni vyema Kamati ya Hesabu za Serikali ikaachwa ikaendelea kushughulikia hoja ya CAG kwa utaratibu wa uendeshaji shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kupitia na kujadili Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye vikao vya Kamati katika kipindi cha Machi hadi Aprili, 2016, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

i) Serikali ihakikishe kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, pamoja na zile za maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017 zinatolewa kwa ukamilifu na kwa wakati, ili kuwezesha majukumu na miradi iliyopangwa kutekelezwe kikamilifu;

ii) Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake, ibuni mbinu za kuongeza uzalishaji ili kujiongezea kipato hususan kupitia Jeshi la Magereza katika fani za kilimo, ushonaji na Ufugaji;

iii) Hatua za makusudi zichukuliwe kuhusu ujenzi wa nyumba katika Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji ili kupunguza uhaba wa makazi kwa wafanyakazi wa ngazi za chini, badala ya kuweka kipaumbele na kutumia gharama kubwa katika ujenzi wa nyumba chache za viongozi. Hali ya fedha itakapoimarika, ujenzi wa nyumba za viongozi uendelee;

iv) Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya Watumishi, Wazabuni na Makandarasi katika Mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kuondoa adha wanayokumbana nayo kutoka kwa wadeni wao;

v) Serikali iruhusu fedha zinazokusanywa na mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kutokana na tozo mbalimbali zitumiwe na mafungu hayo kuboresha utendaji na kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo;

vi) Jeshi la Polisi liongeze usimamizi wa Sheria za Usalama barabarani ili kupunguza ajali, vifo na majeruhi. Aidha, ni vizuri mapendekezo yaliyowahi kutolewa na Kamati mbalimbali kuhusu usimamizi wa Sheria za Usalama Barabarani yakazingatiwa ili yatumike kushauri namna ambavyo ajali zitaweza kupunguzwa. Sambamba na hilo Askari wa Usalama Barabarani ambao wamelalamikiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa wachukuliwe hatua stahiki;

vii) Serikali itoe fedha kwa Jeshi la Polisi kugharamia Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa yaani *Big Results Now* (BRN) unaolenga kuzuia uhalifu, ufanyaji wa doria na operesheni za mara kwa mara. Mpango huu unataka kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa;

viii) Jeshi la Polisi lifuatilie na kudhibiti vitendo vya kigaidi vinavyotaka kujitokeza hapa nchini. Aidha, kesi za madawa ya kulevya na mauaji zipelelezwe kwa makini na haraka kuepusha watuhumiwa kukaa magerezani kwa muda mrefu;

ix) Ili kupunguza msongamano katika Magereza hapa nchini, Kamati inashauri Serikali ijiandae kujenga Magereza katika wilaya mpya. Wakati Serekali ikijiandaa kwa mpango huo wa muda mrefu, ijielekeze katika matumizi ya adhabu mbadala kwa wafungwa kama vile kifungo cha nje, Mpango wa *Parole* na Huduma kwa Jamii;

Aidha, Kamati za Kusukuma Kesi (Case flow Management Committee), ziongeze kasi ya kupitia kesi zote zilizokaa zaidi ya siku 60 bila ya kuwa na

ushahidi unaojitosheleza na kushauri zifutwe. Vilevile Wizara iwe na mpango maalum wa Wakuu wa upelelezi pamoja na mawakili wa Serikali kutembelea magereza mara kwa mara kwa lengo la kusikiliza malalamiko ya mahabusu;

x) Serikali itoe Fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi kwa Jeshi la Magereza ili kuliwezesha kuwafikisha mahabusu Mahakamani kwa wakati na hivyo kutoathiri mwenendo wa kesi zao;

xi) Serikali itoe fedha za kukamilisha miradi ya maendeleo iliyo athiriwa kwa kutopewa fedha hizo kwa mwaka wa fedha 2015/2016, hususan fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Jengo la Bweni, Jiko na Hospitali katika Gereza la Segerea na ukamilishaji wa nyumba za askari kwa magereza yote. Fedha hizi zitolewe kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha;

xii) Serikali itoe fedha kwa Jeshi la Magereza kwa ajili ya kununua vifaa vya kilimo vya kisasa ili liweze kujiendesha lenyewe. Aidha, Serikali itoe kipaumbele kwa kutoa mtaji kwa Jeshi la Magereza ili liweze kuanzisha/kuimarisha viwanda vya viatu na viwanda vya kushona sare kwa ajili ya kuhudumia mahitaji ya sare ya Majeshi yote nchini;

xiii) Serikali ilitolee ufumbuzi suala la adhabu ya kifo ambayo haijatekelezwa kwa kipindi kirefu na hivyo kusababisha wafungwa waliohukumiwa adhabu hiyo kuongezeka Magerezani na kuleta msongamano;

xiv) Serikali itenge fedha za kutosha ili kukamilisha Mradi wa Vitambulisho vya Taifa ifikapo Desemba, 2016 kama ilivyoahidi;

xv) Serikali iandae mpango wa kuwarudisha makwao wahamiaji haramu walioko Magerezani ili kupunguza gharama za kuwahudumia na kupunguza msongamano Magerezani. Aidha, Serikali iimarishe udhibiti wa mipaka ili kuzuia uingiaji wa wahamiaji haramu; na

xvi) Serikali iangalie upya namna ya kuwaongezea fedha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili liweze kuwa la kisasa zaidi.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, napenda kwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ambao ushirikiano wao, maoni yao na ushauri wao vimewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1.Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb, Mwenyekiti
2.Mhe. Kanali (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb, M/Mwenyekiti

3.Mhe. Kapt.(Mst) George Huruma Mkuchika, Mb, Mjumbe
4.Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb, "
5.Mhe. Prosper J. Mbena, Mb, "
6.Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa, Mb, "
7.Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb, "
8.Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb, "
9.Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, Mb, "
10.Mhe. Allan Joseph Kiula, Mb, "
11.Mhe. Cosato David Chumi, Mb, "
12.Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb, "
13.Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb, "
14.Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb, "
15.Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb, "
16.Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb, "
17.Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb, "
18.Mhe. Haji Khatib Kai, Mb, "
19.Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb, "
20.Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb "
21.Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb "
22.Mhe. Lazaro S. Nyalandu, Mb, "
23.Mhe. Stephen J. Masele, Mb, "
24.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb, "

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Charles Kitwanga (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Eng. Hamad Masauni (Mb), Katibu Mkuu Meja Jenerali Projest Rwegasira, Naibu Katibu Mkuu Balozi Yahya Simba pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Pia napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhani Abdallah, Ndg. Grace Bidya na Ndg. Hamisi Mwinyimkuu wakisaidiwa na Ndg. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Balozi Adadi Mohamed Rajabu, **Mb**
MWENYEKITI
KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA
Mei, 2016

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kutokana na kuwa Kamati ya Kanuni bado inaendelea na shughuli pamoja na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, sasa ninamuita Waziri wa masuala ya Bunge aweze kutengua Kanuni, karibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia taarifa ambayo umeitoa sasa hivi mbele ya Bunge lako Tukufu, ninaomba nitumie Kanuni ya 28(2) na (3) kutoa hoja na kuliomba Bunge lako lisitishwe mpaka saa 10.00 na kutoa muda kwa Kamati ya Kanuni kuweza kuhitimisha shughuli ambayo umeipeleka mbele ya Kamati hiyo na baada ya hapo Bunge hili liweze kuendelea na shughuli kwa kadri utakavyotoa maelekezo. Naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatangazia Wabunge wote wa CCM wanatakiwa kufika Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kusitisha shughuli hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 5.00 asubuhi Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, asubuhi nilisitisha shughuli za Bunge na kutoa maelekezo kwa Kamati ya Kanuni ikutane na viongozi wa Kambi ya Upinzani ili kujadili taarifa yao ili kupata muafaka wa namna gani kanuni zetu za Kibunge zisiweze kuvunjwa. Sasa naomba kusoma Mwongozo wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyokumbuka asubuhi ya leo ziliwasilishwa hati mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge; miongoni mwa hati zilizowasilishwa ni Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Baada ya kupitia taarifa hizo, nilibaini kuwa Taarifa ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imezungumzia mambo mengi ambayo kwa maoni yangu niliona yanakiuka masharti ya Kanuni za Bunge.

Hivyo kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za Bunge na kwa kuzingatia wajibu wa Kiti kusimamia Kanuni za Bunge, niliagiza Kamati ya Kanuni za Bunge ikutane ili kupitia na kujadili maudhui ya Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ili kujiridhisha kama taarifa hiyo haijakiuka masharti yoyote ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Baada ya maagizo hayo, Kamati ilikutana katika ukumbi wa Spika ili kuyafanyia kazi maagizo ya Kiti. Kikao hicho kilihudhuriwa na Wajumbe wafuatao:-

Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mwenyekiti; na Wajumbe ni Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa George Masaju, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Zainab Katimba, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Godbless Lema, mwalikwa.

Waheshimiwa Wajumbe, Kamati imepitia na kujadiliana kwa kina kuhusu maudhui ya Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na kubaini kuwa taarifa hiyo imekiuka masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, hivyo imependekeza maneno yote ambayo yanakiuka masharti ya kanuni yarekebishwe kama ifuatavyo:-

(1) Kipengele kinachohusu mauaji ya viongozi wa kisiasa: Maeneo yote yaliyo ndani ya kipengele hiki kuanzia ukurasa wa saba hadi wa tisa wa taarifa yaondolewe.

(2) Eneo linalohusu mkataba tata wa Lugumi na Jeshi la Polisi: Katika kipengele hiki Kamati inapendekeza maneno yote yanayoanzia ukurasa wa kumi aya ya nne hadi ukurasa wa 14 aya ya kwanza yaondolewe. *(Makofi)*

(3) Sakata la kuuzwa kwa nyumba za Serikali: Ukurasa wa 15, aya ya kwanza hadi ya tatu, kuondoa maneno yanayomhusisha Rais na badala yake kuweka neno Serikali. *(Makofi)*

(4) Kipengele kinachohusu rushwa na Bunge kutumika kuwalinda wahalifu nchini: Kamati imependekeza maudhui ya kipengele hiki yanayoanzia ukurasa wa 15 hadi wa 17 yaondolewe, kwani yanakiuka Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

(5) Eneo lingine ni kipaumbele kinachohusu tabia ya Rais Magufuli na Usalama wa Nchi: Vile vile katika eneo hili Kamati inapendekeza maneno yote yaliyopo katika kipengele hicho kuanzia ukurasa wa 19 hadi ukurasa wa 20 yaondolewe, kwani yanakiuka Kanuni za Kudumu za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitia ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kanuni kuhusu suala hili, naomba kutoa maelekezo yafuatayo:-

Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 64(1)(c), (d), (e) na (f), ambayo pamoja na mambo mengine imekataza kuzungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama, kutotumia jina la Rais kwa dhihaka, kutozungumzia mwenendo wa Rais na kutosema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote.

Baada ya kutafakari na kwa kuzingatia maamuzi mbalimbali ya Spika kuhusu uzingatiaji wa masharti ya kanuni ya 64; na kwa kuwa Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, yaliyobainishwa na masharti ya kanuni yanapingana na masharti ya kanuni hiyo; namwelekeza Msemaji Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, aondoe maneno yote yaliyoainishwa hapo juu.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu. Ahsanteni.

Haya, tunaanza, Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

MHE. GODBLESS J. LEMA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya mwongozo wako huo, maana yake ni kwamba hotuba yangu yote nitakuwa nimeiondoa. Basi tu mimi nashukuru kwa mke wangu kufika Bungeni, tuendelee na kazi nyingine za Bunge. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na kuchangia. Sasa namwita Mheshimiwa Almas Maige, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Shukuru. Mheshimiwa Almas, bado? Mheshimiwa Shukuru, atafuatiwa na Mheshimiwa Almas.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa, nitangulie kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti ambayo imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba ulinzi na usalama katika nchi yetu unaendelea kuwekewa mkazo na msisitizo ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Taifa hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaendelea na shughuli zao za maendeleo bila kubughudhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuyapongeza majeshi yetu ya Polisi na Magereza kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya. Wanalitumikia Taifa kwa juhudi kubwa ambayo imetuwezesha sisi kuweza kufanya kazi za kila siku bila ya matatizo makubwa. Nakiri matunda ya kazi zao tunayaona, yamejionesha katika hali nyingi. Kubwa ni hali ya amani na utulivu katika nchi yetu ambayo imetuwezesha kufanya kazi vizuri. Pia udhibiti wa wimbi la ujambazi katika nchi. Ujambazi hakuna katika nchi yetu hivi kama tulivyokuwa tunaathirika huko nyuma, ambapo imepunguza hofu kubwa sana, imepunguza hofu kwa wananchi wetu na kuwawezesha kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hasa kwa Jeshi la *Traffic*, wamejitahidi sana kutusaidia katika Majiji yetu makuu hususan Dar es Salaam, kuhakikisha kwamba msongamano wa magari nyakati za kwenda na kutoka kazini msongamano huu umekuwa nafuu sana. Tunapoteza muda mwingi sana katika kwenda kazini na kurudi kazini, lakini kwa juhudi zao ambazo tunaziona wazi wazi hivi sasa kazi kubwa ambayo wananchi wanaifanya ni kutekeleza wajibu wao ndani ya sehemu zao za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza hali kadhalika linafanya kazi kama hiyo ya kutekeleza wajibu wao. Magereza pamoja na upungufu kadhaa ambao wanao lakini wanajitahidi kuhakikisha kwamba wananchi wenzetu wale ambao wamekabidhiwa mikononi mwao wanawalea vizuri na kuwaweka katika hali ya mafunzo mpaka kipindi wanapotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba kuna upungufu kadhaa ambao naiomba Serikali ijitahidi sana kuhakikisha kwamba upungufu huu unaondolewa. Suala kubwa la uchakavu wa Vituo vya Polisi ni suala ambalo linaathiri Jeshi letu, kuwanyima nafasi ya kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi. Vituo vingi ni chakavu, hakuna ofisi za kufanyia kazi vizuri na hata zile ambazo zipo, pamoja na udogo wake, lakini Polisi wanafikia hata kunyeshewa na mvua katika ofisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri alenge juhudi zake kuhakikisha kwamba vituo hivi vinakarabatiwa kwa haraka iwezekanavyo na pia kuweza kujenga vituo vingi zaidi. Nikitoa mfano wa kule kwetu Bagamoyo, Kituo kile tumekikarabati kwa harambee, kilikuwa kinavuja sana wakati wa mvua hata Ofisi ya *OCD* inabidi asogeze meza huku na kule wakati wa mvua; na hivi sasa baada ya harambee hizi ndipo kinaweza kufanya kazi vizuri. Najua hali kama hiyo inawaathiri wananchi wengi na Askari wengi katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, naomba Serikali yetu Tukufu iweze kuliangalia jambo hili na kuondoa kadhia hii nzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika miundombinu hii ya Vituo vyetu vya Polisi ni suala kubwa la uhaba na uchakavu wa nyumba za Polisi. Hili ni jambo zito sana. Polisi hawana makazi mazuri. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri umekuja na mpango wa ujenzi wa nyumba mpya 4100 na kidogo, lakini hizi hazitatosha kwa sababu uhaba tulionao ni mkubwa zaidi. Tunahitaji mpango mkubwa zaidi wa kuhakikisha kwamba Polisi wana mahali pazuri pa kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Bagamoyo tuna Askari 171, lakini chini ya robo ya Askari hawa wana nyumba za kuishi za Polisi. Wale ambao wana nyumba za kuishi za Polisi hizo chache, usiombe kuingia katika nyumba zile, kwa sababu ukiingia utatoka katika hali ya masikitiko na unyonge. Askari wetu hawa ambao wanatuwezesha sisi kuweza kufanya kazi vizuri na kulitumikia Taifa letu hili vizuri, wana haki ya kupata mazingira bora zaidi ili waweze kutumikia vizuri zaidi na sisi tupate ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wao wanapanga uraiani, sasa unapopangisha uraiani unakaa na wananchi hao hao ambao kesho unataka uwadhibiti, anapokudai kodi na kesho huyo huyo anayekupangisha nyumba ndiye amefanya makosa, sijui yeye kama Askari anafanya kitu gani! Haya ni madhila makubwa ambayo Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana Serikali ikajikita vizuri sana katika kuhakikisha kwamba nyumba; jambo kubwa sana, zito, muhimu katika familia yoyote ya baba mama na watoto; Askari wetu wapate nyumba ambazo ni nzuri zenye hadhi ya kazi yao na ambayo itawawezesha wao kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ningependa kusikia mpango ambao Serikali inauleta kuhusu ukarabati mkubwa zaidi na ujenzi mpya wa nyumba; ujenzi, ametutajia zile nyumba 4,000 lakini je, katika zile zilizopo ukarabati huu ataufanya kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuyataja yale ambayo yanawasibu sana na wakati mwingine kuzorotesha uwezo wa Polisi kufanya kazi. Uhaba

mkubwa wa mafuta na vipuri kwa Jeshi la Polisi ni jambo ambalo halina kificho. Hawawezi kufanya kazi vizuri kama magari yao hayana mafuta; kwanza magari ni machache halafu mafuta hakuna. Wakati mwingine inabidi kuombeleza; hata safari hii nimewapiga jeki kidogo Polisi katika Jimbo langu kwa kuwapelekea pesa za kununulia mafuta. Sasa haiwezekani ikawa mafuta ni ya harambee wakati ulinzi ni jambo la muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yetu Tukufu ihakikishe kwamba jambo hili inalisimamia kwa umakini. Mafungu ya mafuta yawe mazuri, vipuri vipatikane, vitendea kazi kama magari yawe angalau ya kutosha kuwawezesha Polisi wetu wafanye kazi inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii pia kuzungumzia hayo hayo kama nilivyozungumzia Jeshi letu la Polisi kwa Jeshi la Magereza, nao wako katika hali ngumu. Ofisi mbovu, hawana ofisi nzuri, miundombinu ya Magereza siyo mizuri, kwa maana ya mabweni ni haba, kuna mlundikano mkubwa wa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Serikali ikajikita kuhakikisha kwamba inafanya ujenzi mkubwa sana katika miundombinu ya Jeshi letu la Magereza ili nao waweze kufanya kazi vizuri. Pamoja na vitendea kazi lakini pia pamoja na sare. Siyo jambo ambalo linafahamika sana lakini jambo hili limeanza kunyemelea Jeshi letu la Magereza. Hata sare nayo imeanza kuwa pungufu ambayo itawakatisha moyo sana Wanajeshi wetu hawa. Ni muhimu sana Serikali ikajikita kuhakikisha kwamba hili haliwatii unyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri ililenga kufanya Magereza yetu ni Vituo vya Uzalishaji Kilimo, lakini Magereza yetu hayana vitendea kazi vya kilimo. Gereza kubwa kama la Kigongoni lenye zaidi ya ekari 6,000 katika Jimbo la Bagamoyo halina trekta hata moja, halina lori, gari ya Mkuu wa Gereza ni mbovu. Sasa ardhi ile ni nzuri kwa kilimo inayofaa kwa mpunga, safari hii Mkuu wa Kikosi ameweza kulima ekari 50 tu katika ekari 6,000. Kwa hiyo tuweze kufanya kweli…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. DKT. SHUKURU KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda umekwisha, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Almas!

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwanza nitoe pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri, lakini vile vile naipongeza Idara ya Magereza na Idara ya Uhamiaji kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa ujumla kwa kulinda amani na kulinda raia na mali zao hasa wakati wa uchaguzi uliopita huku Bara na uchaguzi ule wa marudio wa Zanzibar baada ya Mheshimiwa Jecha kuufutilia mbali uchaguzi wa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba niongelee suala la kurasimisha Sekta ya Ulinzi binafsi. Sekta hii ya Ulinzi inafanya kazi nzuri sana sambamba na Jeshi la Polisi. Wako Askari wengi sana, lakini naiomba Serikali ilete mchakato wa kuanzisha Sheria ya Ulinzi Binafsi *(Private Security Industry Act)* pamoja na Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Sekta ya Ulinzi Binafsi *(Private Security Industry Authority)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni haya yalianzishwa mwaka 1980 yakiwa mawili tu, lakini makampuni haya yamekua na kuwa makampuni 850 yakiajiri watu zaidi ya milioni moja na nusu kama Askari; lakini yanafanya huduma zifuatazo: ulinzi wa watu *(Man Guarding)* wanafunga mitambo kama hiyo tunayoiona hapo nje tunapoingilia, vilevile wanafanya upelelezi binafsi na wanafanya kazi ya ushauri *(Security Consultancy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu makazi yao yanaonekana, iko haja ya kuwatungia sheria. Sasa hivi hakuna sheria yoyote ya Sekta ya Ulinzi Binafsi na kwa bahati mbaya zaidi hata *GN* ya kuonyesha hii Sekta haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kutaja matukio ambayo yametokea kwa sababu hakukuwa na sheria. Liko tukio la Temeke pale *NMB*, ambapo walinzi binafsi waliuawa na majambazi na pia Polisi wakauawa. Sekta ya Ulinzi Binafsi ilipata tabu kujiamini kwa sababu Polisi walisimamia marehemu, yule wa Polisi na kumhudumia na kusahau yule Polisi au Askari wa Ulinzi Binafsi, jambo ambalo lilileta kidogo mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mnakumbuka kesi ya Kasusura, ambapo walinzi walitumwa kwenda kuchukuwa fedha Dar es Salaam, *Airport* wakaondoka na hizo fedha. Kulikuwa na kesi ya *NMB* wakati walinzi walitumwa kugawa mishahara, wakaondoka wakawavua nguo wakaacha na masanduku wakachukuwa fedha zao. Kwa hiyo, pangekuwa na sheria wangekamatwa wenye kampuni, siyo wale walinzi walioshitakiwa kwa sababu ya jinai!

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko kesi ya Shule ya Upili ya Tabora *Girls,* ambapo walinzi waliokuwa wanalinda lindo hilo mchana, usiku wakarudi wakaja wakaiba na bahati mbaya mlinzi mmoja akapigwa na kuuawa pale. Pangekuwa na sheria, mambo haya yasingetokea. Pia walinzi wanashtakiwa wanapoua, wanapopiga majambazi, lakini Polisi wakiua majambazi wanapongezwa. Hawa nao wanafanya kazi ile ile, kwa hiyo, kungekuwa na sheria, wangetambuliwa hao kwamba walikuwa nao wanapigana wakati wanalinda mali za raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala lingine baya; makampuni haya yalianzishwa mwaka 1980 kwa kupewa vibali, lakini bahati mbaya vibali vile sasa vinakaribia miaka 36 na waliopewa vibali hivyo wameshafariki, wamekufa, hawapo. Watu walioyarithi makampuni yale hawana taaluma kabisa ya Sekta ya Ulinzi Binafsi, lakini bado wanatumia vibali vile kuendesha Sekta ya Ulinzi Binafsi na mbaya zaidi, wana silaha. Kuna kampuni za silaha, mpaka 50, bunduki mpaka 100, mpaka 200 na hawa hawana taaluma yoyote ya ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuongelea kwamba kuna dhana tu kwamba inawezekana ziko sheria ambazo zinatumika kulinda au kuendesha Sekta ya Ulinzi Binafsi. Sheria hizi hazipo na imethibishwa kwamba sheria zote ambazo zipo hapa nchini hazikutungwa wala hazikuandaliwa kwa ajili ya kuendesha Sekta ya Ulinzi Binafsi, kwa sababu Sekta hii imeanza mwaka 1980 na Sheria nyingi zimetungwa kabla ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizitaje Sheria hizo: *Criminal Procedure Act ya Mwaka 1985; Penal Code Cap 16; Law of Contract Ordinance; The Evidence Act ya 1967; Civil Procedure Code ya Mwaka 1966 na; Police Force Ordinance Cap 322.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zote hizi zinaanza kutumika baada ya sheria inayofikiriwa ipo, kufeli, yaani Sekta ya Ulinzi wanalinda raia na mali zao, likitokea tukio, mali ikapotea au maisha yakapotea ndipo sheria hizi zinakuja kuchukua nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza, kwa kuwa makampuni ya ulinzi binafsi yanafanya kazi nzuri sana na kwa upande mwingine yametoa ajira zaidi ya milioni moja na nusu, lakini vilevile kila mahali penye uwekezaji kuna Sekta ya Ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndani mkishafunga Bunge kuna kampuni za ulinzi zinalinda hapa nje, Wizara zinalindwa, lakini vilevile kila mahali ambako sasa hivi kuna gesi, kuna makampuni ya ulinzi binafsi. Makampuni haya hatuwezi kuyaondoa sasa, lakini tunaweza kuyatungia sheria tuweze kuyadhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake, aje na mpango au mchakato wa kuanzisha Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi. Sekta hii ya Kampuni binafsi na kampuni za ulinzi, tunaweza kuitungia sheria na kuiwekea mamlaka ya kuziongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi tatizo ni nini, lakini miaka 25 ambayo nimefanya katika Sekta hii sikuona tatizo. Liko tatizo dogo tu kwamba, baadhi ya Polisi wana makampuni ya ulinzi na hiyo imekuwa inaleta hali ya migongano ya maslahi na wanashindwa kuishauri Serikali kwa sababu na wao ni wadau wa Sekta ya Ulinzi Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wengine wa Polisi wanaendesha kampuni za ulinzi na Ma-*IGP* karibu wote waliopita wana kampuni za ulinzi. Pia wana kampuni za ulinzi, yaani Polisi wengine wapo kazini na mchana ni Maafisa wa Polisi lakini jioni wana kampuni za ulinzi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wamekuwa kikwazo kutunga sheria na kuanzishwa mamlaka, kila mara wanajitetea kuwa eti Ibara 147 ya Katiba, ibara ya (1) inazuia kutungwa kwa Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunatunga Katiba inayopendekezwa, tulitafsiriwa nini maana ya majeshi yanayoelezwa katika Ibara ile ya 147 kwamba, majeshi haya maana yake ni majeshi ya JWTZ, Majeshi ya Anga, Majeshi ya Ardhi na Majeshi ya Maji. Siyo idara ndogo ndogo hizi za Sekta ya Ulinzi Binafsi na ndiyo maana Sekta hii imeendelea kuwepo kwa muda wa miaka 36 na hakuna mgongano kati ya yenyewe na Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni la maslahi binafsi ya viongozi wa Jeshi la Polisi wenye Kampuni za ulinzi; tuseme sasa basi, miaka 36 inatosha kuendesha nchi na Sekta hii bila Sheria, yaani *Private Security Industry Authority* pamoja na mamlaka ya kuendesha sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niachie wenzangu waongee, naunga mkono hoja hii moja kwa moja, lakini pia naomba kurasimishwa kwa Sekta ya Ulinzi Binafsi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Allan Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami nichangie katika Wizara hii. Kwanza naipongeza Wizara, Waziri na timu yake kwa kazi wanayofanya.

MWENYEKITI: Jiandae Mheshimiwa Masoud!

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia matukio makubwa ambayo siyo ya kawaida; Vituo vya Polisi kutekwa nyara, bunduki kuporwa, mauaji na uporaji wa mabenki na wenzetu Askari wanajitahidi kuhakikisha kwamba wanadhibiti hali hiyo. Ninayo maeneo machache ya kuchangia, lakini moja ni suala la watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoona kwenye hotuba zilizotangulia ni kwamba *ratio* ya Askari ni mmoja kwa 1,071 nchini kwetu hapa, lakini katika nchi zilizoendelea ni mmoja kwa 450. Sasa ni muhimu tukahakikisha kwamba tunafanya jitihada za makusudi kuajiri askari zaidi. Tumeona kwamba kuna wanaoajiriwa, lakini uwepo mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba pengo hilo linazibwa ili kuweza kuwa na usalama wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Jeshi la Polisi limekuwa linafanya kazi, lakini limekuwa na uhaba wa magari. Uhaba wa magari ni tatizo; matukio yanapotokea hawawezi kwenda kwa wakati kwa sababu magari hayapo na machache yaliyopo mengine ni chakavu. Kwa hiyo, ni muhimu ukatengenezwa mapango mkakati kuhakikisha kwamba Polisi wetu wanapata magari ya kutosha na yawepo maeneo yote hasa ya Vijijini kwa sababu matukio hayapo mijini tu na vijijini yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia liko tatizo la mafuta; Polisi wetu wamefikia hatua sasa ya kuwa ombaomba. Wanaomba mafuta kwa wafadhili mbalimbali, lakini wanapoomba mafuta, wanaomba kwa mhalifu mtarajiwa. Kwa hiyo, mhalifu mtarajiwa atakapofanya uhalifu, Polisi wanakosa nguvu ya kwenda kumkamata kwa sababu anakuwa ni mshirika kwenye utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wamezungumza suala la *BRN (Big Results Now)*. Suala linalojitokeza hapa ni kwamba mpango umeandaliwa vizuri na ulikuwa uanzie Dar es Salaam, lakini mpango wenyewe haujatengewa fedha za kutosha na hiyo ilikuwa ni *pilot study* ambayo baadaye ingesambaa kwenye mikoa mingine. Sasa ni muhimu ikaangaliwa namna mradi huu ufanyike na tuweze kuupima ndani ya mwaka huu mmoja na tuone kwamba tutasonga vipi mbele, lakini *intent* ya mradi huu ilikuwa kudhibiti vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu pia wana matatizo ya sare. Askari anatakiwa awe na zaidi ya *pair* mbili; lakini inapoonekana Askari anakuwa na *pair* moja tu, tunakoelekea huko Askari watakuwa wanavaa nguo za kiraia kama hatutakuwa makini. Kwa hiyo, ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la makazi, limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge waliopita, lakini tukiweka mkakati wa makusudi kwa

mwaka huu na kwa miaka inayokuja katika kipindi hiki cha utawala wa Serikali, miaka mitano ya utawala uliopo madarakani, tuna hakika kabisa suala hili litapata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo habari ya Magereza. Hapa nataka kugusia suala la msongamano. Msongamano huu, kuna namna mbalimbali ambazo zimeshazungumzwa, adhabu mbadala; wengine wafungwe uraiani wafanye kazi za kijamii. Hilo ni jambo jema, lakini inaonekana utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua sana. Hii ni kwa sababu sheria hizo zilishapita miaka mingi iliyopita, lakini bado hazitekelezwi. Kwa hiyo, nashauri mamlaka zinazohusika zitekeleze kikamilifu ikiwemo ujenzi wa Magereza mapya hasa katika Wilaya mpya ikiwemo Wilaya ya Mkalama. Hilo ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala lingine nyeti; mimi niko kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; tulitembelea kwenye Gereza la Isanga, kuna eneo ambako wako kuna watu waliohukumiwa hukumu ya kifo. Watu hao na wenyewe wanasongamana; na kwa sababu wamesongamana na utekelezaji wa adhabu hiyo unachukuwa muda mrefu, watu wameshakaa muda mrefu sana kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, ni vyema basi kukawepo na tafakari mpya, labda wabadilishiwe kifungo kiwe kifungo cha maisha, lakini waweze kufanya na kazi nyingine na waondoe msongamano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo, wako watu ambao rufaa zao hazijasikilizwa, wana haki ya kukata rufaa, lakini ma-*file* yao yako kwenye kanda nyingine. Kwa hiyo, wamekaa hawajui ma-*file* yao yatakuja lini na wameshakaa kwa muda mrefu. Nashauri zichukuliwe hatua za makusudi kabisa, ma-*file* hayo ya wananchi yaletwe, rufaa zao zisikilizwe na hukumu itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa bado niko kwenye Idara ya Magereza, kumekuwa na changamoto kubwa kwa Askari Magereza kwa sababu dawa haziko za kutosha. Ina maana wafungwa wakiugua Askari Magereza sasa wanachukuwa majukumu la kusaidia kutoa pesa zao mifukoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mahabusu wanapopelekwa kwenye kesi zao Mahakamani, imefikia mahali ambako wanapakiwa kwenye magari ya uraiani; na wenyewe wanatakiwa wawe na magari maalum. Mambo hayo yanatakiwa yaangaliwe kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa bado katika Jeshi la Magereza, kuna miradi mbalimbali kama vile miradi ya mifugo na miradi mizuri, tunasema tunataka nchi hii iwe nchi ya viwanda ikiwemo viwanda vya nyama. Tunaamini kabisa miradi hii ikiwekewa mitaji ya kutosha wanaweza wakatoa mchango katika kupeleka malighafi kwenye viwanda vya nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Jeshi la Magereza linakabiliwa na uvamizi kwenye maeneo yake. Kwa hiyo, tunaomba Wizara iangalie suala hili, viwanja vyote vya Magereza viweze kupimwa na wawe na hatimiliki ili migogoro na wananchi iweze kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, pamoja na mambo yote niliyozungumza, lakini liko jambo moja ambalo naomba Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba ilifanyie kazi. Lenyewe linahusu mfungwa mmoja ambaye ni binti, yuko Gereza la Isanga hapa, yule amekatwa vidole viwili; kidole cha mkononi na cha mguuni na yuko Magereza. Sasa huo ni unyanyasaji na ukiukaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba suala hilo Mawaziri husika walichukuwe, walifanyie kazi na walete taarifa. Binti yule ameshakaa muda kidogo kule ndani; akiendelea kukaa ndani ya Magereza na huku amedhulumiwa kiasi hicho, maana yake ni kwamba haki itakuwa haijatendeka. Ni vyema suala hilo lichukuliwe na lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono na nafikiri ushauri nilioutoa unaweza ukafanyiwa kazi na Wizara. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Masoud dakika tano na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis jiandae dakika tano.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru…

MBUNGE FULANI: Masoud yupi Mheshimiwa?

MWENYEKITI: Mh! Aah, Masoud wa *CUF*. *(Makofi)*

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajibu wetu wa Kikatiba, Ibara ya 63(2) ni kuishauri na kuisimamia Serikali na Serikali inapaswa isiwe na hofu wakati tunaisimamia na kuishauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ili kuepuka wizi, ubadhirifu na ufisadi, mikataba yote yenye utata naomba iletwe Bungeni. Kitendo cha Serikali kusema kwamba mikataba ni siri, ni ushahidi tosha kwamba Serikali inataka kuongeza nguvu katika wizi, ubadhirifu na ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mikataba yote yenye utata ambayo inaashiria wizi, ubadhirifu na ufisadi ni lazima iletwe hapa Bungeni tujue mbivu na mbichi, tuweze kupambanua, tuishauri Serikali tuisimamie Serikali. Mikataba

kuwa siri ni tatizo na ndiyo maana tunaunda Kamati siku hadi siku. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tatizo kubwa ambalo linaonekana ni namna gani ya udhalilishaji na matatizo ambayo yanawakumba wafuasi hasa wa upinzani kule Zanzibar. Tumekuwa tukisema muda mrefu sana kwamba kunakuwa na hila na njama za kuwadhalilisha Wapinzani Bara na Zanzibar, lakini kule Zanzibar tumeripoti Polisi kuhusu kuchomwa kwa Ofisi ya *CUF,* Dimani. Sasa ni mwaka mzima hakuna hata taarifa yoyote ya Polisi imesema. Tumeripoti Polisi, Baraza ya Dimani ya Chama cha Wananchi *CUF* kwamba ilichomwa moto, lakini nasikitika sana Polisi hadi leo hakuna walilojibu. Tumeripoti Polisi Baraza la Kilimahewa, Ofisi ya *CUF* ya Mjini Magharibi, lakini hadi leo hakuna kitu ambacho kimeonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wa *CUF,* Chwaka, walikamatwa, wakapigwa na mtoto wa kike akafanyiwa vitendo viovu, tuliripoti Polisi hakuna kilichotokea! Walivamiwa Mpendae kwenye Ofisi yetu ya *CUF,* wakapigwa, tukaripoti Polisi. Wote wanaopigwa hao ni *CUF,* tatizo ni nini jamani? Mmeruhusu mfumo wa Vyama vingi ninyi wenyewe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi, kuna wengine wanabambikiziwa kesi. Tuambiwe akina Eddy Riyami, Mansour Yussuf Himid, Naibu Katibu Mkuu Mazuruwi, Hamad Masoud wote hao, lakini tunaambiwa wengine wana kauli za uchochezi, tuseme wanaosema kwamba nchi hii hata ninyi *CUF* mkishinda, haikupatikana kwa vikaratasi; huo si uchochezi! Tunaambiwa ninyi *CUF* kama mnataka Serikali Zanzibar, mpindue, hiyo si kauli ya kichochezi! Wanasema kama mnataka Serikali Zanzibar nyie *CUF* pindueni, huo si uchochezi! Mbona hawa hawakamatwi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya hayakubaliki! Hayakubaliki kwa sababu Polisi inaonekana imeegemea upande mmoja. Tumbatu zimechomwa nyumba nane, Shambuli hana mahali pa kukaa, nyumba 61 zimevunjwa, tumeripoti Polisi, hakuna lolote ambalo limetokea; tatizo nini? Kuwa mpinzani ndiyo tatizo! Huo si uchochezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabango ya Kisonge yote yanaandika siku zote, lakini hii ndiyo hali halisi ilivyo. Tunaomba Polisi, mtuambie sasa, Serikali hii ni ya Chama cha Mapinduzi peke yake au ni ya Watanzania wote na vyama vingine? Hili halikubaliki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana vitendo viovu ambavyo vinafanywa na watu, wanafanyiwa wafuasi wa Chama cha Wananchi *CUF* na Vyama vya Upinzani, lakini Polisi wananyamaza; hili ni tatizo kubwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Sarayevo, Dimani tuliripoti vizuri na Polisi walituambia tutafanya uchunguzi wa kutosha, upelelezi haujakamilika. Upelelezi mpaka lini? Hawa akina Mansour, Eddy Riyami na wengine wote, tatizo nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, nimshauri sana Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Ndugu yangu Masauni uwe makini. Hata sisi hapa unapotujibu, unatujibu majibu ya ovyo ovyo ya ufedhuli, ya kiburi na kejeli, ndiyo maana tulikuwa tunakushauri kwamba ni vyema uvae viatu vya Pereira vizuri. Vaa viatu vizuri ili twende vizuri. Vinginevyo sisi tutakuwa hatuendi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ulikuwa ni utangulizi, dakika zenyewe ni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NIDA,* fedha ambazo zimetengwa hazitoshi, wanazalisha vitambulisho 3,000 kwa siku. Watanzania ambao wanatakiwa wapate vitambulisho hawapungui milioni 25; ina maana kwa hesabu, kila mwaka mmoja…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis dakika tano.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara ya kwanza nazungumza katika Bunge hili, basi nawapongeza na kuwashukuru Wapiga kura wa Jimbo la Nungwi kwa ujasiri wao wa kulirejesha Jimbo la Nungwi katika mikono ya Chama cha Wananchi *CUF* na wameielezea dunia kwamba Jimbo haliazimwi, kinachoazimwa ni kiberiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, naanza na ukamataji wa Jeshi la Polisi unaoendelea siku hizi, unakuwa hautofautishi baina ya majambazi na Polisi, namna wanavyowakamata raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya tarehe 19 mwezi wa Tatu, 2016 ndani ya Jimbo langu katika Shehia ya Kidoti, alikamatwa Mwalimu wa Chuoni, anaitwa Mwalimu Haji Mtumbwi. Mwalimu huyo alifuatwa Chuoni na mtu ambaye kavaa vizuri, hamjuwi kama ni Askari, isipokuwa ni mtu mzuri tu, akamwambia nina shida na wewe tuzungumze. Alipofika kwenye gari ambayo ilikuwa ni ya abiria, ndani anakuta watu wana bunduki na wanamwambia uko chini ya ulinzi na wakamwingiza kwenye gari kwa nguvu pasipo kujulishwa familia yake, pasipo

kujulishwa Shehia, pasipo kujulishwa Kituo cha Polisi chochote kilicho karibu. Alipoingizwa ndani ya gari, akafungwa kitambaa cheusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Polisi wana dhamana ya kulinda usalama na raia wake lakini wanakamata kama hawako katika sheria, wanamchukua mtu kama jambazi, siku tatu hajulikani aliko. Hii ni dhuluma. Jeshi letu la Polisi lisiendelee na mtindo huo. Kama kunatakiwa ushahidi, niko tayari twende na Waziri muda huu huu na mhusika yupo. Hii siyo njia nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja Tumbatu. Tumbatu kumekuwa na mgogoro siku nyingi sana. Tangu uanze Mfumo wa Vyama Vingi 1993 na 1995 uchaguzi wa kwanza, basi kumekuwa na migogoro ambayo inasababishwa na Jeshi la Polisi wenyewe. Kwa sababu 1995 alichukuliwa Ngugu Abbas Ali, wakaingia watu wa CCM wakamkamata wakamchinja kama samaki akapoteza *network;* kwa hiyo, akachukuliwa akapelekwa hospitali, alipopata fahamu yake akasema kwamba fulani na fulani ndio walionifanya hivi. Mpaka leo hakuna kesi wala hakuna aliyekamatwa. Nani atakuwa anasababisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 24, mwezi wa Kumi, 2015, siku moja kabla ya Uchaguzi wa tarehe 25 Oktoba, vikosi vya SMZ vilivamia katika Mji wa Jongowe, matokeo yake wakawakamata vijana wanne, wakawakamata wakaenda wakawatesa mpaka wakapoteza fahamu, walipookotwa, kuliko Ulimboka, namna walivyo. Nyang'anyang'a! Ripoti ikapelekwa Polisi Mkokotoni, hakuna hatua iliyochukuliwa. Jeshi la Polisi linashiriki kikamilifu katika kufanya hujuma za kuwaonea wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 29, mwezi wa Kumi, 2015, siku aliyotangazwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. John Pombe Magufuli, sherehe ziliwazidi wana-CCM. Sherehe ziliwazidi wasijifahamu, wakavamia Kijiji cha Kichangani, Tumbatu wakapigapiga watu kwa silaha za kijadi, wakachoma nyumba saba, wakavuruga hali ya amani na utulivu. Matokeo yake, walipokwenda kuweka ripoti hawa waliofanyiwa hivi, wamekamatwa wao na wana kesi wao, kesi namba 116/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa kumi ambao wamekamatwa na naomba nitaje majina yao Mheshimiwa Waziri uyachukue. Wa kwanza ni Baraka Haji Gora, Faki haji Makame, Haji Abdallah Juma, Haji Sheha Makame, Kombo Makame Kombo, Makame Juma Makame, Musa Haji Omar, Omar Haji Omar, Machano Omar, Faridi Hamis; wamefunguliwa mashtaka wao. Hili ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hujuma hizo kuna mama mmoja amechomewa nyumba yake, yumo ndani moto umeshika hadi juu ya paa.

Anapata tabu hajui pa kukimbilia. Alikimbilia uani. Alipokimbilia uani, akamshuhudia mtu ambaye anachoma, yule fulani.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Aaaah… *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Yussuf Kaiza ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa nami niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza kabisa kabla sijachangia nitoe masikitiko yangu kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano ambayo kwa kweli inajisifu kwamba ni Serikali ya Hapa Kazi Tu. Imezuia *television* isionyeshwe lakini *yet* tuko ndani tumejifungia sisi wenyewe, bado mnazuia taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani isisomwe. Inaonesha ni jinsi gani hamjiamini, hamjajipanga na hamjajua ni nini mnataka mlifanyie Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi; kuna mambo makuu mengi sana ya kuyazungumzia na kwa sababu ni dakika kumi, naomba nianze na Jeshi la Magereza. Ni dhahiri kwamba kwenye Jeshi letu la Magereza sheria ambazo zinatumika sasa hivi ni zile ambazo zilikuwa zikitumika wakati wa ukoloni; ni sheria ambazo zimepitwa na wakati. Leo unaweza ukakuta Askari Magereza kwa bahati mbaya, mahabusu au mfungwa ametoroka, atapewa adhabu labda ndani ya miaka mitatu tuseme, ambayo adhabu moja ya mfungwa kutoroka anatakiwa akatwe mshahara wake, nusu ya mshahara au robo ya mshahara, anatakiwa ashushwe cheo, anatakiwa asiende masomoni kujiendeleza na hata ikitokea huyo aliyekimbia amekamtwa, bado huyu Askari Magereza atatakiwa atumikie hiyo adhabu kwa miaka yote ambayo amepangiwa. Hii ni dhuluma na haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo mzima wa uendeshaji wa Jeshi la Magereza kiukweli unatakiwa ufumuliwe upya. Tunahitaji kufumuliwa upya kama walivyofanya kwenye idara nyingine. Kuna malalamiko mengi sana ambayo yamekuwa yakiendelea. Hata bila kufumba macho, ni dhahiri kwamba *Commissioner General* wa *Prison* amekuwa akilalamikiwa sana. Naomba kabisa mchunguze hayo malalamiko ambayo yako dhidi yake, myafanyie kazi. Kwa sababu tumekuwa tukizungumza, mnapuuzia, baada ya muda ukija kuchunguzwa, ripoti ya *CAG* inatoa yale ambayo tunayalalamikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wote wa Umma tumekuwa tukijaza hizi fomu za maadili, mwachunguze mali wanazomiliki, mishahara wanayopewa

ina-*reflect* uhalisia wa mali ambazo wanamiliki? Kuna ufisadi mkubwa sana ambao unaendelea kwa Viongozi Wakuu wa haya Majeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya Askari ni duni sana. Mwaka 2015 wakati wa bajeti nilizungumza hapa na mkasema kwamba mlikuwa mmetenga kujenga zaidi ya makazi 9,000. Leo tunavyozungumza, Waziri umekuja unatuambia mnajenga makazi 4,000. Tunapenda kujua yale ya mwaka 2015, hayo makazi 9,000, yamejengwa kwa kiasi kipi? Leo ninavyozungumza, kule Tarime Askari Magereza makazi wanayoishi hata ukienda kumweka sungura, atalalamika kwa nini anaishi kwenye ile nyumba. Leo unamweka binadamu, tena Maaskari Magereza ambao wana familia, kinyumba ambacho kilijengwa mwaka 1942, enzi za ukoloni mpaka leo hujaboresha na zaidi kipindi hicho walikuwa wakikaa Askari Magereza wachache, leo wanakaa wengi kwenye kijumba hicho kimoja, wana familia na mnajua kuna mambo mengine ya staha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta saa nyingine Askari Magereza wanawajibika kujijengea wenyewe vijumba. Tunaomba mnapokuwa mnasema nyumba 4,000, basi wajalini wale ndugu zetu ambao wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali hii ya Hapa Kazi Tu inakwepa kuzungumzia Lugumi ya Jeshi la Polisi, lakini inasemekana kuna Lugumi nyingine kwenye Jeshi la Magereza. Inasemekana kwamba kuna fedha zilitolewa kwa ajili ya mfumo wa utambuzi wa ndugu zetu ambao wapo Magereza; wafungwa na mahabusu, wanaojulikana kama *OMS (Offender Management System),* ilitolewa ili hizi *system* ziweze kufungwa kwenye Magereza yote nchini, lakini inasemekana hadi leo hakuna *system* ambayo imefungwa kwenye hayo Magereza. Nataka kujua kama ni kweli, hizo fedha zimekwenda wapi? Au hii ndiyo ile dhana ya kuendeleza Lugumi ndani ya Jeshi la Polisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, inasemekana pia kuna fedha zilitolewa kwa ajili ya kununua magari ndani ya Jeshi la Magereza ya kuwabeba mahabusu kutoka Gerezani kwenda Mahakamani na pia wale ambao unakuta wana-*escort*. Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwamba watajitahidi kutenga fedha na kuna baadhi ya wilaya mmenunua, lakini inasemekana kwamba kuna fedha zilitengwa. Sasa nataka nijue, kama hizo fedha zilitengwa na mzabuni alikuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, zimeweza kununua hayo magari mangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli zilitolewa, maana yake inasemekana zilitengeneza magari mabovu ambayo sasa hivi hayafanyi kazi na tunaendelea kuona kwamba Askari Polisi ndio wanasindikiza watu kwenda Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ni cha fedheha, ni *uniform*. *Uniform* mara ya mwisho kutolewa kwa hawa Maaskari Magereza, ambao nimefanya nao mazungumzo, ilikuwa ni 2009, mpaka leo hamjaweza kuwapa *uniform*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hawa Maaskari Magereza, labda hata na wa Jeshi la Polisi, ukiwatazama na wengine wamekuja hapa Bungeni, wana *uniform* tofauti. Viatu vyao vinatofautiana, maana yake wanajinunulia, *uniform* zao ziko tofauti. Halafu Serikali ambayo inawatumia hawa ndugu zetu, tena vilivyo katika kuwakandamiza wapinzani, mnashindwa hata kuhakikisha kwamba mnawastahi na mavazi yao, angalau waonekane ni watanashati, mnawadhalilisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza, kama mmeshindwa kuleta *uniform* kwa hawa Askari, kwenye mshahara wao waongezeeni fedha za posho ya kununua *uniform* zao ambazo wataweza kununua *uniform* zenye kiwango cha juu. Maana inasemekana kuna mtu mmempa tenda ya ku-*supply uniform;* na ni mke wa kigogo wa Jeshi la Magereza. Anafanya kazi *BOT, uniform* zenyewe anazoleta ni za kiwango cha chini, *yet* hawa Maaskari wetu wanakwenda kununua vile vitambaa, wakifua siku mbili havina kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza bado, hii Serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba chombo hiki muhimu kwa mustakabali wa maisha ya Watanzania inawaboreshea makazi yao? Inawapa mazingira mazuri ya kufanya kazi? Siyo tu mnawatumia halafu mnawaacha wanaishi kama watumwa kwenye nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni ucheleweshaji wa malipo; mafao ya Askari wastaafu na Mheshimiwa Waziri nimekupa *copy*. Kuna baba, ni Askari mstaafu sasa hivi ana miaka 70, tena bila huruma, ametumikia Jeshi kwa zaidi ya miaka 32; kuanzia mwaka 1962 mpaka 1995, anaitwa Simon Mirumbe. Amekuwa akihangaikia mafao yake kuanzia 1995 mpaka leo 2016, mnamzungusha tu. Mmemtumia lakini mnashindwa kumpa mafao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati Serikali ya Chama cha Mapinduzi itambue umuhimu wa Jeshi hili la Polisi, msiwatumie tu, bali muwajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni msongamano wa mahabusu kwenye Magereza yetu. Leo ukienda Tarime, lile Gereza limejengwa 1942, uwezo wake ulikuwa ni kubeba wafungwa na mahabusu 209, lakini kuna siku unakuta wapo zaidi ya 500 mle ndani. Miundombinu ni mibovu, choo hakitamaniki, watu wanabanana, magodoro yenyewe ni aah! Tumekuwa tukishauri humu ndani; kuna kesi nyingine hazihitaji hata kumpeleka mtu kwenye Gereza, lakini unakuta mnalundika. Leo ukienda Tarime, kufuatia uchaguzi wa Oktoba, kuna kesi za

kisiasa watu wako mle zaidi ya mia, wakati mnajua kabisa ile ni hatarishi kwa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, nataka kujua; na Mheshimiwa Ummy kama angekuwepo; unakuta mwanamke labda amekamatwa kwa bahati mbaya akiwa mjamzito, anapelekwa mahabusu Gerezani, inatokea anajifungua, yule mtoto aliyezaliwa naye anakuwa ni mfungwa au mahabusu kwenye lile Gereza. Nataka nijue Serikali mnajipanga vipi angalau miezi sita huyu mama muweze kum-*excuse* atoke Gerezani, aweze kumzaa mtoto wake ili mtoto asiathirike kwa yale… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Aah, mmenibania eeh! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Yussuf Kaiza na Mheshimiwa Sixtus Mapunda ajiandae.

MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami na-*declare* kwanza kwamba hii ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili.

MWENYEKITI: Dakika tano.

MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Chakechake kwa kuniamini kuja kuwawakilisha katika nyumba hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme maneno ya utangulizi yafuatayo. Kwa muda mfupi niliokaa katika Bunge hili, nimegundua kwamba kuna dhambi kubwa inayofanywa ndani ya nyumba hii muhimu. Dhambi kubwa ni kwamba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jukumu kubwa la Bunge ni kusimamia, kuishauri na kuielekeza Serikali. Bahati mbaya sana ni kwamba, walioko upande wa Chama Tawala wao wamekuwa Serikali na Wapinzani ndio wamekuwa washauri na waelekezi. Hii ni sawasawa na mkubali tu; ni sawasawa na wale wanaotoka Usukumani kusema wote ni Marais kwa sababu Rais ni Msukuma. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie; historia mara zote inatufunza, hatujifunzi historia. Isiwe shida, kila tunachowaeleza mkawa ninyi ni watu wa ku-*argue* tu. Yako mengi tuliyo-*argue,* yako mengi tuliyowaeleza mka-*argue,* leo mmeyafanya na kwa ufanisi mkubwa. Hiyo faida mmeipata ninyi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu; nilikuwa chuoni mara moja, wanafunzi wakawa wanaandamana kuhusu masuala ya mikopo. Huyu Makonda alikuwa Mwenyekiti wangu mimi nikiwa Katibu Mkuu wa *TAHIRISO,* wanafunzi walikuwa wakiandamana sana, tulipokwenda kuzungumza na Serikali tukawaambia shida siyo wanafunzi kuandamana, shida ni Serikali ya CCM kutowapa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijielekeze kwenye hotuba. Nina mambo matatu tu ya kuelekeza na naomba niyaseme kwa ufupi kwa sababu dakika zangu ni tano. Moja, ni ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na Jeshi la Polisi; na hii nita-*cite* zaidi Tumbatu Zanzibar; Mpendae ambapo Jeshi la Polisi limekwenda likanyang'anya vifaa, simu na baadaye wakawakanyaga wanawake katika vifua vyao na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anapokuja kuhitimisha hotuba yake aje atuambie kabisa ni lini ataileta ripoti ya matukio yaliyotokea Zanzibar? Kwa sababu kuna matukio makubwa ambayo ni ya ulinzi, ni ya kuweka amani na usalama wa nchi yetu. Kuna ulipuaji wa bomu katika nyumba ya Kamishna Mukadam na mengine mengi. Tunaomba Waziri akija hapa atuambie, ni lini ataleta ripoti ya matukio yote yaliyotokea Zanzibar na nani waliofanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, utendaji kazi wa Polisi kinyume na *PGO* yao inavyowaelekeza. Kwa mujibu wa *Police General Order,* kazi ya Polisi ni kulinda raia na mali zao, lakini si vinginevyo. Sasa hivi Polisi ni watu wa kudhalilisha raia wa Tanzania, zaidi Wapinzani. Kuna vitu vimetokea; kuna matukio kadhaa yametokea; kuuawa kwa Diwani wa Muleba, Mkoani Bukoba, kuuawa kwa Alphonce Mawazo, mtuletee ripoti na mtuletee taarifa; lakini pia kuteswa na kuwekwa watu zaidi ya saa 24 ndani ya Polisi bila kupelekwa Mahakamani, mtuambie mnatumia sheria gani? Kwa mujibu wa *PGO* yenu inaonesha kabisa kwamba Polisi anatakiwa kuweka…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Kingu, ajiandae.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Nimezifuatilia hotuba zile mbili vizuri na

michango michache ya waliotangulia, wamenilazimisha kufikiri baadhi ya mambo ambayo ningependa niyaseme jioni ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijiuliza hivi kwa nini kulikuwa na Serikali? Nikajiuliza kwa nini kulikuwa na Polisi, Magereza, Bunge na Mahakama? Ikanirudisha nyuma kwenye kumbukumbu yangu kipindi kile ulimwengu ulipokuwa hauna utawala kwenye *state of nature* na *human nature*. Nikawakumbuka akina Thomas Hobbes walivyokuwa wanaongelea; nikawakumbuka akina John Locke, Montesk, *Jean-Jacques Rousseau* na wengine wengi walivyokuwa wanaelezea dunia ilikuwaje kipindi kulikuwa hakuna utaratibu uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema hivi, kabla ya kuwa na huu mfumo tunaouona leo dunia ilikuwa *nasty,* ilikuwa *brutal,* ilikuwa inakatisha tamaa. Maisha yalikuwa mafupi, vita ilikuwa kwa kila mtu, kwa yeyote. Tena Thomas Hobbes anasema kwa lugha ya Kilatini, katika kipindi kile kulikuwa na *bellum omnium contra omnes,* maana yake *war of all against all,* yaani vita ya wote dhidi ya wote. Ndiyo tukatengeneza huu mfumo. Huu mfumo ulivyotengenezwa ulikuwa ni kwa ajili ya ku-*control* tabia za wanadamu na hulka yake. Usipom-*control,* atatumia mamlaka yake vibaya. Mwisho wa siku unapata kile kitu kinaitwa *survival for the fittest*. Wenye nguvu na wenye mabavu wataendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? nasema hivi ku-*respond* yaliyosemwa hapa na waliotangulia. Askari wanatumia nguvu zilizopitiliza katika kipindi cha chaguzi na wakaelezea maeneo na maeneo. Niwaambie kitu kimoja, kama wako makini, wao ndiyo wamewafanya Askari wafikie hatua hiyo, kutokana na ile ile hulka ya mwanadamu, akishajua kwamba hakuna kitu kinachom-*control* anafanya vitu vya ziada, anapambana katika jinsi anavyoona yeye mwenyewe inamfaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichotokea kwenye uchaguzi uliopita ambao mwenzangu ameusema pale wote ni mashahidi, nani ambaye alikuwa hajui kulikuwa na watu wanaitwa *red brigade* wakavalishwa kininja wakapewa mazoezi ya kupambana? Sasa mlitaka Askari waangalie *red brigade* wakiwa wamevaa kininja wamepambana ili nchi iwe ya makambale, vita *of all against all. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wanafanya kazi yao vizuri, ninyi mnakwenda mnasema yale yasiyowezekana. Nawaombeni ndugu zangu tuelewane. Tusipofika kwenye hatua hiyo, tunarudi kwenye *state of nature,* tunarudi kwenye *human nature*. Vitu hivi lazima viwe *regulated!* Lazima vitengenezewe utaratibu ili twende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utaratibu huu wa migawanyo ya majukumu, hawa ndugu zetu Askari nao lazima tuwaangalie ili wafanye kazi zao vizuri, watulinde vizuri, ili tufike siku wafanye ile kazi inayotarajwa kuifanya nchi hii iwe nchi ya wote yenye amani inayofuata sheria na utaratibu. Wana mambo ya msingi, inabidi lazima nao tuwaangalie. Waliosema Askari kwake kambini, walikuwa wana maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo Askari akatoka nyumbani kwa baba John alikopanga, akaenda ofisini, halafu anarudi akamkamate baba John, hiyo haiwezekani. Turudi kwenye utaratibu wa zamani kuwaandalia Askari maeneo ya kukaa na kuwapatia *facilities* zitakazowasaidia wakafanye *operations* zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi dakika zilizobaki ataongea Mheshimiwa Kingu. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Sawasawa! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa Lema ajiandae.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa heshima na taadhima nakushuru kwa kunipa nafasi. Waheshimiwa Wabunge na ndugu zangu Watanzania ambao tutapata fursa ya kulisikiliza Bunge letu, nina mambo ya msingi mawili ya kuyazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ieleweke kwamba tunaposema kitu kinachoitwa Serikali lazima tujue ya kwamba wajibu na kazi ya Serikali ni kuhakikisha inasimamia masuala mazima ya ulinzi na usalama ukiachilia mbali masuala ya kiuchumi. Nimeshawahi kubahatika kuwa Kiongozi wa Dola katika mbili ya Wilaya katika Taifa hili. Nataka niwaambie tunaweza tukazungumza mambo hapa kwa sababu ya kishabiki na mihemko ya kisiasa, bila kuangalia masuala mazima ya hatma ya nchi. Ninachotaka kukisema, duniani kote ili watu waweze kukaa kwa amani na utulivu, ni lazima Serikali ijulikane kwamba ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala zima la Serikali katika kuwekeza kwa Jeshi la Polisi. Yamezungumzwa maneno mengi, lakini nataka nikwambie sisi wenyewe Wabunge wa CCM haturidhishwi na hali ya Askari wetu wanavyoishi. Tunaiomba Serikali yetu ifanye hatua za makusudi, kwanza kuwapatia posho katika mazingira magumu ya kazi wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka, kuna wakati mimi kama Mkuu wa Wilaya ya Iringa, nimeletewa taarifa mabasi yametekwa pale Igunga.

MBUNGE FULANI: Umeona eeh!

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza na Askari, *OCD* hana mafuta ya kupeleka Askari. Haya lazima tuyaseme kwa sababu tusipoyasema tutakuwa hatulitendei haki Taifa letu. Natoa wito kwa Serikali yangu, natoa wito kwa Jeshi la Polisi, tengenezeni *unit* maalum itakayokuwa ina-*deal* na suala la kuhakikisha *supply* ya mafuta kwa Ma-*OCD* nchi nzima. Mafuta haya yasipite kwa Ma-*RPC* yaende kwa Ma-*OCD* kule kwa sababu wakati mwingine *OCD* anaweza akashindwa kumwambia bosi wake, tunao uzoefu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Sekta ya Madawa ya Kulevya. Wiki tatu zilizopita kabla Bunge halijaanza, Kamati yetu tumefanikiwa kwenda kuangalia *depot* inayohifadhi madawa ya kulevya. Tumekwenda pale, mazingira wanayofanya kazi Askari wetu, Mheshimiwa *IGP* uko hapa, najua utanisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Jeshi la Polisi angalieni namna ya kuwasaidia Askari wanaopambana na watu wanao-*deal* na *drugs* muwa-*treat* kwa *special treatment*. Tumekwenda kumkuta binti mmoja anafanya kazi kwenye lile ghala ndani hana *gloves*, hana chochote, amevaa malapa ndani ya ghala la kuhifadhi madawa; ukiangalia ukuta umechakaa mpaka umeweka rangi ya njano. Sasa je, kwa binti wa Kitanzania anayefanya kazi; naliomba Jeshi la Polisi liweze kuwasaidia katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, tumekuwa tukizungumza suala zima la kupambana na madawa ya kulevya, lakini leo tunazungumza kwamba Jeshi letu la Polisi hawana hata boti za doria baharini. Linapotokea suala la kufanya *surveillance* kwenye bahari, hawana boti. Wanawezaje wakafanya kazi watu hawa? Natoa wito kwa Jeshi letu la Polisi na Serikali, naiomba Serikali ifanye kila inaloweza, wapatieni Polisi boti za kisasa, angalau tatu wakafanye doria baharini kupambana na masula mazima ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho. Kuna mengi yamezungumzwa hapa, mambo ambayo kimsingi nimeshangaa sana! Namheshimu sana dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko, ni rafiki yangu, nampenda, lakini kusema kwamba hotuba ya upinzani imezuiliwa, nimeshangaa kidogo. Kama mmezuia hotuba ya upinzani, hili naomba mlitolee ufafanuzi, kama kuna hotuba imezuiwa kusomwa hapa. Kwa sababu sijaona kama kuna hotuba imezuiwa kusomwa hapa Bungeni, *unless otherwise* kama kutakuwa kuna jambo lingine.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kingu!

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimtie moyo kaka yangu Mheshimiwa Kitwanga, tumekwenda kwenye *unit* inayo-*deal* na kuangalia *sample* za madawa, ndani ya kipindi cha miezi mitatu, Mheshimiwa Kitwanga amesimamia, tumeona *sample* 256 za madawa ya kulevya ndani ya miezi mitatu. Leo tunavyozungumza mipaka yote hakuna madawa yanaingia kwenye nchi yetu. Mheshimiwa Kitwanga fanya kazi, tunakuunga mkono na sisi tunajua mnachokifanya kwa maslahi ya Taifa hili. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema!

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja!

MBUNGE FULANI: Safi sana!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Sixtus akisema dakika zake, nilishamtaja Mheshimiwa Kingu na yeye alikuwa na *slot* yake. Kwa hiyo, yeye alikuwa na dakika kumi kamili. Naomba kuwaeleza, hamna cha aah, *referee* akisimama wewe unakaa kimya tu. Mheshimiwa Lema! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Leo nilikuwa nisome hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni; hotuba hiyo kimsingi haikuwa mbaya hata kidogo. Waheshimiwa Wabunge, wenzangu wa Chama cha Mapinduzi tafuteni hiyo hotuba muisome, muitathmini mwone wapi kulikuwa na makosa ya msingi ya kuiondoa Bungeni, kama siyo tu hotuba ile ilikuwa na busara ya kusaidia Jeshi la Polisi na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nimwambie rafiki yangu Mheshimiwa Kitwanga, nilimwambia Mheshimiwa Sitta kwenye Bunge hili, kipindi kile Mheshimiwa Lowassa alikuwa yuko CCM. Nilimwambia ukiona Kambi ya Lowassa inakushangilia wewe kuwa Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, maana yake usisherehekee, maana yake ujiulize kwa nini nashangiliwa? Hili jambo linalohusu Mkataba wa Lugumi halikuwa kwa ajili ya kuidhalilisha Serikali, ilikuwa ni kwa ajili ya kuiondolea doa Serikali. *IGP* anasemwa, Waziri unasemwa, Jeshi lote la Polisi linasemwa na mkataba mchafu wa Lugumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kitwanga ni rafiki yangu, haya mambo ambayo nimeandika, nimejadiliana naye nyumbani kwake tukiwa tunakula ugali. Nikamwambia mimi ni kipindi cha pili kuingia Bungeni, nazijua siasa za Bunge, nakuomba Mheshimiwa uniambie mimi kama Kambi ya Upinzani naweza nikasaidia mambo gani ambayo Serikali hamwezi kuja nayo *direct*? Nikamwambia usiponiambia, mimi nitakunyooshea na nitataka majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza swali ambalo nimeambiwa niliondoe kwamba, hivi Kamati ya Bunge inavyotembea kote huko kutafuta sakata hili la Lugumi, *CAG* anashindwa kutuambia kama mkataba ule ulikuwa thamani yake ya fedha na vifaa ni *okay* ama ni *no!* Anashindwa kujua!

Nikauliza swali lingine ambalo nimeambiwa niliondoe na Kamati; hivi Mheshimiwa Kitwanga wewe ni mbia wa *enforce* na ni Waziri wa Mambo ya Ndani; na Kampuni hii ya Lugumi iliingia kwenye biashara ukiwa siyo Waziri. Je, kama umekosa taarifa kutoka Jeshi la Polisi ambalo liko chini yako, umekosa pia taarifa kutoka kwenye kampuni ambayo ni mbia, ukijibu haya maswali Bungeni, utaondoa ukakasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikauliza swali lingine ambalo nimeambiwa niliondoe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema…

WABUNGE FULANI: Aaaaaah!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, nakujua wewe ni mzoefu kwenye Bunge, najua uwezo wako. Unatumia njia nyingine kusoma hotuba yako hapo ulipo. Sasa nakusihi, sababu maneno hayo unayosema ndiyo yamekatazwa kuanzia ukurasa wa kumi. *(Kicheko/Makofi/Kelele)*

Unajua Mheshimiwa Lema, hawa wanapiga vijembe kama mpirani. *Referee* akipiga filimbi, watu wanalalamika, lakini Serikali, *referee* anakuwa *strict*. Jiepushe na maneno yaliyopo kwenye ukurasa wa kumi mpaka wa kumi na nne.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajiepusha na hayo maneno, lakini Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, nikiangalia Wabunge wote hapa ni wapya kwa asilimia 50. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: *Seventy!*

MHE. GODBLESS J. LEMA: Ama *seventy*. Wabunge tuliokuwepo Bunge lililopita, hatukuwa hawa ninaowaona hapa. Waheshimiwa Wabunge pamoja na itikadi za vyama vyetu vya siasa, inapokuja kwenye suala la maslahi ya nchi yetu, tuache hizi siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkisema mambo ya msingi kama haya tusiyaongee, ndiyo sababu uliponiita hapo mbele nilisema basi ngoja na mimi tu nimshukuru mke wangu kwa kuja Dodoma. Kama mambo *serious* kama haya Kambi inakatazwa kuongea, tunaisaidiaje Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Mambo ya Ndani, unapokuwa na *IGP* anayesemwa vibaya na hakuna kauli ya Serikali, unafanya Jeshi la Polisi lidharaulike. Unapokuwa na Waziri wa Mambo ya Ndani anatiliwa mashaka kwa mambo ambayo ama ni ya magazeti au mitandao na hakuna majibu, unafanya Wizara idharaulike. Wizara ya Mambo ya Ndani ikidharaulika, ni nchi imedharaulika usalama wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu utakuwa umeipata ambayo ina mambo nimeambiwa nisiyasome. Wewe yajibu tu kimkakati ili uwe na amani. Nakwambia jambo hili halimhusu Lugumi. Lugumi *is nothing in this Parliament!* Mtu anayetafutwa humu ni wewe. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Lugumi niliambiwa nisiseme kuanzia hapa chini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, nitazame mimi.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Zungumza na mimi.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu, hii wanataka kutengeneza mlima kutoka kwenye kichuguu. Hii wanaacha *pressure* iendelee, wanakutafuta wewe. *You will tell me my brother, you will tell me!* Mimi najua siasa za Bunge humu! Unajiuliza, hii hotuba ina makosa gani? Haina makosa, wanataka *pressure* iendelee. Wanasema wewe ni rafiki wa karibu wa Magufuli, nawe ndiyo kiherehere mkubwa, kwa hiyo, wanakutafuta wewe! Wanakutafuta! *(Makofi, Vigelegele/Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mimi nakuambia…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema kaa chini.

MBUNGE FULANI: Waambie hao!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, jina la Rais limetolewa kwenye hotuba yako…

WABUNGE FULANI: *Aaaah! (Kicheko/Kelele)*

MWENYEKITI: Kanuni ya 64, inakataza usitumie jina la Rais humu ndani. Mheshimiwa Lema, Kanuni ya 73. Nikiitumia Kanuni ya 73 adhabu yako itakuwa kukatishwa kuzungumza na ukae chini. Endelea! *(Kicheko/Kelele)*

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu huyu mwema, nikilitumia hivyo kuna shida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu huyu mwema wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni rafiki wa karibu wa Mheshimiwa Kitwanga. Kwa hiyo, nasema kwamba jambo hili siyo jambo dogo, nami maswali niliyokuwa nauliza ambayo nimezuiwa; Waheshimiwa Wabunge, nakatazwa kwenye hotuba yangu hata kuuliza. Jamani leo Mheshimiwa Kangi amenishangaza! Mheshimiwa Kangi anasema, Mheshimiwa Chenge hajawahi kutuhumiwa na *scandal* ya Rada. Mheshimiwa Kangi! *(Makofi/Kelele)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema! *(Kicheko/Kelele)*

Mheshimiwa Lema, nisikilize vizuri. Mbunge au Waziri atakayezungumza jambo au mambo ambayo hayaruhusiwi na kanuni hizi, anaweza kuamriwa na Spika au Naibu Spika au Mwenyekiti akatishe hotuba yake na kukaa pale alipo. Unazo dakika nne na ukienda kwenye *maginal notes* hii ni adhabu. Katika dakika nne hizi nakuomba jikite kwenye mazungumzo ya kawaida. *(Makofi/Kicheko/Kelele)*

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naongea nini? *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Mwambie akuandikie! *(Kicheko)*

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*. Naongea nini? Mbunge yeyote ndani ya Bunge hili, zawadi pekee ambayo anaweza akaipa familia yake ama wazazi wake ama nchi yake ni kuthubutu kusimamia ukweli unaolinda Taifa hili. Yeyote! Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, bendera zetu zisiwe na nguvu kuliko hadhi ya nchi yetu. Tusaidie hii nchi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwaambia na nawaambia tena, hatutashinda uchaguzi kwa sababu ninyi ni wabaya, tutashinda uchaguzi siku ambayo watu wataamua tushinde uchaguzi na kuwepo kwa Demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu amesemwa kwenye Bunge lililopita na kwenye magazeti. Kuna watu walisema mwaka 2015 kwamba kuna siku

tutam-*miss* Kikwete, mimi nimeanza kum-*miss* Mheshimiwa Kikwete. Hakuna mtu alisemwa kama Rais Kikwete! *(Kicheko/Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kweli kabisa!

MHE. GODBLESS J. LEMA: …lakini hakuwahi kuingilia Mhimili wa Bunge. Hakuwahi kuingilia shughuli za Bunge. Bunge hili lilikuwa linamsema Rais Kikwete kwa namna yoyote ile, Mawaziri akina Mheshimiwa Jenista mlikuwepo, hamkuwahi kuingilia! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuisaidie hii nchi, tuvuke mipaka ya *party caucus* zetu tusaidieTaifa hili. Kuna mtu mmoja yuko Magereza huko, alipokuwa jela aliulizwa na Wakili wake; aliambiwa, lakini wewe ulikuwa Waziri, wakati mnapitisha hii sheria ya kwamba ukikamatwa na makosa ya ufisadi wa fedha za umma ni lazima ulipe *50 percent* kama *bail,* ulikuwa wapi? Akasema nilikuwa kwenye kikao hicho lakini sikuona jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikao hivi tunavyofanya shughuli za Bunge, tunavyohudumu kama Wabunge, iko siku dhambi tunazozifanya humu zitakuja kuwala watoto wetu na watoto wetu kwa sababu tulishindwa kusimamia ukweli. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri…

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Lema. Namwita Mheshimiwa Serukamba na Mheshimiwa Msigwa ajiandae. *(Makofi)*

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kitwanga kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ndani ya nchi yetu. Tumeziona juhudi zako za kupambana na ujambazi, madawa ya kulevya, kusafisha pale Uhamiaji, Waziri Kitwanga endelea na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimekishangaa sana Kiti chako kwa sababu, labda Kanuni zinawezekana zimebadilika. Wenzetu wa upinzani walipewa

nafasi ya kutoa maoni ya upinzani. Wameamua wenyewe kwa mapenzi yao, kuondoa hotuba yao mezani. *(Kicheko/Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao hili Bunge wanalifahamu, hii siyo mara ya kwanza, Wapinzani kuambiwa kutoa maneno wakatoa. Hii siyo mara ya kwanza! Mheshimiwa Tundu Lissu aliwahi kuleta wakati wa bajeti, miaka mitano iliyopita, akaambiwa maneno haya hayafai na kwa sababu ni muungwana akaenda kuyatoa akaja akasoma *speech* yake. Leo kwa sababu wanayoyasema kwanza hawayaamini, hawana uhakika nayo, ndiyo maana hawawezi kuyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi ngoja tuseme suala la Lugumi.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti…*(Kelele)*

WABUNGE FULANI: Imezuiwa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Serukamba!

MBUNGE FULANI: Wewe ulipewa shilingi milioni 100 na Manji ukatuletea...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Serukamba! *Order please!*

MBUNGE FULANI: Wewe ulituletea shilingi milioni 100 wakati wa kampeni wewe!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, suala la Lugumi limetolewa kwa pande zote. Naomba mchangie vitu ambavyo kwenye Mwongozo wa Spika yametolewa. Naomba kabisa kwa pande zote zilizokuwemo humu ndani, tunataka tumalize, Serikali ikafanye kazi. Endelea.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kwa kazi kubwa anayoifanya. Mambo mengine yalikuwepo huko nyuma, kuanzia mwaka 2011 hakuna aliyeyaona; mwaka 2012, hayakuonekana; 2013 hayakuonekana; 2015 hayakuonekana. Hayakuonekana kwa sababu Kamati hizo waliokuwa wanaongoza wanafahamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti… *(Makofi)*

TAARIFA

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kwamba taarifa ambayo *PAC* waliifanyia kazi ni taarifa ambayo *PAC* ya mwaka 2013, iliagiza uchunguzi wa *CAG* ufanyike. Kwa hiyo, anaposema kwamba 2011, haikufanyiwa kazi; 2012, haikufanyiwa kazi; 2013 haikufanyiwa kazi, analipotosha Bunge. Nilikuwa naomba aifute hiyo na aendelee na mchango wake. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Serukamba, unaipokea taarifa!

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yenyewe nimepewa na mdogo wangu, kwa bahati mbaya leo naikataa kwa sababu angesubiri nimalize angeweza kunisikiliza vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aeshi amefanya kazi kubwa sana kwenye Bunge hili. Amechukua hatua, jambo analifanyia kazi, Kamati zinazunguka nchini kufanya kazi. Sasa leo anapokuja mtu mwingine, anasema amekuja na maswali, ningetamani niyasikie. Maswali hayo, huyu mtu anawahisha shughuli na inawezekana nia yake siyo njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema nia ni kuisimamia Serikali, Serikali inasimamiwa kwa utaratibu. Wengine inawezekana wamekuja jana ndiyo maana hata heshima ya Kiti hawaijui. Upande wa CCM watu wameongea hakuna watu waliokuwa wanazomea; lakini kwa sababu ya ugeni, mnadhani mkizomea mnafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Aeshi inafanya kazi, tuiache ifanye kazi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, ukiona adui yako anasema anakupenda, ujue huyo ndiyo mbaya wako. Maana kama mtu mmekwenda mmealikana, mmekula chakula, wakati mnaalikana hamkutuambia, lakini mnavyokuja leo mbele ya Bunge hili kusema mliyoyaongea, siyo mapenzi hayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri endelea na kazi na bahati njema yote yanayosemwa, kwa namna yoyote ile huhusiki na hili Bunge litasimama kwenye haki. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Magufuli… *(Kicheko/Makofi)*

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Serukamba hebu kaa kwanza. Waheshimiwa Wabunge, jina la Rais halitakiwi kutumika kwa kejeli. Ndiyo Kanuni! Mpende, msipende, habari ndiyo hiyo! Endelea. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya nchini. Mheshimiwa Rais anarudisha *discipline* ndani ya nchi yetu, anasimamia mapato ya nchi yetu, kazi hii kubwa anayoifanya siyo wengi wangependa, lazima waumie. Naomba tumpe moyo, aendelee kufanya kazi ili apeleke nchi yetu kule tunakotaka iende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Polisi wa nchi yetu. Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa sana. Nchi yetu leo ina amani kwa sababu vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi, vinaheshimika sana duniani. Hakuna jambo la hovyo kama tunavyokutana kama Bunge, tunaanza kukejeli vyombo vyetu vya ulinzi vinavyofanya kazi nchi hii. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana watu wa uhamiaji kwa kazi. Leo hii ukiwa unataka kuomba *passport* utaipata baada ya muda mfupi sana, hili ni jambo jema, naomba liendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia maslahi ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama yaangaliwe upya ili maslahi yao yaongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Mheshimiwa Waziri Kitwanga endelea kufanya kazi, Bunge hili linakuamini na tuna hakika utatupeleka tunakotaka kwenda. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Msigwa na Mheshimiwa Lugola ajiandae.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Baada ya kumaliza uchaguzi wetu wa nchi mwaka 2015, mlishangilia kwa mbwembwe nyingi sana kwamba Serikali na Chama cha Mapinduzi mmeshinda kwa kishindo, mkawaaminisha Watanzania kwamba mnaweza kuongoza nchi hii. Watanzania wakawasikiliza, mkaunda Serikali yenu. Tukaja Bungeni hapa tukaapishwa. Siasa za nje tukazileta Bungeni na ndiyo maana hivi vipaza sauti vimewekwa hapa kwa ajili kuzungumza. *It is about talking!* Ni juu ya *dialogue* hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mnakuja na hoja zenu mnaendelea kuwashawishi wananchi kwamba sisi tuna uwezo wa kuongoza nchi hii, mnaleta hoja. Nasi tuliowapinga tunakuja na hoja zetu kuwakatalia kwamba hizi hoja haziwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo hii Serikali inayosema ni ya Hapa Kazi Tu, Wabunge 250 wa Chama cha Mapinduzi na Serikali yao inashindwa kujibu hotuba ya kurasa 34! Inataka kuwaambia nini Watanzania? Kama kurasa ya 34 Wabunge 250 wa Chama cha Mapinduzi wanaogopa isisomwe, ninyi ni *mature* wa kuongoza nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yetu tunakuja hapa tuna-*dialogue,* sisi ndivyo tunavyoiona Serikali, tunaoliona Jeshi la Polisi linafanyaje? Mikataba ya hovyo ikoje? Mtazamo wetu wa pili kwenye *view* yetu, *this is how we see*. Njooni na hoja mwoneshe udhaifu wetu uko wapi? Muwaaminishe Watanzania kwamba *we are not matured*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla hatujaendelea, hatujazungumza, mnaweka mpira kwapani, mnataka msaidiwe na marefa. Suala la kujiuliza, *you guys are you fit to lead this country?* Kama hotuba ya ukurasa 30 hamwezi kuijibu, nani asiyejua mizengwe ya nyumba zilizouzwa katika nchi hii? Nani asiyejua nchi hii ina mikataba mibovu? *(KichekoMakofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa! *(Kicheko)*

WABUNGE FULANI: Aaaaaaa! *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, mimi sichoki kusimama. Suala la nyumba limekatazwa kwa mujibu wa Kanuni.

WABUNGE FULANI: Aaaaaaa! *(Kicheko/Kelele)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa! *(Kelele)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Sawa Mheshimiwa Mwenyekiti, sitalitumia tena. *(Kelele)*

MBUNGE FULANI: Tulieni mabebi. *(Kelele)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda mwingi hamtumii Bungeni kusikiliza Kiti kinasema nini. Sakata la kuuzwa kwa nyumba za Serikali, ukurasa wa 15 aya ya kwanza hadi ya tatu kuondoa maneno yanayomhusisha Rais. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekusikia, sitalitaja tena. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Alikuwa Waziri wa Ujenzi. *(Kicheko)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Huyu Rais, mwema! *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Mzuri kabisa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Ambaye anatakiwa ashangiliwe kama *King* Kanuti, hatakiwi kuguswa katika Bunge hili. Nirudie maneno aliyozungumza Mheshimiwa Sugu; huyu Rais Mwema mnamfanya wananchi wasimwelewe. Yeye siyo Mungu, ana hali ya ubinadamu anaweza akakosea. Lengo letu hapa tupo kuisaidia Serikali na ndiyo dhana nzima ya kuwa na mfumo wa vyama vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza wenzangu hapa jinsi ambavyo mnawatumia Polisi, wakati wa uchaguzi mnawapa majina mazuri yote, lakini maisha wanayoishi ni ya shida sana. *You are just using them!* Mnawatumia wakati wa uchaguzi. Nawaomba ndugu zangu na niseme nyie mnaosema usalama wa nchi hii ni sababu ya ulinzi na usalama wa Jeshi la Polisi.

Mimi kama Mkristo na Mchungaji, Biblia inasema, Mungu asipoulinda mji…*(Kelele)*

MBUNGE FULANI: Hajasema Rais kauza nyumba jamani!

MWENYEKITI: *Order, order!*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mungu asipoulinda mji, wakeshao wafanyakazi bure.

MBUNGE FULANI: Wewe unamchunga nani wewe?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Tanzania ina usalama…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, hebu kaa. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: *Use brain to think*!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge wa upande huu…

MBUNGE FULANI: Wa CCM!

MWENYEKITI: Kanuni ya 60 hairuhusu mtu kusema kitu bila kibali cha Kiti. Sasa Mheshimiwa Mchungaji Msigwa anazungumza na Kiti, hazungumzi na nyie. Kwa hiyo, nataka amani kwenye Bunge hili. *And I won't fall short* kumtoa mtu yeyote nje. Mmenielewa jamani! *(Kelele/Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Mbona wao wanazomea! *(Kelele)*

MWENYEKITI: Unaona sasa Mheshimiwa Sadifa! Najaribu ku-*maintain order* humu ndani; na ukitaka kusema kitu utasimama nikuruhusu, ndiyo Kanuni zinavyosema. Unaona Mheshimiwa Sadifa, hii ni *last warning!* Kila anayesema, namwonya. Haimaanishi tunaonya upande upi, tunaonya pande zote zinazovunja Kanuni za Bunge. Hii ni *warning* ya mwisho naitoa. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utunze muda wangu tafadhali. Narudia tena, Bwana asipoulinda mji, wakeshao wafanya kazi bure! Biblia inasema mji haulindwi kwa wingi wa silaha anazokuwanazo mfalme. Ni Mungu ameamua ku-*sustain* amani ya nchi hii. Kama tutaendelea kucheza kwa kuamini kwamba bunduki na vifaru vitalinda amani ya nchi hii, tunapoteza muda. Ulinzi wa Muammari Gaddafi ulikuwa ni mkubwa kwa mbali kabisa kulinganisha na ulinzi wa nchi hii; lakini yuko wapi leo? Bwana asipoulinda mji, wakeshao wafanya kazi bure? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Jeshi la Polisi, msitumike vibaya kisiasa, nchi hii ni ya mfumo wa vyama vyingi, sisi hapa hatujaja kwa fedha, tumekuja hapa kwa *merit*. Tuna haki hizo! Mnabambika watu kesi! Kama Mbunge, mimi nimebambikwa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya uchaguzi, kulikuwa kuna yule Mungi sasa mmempandisha cheo ameenda bandarini. Ameagiza Polisi wanakuja kunivamia, wamepiga watu, wamevunja miguu, mikono, mwisho wa siku, wiki mbili zimepita sipelekwi Mahakamani mpaka nikaanza kudai na Wakili wangu kwamba mmetupiga, wakatulaza kwenye bwalo wanawake na wanaume! Mimi ninayezungumza! Tunadai kwa nini hamtupeleki Mahakamani? Napelekewa *charge* eti wewe umemjeruhi Kamanda wa *Field Force*. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Wewe Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mimi Msigwa namjeruhi Kamanda wa *Fied Force;* na la pili nimejeruhi gari la Polisi. Kesi imekwenda Mahakamani wiki mbili, imefutwa; haina mkia wala miguu. *(Kelele/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Jeshi la Polisi, hebu acheni kutumika kisiasa. Tupo kwenye nchi ya vyama vingi. Kazi yetu kubwa hapa ni kuiweka

Serikali sawasawa mwone wenyewe, nanyi Makamanda wa Polisi mnaona jinsi gani Serikali inashindwa kujitetea hapa! Kurasa 34 wanashindwa kujibu, *they cannot!* Nchi imejaa hofu, watu mmejaa hofu, huyu Rais mwema sana amewatia hofu mnaogopa kujitetea na kusema. *Why? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Plato anasema: "*if you cannot die for something, you are not worth living*." Sisi tupo tayari kwa lolote kwa sababu tunataka tuinyooshe nchi kwa faida ya vizazi vijavyo; na wajibu wetu ni kuikosoa Serikali, kuiweka vizuri. Haya tunayoyashauri, mangapi tuliwashauri? Tuliwashauri jambo la Katiba, mkalichukua, ila kwa sababu hamna ubongo wa kuku, mkashindwa. Si mlishindwa! Tuliwashauri, mkachukua. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwashauri suala la elimu bure, mmejikanyagakanyaga, mnashindwa na yenyewe. Mngetupa hapa, hiki ni kisima cha kupata hekima na busara tunataka tuwashauri. *You are incapable of leading this nation.* Hapa ni mahali pa ku-*dialogue*. Ambao hamjasoma historia, nendeni Ugiriki mkaangalie Wagiriki walikuwa wanafanyaje kule *Heathen*. Unakuja na hoja unazijenga! Tumehamisha siasa kule, hapa ndiyo tunajadiliana, njooni na hoja. Sasa mmetunua macho, hamwezi kujitetea, mnajaza hofu watu, wafanyakazi na watu wote wana hofu, tutaendeshaje nchi hii? Bunge mmelifunga, halisikikii, humu ndani mnataka kutu-*paralyse,* sasa hiyo siasa tutafanyaje? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, Kanuni ya 64 na Kanuni zake ndogo zinazofuata…

MWENYEKITI: Samahani hebu sema tena Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Kuhusu utaratibu, Kanuni ya 64 na Kanuni zile ndogo zote za 64. Na-*refer* Kanuni ya 64 kuhusu utaratibu unaovunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64 na vipengele vyake vidogo vinamkataza pia Mbunge kutumia lugha za kuudhi. Anapo-*refer* upande wetu sisi kwamba tumetoa macho, ubongo wetu sijui hauwezi kufikiri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya, ana uwezo tu wa kuchangia hoja zake na akasema kadiri anavyoweza, lakini anapoingiza maneno ambayo kwa kweli ni ya kuudhi, hakuna mtu hapa mwenye ubongo mbovu ambao hauwezi kufikiri na maneno hayo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu, ukielekeze Kiti chako kwa Mheshimiwa Mbunge achangie vizuri, atoe hoja zake, nasi tutajibu kuliko kutumia maneno anayotumia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri nakubaliana na wewe na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ulikuwa unakwenda vizuri, unatoka; unakwenda, unatoka. Hebu nenda, umebakiwa na dakika moja.

MHE. PETER S. MSINGWA: Kuna Wabunge wengine hapa wakati wa kampeni tulikuwa nao na walikuwa wanaleta mizigo ya hela kwenye kambi yetu.

WABUNGE FULANI: Akina Serukamba.

MHE. PETER S. MSINGWA: Ila saa hizi ni watu ambao hawaaminiki hata huko msiwaamini, hawaaminiki, saa hizi wanajikosha kusema sema maneno mazuri hapa wanawadanganya, tulikuwa nao usiku, waongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ukifika muafaka tutawataja, walikuwa wanatuletea na hela za kampeni sasa leo hapa wanajifanya wanadanganya danganya wanatuzunguka waongo, ni wanafiki hawa, hawawafai hata ninyi na hawa hawaifai hata Serikali kuwepo kwa sababu wata… *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Kangi Lugola ajiandae Mheshimiwa Mary Chatanda.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naomba nianze na mambo haya ili kuweka mambo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao tulibahatika kucheza mpira wa soka, kuna wachezaji wa aina mbili, kuna mchezaji ambaye ana uwezo wa kutumia mguu mmoja tu wa kulia na kuna mchezaji mwingine anatumia miguu yote kulia na kushoto. Kwa wale tunaotazama mpira tunajua siku zote mchezaji anayetumia mguu mmoja tu wa kulia maadui wakishamgundua wakambana wakamfanyia *tight making* kwenye mguu wa kulia hawezi akacheza mpira uwanjani, sana sana atatolewa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Kamati ya Kanuni kukaba mguu wa kulia wa hotuba ya Kambi ya Upinzani wameshindwa sasa kutumia mguu wa kushoto na ndiyo maana wamejiondoa na kutoendelea kusoma hotuba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna aina mbili ya wazungumzaji, kuna mzungumzaji mwingine ukishamdhibiti kusema uwongo, ukamdhibiti kutoa lugha ya matusi atajitoa kwenye mazungumzo kwa sababu hana uwezo tena wa kuendelea kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana Mheshimiwa Lema kunizulia mambo ambayo mimi sijawahi kuyasema, hii inatokana na kukabwa mguu wa kulia akashindwa namna ya kuendelea kutumia mguu wa kushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili lipo kwa ajili ya Watanzania, kwa ajili ya kutenda haki na ndiyo maana hakuna kiti wala Kamati ya Kanuni iliyozuia Mheshimiwa Lema kutozungumzia jambo la Lugumi, hakuzuiwa ameambiwa arekebishe maneno fulani yeye anasema amezuiwa, hajazuiwa ni kwa sababu anashindwa kuchangia hoja…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lugola, Waheshimiwa Wabunge jengeni hoja zenu kwenye maeneo ambayo kanuni hazijakataza, naombeni sana. Suala la Lugumi limezuiwa kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho. *(Makofi)*

Jengeni hoja zenu kwenye mambo ya msingi ambayo hayako katika katazo la kanuni nawaombeni sana.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama suala la Lugumi limeongelewa kwenye ukurasa wa 12 na ukurasa wa 13 na Kamati hiyo Mwenyekiti huyo hakuzuiwa na ndiyo ripoti tuliyonayo mezani na hapo ndipo ninapozungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niheshimu busara za kiti chako, niende moja kwa moja..

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kangi hebu kaa kwanza.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaacha nasema naendelea na hotuba nyingine…

MWENYEKITI: Sababu ukianza, kaa kwanza, ukianza kuhoji mamlaka ya kiti unavunja kanuni ya 74 na ni hatari sana. sasa kiti hiki sio kama kina ajabu, maamuzi yangu yanaweza vile vile yakapingwa siyo hapa tumia kanuni ya 5(4)

yeyote asiyeridhika na maamuzi ya kiti na ninyi mnalindwa kwa mujibu wa kanuni. Sasa unaposimama Mbunge unasema kiti hiki ni kosa unadharau mamlaka ya kiti, kanuni ya 74 sasa yule ambaye anaona kiti kinakosea atumie kanuni ya 5(4) endelea.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa nne wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia majukumu ya msingi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwangu mimi majukumu hayo hayawezi yakafanyika kwa ufanisi endapo hatutakuwa na jeshi lenye nidhamu, endapo hatutakuwa na jeshi lenye makazi bora ya askari, endapo hatutakuwa na askari wenye afya bora, hatutakuwa na askari wenye *moral* ya kazi, ufanisi ndani ya majukumu haya hautatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie makazi ya askari, sisi ambao tupo kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tumekuwa tukipata fursa ya kukagua na kutembelea nyumba za askari vyombo vyote hivi vya ulinzi na usalama si Magereza, si Uhamiaji, si Zimamoto, si Jeshi la Polisi, makazi yao ni duni. Alichosema Mheshimiwa Kawambwa kwamba ukiingia kwenye makazi ya Polisi, makazi ya Askari Magereza na vyombo vingine vya ulinzi na usalama amesema unaweza ukatoka ukiwa na masikitiko. Ninayo picha hapa nilikutana nayo kwenye gazeti la uhuru tarehe 17 Novemba, 2015 inahusu ukaguzi wa nyumba za askari uliofanywa na Mheshimiwa Waziri Kitwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, picha hii ambayo nitaileta kwako, utayaona makazi haya ni makazi duni na picha inamwonesha Mheshimiwa Waziri Kitwanga alipokuwa anatoka kwenye nyumba hiyo alishindwa kupita akainama akapindisha mgongo haikutosha ikabidi akunje na miguu ndipo akatoka kwenye nyumba hii. Nyuma yake kuna *AGP* Mangu analia ametoa na kitambaa mfukoni anapangusa machozi, picha hii inasikitisha sana. Kwa nini *AGP* ndani ya dakika chache anaingia kwenye nyumba analia? Je, askari ambaye amekaa kwenye nyumba hiyo miezi nenda rudi, miaka nenda rudi, amelia kwa kiwango gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii picha nitaileta kwako uone jinsi ambavyo *AGP* analia kwa sababu ya uduni wa makazi ya askari. Mheshimiwa Kitwanga kutuambia kwamba kuna fedha za Wachina kujenga nyumba za askari lazima pia tutumie vyanzo vyetu vya ndani tujenge nyumba badala ya kusubiri Wachina. Katika bajeti yakehakuna mahali popote ambapo ametenga fedha za ndani kwa ajili ya kujenga nyumba bora za askari. Ndiyo maana nikasema askari mwenye nidhamu ambaye anatakiwa apatikane kwa urahisi ikitokea dharura ni yule ambaye yupo kwenye nyumba ambazo ni za askari kwenye kituo anachofanyia kazi. Kwa hiyo, kwa stahili hii Wizara ya Mambo ya Ndani itakuwa katika kipindi kigumu sana kama hawatatenga fedha za ndani kwa ajili ya makazi ya askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la posho ya chakula kwa vyombo vyote hivi vya ulinzi na usalama. Nilishasema hapa kwamba posho hii inayoitwa ya chakula ni posho ya lishe kwa ajili ya kuwatengeneza askari, wanatakiwa wapate lishe. Hii elfu kumi kwa siku ni lishe gani ambayo askari anaweza akabajeti akapata lishe halafu akaweza kuhimili kufanya doria, kufanya kazi zenye shuruba. *(Makofi)*

Nimeshangaa sana Kamati ilishasema viwango hivi vya posho ya chakula ya lishe iwe inahuishwa kila mwaka, lakini mwaka huu Mheshimiwa Kitwanga ameshindwa kuhuisha posho hizi. Ndiyo maana juzi hapa Waheshimiwa Wabunge getini kwetu hapa askari ambaye ameshindwa kupata lishe bora amevamiwa na mama mmoja akamchoma kisu yule askari kwa kukosa lishe bora, hana nguvu alishindwa kuhimili kumtoa yule mwanamama aliyekuwa amemchoma kisu. Tunalipeleka wapi jeshi hili, Wizara ya Mambo ya Ndani Mheshimiwa Kitwanga angalia lishe ndiyo inawapa *moral* askari hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *OC* bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani imekatwa bilioni nane kutoka ile ya mwaka wa fedha uliopita. Hapa tunasema jeshi lazima liwe na fedha za kutosha *OC* kwa ajili ya kufanya doria kwenye maziwa, kwenye bahari wakiwa na *marine police* watu wa Uhamiaji waweze kudhibiti mipaka yote kwa ajili ya doria, wakimbizi waweze kushughulikiwa, magereza waweze kufanya shughuli yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inakuwaje Wizara ya Mambo ya Ndani, fedha za *OC* mnadhani na zenyewe ni fedha za maandazi, mnadhani ni fedha za soda, za biskuti. Fedha hizi ni kwa ajili ya shughuli za kutoa huduma kwa ajili ya Watanzania. Sasa mnapunguza fedha mpaka zile za kununulia taarifa za wahalifu ambazo ma-*RCO* wote wanakuwa nazo zikitoka kwa *DCI* yaani *Criminal Investigation Fund*, watafanyaje kazi bila fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Mambo ya Ndani, fedha zake za *OC* zinafanana na fedha za maendeleo kwenye Wizara zingine kwa sababu huduma hizi zinatakiwa zifanyike kila wakati, magari yanahitajika kwenye vyombo vyote, mafuta yanahitajika. Kwa hiyo, msifikiri kwamba *OC* ni fedha za kukata kata tu kila wakati, wakati kwenye vyombo vya ulinzi na usalama fedha hizi ni sawa na zile ambazo zipo kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la vituo vya polisi. Kadiri siku zinavyokwenda mahitaji makubwa ya vituo vya polisi kwenye nchi yetu yanaongezeka. Ndio maana Jeshi la Polisi walikuwa wana utaratibu wa kujenga vituo vya polisi vya tarafa ili kila tarafa iwe na vituo vya polisi. Hata hivyo, matokeo yake ni nini? Tumekuwa tukisubiri fedha zingine hizi za maendeleo ndipo zikajenge vituo hivi vya tarafa, hatutaweza kuvijenga mpaka tuhakikishe zile fedha ambazo wanazikusanya kwenye maduhuli, Bunge hili liwaruhusu

fedha hizi wanapozikusanya wapate ile asilimia ambayo moja kwa moja itakwenda kujenga vituo vya polisi. Vinginevyo tutaendelea kuwalalamikia kwamba uhalifu unatokea polisi ukiwaita hawafiki kwa wakati na hata vile vituo ambavyo vipo maeneo hayo wako kwenye nyumba za kupanga, hawana magari, wengine hawana hata pikipiki, tutaendelea kuwalaumu kama jambo hili hatutalifanya kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie magereza kwenye suala lao lenye mahitaji maalum na ndiyo maana Mheshimiwa Kitwanga katika hili naomba angalau ufungwe siku moja tu ndani ya magereza yetu ili uweze kuona jinsi wafungwa na mahabusu na hawa mahabusu nadhani kuna wakati itabidi tubadilishe sheria kwa sababu ni mahabusu lakini ukienda kule nao wanakula mlo mmoja, ukienda kule na wao mahali pa kujisaidia ni shida. Nimekwenda kule wanakwenda kujisaidia kila mmoja anawaona, tufike mahali Mheshimiwa Kitwanga tusidhani kila mtu aliye…

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mary Chatanda, ajiandae Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hotuba iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani kwa kazi kubwa anayoifanya akishirikiana na viongozi wakuu kwa maana watendaji wakuu wa Wizara hizo pamoja na changamoto mbalimbali ambazo wanakabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeanza na suala zima la magereza. Tumesema kwamba Serikali yetu tunataka nchi hii safari hii iwe nchi ya viwanda; ukiangalia kwenye taarifa ya Kamati imetoa ushauri kwa kuishauri Serikali kwamba tuiwezeshe magereza ili iweze kufanya kazi yake vizuri. Ninavyokumbuka, nilipokuwa nikikua, magereza wamekuwa wakilima mashamba kwa mfano yale magereza ya kilimo walikuwa wakilima mashamba na kuweza kutosheleza mazao ya chakula na ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kinachotakiwa hapa ni kurejesha ule utaratibu wa zamani ili magereza waweze kupatiwa zana za kufanyia kazi, waweze kupatiwa mtaji, kwa ajili ya uzalishaji. Magereza wakizalisha mazao ya kutosha inaweza ikapatikana malighafi ya kupeleka kwenye viwanda ambavyo tunasema tunataka tuwe na viwanda ili kusudi viweze kulishwa na malighafi itakayokuwa imezalishwa na magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii inawezekana kwa magereza kwa sababu wenzetu tayari wana rasilimali watu, tukiwawezesha magereza tukawapa mtaji wa kutosha hakuna kitakachoshindikana. Magereza zamani

walikuwa wanafuga mifugo kwa maana ya ng'ombe wa maziwa. Nakumbuka nilipokuwa pale Mafinga yalikuwa yanatoka maziwa kwenye gereza la Isupilo, yanaletwa huku ukiuliza yametoka wapi, wanasema maziwa yanatoka Gereza la Isupilo. Kwa hiyo, kama tutataka kuanzisha viwanda vya maziwa, magereza hawa tukiwawezesha watafuga vizuri na viwanda hivyo vitaweza kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yangu ili tuweze kuufufua huu uchumi tunaouzungumza wa kutaka tuwe na viwanda tuweze kuwawezesha magereza kwa kuwapa mtaji na hatimaye kuwawezesha kwa zana za kufanyia kazi ili kusudi wao wenyewe waweze kuzalisha kwa maana ya kulisha magereza yao, kuachana na kuendelea kuitegemea Serikali. Wakati huo huo ziada itapatikana kwa ajili ya kuuza na hatimaye kuweza kupata fedha ambazo zitapatikana kama sehemu ya maduhuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Kamishna Mkuu wa Magereza kule kwangu Korogwe kwenye gereza moja la Kwa Mngumi ameanza kufufua mabwawa 30 ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa yale ni makubwa na ameshaanza kupanda samaki mle ndani, lakini anachohitaji hapo kuna changamoto, nimwombe Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi aweze kutembelea lile gereza ili aende akaone yale mabwawa ambayo ameyaanzisha huyu Kamishna Mkuu wa magereza ili aweze kuona ni namna gani ambavyo anaweza kuwasaidia ili kusudi waweze kufanikisha kukamilisha ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kama walivyosema wenzangu suala la maslahi ya askari. Lipo tatizo pamoja na kwamba tunasema bajeti inakuwa ndogo, lakini inakuwa ndogo kwa hawa askari wa ngazi ya chini tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wa ngazi ya chini wanapata shida, wanakwenda likizo bila malipo ya likizo yao, hata wakirudi kutoka likizo wakiomba fedha hizo kulipwa hawalipwi. Niiombe Serikali katika bajeti ile ambayo inatengwa kwa ajili ya Wizara hii ni vizuri tukawapa fedha zote ili kusudi waweze kulipa madeni wanayodaiwa na askari wa ngazi za chini walipwe madai yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine ambalo askari wa ngazi ya chini wanapata shida, suala la upandishwaji wa vyeo, wana utaratibu wa kila baada ya miaka mitatu askari wa ngazi ya chini anatakiwa kupandishwa cheo, lakini hawapandishi kwa wakati na hata wakipandishwa hawalipwi mshahara kulingana na cheo alichopandishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana tusiwafishe moyo vijana hawa askari wa ngazi ya chini hawa mishahara yao ni midogo, wanapandishwa vyeo halafu hawalipwi kulingana na vyeo walivyopewa, wapewe kulingana na vyeo vyao walivyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la kufiwa, askari wa ngazi ya chini akifiwa nitaomba Waziri anipe majibu anapo-*wind up* hivi ni kweli kwamba akiwa na baba yake mzazi, mama yake mzazi anakaa naye pale nyumbani na tuseme bahati nzuri huyu askari yeye kwao labda ni Musoma amefiwa na baba yake alikuwa akimlea hapo nyumbani alikuwa anaugua, askari yule hawezi kusafirisha na mzazi wake yule kupelekwa nyumbani, askari yule anahangaika anatafufa fedha za kusafirisha mwili ule hivi ni kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu askari si mtumishi wa Serikali inakuaje watumishi wa Serikali wengine wazazi wao wakifariki wanasafirishwa iweje askari polisi anafanyiwa kitu cha namna hiyo? Nitaomba majibu kama ni kweli, utaratibu ni huo naomba utaratibu huo ubadilishwe. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Polisi, wenzangu wamezungumza sana, nimefanya ziara yangu nilitembelea taasisi ikiwemo Polisi, Magereza kama walivyosema wenzangu inasikitisha. Askari wa Korogwe Mjini wana nyumba chumba kimoja na sebule, ana watoto watano, wa kike wawili, wa kiume watatu, wote wana umri mkubwa hebu niambieni sasa maadili yako wapi hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, nimeona hapa mnazungumzia suala zima la Serikali kupitia mkopo wa China, sasa nimwombe Waziri atakapokuja ku-*wind up* aniambie huu ni mkopo ambao umeshapatikana au wanakusudia kupewa hizi fedha, naomba waje waniambie. Kama mkopo huu umepatikana, niwaombe askari wa Korogwe wawemo katika mpango wa nyumba hizi 4,136. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nichukue nafasi tena kumpongeza Waziri kwa kuwasilisha taarifa yake vizuri na haya mengine ni mapito, yeye apige mwendo, mti wenye matunda mazuri siku zote huwa unapigwa mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, jiandae Mheshimiwa Khatib Said Haji.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Lema Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa kutoa ndani ya roho yake na ndani ya nafsi yake maudhui aliyekuwa ameyatayarisha kwa ajili ya kuwakilisha kambi. Nizungumze suala moja, mimi binafsi sitaki kuunga hoja na napinga kwa nguvu zangu zote mafungu ambayo yameelekezwa kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu ya Jeshi la Polisi kutumiwa vibaya wakati wa kipindi cha uchaguzi. Wakati wa uchaguzi Jeshi la Polisi kasoro tu hawavai nguo za *green* wanavaa kombati za polisi lakini asilimia 100 wanakuwa wametayarishwa kusaidia Chama cha Mapinduzi kushinda uchaguzi, huo ndio ukweli. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hiyo kwa mifano hai. Mwaka 2005 nikiwa nagombea pale Bukoba Mjini, Jeshi la Polisi lilitumika kunizuia kukusanya matokeo chini ya mtutu wa bunduki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 Jeshi la Polisi limetumika kusimamia uharamia na kubaka demokrasia ya watu kupiga kura kadri wanavyotaka. Nachukua mfano hai wa kwangu, nimewapa taarifa polisi kwamba Mkurugenzi msimamizi wa uchaguzi amebaka uchaguzi kwa kunyofoa karatasi ndani ya vitabu vya kupigia kura na anazisambaza kwa ajili ya kuhakikisha yule mpinzani wangu anashinda na pia wagombea wa CCM wanashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini polisi wakakataa kufuatilia suala, lakini vijana makamanda walikuwa wamejipanga tukazifuma hizo kura zilivyokuwa zimepangwa. Nashukuru vituo vya ITV vilifanya kazi nzuri lakini hata mimi na makamanda tuliweza kuzizingira kura zaidi ya 2000 zikiwa zimetayarishwa kwa ajili ya kuwekwa kwenye masanduku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya kura hizo niliziwasilisha mpaka kwa msimamizi wa uchaguzi. Nilitoa taarifa kwa makamanda wa Jeshi la Polisi wote wakazikimbia, lakini msimamizi wa uchaguzi nilihakikisha kwamba nampelekea sehemu ya kura hizo na nikaandika waraka kwenda mpaka Tume. Mpaka leo ninapozungumza Tume haijawahi kuchukua hatua yoyote na hiyo imeonesha jinsi gani wenzetu wa upande wa pili wanashinda uchaguzi, wananyofoa kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wasimamizi wa uchaguzi wanakuwa ndiyo marefa, lakini kumbe ni wachezaji pia. Polisi inajifanya kusimamia lakini na wenyewe wanaongeza namba, wanacheza namba mpaka wachezaji 16 upande mmoja. Kwa kuthibitisha hilo, sehemu ya kura ambazo sikuzikabidhi ni hizi hapa, wasiwe wanatambatamba kwamba, wanashinda uchaguzi wakati kura bandia zipo tuliziteka, hizi hapa zimepigwa *tick,* mgombea CCM wa Urais

na Makamu wake mkizihitaji nitapeleka mezani njoo mchukue. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hapa nyingine namuuliza Mkurugenzi, hizi zimetokaje katika mfumo wake? Anakimbia, anakimbia hana maelezo. Kwa hiyo, makamanda ninachowaambia kwa jeshi tulilonalo ,kwa chama tawala tulichonacho wameshazoea vya kunyonga, vya kuchinja hawaviwezi, tutapiga kelele hapa, tutaimbiana ngonjera hawa watu sikio la kufa halisikii dawa. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Halisikii dawa.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaeleza ukweli lililopo makamanda ni kujipanga upya kukabiliana na ngoma inayokuja mwaka 2020. Watakuja vingine hawa kwa wizi wa *style* nyingine, wanasema wana-*style* 86. Kwa hiyo, ninachowaomba makamanda hapa ni kutwanga maji kwenye kinu, hawa watu wameshazoea vya kunyonga, vya kuchinja hawaviwezi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona wakati wa uchaguzi, tulikuwa na vituo vyetu vya kuweza ku-*tally* matokeo katika maeneo mbalimbali, chama kilikuwa kimeandaa vijana wa *IT* wa kuweza kusema matokeo CCM wakiwa Milimani City na sisi vijana wetu wakiwa katika maeneo mengine, vituo tulivyokuwa tumeviandaa, lakini Jeshi la Polisi limetumika kuwavamia vijana wetu katika maeneo walipokuwa wana-*tally* kura za uchaguzi, lakini CCM wakaachwa bwelele wakafanya jinsi wanavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu nafikiri huko mbele tunapoelekea hili Jeshi la Polisi ukweli wenyewe tunapopitisha mafungu hapa tunakwenda kuongeza nguvu kuwaelekeza na kupata mafunzo namna ya kubaka demokrasia ya kweli. Hiyo siko tayari kuacha pesa ziende kufanya haramu, Jeshi la Polisi tulilonalo ndugu yangu Kitwanga namfahamu vizuri sana, tena bahati nzuri nilimwona na Shekhe Yahya Simba hawa walikuwa *inside brothers* kwenye *club* moja tukiwa Chuo Kikuu, walikuwa vijana safi, wametulia, wenye maadili, naomba maadili hayo basi hebu ajaribu kurekebisha na kunyoosha Jeshi la Polisi, tuwe na jeshi ambalo linajiita polisi jamii lisiwe polisi...?

WABUNGE FULANI: CCM.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Polisi CCM. Tunaomba, tunaomba suala hili kama jeshi haliwezi kujirekebisha ni vyema tuanze kujenga hoja, tuanze kukusanya sahihi za Watanzania na tuombe ulimwengu, tuombe Taasisi za Kimataifa zije kusimamia uchaguzi mwaka 2020 badala ya jeshi la namna hii

ambalo limebeba sura na taswira ya kubaka demokrasia ni hilo siwezi kukubaliana nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ambalo nataka kuzungumza ni suala la kubambikiana kesi. Makamanda, sisi wengine tunatembea kama wafungwa watarajiwa, kwa sababu ya Jeshi la Polisi kubambikiza kesi, lakini hata hivyo nawashukuru wengine tumejengewa historia ya kusindikizwa na ving'ora kama Rais jambo ambalo hatukulitarajia. Tumejenga dhana, lakini nataka kuomba Jeshi la Polisi lijerekebishe vinginevyo msiufikishe umma, msiwafikishe Watanzania wakaanza kuwa na fikra za kuona wanajipangaje katika majeshi yasiyokuwa rasmi kwa ajili ya kulinda haki yao ya kura wanazozipiga. Hilo litafanyika watalifanya kwa kulazimishwa na hali ya mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze vijana wa Bukoba wakati namaliza, pamoja na mbinu zote hizo zilizokuwa zimepangwa kuleta Mbunge wa kuchonga lakini vijana walikaba mpaka *penalty,* vijana wa Bukoba walikaba mpaka *penalty* na wala hizo dhuluma, hazikuweza kupenya. Makamanda na Watanzania wote nawapa rai, hawa jamaa ni wepesi, ni wepesi kuliko nyama ya utumbo, kama unajipanga hawa jamaa ni wepesi kwelikweli, lakini nawaomba na nyie polisi basi, polisi Mheshimiwa Rais aliwahi kusema kwamba, ukielezwa na wewe changanya...?

MBUNGE FULANI: Na zakwako.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Na za kwako, hebu msitumike, msitumike kwa sababu hawa jamaa huko tunakokwenda naamini *ICC* inakwenda kufanya kazi *The Hague,* angalia na wewe usiwe miongoni mwa *list* ambayo itapelekwa *The Hague*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mwenyezi Mungu pekee kwanza dakika zenyewe ni tano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa khatib dakika tano.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa haya yanayotukuta hapa Bungeni, nimshukuru Mungu kwa kila linalotukuta. Leo nimesikitishwa sana na kilichotokea kwa njia yote ile iliyosababisha hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani kufanya isisomwe hapa ndani ya Bunge imenisikitisha sana. Lakini nataka

nikuambie tu kwamba, mmejaribu kufunga banda farasi ameshatoka. Watanzania wanaelewa kila kilichomo kwenye hotuba ile, taarifa ziko na wote wanajua ni nini, ujumbe gani umekusudia kuwafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niwashukuru wananchi wa Pemba hususani wa Jimbo langu la Konde kwa mapokezi makubwa waliompa kipenzi chao, Maalim Seif Sharif Hamad, jana katika ziara yake aliyofanya kule Pemba. Sasa mapokezi yale ni ishara tosha kwamba, hakika Wazanzibari nyoyo zao ziko na Maalim Seif. Kilicho chema ni chema hakibadili tabia, ni bure mngekisema na mengi kukizulia, Mungu hukipa baraka na amani kukitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo baada ya tukio la kuzuiliwa hotuba, nilimuuliza, ninaye mtabiri wangu wa nyota na mtabiri wa ndoto, nikamuuliza hatua ya mwanzo ndani ya Bunge yamezuiliwa matangazo *live* ya *TV,* wananchi wasione tunachokisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea, leo tayari tumezuiliwa hotuba yetu isisomwe ndani ya Bunge nikamuuliza *what is next?* Jibu alilonileta muda mfupi ananiambia kinachoendelea baada ya kuweka dole mtawekewa vibakuli vya gundi wapinzani tutatia gundi ndi! Tukiingia hapa kimya. (*Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wajibu wetu kuona tunakoelekezwa kwenda, tuna hiari sasa kuamua kukubali kila tunalofanyiwa na wenzetu kwa sababu ya wingi wao au kuangalia ni hatua gani madhubuti tunachukua tukatae dhuluma yote ndani ya Bunge hili. Tukatae kunyamazishwa kwa namna yoyote sauti yetu hata humu ndani pia zisisikike, tukatae kabisa na tukatae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuzungumzia suala moja ambalo linaendelea. Jeshi la Polisi, nimekereka sana na kitendo chao cha kuwashikilia watu zaidi ya muda wa kisheria ambao wanatakiwa kuwa-*hold* katika vituo vya polisi. Hili limesemewa na mimi nalisemea na linaniuma sana, kwa sababu ukiacha hilo kule Zanzibar, Jeshi la Polisi linatumika sana kisiasa, anaweza kutokea tu Mkuu wa Mkoa akasema wakamate hao weka ndani na wanafanya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku kumi hili linaniumiza sana, nalisema sana. Siku kumi kabla ya uchaguzi haramu wa marudio Zanzibar, wananchi wangu wa Jimbo la Konde wasiopungua 30 walizuiliwa katika vituo vya polisi katika muda usiozidi siku 14, wakapelekwa mahakamani, mahakama wakasema hatuoni kesi hawa ya kuwafungulia tulichotegemea kirudishwe vituo vya polisi watapewa dhamana, matokeo yake imetoka amri kutoka hatujui wapi, wanaambiwa endeleeni kuwashikilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumuuliza Waziri wa Mambo ya Ndani, ni yeye, ni Naibu wake au ni nani anayesimamia amri hii haramu ifanyike kwa wananchi wangu. Leo akija hapa Mheshimiwa Waziri mimi na yeye na mshahara wake mpaka tujue nani anayetoa amri haramu ya kuwazuia wananchi zaidi ya muda wa kisheria unaotakiwa uwe nao au uwe umewapeleka mahakamani kwa hatua za mbele zaidi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa sana, hapa alinyanyuka, katika moja ya maneno mabaya aliyowahi kusema kiongozi mmoja mwandamizi wa CCM ambaye sasa hivi ni Waziri, ni pale alipotamka katika mmoja wa mkutano wake akiwa ndani ya kanisa kwamba, tatizo la Zanzibar ni Uislamu, Mheshimiwa Lukuvi, alisema hayo maneno, nataka niseme tatizo la Zanzibar sio Uislamu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, ahsante. Mheshimiwa Hassan King, dakika tano.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Kwanza nimpongeze mzungumzaji aliyemaliza kwa shairi lake kilichochema ni chema hakibadili tabia. Tabia ya Maalim Seif ni kushindwa uchaguzi na nashangaa kwa nini mnamwachia aendelee na tabia hiyo hiyo na ataendelea kushindwa tu. Kwa hiyo, kwa kuwa hakibadili tabia siku zote atashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichangie katika nyumba zitakazojengwa kwa Jeshi la Polisi kwa Zanzibar. Tuweke *proportion* ambayo ni nzuri, lakini cha pili mawasiliano ya redio kwa Zanzibar askari wanaongoza kwa simu kule, kwa hiyo, hili nalo pia ni muhimu tulitazame. Kingine masuala ya umeme wanalipa Wakuu wa Vituo wakati mwingine, kwa hiyo na hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie jambo moja, amesimama hapa kuna mtu alijiita mchungaji, lakini nikimnukuu ndugu yangu mmoja alisema sijui kanisa hilo hawa wafuasi watakuwa wakoje, mimi sisemi. Anasema kwamba, Wabunge 250 wanashindwa labda kuzijibu hoja, upinzani hauna hoja, hapa hawana hoja, hawana ajenda za kuzungumza sasa hivi wamekuwa ni virukia, kuna miti inaitwa virukia haina mizizi. Ikitajwa Lugumi wanajipaka damu za simba kama wao ndio waliomuua simba, ninyi sio, wako wenyewe waliofanya hiyo kazi, mnajipaka damu halafu mnajisingizia ninyi ndiyo mlioua simba, hamna hoja. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Toka wauvae ulitima kwa kulamba joka la ufisadi sasa wanadandiadandia, kwa hiyo hawana hoja ya msingi. Lakini Mheshimiwa Lwakatare kule amesema amethibitisha kwamba, wanatangwa maji kwenye kinu na hayabadiliki kwenye kinu hayawezi kupita *smoothly* kwa sababu ya

kuyatwanga kwenu. Watu wanawashuhudia hata mngeletewa hiyo TV katika hoja zenu za kurukiarukia basi pia msingefanya kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa wale waliokuja na habari za matukio jamani mnasahau? Hamtajwi matokeo ya mabomu nyie? kuwamwagia watu *acid*, kuwaua ma-*padre* mbona hamtaji kama huu ni uvunjifu wa amani, mnazungumza hoja gani katika hili? Zungumzeni kitu ambacho kitaleta amani na utulivu katika nchi hii, wadau wa amani na utulivu wanajulikana na wanaochafua wanajulikana mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unalalamika kupelekewa askari Zanzibar, unalalamika nini, wewe ndiyo mhalifu kama unalalamika, kwanini unakataa kupelekewa askari kama sio mhalifu. Sasa hili ni lazima liangaliwe, nikija kuchangia katika hoja nyingine amezungumzia Mheshimiwa Waziri katika utekelezaji wa bajeti iliyopita kwamba, wamejaribu kuzuia biashara haramu ya kuuzwa watu, hili jambo bado lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ndugu zetu wanapelekwa Oman, Dubai, wanapelekwa Bara Arab wanakwenda kutumikishwa bila ya hiari zao, mikataba inaondoka hapa mingine na wakifika kule wanafanyiwa mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono hoja hii mimi labda hapa nizungumzie kitu kimoja, kuna wenzetu wanajaribu kulipaka matope jeshi letu la polisi, amani na utulivu wa nchi yetu ya Tanzania basi Jeshi la Polisi ndiyo mchango wake mkubwa na waharibifu wa amani hiyo na utulivu ndiyo hawa, nashangaa. Kuna msemo unasema homa mpe paka, maana yake homa mpe paka kwamba wewe kwa kuwa unaumwa ikutoke homa ile kwa kuwa paka haitomdhuru. Sasa hicho sio kitu sahihi wanachokifanya, tunapozungumzia amani na utulivu, majeshi yetu yanakwenda vizuri, kwa hiyo, tunashukuru kwa kutusaidia katika kuweka sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia hapa jambo lingine ambalo ni muhimu sana, ni usafiri kwa Jeshi la Polisi kwa Mkoa wangu wa Mjini Magharibi Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nape dakika tano

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye hoja. Kwanza nimpongeze sana Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya. Najua, yako maneno mengi watawasema lakini sisi

wenzako tunajua unafanya kazi nzuri na tunakuunga mkono endelea kufanya kazi hiyo.

Pili, nilipongeze sana Jeshi letu la Polisi kwa kazi nzuri waliyofanya na hasa wakati wa uchaguzi mwaka jana. Uchaguzi ule umekwisha kwa amani na utulivu kwa sababu ya kazi nzuri iliyofanywa na Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi endeleeni kufanya kazi hiyo, msisikilize kejeli zinazoelekezwa kwenu, Watanzania wanajua mnafanya kazi nzuri pamoja na mazingira magumu endeleeni kufanya kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo nilidhani ni vizuri tukaliweka sawa. Hapa pamefanyika utaratibu ambao ulifikia uamuzi wa Kamati ya Kanuni kwenda kushughulika na hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Bahati mbaya sana ninachokiona hapa, kunatengenezwa upotoshaji kama vile kulikuwa na hoja ngumu, nyingi Serikali imeziona, ikaona tabu kuzijibu, kwa hiyo ikatengeneza utaratibu wa kukimbia. Utaratibu huu wa kupotosha mambo, unaendelea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo liko wazi, kila mahali na hapa Bungeni pana utaratibu wake, wenzetu wamezoea kunyonga, wanapoambiwa kuchinja wanapata tabu. Mimi wala sipati tabu na kelele zao kwa sababu ndivyo walivyofundishwa, wasipoipenda hoja wanatakiwa wazomee, endeleeni kuzomea. Hata hivyo, nataka tuweke jambo hili sawa, kilichofanyika hapa ni utaratibu wa kawaida wa Kibunge, kuna kanuni zake, wamekwenda wamekaa wameshauriwa, hawataki walichoshauriwa wameamua wenyewe kuweka mpira kwapani na kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri Watanzania wakaujua ukweli huu kwamba wenzetu hawapendi kufuata kanuni na taratibu ndiyo maana wanafanya walichofanya na ndiyo maana hata humu ndani wataendelea kuzomea kwa sababu ndiyo taratibu zao.

WABUNGE: Aaaaaa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nape, Mheshimiwa Nape dakika moja. Waheshimiwa Wabunge upande huu nawasihi, Bunge haliendeshwi namna hii, Ubunge siyo mavazi. Nawaomba, kanuni hizi ziko *very clear*, nynyi mmesema, wao wamesikiliza, wacha aseme, ninyi sikilizeni nawaombeni. Mheshimiwa Nape endelea.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lilikuwa la kwanza na nadhani limeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, imetolewa hoja hapa kwamba, Serikali hii haina uwezo wa kuongoza nchi, lakini nataka nimwambie Mchungaji wangu Msigwa, Watanzania ndiyo wametupigia kura, wakatuamini, wakatuleta hapa na kwa muda mrefu siyo jana wala juzi, mmekuwa mkiwaomba wawaamini wamekataa kuwaamini. Wameendelea kutuamini siye na wanatuamini kwa sababu wanaamini tunaweza, tunajua na ndiyo maana wameendelea kutupa na wataendelea kutuamini kuturudisha hapa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeendelea kutoaminiwa kwa sababu ya ukigeu geu mnaoendelea nao mpaka leo, kwa hiyo tupo hapa kwa sababu Watanzania wanataka tuwe hapa, wanatuamini na wataendelea kutuamini na kwa kazi nzuri tunayoifanya, wataendelea kutuamini, kwahiyo hili halina mjadala. *(Makofi),*

La tatu, endeleeni kupiga kelele kwa sababu ndivyo mlivyotumwa kufanya. La tatu….

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nape zungumza na kiti. Waheshimiwa Wabunge *time* inalindwa na kiti siyo nyie.

WABUNGE FULANI: Aaaaaaah!

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwisho. Imetolewa hoja hapa pia, inatuhumu kwamba Jeshi la Polisi limekuwa likitumiwa na Chama cha Mapinduzi hasa kwenye uchaguzi. Nadhani hili nalo si suala la kuliacha liendelee kuzungumzwa, kama Jeshi la Polisi na hapa maneno haya ni ya kulidharau na kulidhalilisha Jeshi la Polisi na ndiyo maana Mheshimiwa Lwakatare anasema, hawa jamaa laini sana maana yake Jeshi la Polisi laini sana. Hivi kama kweli…

MWENYEKITI: *Order.* Ahsante Mheshimiwa Nape.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO: Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG dakika kumi.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nami niweze kuchangia, kwa mara nyingine tena nimshukuru Mwenyezi Mungu. Kwanza naunga mkono hoja iliyoko katika meza yako. Naomba nitoe ufafanuzi wa mambo mawili matatu ambayo yamezungumzwa hapa. Hoja ya kwanza ni iliyoletwa na Mheshimiwa Esther Matiko kuhusu uhifadhi na utunzaji wa watoto walioko magerezani.

Sheria ya Mtoto, *The law of the Child* ya Mwaka 2009, katika kifungu cha 144 inaeleza namna gani mtoto aliyeko gerezani kwa sababu amekwenda kule na mama yake au na mzazi, anavyopaswa kutunzwa. Naomba niisome sheria yenyewe na ambacho tumefanya katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa sababu ya umuhimu wa sheria hii, tuliamua kuitafsiri, kwa hiyo, iko kwa Kiswahili. Ni sheria muhimu sana na naomba Waheshimiwa Wabunge mtafute hii sheria muisome, itatusaidia sana kwenye maeneo yetu kule tunapokuwa tunaongelea haki za watoto, haki za Watoto wanaoshtakiwa Mahakamani, walioko mbele za Polisi na hawa ambao sasa wanakwenda magerezani wakiwa na mama zao au wamezaliwa kule magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 144 cha sheria hii kinasema hivi:-

(i) Pale ambapo mama atakuwa gerezani na mtoto wake katika mazingira yoyote yale, hatua zote zitachukuliwa na uongozi wa magereza kuhakikisha kuwa mtoto anapata matunzo yanayohitajika kutoka kwa mama inavyostahili, mlo kamili, virutubisho na huduma ya afya pamoja na chanjo.

(ii) Uongozi wa Magereza utamfahamisha Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya kuhusu mtoto aliye gerezani na mama yake na ambaye ameacha kunyonya.

(iii) Endapo Afisa Ustawi wa Jamii amepokea taarifa kutoka katika uongozi wa gerezani, ataamua sehemu stahili ya kumweka mtoto huyo ambayo inaweza kuwa;

(a) Mzazi ambaye hayuko gerezani;

(b) Ndugu;

(c) Mlezi; na

(d) Mtu anayefaa kumlea huyo Mtoto.

(iv) Iwapo watu waliotajwa chini ya Kifungu kidogo cha (3) wanakosekana, Afisa ustawi wa Jamii ataagiza mtoto huyo apelekwe katika makao yaliyothibitishwa hadi hapo mama yake atakapoachiliwa kutoka gerezani

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utakuta sheria imeweka utaratibu na mwongozo mzuri. Inawezekana kukawa na changamoto Waheshimiwa Wabunge mnapokwenda kule mnazipata, haya basi mzijulishe mamlaka zinazohusika ili hatua zile zirekebishwe. Magereza wenyewe wana utaratibu mzuri sana wa kuwaangalia hawa watoto wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo ningeomba kushauri, hili ni wajibu wa kikatiba wa kila mwananchi. Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naomba kuisoma tu hii inasema hivi: "Kila mtu ana wajibu wa kuifuata na kuitii katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano." Sasa Bunge hili na lenyewe linaongozwa na katiba, sheria na kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika chombo kama hiki ambacho kinafikia maamuzi yake kwa majadiliano, maana maamuzi hapa yanafikiwa baada ya kujadiliana, inafaa sana zile sheria ambazo tumejiwekea za kuongoza majadiliano humu ndani ili tufikie Maamuzi ziheshimiwe sana na sheria zenyewe kwanza ni Katiba yenyewe; pili, sheria ya haki na kinga za Bunge, tatu na kanuni hizi ambazo zinatungwa kwa mujibu wa ibara ya 89, tukifanya hivi, Waheshimiwa Wabunge shughuli zetu hapa zitafanyika kwa amani, kwa hekima kubwa, kwa ufanisi mkubwa, kila tunachotaka kuishauri Serikali kitafika kwa wakati maana hakutakuwa na kuingiliana na Serikali itachukua hatua kukifanyia kazi. Huo ndiyo ushauri wangu, vinginevyo hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili naona niliomba nilifafanue kusudi turudi katika utamaduni wa Bunge hili wa kufanya shughuli zetu kwa amani, kwa ufanisi, kwa kuzingatia katiba na sheria na kanuni ambazo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu na la mwisho ambalo ningeomba kushauri hapa, Jeshi la Polisi mimi nafanya nalo kazi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inafanya kazi kwa karibu sana na Jeshi la Polisi. Ni jeshi ambalo linafanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana kuhakikisha kwamba amani na usalama katika nchi hii vinaendelea kuwepo. Unaweza ukawepo upungufu kwa baadhi ya askari, lakini haiwezi ikachukuliwa kwamba ni jeshi lote na haiwezi kuwa kwamba, kama wote hawa wangekuwa ni wala rushwa, kama wote hawa wangekuwa wameshiriki ku-*league* uchaguzi, basi baadhi ya Wabunge leo wasingekuwa humu ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu, baada ya Uchaguzi Mkuu kulikuwa na mashauri 52 ya uchaguzi ambayo yamefunguliwa lakini katika mashauri yote hayo wako wa Chama cha Mapinduzi, wako wa Vyama vya Upinzani CHADEMA, *CUF* na *NCCR*, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imewatetea na sasa mashauri 39 yameshamalizika Mahakamani. Kwa hiyo, kama kuna kasoro zimetokea hoja siyo kuleta humu Bungeni, kwa mfano, aliyosema Mheshimiwa Lwakatare kama kungekuwa na shida pale hoja ingekwenda mahakamani pale, lakini hakuna hata *election petition* kutoka kwenye lile Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba, Waheshimiwa Wabunge tujizuie sana kutoa majumuisho ya jumla jumla ya

kulaumu jeshi kwamba linafanya hivi, linafanya hivi, lazima tuishi tu kwa kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri dakika kumi na tano. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru kabisa kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa imani kubwa aliyokuwa nayo kwangu na kuniteua kushika dhamana hii. Pia nimshukuru na Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile nichukue fursa hii kuishukuru familia yangu na Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo ananiongoza vizuri, nafanya nae kazi kwa karibu sana na pia kwa ushirikiano wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo, naomba sasa nichukue fursa hii kuweza kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizokuwa zimewasilishwa leo hii na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako hili Tukufu. Naomba nianze na hii hoja ya makazi ya askari pamoja na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imezungumzwa ama imechangiwa kwa maandishi na kwa kuzungumza na wachangiaji wengi, lakini nitawataja wale ambao nimebahatika kuwabaini. Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Kiula, Mheshimiwa Masare, Mheshimiwa Kigula, Mheshimiwa Kingu, Mheshimiwa Shekilindi, Mheshimiwa Komanya, Mheshimiwa Omari, Mheshimiwa Kangi Lugola na Mheshimiwa Kingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba majeshi yote takribani yana changamoto kubwa sana ya makazi ya askari pamoja na vitendea kazi na kimekuwa hiki ni kilio cha Waheshimiwa Wabunge takribani cha muda mrefu. Tunakiri juu ya changamoto hii na ndiyo maana hivi tunavyozungumza, kuna mipango kabambe ya Serikali ambayo inalenga kuhakikisha kwamba inapunguza matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Polisi, tayari kuna utaratibu wa kujenga nyumba takribani 4,136 ambapo zinatarajiwa kujengwa kupitia mkopo wa Serikali ya China kupitia *EXIM BANK*. Wakati huo huo kuna Ujenzi wa makazi ya nyumba za askari Mabatini-Mwanza ambao zinachukua familia 24, Buhekela - Kagera familia 12, Musoma - Mara familia 24, Ludewa - Njombe familia 12. Aidha, Serikali imejenga nyumba 22 za maafisa wa

Mikocheni ambazo ziko Mikocheni na maghorofa 22 ambayo yatakuwa Kunduchi pale kwa ajili ya familia 333 za askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa magereza, pia kuna mchakato wa kujenga nyumba takribani 9,500 lakini pia kwa upande wa vitendea kazi kwenye Jeshi la Polisi kuna mradi ambao programu ya kuleta magari 777 ya aina mbalimbali, miongoni mwao yameshaanza kufika na mengine yatakuja hatua kwa hatua, ni magari ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa Jeshi la Zimamoto katika bajeti yetu hii kwenye bajeti ya maendeleo tumetengewa takribani shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuongeza magari mawili ya kuzimia moto. Kwa hiyo, hizo ni miongoni mwa hatua ambazo tayari Serikali imeanza kuchukua kwa ajili ya kukabiliana na changamoto ya masuala haya ya vitendea kazi pamoja na makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna hoja ambayo imechangiwa na wajumbe wengi wakiwemo Mheshimiwa Mohamed Amour, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Lwakatare, Mheshimiwa Kiula, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Yusuf, Mheshimiwa Mukasa, Mheshimiwa Kaiza, Mheshimiwa Anatropia na wengineo. Hoja hii zaidi ilikuwa inazungumzia kuhusiana na kubambikiwa kesi, wamelishutumu sana Jeshi la Polisi kwamba limekuwa likibambikia kesi, lakini nichukue fursa hii kuwapongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya pongezi hizo ambazo nawapa Jeshi la Polisi, haiondoi ukweli kwamba kuna askari wachache sana, nasisitiza kwamba ni wachache sana ambao wamekuwa wakichafua taswira nzuri ya Jeshi la Polisi miongoni mwa wananchi na hatua nyingi zimechukuliwa katika kukabiliana na askari wa namna hii. Kuna mikakati ya kijumla na mikakati mingine ya mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati iko mingi, siwezi kuitaja yote, lakini wameweza kutoa mwongozo wa mara kwa mara kwa Wakuu wa vituo na Wakuu wa Upepelezi kuwa makini sana kwa majadiliano na mashauri yanayofunguliwa na kutoa maelekezo kwa wapelelezi wa kesi ambao watasaidia kufuatilia mwenendo wa kesi hizo. Pale ambapo askari wamegundulika kufanya matatizo kama hayo ya upendeleo, basi wamekuwa wakichukuliwa hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kesi moja ambayo inazungumzwa sana ambayo Mheshimiwa Kiula aliizungumza baada ya kufanya ziara ya Kamati katika gereza hapa Dodoma, lakini kesi hii hii na mimi naifahamu vizuri. Tumekuwa tuna utaratibu mzuri kupitia Mheshimiwa Waziri wangu, Waziri wa

Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Mwakyembe kwa kufanya kazi kwa pamoja. Wakati huu niliweza kumwakilisha Mheshimiwa Waziri kufanya ziara katika lile gereza na kumshuhudia huyu msichana ambaye anazungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli msichana huyu alikatwa vidole viwili vya miguu na viwili vya mikono na baada ya kukatwa vidole hivi vya mikono yeye ndiyo akafungwa miaka minne. Ni jambo ambalo linasikitisha sana. Hizi ziara tumekuwa tukizifanya katika maeneo mbalimbali tunapopata fursa, tumefanya katika magereza mengi ili kuweza kubaini kama kuna wananchi ambao wamekuwa wakibambikiziwa kesi ili hatua za haraka zichukuliwe na tumechukua hatua nyingi tu.

Katika hatua *specific* ambayo ameizungumza Mheshimiwa Kiula kwa huyu msichana ni kwamba, mpaka sasa hivi tunavyozungumza wale watu ambao walimkata kidole wameshafungwa, wamehukumiwa kufungwa nadhani miaka mitatu kama sikosei au minne tunavyozungumza sasa hivi. Pia ile kesi yake ambayo alibambikiwa ya kuvunja nyumba nayo imefutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wale askari ambao walishiriki kwa namna moja ama nyingine kutomtendea haki huyu kijana tumeagiza wasimamishwe kazi mara moja na wachukuliwe hatua za kisheria. Kwa hiyo, kazi hii tumekuwa tukiifanya kimya kimya kuweza kutembelea kwenye magereza mbalimbali na kuweza kubaini watu ambao wanabambikiwa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusiana na hoja hii malalamiko yamekuja upande wa masuala ya kisiasa. Mimi niseme tu kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu. Katika kutimiza wajibu wake, wananchi tunapaswa kuwapa ushirikiano. Unapotakiwa na askari kutii lazima utii, wanaita sheria bila shuruti. Askari anapokuambia umefanya kosa fulani akakukamata basi ufuate sheria usilazimishe askari kutumia nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya masuala yamezungumzwa sana lakini niseme kwamba Jeshi la Polisi limechukua hatua mbalimbali kulingana na taarifa ambazo imezipokea. Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamika hapa mara nyingi kwamba kuna jambo fulani limetokea, lakini hakuna hatua iliyochukuliwa lakini ukimuuliza umepeleka taarifa hizo katika kituo gani cha polisi, hakuna. Kuna taarifa nyingi ambazo Jeshi la Polisi limezichukua na kuzifanyia kazi kwa sababu tuna lengo la kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kubakia katika amani na utulivu hasa kipindi cha uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, mnakumbuka wakati wa uchaguzi hasa Zanzibar kuna matukio mengi ya

uvunjifu wa amani yalikuwa yametokea. Kuna watu waliua wanyama, walichoma mashamba, walipiga nyumba alama ya "X", wamechoma nyumba za watu, wamechoma maofisi ya vyama na wametega mabomu. Katika hali kama hii mnatarajia kwamba Jeshi la Polisi likae kimya? Ni Serikali gani ambayo itakubali amani ya nchi inachezewa halafu ikabakia kimya? Yaliyofanyika ni kuhakikisha kwa mujibu wa taarifa zilizopo na uchunguzi uliofanyika kuwakamata watuhumiwa mbalimbali, kufanya upelelezi na kuweza kuwafikisha panapostahiki na panapostahiki kwa mujibu wa sheria za nchi yetu ni kwa *DPP* ili baadaye waweze kupelekwa mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamefanyika sina haja ya kuyarudia kuyazungumza hapa. Nashukuru leo hayajazunguzwa kama kipindi kilichopita lakini nilikuwa nimejiandaa kwelikweli maana nina ripoti ambayo ni *very comprehensive* ina ushahidi wa kila jambo ambalo limefanyika ambapo watu wanaolalamika humu ndani leo ndiyo wafuasi wao walikuwa mstari wa mbele kufanya mambo hayo, lakini leo wamekimbilia kwenye hoja nyingine. Mimi niseme tu kwamba tusaidiane, kama kuna mambo ambayo mnaona hayajachukuliwa hatua na ni matendo ya kihalifu yote yataweza kufanyiwa kazi ili mradi muwasilishe katika sehemu stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo lingine limezungumzwa hili suala la mashehe. Wanasema kuna mashehe wamekamatwa kwa nini wanashtakiwa Dar es Salaam lakini kwa nini mashehe hawa wamedhalilishwa. Kwa ufupi kabisa kwa kuwa muda haupo, niseme tu kwamba mashehe hawa wameshtakiwa kwa makosa ya kigaidi…

WABUNGE FULANI: Eeeh!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Makosa haya yamefanyika Tanzania Bara. Ndiyo maana walipokwenda kuhukumiwa Zanzibar wakasema haya makosa yamefanyika Tanzania Bara kwa hiyo wakaletwa Tanzania Bara kwa sababu ndiyo walifanyia huku makosa.

MBUNGE FULANI: Muogope Mungu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Sasa wanasema wamedhalilishwa, naomba niweke mezani ripoti hii ya uchunguzi ambapo walipelekwa hospitali, wakafanya uchunguzi hakuna hata mmoja alionekana ana uthibitisho wowote wa kudhalilishwa. Ripoti hii hapa naiweka mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sasa katika hii hoja ya wahamiaji haramu ambapo wachangiaji wengi wamechangia lakini kutokana na muda naomba nisiwataje. Ni kweli tulifanya operesheni, ilikuwa ni operesheni kabambe

ambayo ilianzia tarehe 24 Disemba mpaka tarehe 31 Januari. Katika operesheni hii tulifanya mambo kadhaa ikiwemo upelelezi, doria, misako, ukaguzi na kadhalika. Mafanikio tuliyoyapata ni makubwa sana ambapo takribani wahamiaji haramu 3,339 kutoka mataifa 33 wameweza kukamatwa. Aidha, hatua mbalimbali zimechukuliwa dhidi ya wahamiaji haramu hawa, wengine wamerudishwa majumbani kwao, wengine walikuwa wakimbizi wakarudishwa makambini, wengine wamepigwa *PI Notice* wameondoshwa, wengine wameamriwa kuondoka na wengine wanaendelea kuchunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili lilikuwa na mafanikio makubwa kwani tumeweza kufanikiwa kukusanya takriban dola za Kimarekani laki moja na tisini na kitu elfu ambazo zilipatikana kupitia *special visa* kwa ajili ya wahamiaji haramu 317 ambao walikuwa wanaishi kinyemela. Vilevile zoezi limesaidia sana kuibua mwamko na hamasa kwa wananchi kuhusiana na madhara ya kukaa na wahamiaji haramu. Ndiyo maana tumeweza kupata karibu taarifa 750 kutoka kwa raia wema zilizoweza kusaidia kuwakamata hawa wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wageni walio wengi wanafuata sheria na ndiyo maana tunasema kwamba baada ya operesheni hii kabambe tumekuwa na mfumo mzuri wa kuwashughulikia. Hivi ninavyozungumza nadhani kesho watendaji wa Idara ya Kazi watafika hapa na watendaji wetu wa Idara ya Uhamiaji wako hapa tutakaa pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi ili tuweze sasa kuwa na mkakati wa pamoja wa kufanya zoezi letu liwe endelevu. Mkakati huu utasaidia sana kuendeleza mafanikio makubwa ambayo tumeyapata.

Mheshimiwa Mweyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ambayo inazungumzia hili suala la zimamoto. Wachangiaji wengi wamelalamika hapa kwamba mara nyingi moto unapotokea kwenye majengo marefu kikosi chetu hakina uwezo. Mheshimiwa Lucy Owenya alisisitiza sana hoja hii katika mchango wake wa maandishi na wachangiaji wengine walisisitiza kwamba unapotokea moto katika majengo marefu kikosi chetu cha zima moto hakina uwezo wa kuzima moto, ni kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza kwa mujibu wa vitendea kazi ambavyo tunavyo, tuna gari ambayo yanaweza kufika mwisho ghorofa 18 na wakati sasa hivi tuna majengo yana mpaka ghorofa 17. Ndiyo maana tukasisitiza kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2007 na kanuni zake ni lazima majengo mapya yatakayojengwa yazingatie usalama kwa kuweka vifaa vya kisasa ikiwemo *automatic fire system* na *automatic fire detection and suppression system*. Mfumo huu utasaidia sana kuweza kupunguza madhara yatakayoweza kutokea moto utakapotokea katika majengo ambayo ni marefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo sasa hivi tunafanya jitihada za kuhakikisha kwamba tunapunguza madhara ya moto kwa kuongeza vifaa vya kuzimia moto. Juzi nilizungumza hapa kwamba miongoni mwa mambo ambayo tunajaribu kufanya ni kuhakikisha kwamba tunatumia magari yaliyokuwa ya washawasha, yale 32 ambayo yameingia pia yaweze kusaidia katika shughuli ya uzimaji moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti naona nimetumia muda wangu vizuri, yale ambayo tumekubaliana niyazungumze nimeyazungumza. Naomba sasa nimuachie Mheshimiwa Waziri na yeye aweze kuendelea na pale ambapo mimi sikupagusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge 77 wamechangia. Kwa muda mfupi huu wa jioni, Wabunge 77 wameweza kuchangia hoja hii na kati yao 20 wamechangia kwa mdomo na wengine 57 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaanza kujibu hoja, naomba niwataarifu Wabunge vitu vitatu. Cha kwanza, niko Serikalini sasa hivi kwa miaka 35. Nimeanza kazi mwaka 1984. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, natambulika kwa jina la utani *Mr. STK* (Mzee wa STK) kwa maana ya sheria, taratibu na kanuni na la tatu ni kwamba nimewasilisha fomu yangu ya kwanza Tume ya Maadili mwaka 1998. Vitu vitatu hivyo vinatosha kuwapeni taarifa na mjue mimi ni mtu wa namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, huwa sipendi kusema sana, napenda kutenda. Kwa sababu hiyo basi nitajibu kwa kifupi sana lakini tutajitahidi kuwaleteeni majibu kwa maandishi kwa hoja zenu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nitajibu hoja chache ambazo zimetolewa kwanza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama halafu nitajibu kile ambacho Mheshimiwa Lema aliniomba nijibu na jibu langu ni fupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli baada ya kusoma ile bajeti mbadala nimesikitika sana, bila CCM nchi hii haina uongozi mwingine. Kwa sababu

hotuba yote ina-*refer* magazeti na inapiga vijembe na hakuna bajeti mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo, bado tuna kazi kubwa sana ya kuandaa Kambi ya Upinzani maana iliyopo ni Kambi ya Upingaji. Kwa sababu kilichoandikwa ni kwamba kutokana na magazeti, tunasikia, huwezi kutueleza hapa yaliyoandikwa kwenye magazeti na uliyosikia, tuambie unayoyawaza wewe. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Jibu hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua wako wapiga kelele, natambua wako wajenga hoja wachache na hoja zao walizozisema Serikali itazichukua na itazifanyia kazi maana ni za maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Kamati ya Kudumu ya Bunge, mengi yaliyosemwa ni mapendekezo au ushauri mbalimbali na ushauri huo Serikali itauchukua na kuufanyia kazi maana Serikali hii ni sikivu na haipigi kelele, *it doesn't shout*. Utawasikia tu wataanza ku-*shout, we don't work like that, we are professionals* na ndiyo sababu nina miaka 35 Serikalini. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Jibu hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Kamati au Kamati inapendekeza kwamba Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi, wazabuni na wakandarasi katika mafungu yaliyopo katika Wizara yetu. Nilifahamishe Bunge lako, sasa hivi Serikali imeamua kuweka madeni yote kwa pamoja. Kinachofanyika ni kwamba madeni yanahakikiwa na yakishahakikiwa kutoka Fungu Kuu *(Treasury)* yanalipwa na baadhi ya wafanyakazi pamoja na wakandarasi wa Wizara yangu tayari naadhi yao wameshalipwa na tunaendelea kuhakiki na wale ambao tunaona ni halali tutafanya hivyo kwa kuwalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa *NIDA* kuna wafanyakazi ambao wanaidai Serikali, tulipoita wale wafanyakazi 50 hawakuonekana kabisa na wengine ukiisoma mikataba yao huwezi kuelewa ndiyo sababu tunafanya uhakiki kwa kushirikiana na *Treasury*. Pale ambapo tutajiridhisha kwamba huyu kweli anaidai *NIDA* na ni mfanyakazi halali, watalipwa, pesa iko katika akaunti ya *NIDA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendelea na hali ile ya zamani ya watu kufanya longolongo na msitusukume kuingia katika mambo ambayo hatuyapendi na ndiyo sababu tumeyafanyia kazi. Kwa taarifa yenu tu pale

NIDA sasa hivi tuna vyombo vitatu vinahakiki yote yaliyotokea nyuma. Wa kwanza, *Controller and Auditor General* yuko pale, *PCCB* wako pale na *PPRA* wako pale. Hizi ni *initiative* ambazo Wizara yetu tumezifanya katika kuhakikisha kwamba maeneo yote tuliyokuwa tukiyatilia mashaka tunapeleka vyombo hivyo vitatu ikiwa ni pamoja na Uhamiaji. Tutafanya hivyo maeneo yote tutakayoona kwamba kuna wasiwasi. Mtuamini, sisi ni watu wa Hapa Kazi Tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa ni lile la usimamizi wa sheria barabarani. Hili nalo tunalifanyia kazi kwa nguvu zetu zote. Tayari aidha, tumewaondoa baadhi ya askari katika Kitengo cha Usalama Barabarani au tumewafukuza, hakuna maneno. Tunatambua kwamba kuna Watanzania wengi ambao hawana kazi, mtu yeyote tutakayempa kazi na akaichezea atupishe tutapeleka watu wengine chuo chetu kule Moshi, watapata *training* waje waajiriwe Jeshi la Polisi. Hivyo ndivyo ilivyo na ndiyo sababu nikawapa kwanza yale maelezo ya mwanzo manne. Ni Jeshi la Polisi jipya, ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mpya, tupitishieni bajeti tukafanye kazi.

MHE. HALIMA J. MDEE: *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Endelea tu unajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye hoja mbalimbali zilizochangiwa na Wabunge. Uchakavu wa vituo vya polisi na nyumba na hili limezungumzwa na Mheshimiwa Kangi Lugola amesema atakuletea ile picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilivyotembelea mimi mwenyewe nilisikitika na ndiyo sababu tukafanya juhudi kuhakikisha kwamba tunajenga nyumba za askari. Tunajenga nyumba za polisi 4,136 kwa mpangilio uliopo sasa hivi lakini vilevile tunajenga nyumba 9,500 za magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala haliwezi kuchukua mwaka mmoja. Unapoanza kujenga nyumba labda sijui tuchukue wakandarasi wangapi, tunapopanga kuna kitu kinaitwa *absorption capacity,* tukisema kwamba mbona nyumba ni 4,136 tu, je, tukisema tujenge nyumba 10,000 tutazijenga mwaka mmoja na kwa utaratibu upi?

Kwa hiyo, hayo ya nyuma yameshatokea, kilichopo ni kuboresha tukienda mbele na tunasema tunaanza na nyumba 4,136 kwa polisi, nyumba 9,500 kwa magereza na hili halitafanyika katika kipindi cha mwaka mmoja tu. Tumeona mfano wa nyumba za polisi tulizozijenga Kurasini, zinazojengwa Mwanza, tumeona nyumba ambazo tumezijenga kwa Jeshi la Wananchi hazikuchukua mwaka mmoja, lakini tuna mpango huo na tutahakikisha

kwamba tunaendelea kujenga kwa kadri uwezo utakavyokuwa unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limejitokeza sehemu mbalimbali ni uhaba mkubwa wa mafuta na vipuri. Ni kweli katika magari yetu ya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto kuna uhaba wa mafuta na vipuri, hili na sisi tumeliona, tunashukuru kwa vile na ninyi mnaliona lakini tushirikiane kwa pamoja kupeana taarifa pale ambapo kunakuwa na ukosefu wa vifaa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lililotolewa na baadhi ya wenzetu ni kwamba mafuta yaende moja kwa moja kwa *OCDs* yasipitie kwa *RPCs*, pendekezo hili tunalichukua, tukalifanyie kazi na tukiliona linawezekana kufanyika basi tutafanya hivyo lakini kwanza tulifanyie utafiti tuone kama linawezekana kufanyika. Kama haliwezi kufanyika basi tutaona namna ambavyo tunaweza ku-*improve system* iliyopo sasa hivi iweze kuwa ya haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweneyekiti, eneo lingine ambalo limezungumziwa kwa hisia sana ni ulinzi binafsi kutokuwa na sheria. Hili na sisi katika Wizara tumeliona, tumewapa Jeshi la Polisi waweze kuangalia na kuona kama tunaweza kuwa na sheria ya haraka zaidi ambayo tunaweza tukaipitisha ili tuweze ku-*regulate* huu ulinzi binafsi. Nadhani ni wazo zuri na sisi tunalichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa ni msongamano katika magereza yetu. Ni kweli, mimi nimetembelea magereza yote Dar es Salaam na mengine mikoani, msongamano kwa kweli ni mkubwa. Kama nilivyosema kwenye bajeti yetu kwa mwaka huu tutakarabati mabweni 49 na tutajenga mengine na tutaendelea kujenga magereza sehemu mbalimbali hasa hasa kwenye maeneo mapya ya utawala kama ambavyo imependekezwa lakini hii itategemea na upatikanaji wa fedha mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzungumzie suala la mikataba. Mikataba yote ina matatizo, Mheshimiwa Masoud ndivyo alivyokuwa anasema. Nadhani *solution* siyo kuleta mikataba hapa kwa sababu hadi leo hii kuna utaratibu maalum kama Mbunge au Kamati ingependa kuona mkataba, utaratibu upo wazi kabisa. Sidhani kama tutakuwa tunachukua mikataba halafu tunakuja tunaigawa humu yote kila mtu aone kwa sababu kila mtu ana nia yake. Lazima itambulike kwamba mkataba kati ya *institution* na *supplier* ni mikataba ya watu wawili, sidhani kama wewe ungependa mkataba wako na mtu fulani upelekwe mahali pengine au kwa mzazi wako lakini utaratibu upo hata mkitaka kuona mkataba wa Lugumi, tungeweza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwaonye na niwaambie ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge haya mambo ya *security* tunaiweka nchi katika hali ya utata. Tuyafanye kwa utaratibu ambao hauta-*disclose information* kujua kwamba kumbe polisi wana mkataba na mtu fulani kwa hiyo wana *system* fulani hao wahalifu watajua *system* uliyonayo na wataikwepa. Kinachotakiwa hapa, tutumie utaratibu wetu wa kawaida ambao upo hata mkitaka mikataba yote mtaiona, upo na upo *very clear*.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunapiga kelele, tunaandika kwenye magezeti, *we are putting our country at risk*. Nichukulie tu mfano huu mkataba wa *AFIS,* sasa hivi kila mtu anajua kwamba Tanzania wanatumia mashine fulani za kutoa *finger prints*. Sasa ukishafanya hivyo mtu aliyekuwa anataka kutenda jambo bovu ataji-*protect*. Hivi sasa hao wanaotenda mabovu wakianza kuvaa *gloves, don't you see that you are putting your country at risk?*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachowaomba jamani tukihitaji mikataba au tukihitaji kujua *facts* tufuate utaratibu wa Kibunge badala ya kwenda ku-*shout* na kupeleka haya mambo kwenye magazeti. Hakuna mtu anayeficha kitu, *after all* sisi wenyewe tunapenda sana kupata ushauri wa watu ambao ni *the right channel,* lakini tutumie utaratibu ulio sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa sana, ndiyo sababu hamjaniona hata siku moja nimejibu chochote kwenye magazeti, lakini *we shout a lot* kwenye magazeti. Hilo nawashauri kama Wabunge wenzangu ninyi mna *responsibility* ya kulinda usalama wa nchi yetu. Kama Wabunge tumieni *the right channel* ku-*request information* mnayoihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumzwa na watu wengi sana ni maslahi ya askari mbalimbali. Kweli mimi nakubaliana nalo. Ukiangalia hotuba yangu kuna maeneo mbalimbali ambayo tunajaribu kuboresha maslahi ya askari na hili kwa kweli mimi nitalipigania kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira mengine siyo mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nataka nikiseme, kuna jambo limesemwa na upande huu kwamba askari wanatumiwa na Chama cha Mapinduzi. Jamani mtakapomaliza hapa si mtakwenda kwenye mikutano ya hadhara, niambie askari achana nao, ninyi hamuwatumii askari kwenye mikutano yenu? *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi unajua huwa ni mkweli kupita kiasi na nasimamia Wizara hii kwa kufuata STK, nitahakikisha kwamba sheria, taratibu na kanuni zinafuatwa, basi.

MBUNGE FULANI: Wewe ni mwaminifu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Sasa kama mimi ni mwaminifu au nini lakini ukweli unabaki pale pale, tufanyeni kazi kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni. Askari yeyote ambaye hatafuata sheria, taratibu hata kanuni nimesema *consequence* atakazozipata. Kama kuna askari ame-*misbehave* mwambie Mkuu wa Wilaya, *RPC* au *OCD* wake na kama unashindwa namba yangu iko wazi nipigieni, uwe Mbunge wa CCM, CHADEMA, CUF na hilo mnalitambua, Mheshimiwa Masoud unalitambua. Mheshimiwa Masoud anatambua kwamba mimi sibagui kwa sababu Jeshi letu la Polisi linalinda usalama wa raia na mali za Watanzania wote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *suggestion* kwamba tuongeze boti za doria hasa baharini. Hilo na sisi tumeshaliona na siyo baharini tu, wale wenzetu wanaotoka Mkoa wa Kagera, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa wana tatizo hilo. Kwa hiyo, tunaliangalia *comprehensively* tuone ambavyo tunaweza kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msigwa anasema…

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Muda umeisha?

MBUNGE FULANI: Bado.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Ya kwanza.

MBUNGE FULANI: Malizia.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Nimalizie kidogo? Si mnapata ukweli? Nashukuru sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msigwa anasema alibambikwa kesi, kama kweli alibambikwa kesi njoo niambie. Wewe ni Mheshimiwa una-*access* ya kuniona wakati wowote tuone ni kwa namna gani tunaweza tukalirekebisha hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lugola amezungumzia yale yaliyokwishazungumzwa na yameshajibiwa na mwenzangu, lakini moja ambalo amelisisitiza ni kwamba tuwe na vituo vya kutosha katika maeneo mbalimbali. Ni kweli kama nilivyosoma kwenye hotuba yangu tunakwenda polepole, lakini ni kwa kulingana na uwezo tuweze kujenga vituo katika maeneo mbalimbali hasa Wilaya mpya au maeneo mapya ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lwakatare amezungumzia suala la kubambikwa kesi nimeshalijibu.

Mheshimiwa Khatib nadhani nimekusikia na tuna mpango wa pamoja wa kutembelea maeneo aliyoyasema, tumeshaongea, nitaenda hata kwako, usifikiri siendi upande wa CUF naenda tu, wote ni raia. Mbunge yeyote ambaye ana nia ya kwenda na mimi tujadiliane, tuone tukiwa na nafasi tutakwenda tu tuone kwa sababu nia ni kuhakikisha kwamba nchi nzima inakuwa salama na kuna usalama. Kwa sababu anapotoka Mheshimiwa Khatib pale siyo wote ni CUF, kuna wengine ambao ni CHADEMA, kuna wengine ambao ni CCM na Serikali yetu kama ambavyo Mheshimiwa Rais wetu anavyosema ni Serikali ya Watanzania wote na yeye ni Rais wa Watanzania wote na mimi ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani niishie hapo kwa kusema naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono, Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management*…….....Sh.1,236,434,000

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimeshapata majina, tumeanza moja kwa moja na Fungu 51, Mheshimiwa Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Swali langu linahusu Ofisi ya *NIDA*. Kazi ya *NIDA* ni kutoa vitambulisho kwa raia wote wa Tanzania na wale wakazi ambao wamekubalika kuishi nchini,

lakini kazi hii imekuwa ikisuasua kwa muda mrefu. Kipindi kilichopita tuliambiwa kwamba inawezekana *NIDA* wakatoa vitambulisho kwa takribani asilimia 80 ya Watanzania lakini mpaka sasa kazi hii inasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia hotuba ya Waziri sikuridhika na maelezo yaliyotolewa. Maana katika ukurasa wa 52 wa hotuba yake ameonesha kwamba ni mikoa nane tu ambayo ina ofisi za kutambua na kusajili wananchi na kuna Wilaya kumi na mbili tu ambazo wala siyo za pembezoni na wahamiaji haramu wanaoingia wanaingia kupitia Wilaya zetu za pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani kazi hii ingekuwa rahisi kama *NIDA* wangeshirikiana na ofisi ya *RITA* maana *RITA* wanasajili wanaozaliwa, lakini mawasiliano hayo hayapo. Je, Waziri ananieleza nini au anawaeleza nini Watanzania kuhusu Ofisi za *NIDA* kujengwa Wilaya za pembezoni? Nisiporidhika na majibu ya Waziri nitatoa shilingi na nitaomba Wabunge mniunge mkono.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika hotuba yangu ni kweli kumekuwa na kusuasua, lakini kama tutapata pesa kwa mwaka huu matarajio yetu kufikia tarehe 31 Disemba, 2016 Watanzania milioni 22 watakuwa wamepata utambulisho. Labda nitofautishe kati ya utambulisho na kitambulisho. Utambulisho maana yake ni kwamba tutakuwa tumewatambua kwamba huyu ni Mtanzania, rekodi zake tunazo na tumemuweka kwenye *database* lakini wakati huo huo kwa sababu uwezo wa mashine tulizonazo za kuzalisha vitambulisho mdogo basi hao watu watakuwa wakisubiri vitambulisho vikiwa vinakuwa *produced* siku hadi siku. Sasa hivi tumepanda, kuna mtu alisema tunatoa vitambulisho 2,500 tu, tumepanda kutoka 2,500 mpaka 5,000. Tumepunguza watu lakini sasa hivi *efficiency* imekuwa kubwa na tunatarajia kwamba hizo Wilaya zilizoko pembezoni na zenyewe zitakuwa zimefikiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri na ukizingatia ndugu yangu Mheshimiwa Nsanzugwanko pale, ndugu yangu Mheshimiwa Zitto Kabwe, wale ambao wanatoka Kusini huku mpakani na Malawi, mpakani na Kenya, Uganda, kila siku kuna wahamiaji haramu ambao wanatusumbua, nilitegemea kwamba Waziri angenipa majibu ya kuridhisha. Ninapoangalia fedha za maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya *NIDA* ni shilingi bilioni 30 tu. Hata fedha zilizotengwa mwaka jana hazikutoka zote.

Kwa hiyo, sina uhakika kama hizi shilingi bilioni 30 zitatoka na sina uhakika kama fedha hizi zitatosha kujenga ofisi na kuwaandikisha raia wa Tanzania kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono kwamba suala hili sasa litizamwe kwa jicho lingine na ofisi zijengwe katika maeneo ya Wilaya za pembezoni lakini pia Watanzania wapate utambuzi na vitambulisho kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Watakaochangia hoja hii ni Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Venance, Mheshimiwa Paresso, Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Nditiye. Tunaanza na Mheshimiwa Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Ni kweli kwamba kuna umuhimu wa *NIDA* kuongezewa fedha za kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yaliyoko mbele yake. Kama mtoa hoja alivyosema imetengwa fedha kidogo na tunatambua kwamba hivi vitambulisho kwa sasa bado hata havijaanza kutumika na kutambulika mfano kwenye mabenki na mahali pengine. Kwa hiyo, maana yake tunahitaji kuwaongezea uwezo *NIDA,* tunahitaji fedha zipelekwe kwa wingi ili yale matarajio ambapo *NIDA* inatakiwa iwafikie Watanzania milioni 40 katika maeneo mbalimbali na hasa ukizingatia jiografia ya nchi hii yaweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *NIDA* ni juzi tu wamepunguza watu wengi tu wanasema wanataka wawe na watu wachache kuliko kubeba mzigo wa watu wengi ambao ni watu wa muda, wao walikuwa wanawachukulia kama ni wafanyakazi wa *temporally,* wanaoingia mkataba kwa muda fulani. Sasa wanawaondoa hawa wafanyakazi, wanawatengea fedha kidogo, halafu unataka ufanisi uwepo, huu ufanisi utatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kweli kwamba Serikali hapa mlikimbilia kuanzisha *NIDA* kutaka kuwaandikisha Watanzania bila kujiandaa. Jambo hili mlikurupuka tu mkalichukua. Sasa kwa sababu mmelikubali, mmelibeba hili zigo ni muhimu mhakikishe mnatenga fedha za kutosha *NIDA* ifanye kazi ambayo inatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga hoja ya Mheshimiwa Bura. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Chenge.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi niiunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili ni muhimu sana na hasa kwa lengo la kupanua wigo wa walipa kodi. Chombo hiki kikiwezeshwa vizuri na Serikali na mimi naomba sana Bunge hili tuwe *pro-active* katika kuiombea fedha *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho hivi vitasaidia sana *not only* kwa mapato ya Serikali ambayo tunataka tuone yanapanuka, lakini pia mifumo hii tukiifanya *intergrated,* vizazi na vifo, uchaguzi lakini pia hata leseni za magari itasaidia sana mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu nchi jirani ya Uganda walituambia mapema sana, mimi nikiwa Waziri wa Mambo ya Afrika Mashariki wakati ule kwamba jaribuni kuwa na mfumo ambao utakuwa *intergrated* na itawasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya naona kila mmoja amekuwa anavutia kwake lakini tukifika tukaangalia maslahi mapana ya nchi yetu, *NIDA* kupitia vitambulisho hivi tutaweza kunufaika sana kwa kuwatambua Watanzania, kwa mapato ya Serikali lakini pia ufanisi ndani ya mifumo yetu mingi na upande wa fedha pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwijage.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja ya kutambua Watanzania raia na Watanzania wakazi ni hoja ambayo mtu yeyote hawezi kuipinga. Hata hivyo, mapendekezo ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba tunaendelea na kasi ya kutambua watu hawa. Pamoja na kupunguza wafanyakazi kasi au ufanisi wa utendaji kazi umeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa namshawishi Mheshimiwa Bura tukubaliane na mtazamo wa Waziri, tumpe nguvu aendelee na kasi yake, tutaendelea kuwasajili watu hawa. Niazime wazo la Mheshimiwa Chenge, kuunganisha taasisi na mamlaka ni jambo ambalo kila mtu anakubali, *TRA* na wote wataingia pale. Mimi nina imani na pesa alizopangiwa Mheshimiwa Waziri, tuendelee na kwa sababu wote tuko hapa, pale itakapopungukiwa tutaweza kuongezea kulingana na mahitaji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshauri Mheshimiwa Mbunge arudishe shilingi ya mchapakazi (STK) aende kazini halafu tuweze kuona mambo yanavyokwenda.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nditiye.

MHE. *ENG*. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi niungane na Mbunge mwenzangu hapa kuiondoa shilingi. Kusema kweli sisi Wabunge ambao tunatoka pembezoni, mimi natoka Wilaya ya Kibondo, sehemu kubwa sana tunapakana na nchi ya Burundi yaani pale hakuna mpaka ambao unaeleweka kiwaziwazi, watu wanaingia na kutoka, watu wanalala upande wa huku na huku. Nashangaa na mpaka sasa hivi bado sijaelewa ni mantiki gani iliyotumika kufanya Serikali iamue *NIDA* waanzie zoezi lao katika mkoa wa Dar es Salaam. Wakatoka hapo wakaenda Morogoro na Pwani wakati kuna mikoa ambayo uhakika wa raia ni yupi haupo kama mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kutetea kuongezeka kwa bajeti ya *NIDA*. Tukumbuke kwamba sakata lililowakuta *NIDA* lilikuwa linahusisha zaidi ya shilingi bilioni 198 lakini vitambulisho hata robo hawakutoa. Sasa hivi licha ya watumishi kupunguzwa, hata waliobaki wanafanya kazi kwa mashaka makubwa sana. Watu wanaweza wakaenda ofisini hawafanyi kazi yoyote. Naomba sana hili suala la kuanzia zoezi mikoa ambayo haiko pembezoni liangaliwe vizuri sana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Masoud ajiandae Mheshimiwa Venance.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zimetengwa ni shilingi bilioni 30, uwezo wa mashine za *NIDA* kuzalisha ni 3,000 kwa siku, siku za kazi ni 22 katika mwezi, vitambulisho ambavyo vitazalishwa ni 66,000 na kwa mwaka ni 800,000 tu. Kwa Watanzania ambao amesema Mheshimiwa Waziri milioni 22, tunachukua miaka 22 ndiyo tupate vitambulisho. *(Makofi)*

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: *Yes!*

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 fedha ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya *NIDA* ni shilingi bilioni 151 wakapewa shilingi bilioni 60 tu. Mwaka 2014 zilitengwa shilingi bilioni 160 wakapewa shilingi bilioni 56 tu. Mwaka 2015/2016 zilitengwa shilingi bilioni 45

wakapewa shilingi bilioni mbili tu. Serikali haiko *serious,* sisi tunashangaa! Hii ni takwimu sahihi. Si ya kupika ni sahihi kabisa kwamba Serikali haiko makini, haiko tayari. Iliingia mkataba na kampuni ya Malaysia mwaka 2011 sasa miaka mitano imepita hakuna kitu, mtachukua miaka 22 ndiyo Watanzania wapate vitambulisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwa hili tuko pamoja mengine, hapana, Serikali iongeze fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Venance jiandae Waziri wa Fedha.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia niungane na wenzangu ambao wameleta hoja hii. Mimi binafsi ningependa kusema kwamba ingekuwa vema sasa wenzetu wa vitambulisho *(NIDA)* wajiangalie upya. Kwa sababu ukiangalia hata vitambulisho ambavyo tayari vimeshasambaa vingi watu wameanza kutengeneza kama vilevile na ushahidi upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wasiwasi kwamba mikoa hii ya pembezoni ambayo Waheshimiwa wamesema, wenzetu wengi wakapata hivyo vitambulisho vya kutengeneza madhara yake baadaye yatakuwa ni makubwa. Tutaingiza watu kwenye fani mbalimbali mpaka kwenye uongozi bila kutegemea kwa sababu tayari watakuwa na vitambulisho. Kwa hiyo, mimi nafikiri tuangalie upya aina ya vile vitambulisho kabla mambo hayajaharibika kama ambavyo hata Mheshimiwa Rais aliwahi kushauri na wachukuliwe hatua.

MWENYEKITI: Ahsante, Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimuombe mtoa hoja arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa maana kwamba kwanza kikubwa ambacho kinatakiwa ni kuangalia upya mifumo ya *NEC* na *NIDA* ili tuhakikishe kwamba zile mashine ambazo ziliagizwa kwa ajili ya kutumika kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu zinaweza zikatumika pia kwa ajili ya kutengeneza Vitambulisho vya Taifa na hivyo kuharakisha zoezi zima bila kuhitaji kutumia fedha nyingi ambazo zinaombwa. Hakuna mtu yeyote ambaye anabisha juu ya umuhimu wa Vitambulisho vya Taifa lakini umuhimu pia wa kuunganisha hii mifumo ili tuweze kwenda kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, dhamira ya Serikali kwanza ni kuhakikisha kwamba tunatumia vizuri zaidi hizi *assets* ambazo tayari zipo ili tuweze kuharakisha zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: *Commitment, intergration* hiyo inaanza lini?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *intergration* tutaianza mara moja katika mwaka ujao wa fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, una jambo lolote la kuongeza?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari *NEC* wameshakubali kutupa zile *BVR* 5,000 na tunatarajia kwamba tutafungua ofisi kwenye kila Wilaya. Labda niseme tu uwezo wa mashine zilizopo sasa hivi zinaweza kutengeneza vitambulisho 24,000 kwa siku. Kwa hivyo, tunachotafuta ni *efficiency* lakini kwa sasa tumeshafikia vitambulisho 5,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikubwa zaidi ambacho kinachukua muda siyo kutengeneza vitambulisho ni kuwatambua hawa watu. Kwa sababu *process* inaanzia kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kijiji au Mtaa, hao ndiyo wanaofahamu wananchi wanaoishi katika maeneo yao. Wakishakuwa wamemaliza wanabandika kwenye mbao za matangazo, zinapita siku saba ili mtu aweze kwenda kutoa pingamizi kwamba huyu si raia au ni raia. Ikishamalizika hapo zinakwenda kwenye Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya. Hivyo, ile *process* ya kuhakikisha kwamba huyu mtu anatambuliwa kama Mtanzania ni ndefu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunajadiliana na wenzetu wa *NEC* ili watupe ile *database* waliyonayo lakini ina *information* chache. *Information* zilizoko kwenye *data base* ya *NEC* ni kama *item* 32 lakini zinazohitajika kutambua kama huyu ni raia ni kama *item* 70 na kitu. Kwa hiyo, tunachukua hii *data base* lakini tutaendelea kuwatambua lakini watakuwa wameturahisishia kwamba hawa tayari tunao na hiyo *process* itaendelea. Pamoja na hayo ndiyo sababu tunasema, sawa, kama mtatuongezea pesa tutanunua mashine nyingine ili tusitengeneze vitambulisho 24,000 tu tuweze kutengeneza hata vitambulisho 50,000 kwa siku. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bura, *commitment* umeiona, *strategy* imewekwa, naomba uwarudishie hela yao.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumtambua Mtanzania na kumpa kitambulisho ni kitu muhimu sana kwa sababu mipaka yetu siyo salama. Kila siku tuna wakimbizi kutoka Burundi, kila siku watu wa Ethiopia wanakamatwa hapa katikati, hili suala lazima Serikali iliangalie kwa jicho lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudisha shilingi ya Waziri kutokana na *commitment* niliyopata kutoka kwa Waziri wa Fedha na kutoka kwake yeye

Waziri STK. Ninakuomba kwa jina lako hili la STK, hili suala lifanyike haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bajeti ijayo sitakubali kurudisha shilingi kwa Waziri kama haya yote waliyoji-*commit* hayatatekelezwa. Naunga mkono hoja na hiyo shilingi namrudishia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina shida ya mshahara wa Waziri, nachotaka kufahamu, pamoja na kazi nzuri ya kujenga nyumba 2,900 za Askari Magereza, naipongeza sana kazi hii. Hata hivyo, kuna nyumba ambazo zimejengwa na maaskari kwa kujitolea katika magereza mbalimbali na hazijakamilika mpaka sasa likiwemo Gereza la Mpwapwa.

Je, Mheshimiwa Waziri, ananiahidi nini katika kukamilisha hizi nyumba ambazo zimeachwa tu kama magofu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, yeye hana haja na shilingi yako.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru mtani wangu kwa sababu hataki kutoa shilingi yangu angalau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa kwa juhudi walizozifanya katika gereza lao. Nachukua hili na nitazungumza na Kamishna Jenerali wa Magereza tuona ni kwa namna gani tunaweza na sisi kama Serikali kuongezea pesa pale ili waweze kukamilisha hizo nyumba. Itabidi tuongee na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye Mfuko Mkuu kwa sababu katika bajeti yetu huku hatukuweza kuweka suala hilo, tumeweka maeneo *very specific* kwa mwaka kesho. Tutazungumza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuone ni kwa namna gani anaweza akatuongezea pesa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati wa majibu ya Mheshimiwa Waziri nilimwelewa *sensitivity* yake kuhusu masuala ya mikataba, lakini vilevile kuna mambo ambayo katika majibu yake nina-*understand* kwamba hayana hiyo *sensitivity* anayoisema. Kwa mfano, mkataba wa majeshi yetu na *any kind of construction* hayana *sensitivity* kama mikataba ya vifaa vya kijeshi dhidi ya majeshi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *sensitivity* hii Mheshimiwa Waziri alikuwa anaijua na hapa amesema kwamba yeye ni mtu wa *action* (STK), hapendi kufuatilia mambo ya umbea wa magazeti. *Sensitivity* hiyo hiyo alipaswa kuwa

nayo vilevile anapoona jeshi letu linakuwa *demoralized,* lina dhalilishwa na wakati alikuwa na kauli ya kuisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina mambo mawili. Ni kwa nini kauli hiyo hakuitoa siku zote amesubiri kuja kuitoa leo wakati kuna *damage* kubwa sana imeshafanyika?

Mbili, ni hili la mkataba wa Polisi Oysterbay pamoja na wawekezaji, nalo linahitaji *sensitivity* kwamba hawezi kutuambia ni nini kinaendelea kwa sababu hata Mheshimiwa Rais mpendwa, ndugu yetu mtukufu Magufuli, naye amelitilia mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asiponipa majibu ya kuridhisha nitatoa shilingi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, magazeti yanapoandika Serikali haifanyi kazi kwa magazeti. Hutonisikia hata siku moja najibu suala la Wizara yangu au la Serikali kwa yale yaliyoandikwa kwenye magazeti. Hata wakiniandika mimi siwezi kujibu kitu chochote kwa sababu magazeti yetu tunayafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijazungumza na gazeti lolote kuhusu hayo mambo yaliyotokea hapa lakini unakuta *page* nzima gazeti limeandika nimezungumza na Mheshimiwa Kitwanga wakato hujazungumza naye hata siku moja, sasa nichukue huo uongo niufanyie kazi wa nini? Leo nimezungumza kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hasa wewe umeuliza kwenye sehemu mahsusi. Ningefuatwa na hii Kamati Ndogo iliyoundwa na Mheshimiwa Aeshi kuja kuulizwa ningejibu. Kwenye Kamati yetu ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama nilienda na *document* niliwajibu, kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu hii mikataba mingine kwa mfano wa ujenzi wa kawaida ambayo haiko *sensitive* ni jambo la kawaida tu kuipata kama utahitaji. Nilichosema ni kwamba kuna utaratibu wa Kibunge ambapo mkihitaji mkataba hata ule *sensitive* unaweza kupatikana. Uko utaratibu unamuomba Katibu wa Bunge, Katibu wa Bunge anauomba mkataba huo na unakuwa ofisini kwake, unaenda ofisini kwake unasoma unauacha hapo. Si ndivyo utaratibu ulivyo jamani? Wazi kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge hakuna kitu kinachokatazwa, tufuate tu utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye hili lingine la mikataba ile hata yenyewe, fuateni tu utaratibu mtapata. Kama mnahitaji mkataba mwandikieni Katibu wa Bunge, unayetaka kuuona atakuonesha ofisini kwake ukishasoma

utauacha hapo na hutakiwi kuupiga kopi na kadhalika. Kuna utaratibu sina *details* lakini zipo. Kwa hiyo, haya yote yanawezekana lakini nilichokuwa nasisitiza ni kwa sisi ambao ni walinzi wa usalama wa nchi yetu kuanza kwenda kwenye magazeti bila kupata uhakika wa kile ambacho tunakihitaji.

MWENYEKITI: Waziri amejieleza vizuri Mheshimiwa Lema na nimekuona unatikisa kichwa, kwa hiyo, nafikiri kuwa *fair* na wewe, mrudishie fedha yake.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno ya Waziri, ni kweli nilikuwa natikisa kichwa lakini kwa *sensitivity* ya jambo hili na maneno ya Waziri, naomba nitoe shilingi na naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono kwa sababu kama maneno ya Waziri ndivyo yalivyo maana yake Kamati Ndogo ya Bunge inayokwenda kufanya *investigation* inahitaji kurudi na kufuata utaratibu ambao Mheshimiwa Waziri ameueleza. Kwa hiyo, natoa shilingi naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono na naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Haya watakaochangia ni Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa *AG*, Mheshimiwa Chegeni, Mheshimiwa Manyanya, Mheshimiwa Bura, Mheshimiwa Serukamba na Mheshimiwa Bashe. Tunaanza na Mheshimiwa Mbowe.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kuunga mkono hoja nikikazia maneno ambayo amezungumza Mheshimiwa Lema kwamba ushauri mzuri ambao ameutoa Mheshimiwa Waziri wa kufuata utaratibu basi ufuatwe tu ili Bunge lako na Kamati mbalimbali zinazotumwa kwenye majukumu maalum na kipekee jambo hili ambalo limeonekana leo kutukwaza sana pande zote mbili lipate ufumbuzi ambao utakuwa ni wa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekuwa lina hisia nyingi na pengine watu wengi wameshindwa kupata ukweli wa mambo ni nini *exactly* kinachoendelea. Kwa sababu hali hii ya hofu na hisia imeachiwa ikatamalaki kwa muda mrefu na Mheshimiwa Waziri ameeleza *procedure* ambayo inaweza ikatusaidia kutoka kwenye tatizo hilo, nafikiri ni jambo jema kuliunga mkono ili basi jambo hili angalau liweze kufikia tamati ambayo inaweza kuwa na muafaka kwa Taifa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ambayo Mheshimiwa Lema alimuuliza Waziri, aligusia suala la mkataba wa ujenzi wa *Oysterbay Police* kwenye ardhi ile ya Oysterbay na majibu ya Waziri

hayakutosheleza. Ninachotaka kufahamu mimi ni kwamba kuna *problem* gani pale Oysterbay?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ambayo Naibu Waziri amesema, amesema kwamba kuna nyumba za askari 22 zinajengwa Mikocheni, kuna nyumba za askari 350 zinajengwa Kunduchi, *I don't know* ni nyumba 350 au ni maghorofa 350, mimi sijui. Hata hivyo, Waziri ameliacha na bahati nzuri limeelezwa katika hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni ambayo imezuiwa na hili ni jambo ambalo linahitaji maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais alipokuwa anazungumza na Makamanda wa Jeshi la Polisi nchi nzima alizungumzia mkataba huu na akasema kwamba Jeshi la Polisi lingeweza kwenda kukopa benki, sitaki kuelewa kwamba Rais hafahamu kwamba Jeshi la Polisi haliwezi kukopa benki na kwamba kazi ya ujenzi wa shughuli za Jeshi la Polisi ni kazi ya dola. Nataka nifahamu kama ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliyemwambia hivyo Rais au kuna nini ambacho kimetokea? Kwa hiyo, naomba maelezo ya Serikali katika jambo hili ambalo Mheshimiwa Lema ameliuliza lakini hatujapata majibu ya Serikali kuhusiana na suala zima la ujenzi wa Oysterbay. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri, kwa vile Mheshimiwa Waziri amezungumza kwa kina hapa na kwa vile Serikali imekuwa ikifanya kwa utaratibu na Bunge lina utaratibu wake wa kupata taarifa inapozihitaji na kwa muda unaotakiwa, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa upande wa pili na hasa mtoa hoja, hili suala bado lina nafasi yake ya Waziri kulileta hapa Bungeni na tukalizungumza vizuri zaidi kama Bunge na tukapata muafaka ambao unaelekea zaidi. Kuliko sasa hivi kumwambia Mheshimiwa Waziri tunataka hiki utupe *commitment* au ufanye namna hii, nadhani Bunge lina utaratibu mzuri tu na nia ya Mheshimiwa Lema hapa ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mimi namfurahia Mheshimiwa Lema kwa sababu anazungumza anachoona kinafaa kwa maslahi ya Watanzania na sisi Wabunge wote tunasema kwamba kama kuna tatizo au kama kuna hoja ya kutaka kuelewa zaidi Mheshimiwa Waziri tutamwambia hapa tena ataleta kwa utaratibu ambao bado Bunge likapata nafasi ya kuelewa kwa undani wake zaidi. *(Makofi)*

Meshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuombe tu Mheshimiwa Lema mtoa hoja, nadhani Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana kulizungumza suala hili na amekuwa muungwana katika hili. Mbunge mmoja alisema kwamba kwa vile Rais ni Msukuma basi Wasukuma wote ni Marais, siyo hivyo, hoja inabaki

kwamba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane suala hili Mheshimiwa Waziri tumpe nafasi alilete hapa Bungeni tulijadili na tulimalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Sasa unatoa hoja tena Shehe? *(Kicheko)*

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bashe, ajiandae Mheshimiwa Serukamba. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104 naongeza muda wa nusu saa.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nataka tu niseme jambo moja. *Concern* ya Mheshimiwa Lema na kama alivyosema wakati anachangia kwamba *is a high time* kama nchi tusahau bendera za vyama vyetu, ni *concern* muhimu sana. *(Makofi)*

Mimi ningeomba kutumia *spirit* hiyo hiyo kwamba anachokitaka leo Mheshimiwa Lema *deep in his heart* anajua kabisa kwamba Waziri hawezi kukifanya sasa hivi na wala hakiwezi kupata majibu sasa hivi. Kwa hiyo, kwa kuwa *concern* yake inahusu mikataba na Waziri yuko *open* kutumia utaratibu wa Kibunge kuitoa na mtu yeyote anaweza kwenda ku-*review* na kwa kuwa kuna Kamati Ndogo iliyoundwa na Kamati ya *PAC* kwa ajili ya kufanya kazi hii, nadhani tusifanye *preemptive* na tusifanye kazi za Shehe Yahya kufikiri majibu yatakayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungefanya jambo moja, tungesubiri ili Kamati ile Ndogo itakapokuja kama hatutoridhika na kazi yake sisi kama Bunge tuna uwezo wa kushauri hatua za kuchukua na namna gani tunaweza kufikia kiu yetu kama Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningemuomba ndugu yangu Mheshimiwa Lema, tumruhusu ndugu yetu STK, Mheshimiwa Waziri aendelee na bajeti yake kwa sababu haya tunayomshika nayo hakuwepo wakati yanapikwa, tusimhukumu kwa makosa ya wengine, tusubiri ya kwake, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Bunge na lina taratibu zake ya kufanya kazi. Nimepata bahati kuwa Mwenyekiti wa Kamati, *PAC* inavyofanya kazi inafanyia kazi yaliyoandikwa na *CAG*. Wakishayapitia

wanakaa na CAG, wanaweza waka-*pick* jambo wakaamua jambo hili ngoja tulichunguze kwa kina. Kwa suala la Kibunge jambo hili lililoletwa na Mheshimiwa Lema linashughulikiwa na Kamati ya Aeshi. Kwa hiyo, sisi jukumu letu kama Wabunge tuache kazi ile ya Kamati Ndogo iendelee…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Serukamba, nataka kuweka kitu *on record,* hoja ya Mheshimiwa Lema haiko *specific* kwenye *issue* hiyo… *(Makofi)*

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Nisikilize, naendelea Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Iko *in general,* mbebe zote Oysterbay na kila kitu kwa sababu ukienda huko…

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mwenyekiti…

MWENYEKITI: Nisubiri basi, nilishaelewa hoja yako, najaribu kuiboresha tusijielekeze *only* kwenye hoja hiyo ambayo inazungumzwa, anakwenda *in detail* kwenye *basket* nzima ya mikataba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naenda huko, haiwezekani watu wote tuongee kwa namna moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema hapa kuna hoja ya mikataba, kuna hoja amesema Mheshimiwa Lema hakuna sababu Kamati iendelee, irudi, amesema hapa! Kuna hoja ya mkataba wa Oysterbay, yamesemwa yote kwa pamoja. Ndiyo maana nasema suala la Kamati Ndogo haliwezi kurudi, waendelee na kazi.

Suala la pili la mikataba Waziri amesema vizuri sana kwamba uko utaratibu wa kupata mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachosema mimi sikubaliani na hoja ya Mheshimiwa Lema kwa sababu kuna maeneo anataka kuwaisha shughuli wakati shughuli bado inaandaliwa na kuna maeneo ambayo amepewa utaratibu. Kwa hiyo, mimi namuunga mkono Waziri kwa utaratibu aliouweka. Pia Bunge letu na sisi kama Bunge, kama Kamati mbalimbali tuna utaratibu wa kupata taarifa ili tuweze kuzileta Bungeni zijadiliwe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi naungana na wale ambao wanamuunga mkono Mheshimiwa Waziri hoja yake iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, napenda kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa sababu ya utulivu huu aliouleta sasa hivi kiasi kwamba Waheshimiwa Wabunge tunasikilizana. Kwa sababu naamini wote tupo kwa ajili ya nchi yetu na pale kwenye hoja ya msingi lazima tu tutapata njia ya kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisikiliza baadhi ya majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyazungumza, kimsingi mpaka sasa anaonesha hali ya uwazi wa roho yake kwamba hakuna anachokificha. Pengine tulikuwa na hisia maana hii nchi ni yetu lazima wote tuwe na hali ya kupenda kujua nini kinachoendelea, hakuna makosa hata kidogo. Kwa mfano, hata yale ambayo yameshaendelea kwa upande wa Kamati kuamua kuunda Kamati Ndogo ni hali ya kawaida kunapotokea kuna jambo mnapenda kujifunza zaidi mnaweza mkajiweka wenyewe kwenye Kamati Ndogo ikafanya utafiti zaidi, lakini vilevile ikishindikana kwa siku za nyuma watu tumeenda mpaka hata kwenye Kamati Teule, tumezifanya humu Bungeni. Kwa hiyo, haya siyo mambo ya ajabu na wala siyo mwanzao leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wengine wameshasema, mimi nizidi tu kuliomba Bunge lako Tukufu na nakushukuru sana wewe mwenyewe jinsi ulivyotuongoza, kwa kweli kama tutaendelea kujadiliana kwa sura kama hii siamiani kama kuna mtu atakuwa anakosa jibu humu ndani. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na namuomba kaka yangu Mheshimiwa Lema aiachie hiyo shilingi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Godbless Lema, Mbunge wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe pole Mheshimiwa Waziri, katika historia ya Bunge hili la Kumi na Moja, mkutano huu wa bajeti Wizara yake imeingia kwenye historia, Bunge limeahirishwa kwa sababu ya kwenda kujadili mambo ya msingi yanayogusa bajeti yake. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bobali twende kwenye hoja uliyokuwa nayo.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hoja zilizoelezwa na Mheshimiwa Lema siyo hoja za Mheshimiwa Lema ni hoja za Watanzania. Leo ukisoma kwenye mitandao ya kijamii, ukifuatilia vyombo ya

habari, *tension* hizi zilizoelezwa na zinazoonekana humu ndizo zilizopo nje. Suala la mikataba ya nyumba na hiyo mikataba mingine ambayo haitajiki leo hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono suala la Mheshimiwa Lema ili hili suala lifike mwisho maana kama ungekuwa ni moto sasa moto unaendelea kuwaka tu. Tusije tukaendelea kuuchochea moto huo mwisho wa siku ikawa Watanzania na wenyewe hawaelewi, tunawaingiza kwenye *tension* kubwa na ni hoja ambayo inaweza ika-*create* jambo lingine ambalo mimi sitarajiii kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Lema jambo hili ifike wakati lifike mwisho. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lina namna ya kufanya kazi zake na hasa pale linapo-*doubt* kuhusu jambo lolote. Bunge tumepewa *CAG* kama jicho letu la kutusaidia kuangalia maeneo yenye ufanisi na maeneo yasiyo na ufanisi na *CAG* akishaangalia analeta taarifa Bungeni. Bunge hili lina uwezo wa kumtumia *CAG* kadri linavyoona inafaa na Kamati ya *PAC* imeona kazi iliyofanywa na *CAG* na Kamati Ndogo ikaundwa kwa ajili ya kufuatilia mambo ambayo hawakuridhika. Baada ya hapa masuala yote yataletwa Bungeni kujadiliwa na Wabunge kadri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Lema asubiri taarifa itakayoletwa na *PAC* na pia taarifa ambayo Bunge likimuagiza *CAG* kufanya ataifanya. Nimsihi Mheshimiwa Lema arudishe shilingi ya Waziri na masuala haya yatatekelezwa kadri itakavyoonekana inafaa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kuna la kuongeza?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hoja ya mkataba wa Oysterbay, tulikubaliana kwamba tufanye *cash projection* ili kutumia mwanya wa kufanya *review* kwenye mkataba ambao unaruhusu ili kuweza kuuboresha zaidi. Suala hili la mkataba nadhani si tatizo kwa sababu kupitia Kamati, kwa mfano sisi tuliwahi kuambiwa na Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tuwasilishe mkataba huo na Polisi wakauwasilisha. Sasa hivi hii Kamati Ndogo ya *PAC* inafanya kazi kwa mujibu wa hadidu za rejea ambazo imepewa na Kamati. Kwa hiyo, nadhani tuwaachie tu waendelee na utaratibu wao, pale ambapo itahitajika ushirikiano wowote basi tutakuwa tayari kuutoa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema baada ya yote haya si ukubali yaishe?

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri naelekea huko lakini kwenye suala la *PAC* wamepewa hadidu rejea moja tu, kwenda kuangalia kama vifaa viliwekwa, hakuna kingine wanaenda kutafuta kule. *Issue* aliyoiongea Mheshimiwa Waziri ni *sensitivity* ya mikataba ya vyombo vya ulinzi pamoja na watu binafsi kuwa *public,* ameeleza sana hapa kwamba kuna vitu hawezi kuweka wazi kwa sababu ya *sensitivity* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba haya mambo yanayohusu ulinzi na usalama yanapoachwa muda mrefu katika kiwango kama hiki ambacho yalifikia hata kama hilo jambo lilikuwa lina sura ya malaika litabadilika kuwa na sura ya shetani. Kwa sababu sasa Mheshimiwa Waziri amesema utaratibu wa Wabunge kupata mikataba kupitia *process* za Kibunge ni rahisi na kwa sababu amekwishaiona na alishawahi kuipeleka kwenye Kamati ya Mambo ya Nje na Ulinzi na Usalama, aweke *commitment* tu ya yeye kuleta huo mkataba siku yoyote na siyo…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, ameshakueleza *process* sasa usimrudishe huko. Wewe umeshaelewa vizuri baada ya hapa unaweza ukamu-*engage* baadaye, mkaelezana zaidi namna ya kupata hiyo mikataba.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nitamu-*engage* baadaye naondoa shilingi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Riziki Shahari.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Bismillah Rahman Rahim,* Mimi natoa shilingi ya mshahara wa Waziri na suala langu ni kuhusu mashehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bunge lako hili aliyekuwa Waziri kwenye nafasi hii ya Waziri wa sasa aliliahidi Bunge hili kwamba wale mashehe wataenda kuulizwa na kujua ni nini hasa kilichowasibu. Hapa hapa tunachangia Wizara ya Utawala Bora nililisema hili, ilipokuja kuzungumzwa Wizara ya Sheria likasemwa hili, Kamati ya Kudumu ya Bunge inayohusiana na Wizara hii imekwenda Segerea imeonana na hawa mashehe mbele ya Maofisa wa Magereza, wamelalamikia hali zao na wamesema hawajaenda kuulizwa.

Leo Mheshimiwa Naibu Waziri ananijia na karatasi anaiweka pale ambapo mimi naiona karatasi yenyewe imezeeka, sijui ni ya lini na haikuwa *issue* ya daktari aandike karatasi lake ampe Naibu Waziri ilikuwa watu hawa waende wakaulizwe kilichowasibu. Je, kwenye hiyo ripoti ya Naibu Waziri na huyo daktari wake, *who was the independent third party* aliokuwa nao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani *Chief Justice* wa Kenya alisema unapofikiria kuwadhuru watu, kumdhalilisha mtu wafikirie wanaowapenda. Mashehe hawa wana wafuasi nyuma yao, mimi mmoja wao nawapenda, naumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashehe hawa ni waume wa wanawake kama mimi naumia, mashehe hawa wana wazazi wao wengine bado wako hai, wanashuhudia watoto wao wamedhalilishwa na vyombo vya usalama. Wamesema mahakamani wale mashehe tumefanyiwa visivyo, wengine tumetiwa vitu kwenye tupu za nyuma na hali imekuwa hivi, leo hapa Naibu Waziri anatuletea kikaratasi anatuambia hakuna kilichotokea. Nashika shilingi naomba mniunge mkono Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama kuunga mkono hoja ya Mhe. Riziki S. Mngwali)

MWENYEKITI: Jamani, utaratibu sio huo, subirini kwanza. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nilipokuwa naelezea pale Mheshimiwa alikuwa hajanifahamu vizuri labda nichukue fursa hii kufafanua.

Kwanza, kuna kitu kimoja lazima kieleweke kwamba hawa mashehe toka kipindi ambacho wamelalamika kwamba wamedhalilishwa na kipindi ambacho wamekamatwa ilipita takribani miaka miwili, kwa hiyo katika hali ya kawaida kwanza lazima upate mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kwamba nilichokisema mimi na ambacho kipo katika hizi *document* ambazo nimeziwasilisha mezani, tarehe 27/4/2016 watuhumiwa 23 waliokuwa mahabusu waliopo Gereza la Segerea, ndiyo hao mashehe anaowazungumza walifanyiwa uchunguzi wa afya Hospitali ya Muhimbili baada ya kulalamika na ripoti ya daktari ndiyo hii ambayo nimeiwasilisha, hawakuonekana na tatizo lolote la kudhalilishwa.

MBUNGE FULANI: *It was independent?*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: *Ndiyo maana nikasema vitu vingine ni maneno ya mitaani tu…* **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

MBUNGE FULANI: Aaah.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: ....tukiyaleta hapa Bungeni inakuwa haipendezi. Nadhani cha kufanya mchukue hii ripoti muipitie, muone kama kuna ukweli au haupo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Riziki.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa wanasema sana kuhusu lugha ya kuudhi, hii ni lugha ya kuudhi. Mimi nina heshima zangu, nina *integrity* yangu, siwezi kuchukua maneno ya mtaani nikayaleta hapa. Ninayoyaleta hapa nina uhakika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikauliza hiyo ripoti anayosema wamekwenda kuchunguzwa ni nani *independent third party?*

Mimi jana nimezungumza na mawakili wao, nani *independent third party* alikuwa na hao watu wako, sijui madaktari wakati wanawapima hao mashehe? Mimi nasema *issue* haikuwa kupimwa afya, ilikuwa Waziri Chikawe kaahidi hapa, ingawa baadaye alimalizia kwa stihizai lakini alisema hapa kwamba atapeleka jopo likawaulize wale mashehe waseme kilichowasibu. Wale mashehe walikwenda wakasema mbele ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge wakati ilipotembelea kule Segerea Kamati. Leo Mheshimiwa Naibu Waziri ananiambia maneno ya mtaani, natoa shilingi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa toa hoja.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Ametoa.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti nimetoa hoja kwamba kwa misingi ya haki za binadamu, nchi hii lazima...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto hajatoa hoja mimi ndiyo najua.

WABUNGE FULANI: Ametoa hoja, ametoa hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mimi nazungumza na Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Riziki kasema anatoa shilingi lazima aseme natoa hoja.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Alitoa.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Haya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib kaa chini.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Nakaa, lakini alitoa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Riziki nimeshakuelewa kaa chini. Haya watakaochangia wasimamie, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla...

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Maftaha Nachuma huku.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *AG,* Mheshimiwa Adadi, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Zitto…

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Chumi unaniruka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ali Khamis, Mheshimiwa Maryam.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Muda wote unaniruka Mwenyekiti.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Hoja yetu hii Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Si Ali Khamis?

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Chumi unamruka.

MWENYEKITI: Ali Khamis nimeshamtaja.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Maftaha.

MWENYEKITI: Haya na Mheshimiwa Maftaha kama muda utatosha na Mheshimiwa Chumi.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Aah ni haki yangu kama Mbunge.

MWENYEKITI: Tunaanza na wewe Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona.

Mimi kwanza niseme ni Mjumbe wa Kamati hiyo ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na mimi nilikwenda Segerea katika ziara yetu ya Kamati na tulizungumza na wafungwa na mahabusu katika ujumla wake kila watu kwa makundi yao na kusikiliza malalamiko, mapendekezo na hoja zao mbalimbali. Hilo ambalo Mheshimiwa aliyetoa shilingi amelisema, sisi kwetu hatukulisikia.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati nilikuwepo pale na kama ambavyo Kamati yetu imetoa mapendekezo, tulitoa fursa katika namna ambayo ni ya uwazi

kabisa na tulioneshwa baadhi ya wafungwa ndani ya wafungwa yaani wale ambao wanakuwa wanafanya makosa ndani ya jela wanawekwa sehemu nyingine ikiwemo makosa kama haya ya kuwasumbua wenzao wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi kwa upande wangu, niko upande wa kumuomba Mheshimiwa aliyetoa shilingi airejeshe kwa sababu haya yaliyosemwa kwangu mimi sikuyasikia na nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati ile. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Adadi.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningemuomba Mheshimiwa Mbunge ajaribu kurudisha shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Nasema hivyo kwa sababu ni kweli kabisa Kamati yangu ilikwenda Segerea na Segerea kule tulikuta malalamiko mbalimbali yakiwepo hayo ya mashehe. Mjumbe mwenzangu alikuwa sehemu nyingine hakuwepo pale kwa mashehe, lakini hao mashehe walilalamika kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na malalamiko yao, tulimuagiza Waziri kwamba achukue malalamiko hayo na ayafanyie kazi. Malalamiko ambayo walikuwa wanalalamika kwanza ni kukamatwa na kushtakiwa isivyo halali wanaona kwamba hawana makosa yoyote yale. Pili, ni hayo mateso ambayo ameyazungumza hapa Mheshimiwa. Matokeo ya Mheshimiwa Waziri ni kama hayo kwamba mashehe wamefanyiwa utafiti na madaktari na hawakuonekana na hayo matatizo waliyokuwa wanayazungumza.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: *Was it independent?*

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho Kamati ilimuagiza Waziri kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Mashtaka, kwanza ni kuhakikisha kwamba hiyo kesi ya hao mashehe kama ipo inasikilizwa haraka. Hilo *file* lipelekwe kwa Mkurugenzi wa Mashtaka alitolee maamuzi. Baada ya maamuzi hayo kama kesi hiyo ipo na inasikilizwa, ina ushahidi basi isikilizwe na kama hakuna ushahidi basi wale mashehe watolewe. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Baada ya hao mashehe kutolewa kama watakuwa na malalamiko mengine nje ndiyo wataleta hayo malalamiko mengine watai-*sue* Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Cha msingi sasa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante muda wako umekwisha.

MBUNGE FULANI: Bora wewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbowe.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo tunalolizungumza na hawa wahusika tunaozungumzia ni viongozi na zaidi ni viongozi wa kidini, wa kiimani. Tunapoanza kuwachanganya viongozi wetu wa kiimani na tuhuma ambazo zinashindwa kuthibitishwa kwa zaidi ya miaka mitatu, sijui tunataka kulijenga Taifa la namna gani? *Justice delayed, is justice denied*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalali wowote wa mashtaka yanayowahusu watuhumiwa hawa ambao kwa bahati mbaya sana Mheshimiwa Waziri alizungumza hapa kama vile anaona ni jambo jepesi tu. Viongozi wa kiroho wanarundikwa ndani, huu ni mwaka wa nne, *investigation* haikamiliki, wengine wanapigwa risasi, ninyi mnaona ni mambo ya kawaida tu, ni mambo mepesi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine la msingi hapa, jambo linalotia uchungu zaidi ni pale zinapojengwa hisia kwamba viongozi hawa wa kiimani pengine wanaonekana wana misimamo ya kusimamia ama kuunga mkono mlengo fulani wa kisiasa.

Kwa hiyo, unakuwa ndiyo msingi wa kujenga chuki na kubambikiza watu kesi na makosa *serious* kwa kiwango hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni watu wazima, watu wamekaa miaka minne wakiteswa, wakidhalilishwa, wakinyimwa dhamana…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbowe ahsante. Mheshimiwa Maftaha na tunamalizia na Mheshimiwa *AG*.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda na muda haiwezekani kila mtu akapewa nafasi.

MBUNGE FULANI: Wengine bado.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maftaha.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa sababu nimekuwa nikiomba tangu asubuhi sionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Riziki ya kutoa shilingi kwa sababu kwa masikitiko makubwa kabisa mimi tangu nakua nchi hii nimekuwa nikisikia na nikiona sana viongozi wa kiislamu hasa hasa mashehe wanadhalilishwa sana na wanapigwa sana. Miaka kadhaa iliyopita sisi wote ni mashahidi humu ndani bila kujali itikadi za vyama vyetu tulishuhudia mashehe pia wanaburuzwa katika nyumba zao za ibada kwa maana ya misikitini pamoja na kupigwa risasi katika lile sakata Mwembechai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hilo tu, leo hii kuna mashehe wapo jela hivi tunavyozungumza takribani ni zaidi ya miaka mitatu lakini hawajapelekwa mahakamani, wanasingiziwa eti ni magaidi. Naomba kuuliza hivyo nchi hii magaidi ni waislamu tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba Mashehe...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla dakika moja ukiwa kama daktari halafu *AG*.

WABUNGE FULANI: Aaaah.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa dakika moja. Kwanza kwenye mambo ya *forensic medicine,* mambo ya uchunguzi wa kidaktari ambayo huwa inapelekea kutolewa kwa ripoti kama aliyoiweka mezani Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, ripoti ya daktari huwa ni *final* (mwisho) na ripoti ya daktari ikishatolewa huwa haihojiwi…

WABUNGE FULANI: Aaah.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Kwa sababu daktari wakati anaitoa, anaitoa kwa sababu za kitaalam na anaitoa akiwa chini ya kiapo na si kiapo tu hiki cha kawaida lakini ana kiapo cha kidaktari ambacho kina heshima ya kipekee katika maisha ya *professionalism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka nitoe hiyo taarifa tu, kumuondoa shaka Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali kwamba…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa *AG*.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Wacha tumalize kazi hii.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Taarifa kabla hajaongea *AG*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto kaa chini, *please*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani suala la msingi hapa ni hilo aliloshauri Mheshimiwa Adadi kwamba shauri hili lisikilizwe kwa sababu liko mahakamani hata kulijadili hapa tunakosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kosa hili la ugaidi halina dhamana. Kwa hiyo, siyo kwamba wako gerezani kwa sababu tu ni waislam wanazuiliwa kule…

MBUNGE FULANI: Ndiyo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Ila ni kwa sababu kosa ambalo wanashtakiwa nalo la ugaidi huwa halina dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu ni hili ambalo amelisema Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, lazima Waheshimiwa Wabunge tujenge tabia ya kuwaheshimu madaktari…

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya Sheria ya Magereza inaruhusu mahabusu na wafungwa kwenda kutibiwa hospitalini lakini haiweki masharti ya kuwepo na *third part,* hilo la kwanza.

La pili, Sheria ya Polisi inaruhusu mtu yeyote awe mfungwa awe mahabusu, awe raia ambaye hajakamatwa, anayelalamika kwamba ameumizwa kwenda polisi akachukua *PF3* akaenda kwa daktari lakini hakuna sharti la kuwepo na *third part*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Nne, siku tulipojadili Wizara ya Katiba hapa taarifa zilitoka …

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa *AG*, Waziri dakika moja.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nili-*withdraw* lile neno ambalo limemuudhi Mheshimiwa Riziki, sikukusudia kuku-*offend* kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuliondoa neno hilo, baada ya kueleza haya nitakayoeleza basi nikuombe shilingi yako uirudishe nikiwa na imani kabisa utaridhika na maelezo yangu haya ambayo nitaeleza sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka niseme ni kwamba, unajua sisi kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hatuhusiki kuhusiana na uhalali wa makosa, hiyo ni kazi ya mhimili mwingine, sisi tunazungumzia hoja ya magereza ambayo ndio wanahifadhi wale watu. Bahati nzuri nadhani kama mtapingana na maneno ambayo nayazungumza basi kila mmoja kwa wakati wake afanye utaratibu wa kufanya *verification* jinsi ambavyo Askari wa Magereza wanavyokuwa rafiki na wafungwa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Askari Magereza ni rafiki kweli kweli…

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Riziki una dakika moja.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naishikilia shilingi sijaridhika na kilichoelezwa hapa. Kama hiyo taarifa iwekwe upya, humu ndani kuna kiapo/sala ile tunaiomba hapa kila siku asubuhi kusimamisha haki katika nchi hii, haki gani imesimama hapa? Natoa shilingi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kanuni 104(2) siwezi kuongeza muda, tunaingia kwenye *guillotine*.

WABUNGE FULANI: Hoji, hoji.

Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Kifungu 1001 - *Administration and HR Management* ……..Sh.1,236,434,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*……Sh.384,634,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*……..Sh.14,189,793,000
Kifungu 1004 - *Probation and Community Services Division*…..Sh.2,017,386,000
Kifungu 1005 - *Government Communication Unit*……...Sh.115,319,000
Kifungu 1006 - *Management Information System Unit* ……..Sh.131,500,000
Kifungu 1007 - *Internal Audit Unit* ……...Sh.85,074,000
Kifungu 1008 - *Procurement Management Unit* ……....Sh.189,543,000
Kifungu 1009 - *Complaints Division* ……....Sh.98,099,000
Kifungu 1010 - *Legal Division*…….....Sh.316,242,000
Kifungu 4001 - *Refugees Unit*……...Sh.607,964,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 93 -Idara ya Uhamiaji

Kifungu 2001 - *Immigration Zanzibar* ……Sh.5,220,644,000
Kifungu 2002 - *Immigration Mainland* ……Sh.35,591,510,000
Kifungu 2003 - *Regional Immigration Offices* …Sh.5,547,344,000
Kifungu 2004 - *Tz Regional Immigration Training Academy*…Sh.198,102,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 14 - Jeshi la Zima Moto na Uokoaji

Kifungu 3001 - *Fire and Rescue Service*…….Sh.18,713,966,000
Kifungu 3002 - *Fire and Rescue Services Training Inst*. …Sh.478,576,000
Kifungu 3003 - *Fire Safety* ……...……Sh.130,000,000
Kifungu 3004 - *Operations* ……..Sh.487,336,000
Kifungu 3005 - *Dar es Salaam Regional Office*…..Sh.657,301,000
Kifungu 3006 - *Arusha Regional Office* ……Sh.388,700,000
Kifungu 3007 - *Dodoma Regional Office* ……..Sh.300, 900,000
Kifungu 3008 - *Mwanza Regional Office* ……Sh.500,300,000
Kifungu 3009 - *Mbeya Regional Office* ……Sh.313,100,000
Kifungu 3010 - *Kinondoni Regional Office* ……Sh.475,100,000
Kifungu 3011 - *Mara Regional Office* ……..Sh.232,500,000
Kifungu 3012 - *Kigoma Regional Office* ……..Sh.203,700,000
Kifungu 3013 - *Pwani Regional Office* ……Sh.380,100,000
Kifungu 3014 - *Manyara Regional Office* ……Sh.225,300,000
Kifungu 3015 - *Geita Regional Office* ……..Sh.171,300,000

Kifungu 3016 - *Temeke Regional Office* …….Sh.536,300,000
Kifungu 3017 - *Singida Regional Office* ……..Sh.210,900,000
Kifungu 3018 - *Tabora Regional Office* ……Sh.300,900,000
Kifungu 3019 - *Iringa Regional Office* ……..Sh.299,800,000
Kifungu 3020 - *Rukwa Regional Office* ……Sh.174,900,000
Kifungu 3021 - *Ruvuma Regional Office* …….Sh.254,100,000
Kifungu 3022 - *Kagera Regional Office* ……..Sh.236,100,000
Kifungu 3023 - *Mtwara Regional Office* …….Sh.246,900,000
Kifungu 3024 - *Lindi Regional Office* ……Sh.214,500,000
Kifungu 3025 - *Njombe Regional Office* …….Sh.174,900,000
Kifungu 3026 - *Shinyanga Regional Office* …… Sh.292,100,000
Kifungu 3027 - *Ilala Regional Office* ……... Sh.532,700,000
Kifungu 3028 - *Kilimanjaro Regional Office*……Sh. 340,500,000
Kifungu 3029 - *Morogoro Regional Office* …… Sh.344,100,000
Kifungu 3030 - *Katavi Regional Office*…… Sh.167,700,000
Kifungu 3031 - *Tanga Regional Office* …… Sh.326,100,000
Kifungu 3032 - *Simiyu Regional Office*…… Sh.156,900,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani walitoka nje ya Ukumbi wa Bunge)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mnawadhalilisha mashehe tukae humu ndani.

Fungu 28 -Jeshi la Polisi

Kifungu 1002 - *Finance and Accounting* ……Sh.1,743,823,000
Kifungu 2001 - *Police Mainforce*……..Sh. 204,566,498,000
Kifungu 2002 - *Police Marine*…… Sh.1,498,821,000
Kifungu 2003 - *Railway Police division* …… Sh.1,623,954,000
Kifungu 2004 - *Police Signals Branch* ……Sh.1,672,183,000
Kifungu 2005 - *Police Zanzibar* ……..Sh.7,701,878,000
Kifungu 2006 - *Police Air Wing* …… Sh.1,202,566,000
Kifungu 2007 - *TAZARA Police* …… Sh.1,933,018,000
Kifungu 2008 - *Field Force Unit* …… Sh.1,738,064,000
Kifungu 2009 - *Traffic Police*…… Sh.954,398,000
Kifungu 2010 - *Police Airport* …….. Sh.2,221,011,000
Kifungu 2011 - *Police Dog and Horses* ……Sh.1,131,511,000
Kifungu 2012 - *DSM Special Zone* ……Sh.9,122,864,000
Kifungu 2013 - *Police Ilala* ……Sh.9,866,488,000
Kifungu 2014 - *Police Kinondoni* ……Sh.11,004,179,000
Kifungu 2015 - *Police Temeke* ……Sh.8,019,743,000

Kifungu 2016 - *Police Arusha* Sh.12,070,262,000
Kifungu 2017 - *Police Iringa* Sh.7,062,955,000
Kifungu 2018 - *Police Kilimanjaro*..... Sh.10,956,158,000
Kifungu 2019 - *Police Kigoma* Sh.9,621,779,000
Kifungu 2020 - *Police Kagera* Sh.12,177,256,000
Kifungu 2021 - *Police Lindi* Sh.6,640,168,000
Kifungu 2022 - *Police Mwanza* Sh.12,230,382,000
Kifungu 2023 - *Police Mara* .....Sh. 8,823,754,000
Kifungu 2024 - *Police Tarime – Rorya* Sh.6,123,504,000
Kifungu 2025 - *Police Mbeya* Sh.11,815,357,000
Kifungu 2026 - *Police Mtwara*..... Sh.8,984,434,000
Kifungu 2027 - *Police Morogoro* Sh.13,078,380,000
Kifungu 2028 - *Police Manyara* Sh.8,260,831,000
Kifungu 2029 - *Police Singida* Sh.8,638,740,000
Kifungu 2030 - *Police Pwani* Sh.9,341,816,000
Kifungu 2031 - *Police Ruvuma* Sh.7,309,773,000
Kifungu 2032 - *Police Rukwa* Sh.6,089,606,000
Kifungu 2033 - *Police Shinyanga* Sh.6,095,432,000
Kifungu 2034 - *Police Tabora* Sh.7,789,004,000
Kifungu 2035 - *Police Tanga* Sh.9,368,147,000
Kifungu 2036 - *Police Mjini Magharibi* Sh.12,099,015,000
Kifungu 2037 - *Police Kusini Unguja* Sh.5,534,672,000
Kifungu 2038 - *Police Kaskazini Unguja* Sh.4,458,028,000
Kifungu 2039 - *Police Kusini Pemba*..... Sh.4,114,940,000
Kifungu 2040 - *Police Kaskazini Pemba* Sh.4,120,614,000
Kifungu 2041 - *Police Dodoma* Sh.9,387,664,000
Kifungu 2042 - *Police Geita* Sh.6,829,459,000
Kifungu 2043 - *Police Katavi* Sh.4,143,833,000
Kifungu 2044 - *Police Njombe* Sh.5,145,628,000
Kifungu 2045 - *Police Simiyu* Sh.4,743,640,000
Kifungu 3001 - *Police Collage Moshi* Sh.4,872,447,000
Kifungu 3002 - *Police College* Sh.2,002,726,000
Kifungu 4001 - *Police Vehicles Maintenance Unit*.....Sh.2,006,328,000
Kifungu 5001 - *Police Medical Unit* Sh.2,115,991,000
Kifungu 6001 - *Police Building Brigade* Sh.2,504,096,000
Kifungu 7001 - *Criminal Investigation Division*.....Sh.6,808,028,000
Kifungu 7002 - *Stock Theft Prevention Unit*..... Sh.475,419,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 29 -Jeshi la Magereza

Kifungu 1001 - *Prisons Headquaters* …… Sh.6,201,968,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* …….. Sh.6,281,868,000
Kifungu 2001 - *Parole Department* ……..Sh.907,256,000
Kifungu 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation*……Sh.161,898,316,000
Kifungu 2003 - *Resettlement of Offenders*…….. Sh.3,399,864,000
Kifungu 2004 - *Prisons Arusha* ..…… Sh.448,332,000
Kifungu 2005 - *Prisons Dar es Salaam* ……. Sh.1,137,702,000
Kifungu 2006 - *Prisons Dodoma* …… Sh.427,972,000
Kifungu 2007 - *Prisons Kigoma* …… Sh.291,565,000
Kifungu 2008 - *Prisons Tanga* …… Sh.495,110,000
Kifungu 2009 - *Prisons Kagera* …… Sh.404,922,000
Kifungu 2010 - *Prisons Mwanza* ……..Sh.498,172,000
Kifungu 2011 - *Prisons Tabora* ……..Sh.363,732,000
Kifungu 2012 - *Prisons Mbeya* …… Sh.477,934,000
Kifungu 2013 - *Prisons Singida* ……Sh.315,868,000
Kifungu 2014 - *Prisons Coast* …….. Sh.413,060,000
Kifungu 2015 - *Prisons Lindi* …… Sh.358,852,000
Kifungu 2016 - *Prisons Manyara* ……..…… Sh.315,570,000
Kifungu 2017 - *Prisons Mtwara* ……..Sh.375,628,000
Kifungu 2018 - *Prisons Ruvuma* …….. Sh.329,188,000
Kifungu 2019 - *Prisons Rukwa* ……..Sh.349,664,000
Kifungu 2020 - *Prisons Mara* ……Sh.357,596,000
Kifungu 2021 - *Prisons Iringa* …….. Sh.399,112,000
Kifungu 2022 - *Prisons Kilimanjaro* …… Sh.422,348,000
Kifungu 2023 - *Prisons Morogoro* …….. Sh.817,719,000
Kifungu 2024 - *Prisons Geita* …… Sh.41,635,000
Kifungu 2025 - *Prisons Katavi* …… Sh.41,635,000
Kifungu 2026 - *Prisons Njombe* …… Sh.41,635,000
Kifungu 2027 - *Prisons Simiyu* …… Sh.41,635,000
Kifungu 2028 - *Prisons Shinyanga*…….…… ..Sh.302,660,000
Kifungu 3001 - *Prisons Staff College* ..…… Sh.3,330,111,000
Kifungu 3002 - *Prisons Driving School* ..…… Sh.569,807,000
Kifungu 3003 - *Prisons Trade School* …… Sh.935,458,000
Kifungu 3004 - *Prisons College Kiwira* …… Sh.1,873,531,000
Kifungu 4001 - *Prison Building Brigade* …… Sh.1,340,040,000
Kifungu 4002 - *Prison Industries* ..…… Sh.687,720,000
Kifungu 4003 - *Prison Farms* ……..Sh.1,251,220,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 14 - Jeshi la Zima Moto na Uokoaji

Kifungu 3001 - *Fire and Rescue Services* …… Sh.3,500,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 28 – Jeshi la Polisi

Kifungu 2001 - *Police Mainforce*…… Sh.3,077,541,105
Kifungu 2005 - *Police Zanzibar* ……..…… Sh.200,000,000
Kifungu 2020 - *Police Kagera* …….....Sh.450,000,000
Kifungu 2022 - *Police Mwanza* …….. Sh.565,000,000
Kifungu 2023 - *Police Mara* ……Sh.535,000,000
Kifungu 2026 - *Police Mtwara* ……..Sh.12,500,000
Kifungu 2044 - *Police Njombe*…… Sh.530,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 29 - Jeshi la Magereza

Kifungu 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation* …Sh.53,380,000
Kifungu 4001 - *Prison Building Brigade* ……..Sh.3,000,000,000
Kifungu 4003 Prison Farm …….....Sh.0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ……Sh.30,000,000,000
Kifungu 4001 - *Refugee Unit* ……..Sh.0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

Kifungu 2002 - *Immigration Mainland* ……..Sh.6,000,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Mtoa hoja taarifa.

MHE. KABWE Z.R. ZITTO: Naomba Mwongozo kabla ya taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto ngoja tumalize kazi.

T A A R I F A

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bajeti ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda na bajeti imepita.

MHE. KABWE Z.R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo.

MWENYEKITI: Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri mliyoifanya wewe na timu yako, lakini niwapongeze na Wabunge kazi hii siyo rahisi, ni kazi ngumu, inahitaji busara na hekima. Siyo rahisi kila mtu kwenye mshahara wa Waziri akapata nafasi, tunaweza kuandika watu kumi siyo wote wakapata

nafasi. Kwa hiyo, ni busara ilitumika ku-*balance* kila upande wa kambi ambazo tunazo. Kwa hiyo, mimi niwashukuru…

MHE. KABWE Z.R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto, haya mwongozo.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. KABWE Z.R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 68, wakati Bunge lipo kwenye Kamati ya Matumizi kujadili kuhusiana na Wizara ya Mambo ya Ndani, imetokea hoja kuhusiana na mashehe ambao wameteswa kwenye magereza yetu. Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ametoa taarifa ambapo anaeleza ni taarifa ya kidaktari inayothibitisha kwamba hawakufanywa hivyo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Wizara husika ameliambia Bunge lako Tukufu wakati limekaa kama Kamati ya Matumizi kwamba kulikuwa kuna malalamiko ya mashehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kiti chako kiruhusu uchunguzi huru *(independent verification)* ya ripoti ya madaktari ambayo Serikali imewasilisha kwenye Bunge hili Tukufu ili ukweli kuhusu jambo hili uweze kufahamika. Jambo hili siyo dogo, jambo hili ni *very sensitive* na umesikia hoja za Wabunge, ni jambo ambalo linaweza likaligawa Taifa. Sisi kama Wabunge ambao tunatoka kwenye imani tofauti tofauti tukilikalia kimya jambo hili nchi yetu haitabaki sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utumie busara zako uagize iundwe *independent commission* kwa ajili ya kufanya *verification* ya ripoti ya madaktari kwa ajili ya kwenda gerezani kuwahoji mashehe hawa wanaolalamika na ripoti ile Bunge iweze kuletewa. Siyo *commission* ya Bunge, namaanisha *commission* ya *experts,* watu wa haki za binadamu, madaktari na kadhalika ili jambo hili ukweli wake uweze kufahamika. Tukiliacha jambo hili bila kutolea ufafanuzi na ukweli, nchi hii haitabaki salama. Naomba uweze kutoa maelekezo hayo ili jambo hili liweze kufanyiwa kazi.

MWENYEKITI: Waziri wa Sheria naona unatikisa kichwa vipi unataka kusema?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Hapana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto nimekuelewa na hili siyo suala la kulitolea majibu papo kwa hapo, nalipokea na muda muafaka nitakujibu kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kiti kinaendesha Bunge kwa Kanuni. Nimeona upande huu wakisema kwa nini siwahoji wakati muda wa *guillotine* umeingia, sasa sijui wameitoa wapi. Kanuni ya 104(2) ambayo ndiyo niliyoitumia kumaliza mjadala na kuingia kwenye *guillotine* inasema; "Iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kumaliza muda ulioongezwa chini ya fasili ya (1) na Kamati bado haijamaliza kupitisha mafungu yote, Mwenyekiti atafunga mazungumzo yanayoendelea na papo hapo na atawahoji Wajumbe kuhusu mafungu yaliyosalia, kama yapo." *(Makofi)*

Kwa hiyo, nachokihoji ni mafungu yale, Fungu 51, Fungu 52, Fungu 54 siyo kuwahoji Wabunge kama wameniruhusu nifunge mjadala au nisifunge. Sasa vitu vingine Mheshimiwa Waziri wa Nchi kweli inabidi kuwe na semina elekezi ili Wabunge waelekezwe hizi Kanuni zinavyosema. Kwa hiyo, Kiti hakijakosea, Kiti kipo *perfect* na Kanuni imesema sahihi labda kama wametoka kwa hisia zao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lingine katika mchango wa Mheshimiwa Khatib na nimshukuru Mheshimiwa Nape naye kalisema, wapinzani hawakukatazwa kuweka taarifa yao au kusoma, waliambiwa kuna maneno yanavunja Kanuni na Bunge linaendeshwa na Kanuni. Sasa wame-*withdraw* wao wenyewe, nataka iingie kwenye rekodi. *(Makofi)*

Baada ya maneno haya, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 2.30 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 17 Mei, 2016, Saa Tatu Asubuhi)